

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Sita – Tarehe 4 Februari, 2020**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Mkutano wetu wa Kumi na Nane, kikao cha leo ni kikao cha tano, Katibu

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazi Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

- (i) Toleo Namba 46 la tarehe 8 Novemba, 2019
- (ii) Toleo Namba 47 la tarehe 15 Novemba, 2019
- (iii) Toleo Namba 48 la tarehe 22 Novemba, 2019
- (iv) Toleo Namba 49 la tarehe 29 Novemba, 2019
- (v) Toleo Namba 51 la tarehe 13 Desemba, 2019
- (vi) Toleo Namba 52 la tarehe 20 Desemba, 2019
- (vii) Toleo Namba 53 la tarehe 27 Desemba, 2019
- (viii) Toleo Namba 1 la tarehe 3 Januari, 2020
- (ix) Toleo Namba 2 la terehe 10 Januari, 2020
- (x) Toleo Namba 3 la tarehe 17 Januari, 2020
- (xi) Toleo Namba 4 la terehe 24 Januari, 2020

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu shughuli za Kamati hii kwa Mwaka 2019.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kmaati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli zilizotekelawa na Kamati hiyo kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhuus shughuli zilizotekelawa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Ntemi Chenge. Katibu tuendelee.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.66

**Kuboresha Kituo cha Afya Kiagata – Butiama**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya Kituo cha Afya cha Kiagata kwani Wananchi wote wa Wilaya ya Butiama wanategemea Kituo hicho.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeiti, katika mwaka wa fedha 2017/2028 Serikali ilidhinisha na kutoa kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuboresha miundmbinu ya Kituo cha Afya cha Kiagati. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa nyumba ya mtumishi, wodi ya wazazi, jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la kuhifadhi maiti na kichomea taka. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Butiama kupitia mapato yake ya ndani imetumia kiasi cha shilingi milioni 37.5 kwaajili ya kukamilisha miundombinu iliyosalia pamnoja na kununua Jokofu la kuhifadhi maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hicho cha afya kwa sasa kinatoa huduma za upasuaji wa dharura, huduma za *ultrasound*, huduma za Mama na Mtoto na kulaza wagonjwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina swali la nyongeza.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Kaka yangu Kandege, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana iliyofanya ya kuboresha hiki kituo muhimu cha Kiagata ambacho sasa kinatoa huduma kwa kiwango cha ufanisi, na pia kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri sana iliyofanya ya kujenga vituo zaidi ya tisa katika Mkoa wa Mara, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuayavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa kituo cha Kiagata na hata hospitali ya Wilaya ya Butiama ina upungufu wa wataalam kwa kiwango cha asilimia 70, kwamba pia lipo tatizo kubwa la wataalam wa mionzi lakini vilevile hakuna x-ray kwa Wilaya nzima ya Bitiama ikiwemo hospitali ya Wilaya na hata kituo cha Kiagata.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inapeleka wataalam katika hospitali ya Butiama na Kituo cha Kiagata na hasa kipaumbele kikiwa ni wale watalam wa mionzi kwa ajili ya wakina Mama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Wilaya ya Butiama kwa mujibu wa sensa ina watu zaidi ya 200,003 na Butiama ni Wilaya ya kazi, watu wanakula wanashiba, population ya watu inaongezeka.

Vilevile kwa kuwa Wilaya ya Butiama ina kata 18 na ina vitongoji 370 lakini Kituo cha Afya ni kimoja tu cha Kiagata ambacho kinahudumia hata wananchi wote wa Wilaya y Butiama; Tarafa ya Makongoro iko mbali na Kiagata, Wananchi wa Makongoro wanapata shida sana kwenda Kituo cha Afya cha Kiagata;

- (i) Ni mkakati gani sasa wa Serikali wa kuboresha Kituo cha Bisumwa ili kiwe sasa kituo cha afya, ili kisaidie Kata saba?
- (ii) Serikali ina mkakati gani wa kuboreshga Zahanati ya Kirumi ili sasa isaidie Kata sita?
- (iii) Na Serikali ina mkakati gani wa kuboresha Zahanati ya Buhemba ili iweze kusaidia wananchi wa Wilaya ya Butiama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Amina Makilagi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nipokee pongezi ambazo ametoa kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi inayofanya ya kupeleka huduma za afya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, anaongelea suala zima la uharaka wa kuhakikisha kwamba wanakuwepo wataalam, na hasa wataalam wa mionzi, ili kazi nzuri iliyofanyika Kituo cha Kiagata iweze kutoa matunda. Naomba nitumie fursa hii kumuagiza Mganga Mkuu wa Wilaya, miongoni mwa wataalam waliopo atue angalau mtaalam mmoja akasomee kazi ya mionzi ili huduma ianze kutolewa ili huduma ianze kutolewa wakati Serikali inafikiria kupeleka wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametaja kituo cha afya lakini na zahanati kama tatu, sina uhakika kama ni swali moja lakini naomba itoshe tu nimambie Mheshimiwa Makilagi, kazi kubwa, nzuri ambayo anaipigania kuhakikisha hasa akina mama wanapata huduma ya afya, sisi kama Serikali tuko pamoja na yeye.

Naomba nitoe wito kwa halmashauri kuhakikisha kwamba maombi yote ambayo Mheshimiwa Amina Makilagi ameyatoa hapa yanazingatiwa katika bajeti hii ambayo inaanndaliwa na sisi Serikali Kuu hakika hatutamuangusha. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga Mbunge wa Mbozi sasa aulize swali lake

Na. 67

### **Ujenzi wa Wodi ya Wakina Mama Wilaya ya Mbozi**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Wastani wa akinamama wanaojifungua kwa siku ni 18 - 20 katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi; licha ya idadi kubwa ya akinamama wanaojifungua, kuna ufinyu wa majengo mbalimbali ikiwepo na wodi ya akinamama.

(a) Je, ni lini Serikali itashughulikia ujenzi wa wodi ya akina mama katika hospitali hii?

(b) Hospitali ya Wilaya ya Mbozi inatumika kama Hospitali ya Mkoa wa Songwe na haina maji safi na salama. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya maji safi na salama katika hospitali hii?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imefanya tathmini na kubaini zinahitajika jumla ya shilingi milioni 37 kwa ajili ya upanuzi wa wodi ya akina mama wanaojifungua. Mradi huo umepewa kipambele katika mpango wa bajeti wa mwaka 2020/2021 ili kuanza ujenzi.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri imeidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 12 kwa ajili ya kuchimba kisima cha maji katika hospitali ya Wilaya ya Mbozi ili kututua changamoto ya maji katika hospitali hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza; kwa kuwa katika majibu ya Serikali ni kwamba zimetengwa milioni 37 zitakazotumika katika kuboresha wodi ya akina mama wanaojifungua; na kwa kuwa wodi hiyo ni wodi ambayo kwa kweli akina mama wanapata shida, wanalala akina mama wawili katika kitanda kimoja na kuna msongamano mkubwa sana;

Je, Serikali sasa inaweza ikatupa majibu rasmi wana Mbozi na wana Songwe kwamba hizo fedha ni lini sasa zitakwenda rasmi? Kwasababu tatizo hili si dogo, ni kubwa sana. Akina mama wanapata shida na wanaweza kupata magonjwa kwasababu kuna msongamano ambaao kwa kweli si wa kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa pia katika Hospitali hii ya Wilaya ya Mbozi ambayo pia inatumika kama Hospitali Teule ya Mkoa wa Songwe kuna tatizo la ufinyu wa OPD; na OPD iliyopo pale ni ndogo sana na kuna msomngamano mkubwa sana.

Je, Serikali ipo tayari sasa kufanya upanuzi wa ile OPD ili iweze kuboreshwa na ichukue wagonjwa walio wengi zaidi kuliko hali iliyoko sasa ambayo wagonjwa ni wengi na OPD ni ndogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kujibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Haonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nimewmbia Mheshimiwa Mbunge commitment ya Serikali kwamba katika bajeti ya mwaka 2020/2021 milioni 37 zimetengwa. Tafsiri yake ni nini? Ni kwamba hiyo inaonesha seriousness ya Serikali katika kuahidi na kuweka katika maandishi. Naomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuiamini Serikali, tukiahdi tunatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anaongelea juu ya suala zima la ufinyu wa wodi, kwa maana kunakuwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa katika ile hospitali ambayo inatumika kama ndiyo hospitali ya rufaa ya Mkoa. Ni ukweli usiopingika kwamba hospitali ile mwanzo haikuwa imekusudiwa kuwa hospitali ya Mkoa; lakini pia ni ukweli usiopingika Serikali imekuwa ikifanyakazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba huduma ya afya inasogezwa na ndiyo maana hata ukienda kwa Mheshimiwa Haonga unakuta kuna kituo cha afya cha Kisansa ambacho tukienda tukafanya shughuli nzuri na yeye ni shuhuda. Aendelee kuiamini Serikali, kwamba tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba pale ambapo inahitajika tufanye upanuzi tutafanya pasi na kusita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Joseph Musukuma halafu Mheshimiwa Selasini; naomba maswali yawe kwa ufupi tafadhali.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa hospitali ya Wilaya Mpwapwa ilijengwa Mwaka 1975 na kwa kuwa wodi ya Wakina Mama wanaojifungua ni ndogo. Kama walivyosema wenzangu akina mama wanalala wawili, wanalala watatu ambapo ni hatari kaisa kuambukizana magonjwa.

Je, Mheshimiwa Waziri katika bajeti inayokuja, utatenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo kubwa la wodi ya akina mama katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Seneta Lubeleje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba hospitali za wilaya zilizojengwa miaka ya zamani ukilinganisha na uhalisia wa sasa hivi kumekuwa na upungufu wa baadhi ya majengo au msongamano umekuwepo kwasababu idadi ya watu inaongezeka. Naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na kazi nzuri ambayo inafanya na Serikali. Tumeanza na hizo hospitali 67; kwa kadri Bajeti itakavyoruhusu na uhalisia na kwake pia tutatazama nini cha kufanya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali katika kujenga vituo vya afya na hospitali lakini vilevile vifaatiba pamoja na wataalam ni muhimu sana; na muhimu zaidi ni elimu kwa Watanzania namna ya kutumia hizi hospitali na vituo vya afya. Kwasababu tumeshuhudia sasa hivi wamezuka watu wanawadanyanya Wananchi wavue nguo zao za ndani wapungie juu wapate ujauzito, sijui wanawanyweshwa jiki na vitu kama hivyo vya aibu tena wanaofanyiwa aibu hizi ni akina mama.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa Watanzania ili wajue wkamba kuna mambo ambayo yanahitaji utaalam wa kidaktari na si uongo wa watu wanaojilita mandabii na wachungaji wanaodhalilisha Watanzania katika mambo mbalimbali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa

Joseph Raman Selasini, Mbunge wa Rombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kujenga vituo vya afya na kupeleka huduma ya afya kama haitumiki hata umaana wenyewe unakua haupo. Naomba nikubaliane an Mheshimiwa Mbunge Selasini; lakini pia tukubaliane kwamba hii kazi si kazi ya Serikali peke yake. Sisi Waheshimiwa Wabunge tuna fursa katika forum mbalimbali ambazo tunakutana nazo, ni vizuri tukatoa elimu lakini pia hata maeneo ya makanisa, misikiti ni vizuri elimu ikapelekwa; si suala la kuiachia Serikali peke yake lakini pia Serikali haikwepi wajibu wa kuhakikisha wkamba elimu inapelekwa kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuskhuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuulizwa swali la nyongeza.

Jimbo la geita Vijiji lina population ya watu takribani 450,000 mpaka 500,000 na halina Kituo cha afya hata kimoja. Je, Serikali haionti umhimu wa kutupatia kituo chaafya katika Kijiji cha Ibisabageni, Tarafa ya Isuramtundwe kwa ajili ya kuokoa wale akina mama wanaosafiri kwa umbali wa Kilometra 80 kuipata hospitali ya Wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musukuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba uniruhusu kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Musukuma jinsi ambavyo amekuwa akipigania suala zima lafya na yeze amekuwa akijinasibu kwamba katika maeneo ambayo yamefanikiwa kujengwa hospitali nzuri ya Wilaya ni pamoja na kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inasogeza huduma za afya kwa wananchi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo amekuwa akitoa imani kwa Serikali azidi kuiamini kwamba pale ambapo wananchi na hasa sehemu ambayo population ni kubwa kama ambavyo ametaja katika eneo lake hakika kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu kwa siku za usoni na wao tutawajengea kituo cha afya.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendeleana Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 68

### **Maji Baridi Kuchanganyika na Maji Chumvi**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Dalili za maji safi na salama kuchanganyika na maji chumvi (bahari) zinatishia ustawi.

Je, nini utatuzi wa tishio hili?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa maji safi na salama kuchanganyika na maji chumvi bahari yanatishia ustawi wa jamii na kilimo. Hali hiyo inasababishwa na athari ya mabadiliko ya tabianchi, kutokana na kuongezeka kwa joto la dunia linalosababisha na kuyeyuka kwa barafu kwenye ncha za dunia na kwenye vilele vya milima mirefu. Kuyeyuka huko kwa barafu kunasababisha maji kutiririka kwenda baharini na kuongeza ujazo wa maji ya bahari na kusambaa katika maeneo ya mwambao ambayo yana shughuli muhimu za kijamii kama vile visima vya maji, kilimo na miundombinu muhimu ambayo huingiliwa na maji chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya sita ya jopo la watalaam inaonesha kuwa ujazo wa bahari umeongezeka kwa sentimita 19 katika miaka ya hivi karibuni na kusababisha mmomonyoko wa kingo za bahari na baadhi ya maeneo ya Pwani yameingiliwa na maji chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa kudumu wa suala hili unahitaji ushirikiano wa Kimataifa hususani katika kupunguza gesi joto ambazo huchangia ongezeko la joto duniani ambalo husababisha mabadiliko ya tabia nchi. Kwa kuwa suala la kupunguza gesi joto sio rahisi kufikiwa katika kipindi kifupi nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zinahimiza kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo kuchimba visima vipyta, kupanda miti ya mikoko katika maeneo ya kandokando ya bahari, kujenga kuta na makinga maji pale panapowezekana na kuhamasisha shughuli za kilimo kufanya katika maeneo mengine ambayo haya jaa thirika. Sambamba na suala la kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, nchi zinazozalisha gesi joto kwa wingi zinahimizwa kupunguza gesi joto ili kuzuia athari zaidi za mabadiliko ya tabianchi. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau, Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira kwa suala lake zuri ambalo alilolitoa hivi sasa hivi hapa. Lakini pia nimpongeze kwa suala langu la Bunge lilipopita wakaja Zanzibar wakaja kutuhimiza ahadi yake ya kuja kuangalia mambo ya hali ya hewa ya mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa mikoko ina mchango mkubwa wa kunusuru mazingira nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha inaotesha mikoko ambayo inauwezo wa kunusuru maji chumvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili bila maji baridi hatima ya kilimo na uhai wa binadamu viko hatarini. Je, kuna tafiti zozote za kuyalinda kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji baridi ahsante? (Makof)

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji Mbunge wa Viti Maalum ni kweli amekuwa mstari wa mbele na sasa hivi amekuwa mwana mazingira tunamtumia sana hasa kwenye eneo hili la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwa maswali yake mawili; moja, tunao mkakati maalum na unaendelea kwa kushirikisha wenzetu wa Serikali za Mitaa hasa kwenye

halmashauri zetu kuhakikisha wanaweka miche kwa ajili ya mikoko ambayo itatumiwa kwenye maeneo hayo tuliyoyaeleza ya Pwani pembezoni mwa bahari. Na mkakati huo unaendelea na miche ipo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, utafiti zinaendelea na mpaka sasa tupo na utafiti unaendelea na wakati wowote tutaweka suala hili katika utaratibu ambao tutahakikisha maeneo haya kunakuwepo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye kila eneo ambalo kuna mwambao wa bahari ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa nikauliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri tunajua ama ni ukweli kwamba mazingira hasa kwenye upande wa carbon and mission ni nchi ambazo zilizoendelea ndio zinazemit hii carbon na athari kubwa inatokea kwa nchi ambazo zinaendelea ikiwemo Tanzania. Lakini nchi hizo ambazo zinaharibu sana mazingira haya zimekuwa zinasita kutoa finance kwenye climate change. Labda Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipangaje kuhakikisha kwamba inapambana katika kukabiliana na matatizo haya ya climate change ikiwemo mitigation adaption? (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Muungano Mheshimiwa Azan Zungu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli kuna baadhi ya nchi kubwa duniani ambazo zimejitoa kwenye mkataba huu wa tabianchi kutohana na maslahi yao binafsi, lakini vilevile nchi zilizobakia zikiongozwa na Ufaransa na Qatar na nchi zingine wameanzisha mfuko wa one bilioni 100 Us dollars ambazo zitatumika kwa nchi zote ambazo zitahitaji pesa hizi kuboresha mazingira katika nchi zao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatuko nyuma tulishaanza mkakati wa kuziomba pesa hizi na program mbalimbali za kuhakikisha nchi yetu inafaidika na pesa hizi na kulinda mazingira. Programu ya kwanza ni kuhakikisha tunapanda miti Mlima Kilimanjaro zaidi ya miti bilioni moja ili kulinda barafu ambayo ipo katika nchi yetu. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Muungano. Tunaendelea na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge wa lleje sasa aulize swali lake.

Na. 69

#### Kutoza Ada Mkaa Unaosafirshwa Nje ya Nchi

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. JANET Z. MBENE)** aliuliza:-

Uchomaji wa mkaa kwa kiasi kikubwa unatumia miti ya asili pamoja na mapori ya akiba, ukataji wa miti hauendi sambamba na upandaji wa miti na hii ina athari kubwa sana kwenye mazingira yetu ikiwemo kupungua kwa mvua na kukauka kwa vyanzo vyaa maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoza ada kwa mkaa unaosafirshwa nchi za nje ili iweze kurejesha mazingira katika hali yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge lleje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uchomaji wa mkaa hutokanao na miti kwa kiasi kikubwa unatumiamiti ya asili pamoja na mapori ya Akiba na nidhahiti ukatajia wa miti hauendi sambamba na upandaji wa miti na hii ina athari kubwa sana katika mazingira yetu. Ikiwemo kuendelea kupotea kwa *Bionuai*, kupungua kwa mvua na kukauka kwa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mkaa inafanyika katika kwa mujibu wa sheria ya misitu ya mwaka 2002 kanuni za mwaka 2004 ni miongozo mbalimbali. Aidha, usafirishajji wa mkaa nje ya nchi umezuiiliwa kwa mujibu wa kifungu Na. 16 cha sheria inayozuia usafirishajji wa baadhi ya bidhaa nje ya nchi yaani *The export control Act cape 381RE 200* pamoja na makatazo mengine. Vilevile tangazo la Serikali Na. 417 la tarehe 24 Mei, 2019 kifungu Na. 21(1) limetoa zuij kwa mtu yoyote kusafirisha mkaa kwenda nje ya nchi isipokuwa mkaa mbadala yaani *charcoal briquettes* na kwa kibali maalum kutoka kwa Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa sasa Serikali haisafirishi mkaa unaotokana na miti kwenda nje ya nchi kama ilivyotoa ufanuzi hapo juu gherama za kurejeleza au kung'oa kuondoa maeneo yaliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwemo mkaa zitatokana na mapato yanayopatikana kuitia tozo mbalimbali zilizoainishwa kwenye sheria ya misitu ya mwaka 2002 ikiwepo asilimia tano ya ushuru wa halmashauri inayotozwa kwa wafanyakishara kwa mazao ya misitu. Aidha, tozo nyingine zinazotokana na tozo za ukaguzi wa biashara ya mkaa unaotokana na mabaki ya miti au mimea kwa maana ya *briquettes* ambaa unaruhusiwa kwenda nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Victor Mwambaliaswa kwa niaba ya Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri saa ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu swalii hili nina maswali ya nyongeza mawili. La kwanza nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akiongelea *charcoal briquettes* bada la mkaa wa kawaida kutumia *charcoal briquettes* ambaa utengenezaji wake sio lazima utumie miti unatumia majani ya miti, majani ya kawaida haya kuweza kutengeneza mkaa huo ambaa una nguvu kuliko mkaa wa kawaida.

Je, ni lini Serikali itaanza kuhamasisha wananchi waaenze kuchoma *charcoal briquettes* badala ya kutumia miti kuchoma mkaa hilo la kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimefurahishwa sana na majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwenye swalii la nyongeza la swalii namba 68 kuhusu kupanda mamilioni ya miti kwenye Mlima Kilimanjaro ili kuupunguzia *climate stress* huu Mlima Kilimanjaro.

Je, ni lini Serikali itaanza kampeni hiyo ya kupanda miti sio tu kwenye Mlima Kilimanjaro bali nchi nzima wananchi waanze kupanda miti? (Makofu)

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa swalii la pili mkakati unaandaliwa sasa hivi wa kupanda miti katika Wilaya zote na sasa sio kupanda miti tu, kupanda na kuitunza miti ili isije ikafa. Mara nyingi sana halmashauri wanahamasika kupanda miti lakini baada ya muda mfupi miti ile inakufa na tutaweka aina maalum ya miti kwa Wilaya ambayo itakayoweza kufaa kuna miti mingine haifai kwenye Wilaya

mbalimbali, miti hii inapandwa kwa gharama kubwa na inakufa. Kwa hiyo, program kaguzi tutaanza tutashirikiana na halmashauri zote kuhakikisha miti inapandwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu, nchi yetu imebarikiwa kuwa na asilimia 39.9 kuwa ni misitu, misitu hii inapotea. Kuanzia mwaka 1990 mpaka 2010 tumeshapoteza takribani hekta milioni nane ya misitu na hii ni hatari kubwa sana kwa Watanzania tuhakikishe tuache kukata miti tutunze miti kama fursa ya kibiashara, tutumie miti badala ya kukata tuweke mazao ya nyuki. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante halmashauri zimekuwa zikichukua hatua kali sana kwa hawa wafanyabishara wa mkaa hususani katika mikoa ya pembezoni.

Sasa nataka nifahamu mkakati wa Serikali pamoja na juhudini ambazo mnazifanya za kuhakikisha tunatunza mazingira na ukizingatia uuzaaji wa gesi bado ni gharama kwa mwananchi ambaye hana kipato kikubwa. Serikali mna mkakati wa gani wa kuhakikisha haya matumizi ya gesi kwa bei ya chini yanaenda sambamba na kupunguza gharama za manunuza ya mkaa? (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Muungano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kuleta gesi wananchi watumie umeshanza. Napongeza Wizara ya Nishati Pardon Project imeshaanza na imeshaanza kuonesha gharama ni za chini na hivi karibuni Wizara ya Nishati itaanza mkakati kuhakikisha gesi tunapitisha katika nyumba zote Dar es Salaam na tukitoka Dar es Salaam tunakwenda mikoa mingine Iringa kwa Msigwa kule. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Azzan Zungu Waziri wa Muungano tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Desderius John Mipata Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 70

### **Mahakama ya Mwanzo**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Tarafa ya Wampembe ina Kata za Kala, Wampembe, Kizumbi na Ninde na ambazo zote ziko umbali wa zaidi ya km 80-150 kutoka Makao Makuu au mahali ambapo huduma za Mahakama zinaweza kupatikana:-

Je, ni lini Serikali itajenga walau Mahakama ya Mwanzo katika moja ya Kata hizo hususani Kata ya Wampembe ili kusogea huduma hiyo kwa Wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa na huduma za haki zinazozingatia karibu na wananchi Mahakama ya Tanzania imeazimia kuwa na Mahakama Kuu na

Mahakama ya Mahakimu Mkazi kwa kila Mkoa, Mahakama ya Wilaya kwa Wilaya na katika ngazi za tarafa kuwa na walau Mahakama moja ya mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Wampembe aliyouliza Mheshimiwa Mbunge tayari Mahakama ya Mwanzo ipo na inatumia jengo la Ofisi ya Tarafa. Ni kweli kwa muda mrefu wananchi wa Tarafa hii wamekuwa wamekuwa wakifuata huduma za Mahakama umbali mrefu. Lakini kuanzia tarehe 23 Aprili, 2018 Mahakama ya Mwanzo ya Wampembe ilifunguliwa na mpaka sasa inaendelea kutoa huduma kwa wananchi kwa eneo hilo na maeneo ya jirani. Pamoja na jitihada hizo Mahakama inaendelea na kuratibu na kupata eneo katika Tarafa hiyo ili uweze kujenga jengo la Mahakama ya Mwanzo Wampembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha Wizara yangu, kwa kushirikiana na Mahakama tumeponga kujenga jengo la Mahakama ya Wilaya ya Nkasi, ambalo pia litatumika na Mahakama ya Mwanzo ya Yanamanyere. Ujenzi huu unatarajiwa kuanza mwezi Mei mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Mbunge wa Halmashauri ya Wilaya kwa kujitahidi na kuuliza swali hilo na jitihada zote zinazofanyika kuwezesha upatikanaji wa jengo la kuendesha Mahakama ya Mwanzo Wampembe ambalo linatuwezesha kutoa huduma kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo jirani wakati tukiendelea na taratibu za kupata jengo la Mahakama ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Desderius John Mipata swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nishukuru sana majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza katika majibu ya Serikali nimeeleza kwamba kuna juhudhi zinafanyika za kupata eneo ili jengo la Mahakama ya Wampembe lipatikane. Lakini niseme tu kwamba tatizo la kupata eneo si tatizo kupata eneo mimi na wananchi tunaahidi kutoa eneo kwa haraka. Tunaiomba Serikali kuititia na kwa vile sasa hivi tunaenda kwenye bajeti.

Je, Serikali itakuwa tayari kuweka au kutenga pesa ya ujenzi wa jengo hilo la Mahakama ya Wampembe kwa mwaka huu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuititia bajeti ya Serikali tumekuwa tukiahidiwa wananchi wa Nkasi kupata Mahakama ya Wilaya miaka mitatu mfululizo na leo kwenye kuititia majibu ya swali hili Serikali inatoa ahadi kwamba mwezi wa tani ujenzi huo utaanza. Je, zile sababu ambazo zipelekea tukashindwa kujenga na wananchi wakaanza kutuona Wabunge tunapoenda kuwaambia tutapata jengo kwamba ni waongo? Je, zimeondoshwa? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ingawa hatutajenga Mahakama katika eneo hilo mwaka huu katika bajeti yetu lakini tutatoa kipaumbele katika bajeti itakayofuata mwaka kesho kama inaavyosema tufanye kazi kwa pamoja na tutajitahidi kutumia Mahakama ambayo sasa hivi iko katika hilo jengo ambalo tumeliazima lakini tunajitahidi tuingize katika bajeti ya mwaka kesho suala hili la ujenzi wa Mahakama haki. Tunatoa kipaumbele kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lako la pili tumejitetahidi na mmjeitahidi na tunashukuru tumeondo vikwazo vyote tumeingiza kwenye bajeti ya mwaka huu na mwezi Mei, nakuhakikishia ujenzi wa Mahakama hiyo utaanza bila wasiwasi ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka, Mheshimiwa Mariaum Kisangi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale ni wilaya ambayo ilianzishwa mwaka 75 leo ina umri wa miaka 45. Wilaya ile ina kata 20 lakini Mahakama mbili tu Mwanzo, na Mahakama ya Mwanzo ya Liwale Mijini ndio inayochangiwa na Mahakama ya Wilaya kwa maana kwamba Mahakama ya Wilaya hawana jengo. Lakini nilipouliza swali hili mwaka 2017 Mheshimiwa Kabudi akiwa hapo kwenye hicho kiti alisema mwaka 2018 inajengwa hospitali ya Wilaya. Je, Serikali kwenye majibu yale mlikuwa mnanidanganya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri najua mlikuwa hamdanganyi, karibu kwa majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavoyelewa ni kwamba huwa kunakuwa na jitihada za pekee, kama Waziri anatoa majibu, anafanya kila njia kuweza kuhakikisha kwamba inatekelezwa. Ningependa kurudi na kutazama rekodi za mazungumzo hayo na jitihada ambazo zilifanywa, lakini Liwale ni mahali ambapo kama ulivyoona mchakato wa kufungua Mahakama katika Wilaya za Lindi na Mtwara, umekuwa ukiendelea kwa kasi sana. Kama kulikuwa na ahadi kama hiyo, Wizara tungependa kufuatilia na Mahakama iendelee kujitahidi kutekeleza ahadi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafuatilia pia masuala mengine yanayohusiana na Mahakama ya Liwale. Mheshimiwa Mbunge tumekuwa tukizungumza mara kwa mara. Nataka kumhakikisha kwamba sisi ni wasikivu na tunafuatilia kwa karibu mahitaji yenu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kwa ridhaa yako naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wake wa Ilani wa ujenzi wa Mahakama za Wilaya nchini Tanzania. Tunashuhudia Mahakama mbalimbali za Wilaya zikizinduliwa zikiwemo za Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuboresha Mahakama za Mwanzo za Kariakoo, Magomeni, Ilala, Temeke na Mbagala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ni mahali pa watu wengi, mashauri ni mengi na kioo cha Taifa na cha Wizara yangu. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba Mahakama hizi zinakuwa na sura nzuri na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha ina maana tatu. Kwanza ni kufanya ukarabati wa kuhakikisha kwamba Mahakama hizi ziko katika hali nzuri. Kuboresha pia kunamaanisha kwamba, Mahakama hizi zipewe teknolojia ya kisasa hasa katika uwezo wa kuandikisha Mahakama na kuweza kusikiliza kesi hizi. Tunaingiza utaratibu wa teknolojia ya kuweza kusikilizwa kesi hizi na kuandikisha na Mahakama za Dar es Salaam zinapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mkakati wetu wa kutumia magari ya kusikiliza kesi, tumeanza utaratibu huo na kufanya majoribio katika Mkoa wa Dar es Salaam. Katika uboreshaji wa aina hii mwanzo itakuwa ni Dar es Salaam kabla hatujapeleka sehemu nyingine zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake, Wizara hiyo hiyo ya Katiba na Sheria.

**Ushahidi Kwenye Kesi za Ubakaji**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wakuleta Bungeni marekebisho ya Sheria ili kupunguza kiwango cha ushahidi kwenye kesi za ubakaji na hasa ubakaji wa Watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo namba 71.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushahidi katika kesi za daawa ya jinai hususan kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 yanaadhidiwa kwa mujibu wa Kifungu cha 130(1) na 13(2)(e) cha Kanuni za Adhabu, Sura ya 20. Makosa haya kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi yanahitaji kuthibitishwa pasipo kuacha shaka yoyote ili mtuhumiwa atiwe hatiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiwango cha kuthibitisha mashauri ya jinai pasipo kuacha shaka yoyote, kiwango cha ushahidi kitategemea mazingira ya kosa husika na namna yalivyoendeka na mashahidi walioshuhudia kutokea kwa tukio hilo. Sheria haijatoa masharti ya idadi ya mashahidi wanaotakiwa kutoa ushahidi. Hivyo, kila kesi huangaliwa kwa kuzingatia mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo na kwa lengo la kumlinda mtoto aliyeathirika na tukio la ubakaji, mwaka 2016 Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho katika Kifungu cha 127 cha Sheria ya Ushahidi kwa kuondoa masharti ya kumhoji mtoto ili kupima ufahamu wake na badala yake kuweka masharti ya Mahakama kujiridhisha kuwa mtoto ana uwezo wa kusema ukweli pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali inaendelea na itaendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai ili kuondoa vikwazo vyote vinavyokwamisha usikilizwaji, siyo tu wa mashauri ya namna hii, bali mashauri yote yanayohusu makundi ya watu katika jamii yetu ili kulinda utu wao ikiwemo watoto, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu wanaoathirika na vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na ubakaji. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba kuna changamoto kubwa sana ya ukatili kwa wanawake, ikiwemo na watoto kwenye masuala ya ubakaji. Nasi tunafahamu kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inataka kuwashakikishia usalama Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye makosa ya ubakaji, kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 5 cha Sheria ya Sexual Offences Special Provisions Act ya Mwaka 1998 ambayo imeenda kufanya marekebisho ya Kifungu cha 130 cha Sheria ya Adhabu (*Penal Code*), tunaona kwamba, kigezo au masharti ya kuthibitisha kosa la ubakaji ni mpaka yule aliyebakwa athibitishe kwamba kulikuwa kuna kuingiliwa (*penetration*). Mazingira hayo ni magumu sana katika utaratibu wa kawaida kuthibitisha kwamba mtu amekuingilia, yani ku-prove *penetration* siyo kitu kirahisi na hasa kwa watoto. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni swali la kwanza. Nataka kufahamu: Je, Serikali haioni katika mazingira haya kwamba kufanyike marekebisho ya sheria, ili standard of proof au ili

kuthibitisha kosa la ubakaji ipunguzwe kiwango chake ili kusiwe kuna haja ya ku-prove penetration kwa sababu, watoto siyo rahisi kwao kuweza kuthibitisha jambo kama hilo, lakini mazingira yote kiujumla ya kosa hilo yaangaliwe ili kuweza kutoa haki. Hilo swalii la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili: Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuongeza adhabu kwa wale watakaothibitika kwamba wamefanya kosa la ubakaji ili adhabu yao iwe kali ili kuhakikisha kwamba makosa haya ya ubakaji yanakwisha na watu waogope?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Serikali haioni kwenye kosa la ubakaji, mbakaji apewe adhabu ya kuhasiwa ili asije akarudia tena kufanya kosa kama hilo ambalo linaleta ukatili mkubwa sana kwa wanawake na watoto na linawaathiri kiasi kwamba, hata kama mtu amechukuliwa hatua, bado wale ambaa wameathirika wanapata athari kwa muda mrefu zaidi? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kusimamia haki za watoto na hasa wanawake katika kutoa ushahidi kwenye makosa ya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika majibu yangu nimesema, la kwanza tumeondoa baadhi ya vigezo ambavyo vilikuwepo vya hasa watoto kuweza kutoa ushahidi wenyewe na kuachia Mahakama uamuvi wa busara na wa kitaalam kuweza kutoa ushuhuda huo kama kitendo hicho kimetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimesema katika jibu langu kwamba sasa hivi kuna mfumo wa kutazama na kuboresha mfumo mzima wa kesi za jinai. Na katika hilo litakuwa hilo lingine linalohusiana na ubakaji; na kama itatoa mapendelekezo, nina hakika pia mapendelekezo hayo yatafuatana na adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie kweli kwamba, kwa makosa haya adhabu ambazo zipo mpaka sasa, ni kali na inafika mpaka miaka 30 na mmejadili katika Bunge hili. Kama itabidi kuongeza adhabu hizo baada ya marekebisho na mapitio ya sheria hizi, ninashauri kwamba Bunge hili likae na tushauriane na tuweze kuzungumzia suala hili. Linahitaji uamuvi wa kisheria kama tunataka kufanya adhabu kali zaidi kuliko zilizopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia mwenyewe Magerezani kuwaona watu wenyewe makosa kama haya wamepewa adhabu ya miaka 30 na wengi wao pengine watafia Magerezani. Ahsante sana. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, karibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba tu niongezee katika majibu mazuri sana aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kuhusu swalii la nyongeza la kwanza la Mheshimiwa Zainab kwamba bado vigezo inaonekana ni vikubwa sana katika kuthibitisha makosa; napenda tu kumwambia kwamba katika ile Sheria ya Sexual Offences Special Provisions Act ilipopitishwa, mojawapo ya masuala iliyoyaondoa kwenye Sheria ya Ushahidi ilikuwa ni ile requirement ya collaboration. Collaboration ilikuwa ni lazima uoneshe kwamba kuna ishara fulani zilizosalia baada ya lile tendo la ubakaji na hiyo ilikuwa inadhalilisha. Kwa hiyo, sheria hiyo iliondoa kitu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku ni lazima haya yote yafuate misingi ya sheria za jinai, kwamba, lazima kuthibitisha pasipo kuacha shaka ili pia anayetuhumiwa asije akatuhumiwa isivyo sahihi au akapewa adhabu isivyo sahihi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili suala la kuongeza adhabu, tayari sheria ile kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, imeongeza adhabu imekuwa kali sana ni miaka 30. Sasa hili pendekezo la kuhasiwa lina tatizo moja, litatusababisha kuvunja Katiba, kwa sababu, Ibara ya 13(6) inaeleza kwamba ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhaliilisha. Kwa hiyo, tukichukua pendekezo la kuhasiwa linatupeleka tena katika upande mwingine ambapo tutaweza kuvunja Katiba. Nafikiri adhabu zilizopo zinajitosheleza kwa sasa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu, lakini hicho kifungu hakimhusu mbakaji kwamba, naye anamtesa yule mtoto? Siyo adhabu hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ummy Mwalimu, naomba maelezo ya ziada.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama sambamba na majibu mazuri ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Katiba na Sheria na swali zuri ambalo ameliuliza Mheshimiwa Zainab Katimba. Nilitaka tu kuweka mkazo. Sheria peke yake, hata tuwe na sheria kali kiasi gani hatutamaliza tatizo la ubakaji na ulawiti wa watoto na wanawake nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesimama hapa kuendelea kutoa msisitizo kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kutimiza wajibu wetu wa malezi na ulinzi wa watoto. Inasababisha mtoto anabakwa miezi mitatu bila mzazi kujua. Unajiuliza hivi huyu mtoto ana wazazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, narudisha mzigo kwa wazazi na walezi tutimize wajibu wetu, tuwafuatilie watoto wetu, tuwakague watoto wetu, tuwaulize watoto wetu, tujenge urafiki wa watoto wetu kutueleza changamoto na matafizo ambayo wanayapata. Tutaweka sheria kali, wazazi wata-negotiate na wabakaji mwisho wa siku hakuna hatua ambazo zitachukuliwa. Nakushukuru sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy. Mimi nakubaliana nawe moja kwa moja kwa sababu hayo ndiyo yanatakiwa. Ushirikiano katika jamii ni muhimu zaidi, lakini bado naenda na Mwanasheria Mkuu tuangalie vifungu vyta Katiba ambavyo vinamlinda yule mbakaji asiteswe wakati watoto wetu wanaendelea kuteseka na kubakwa. (Makof)

Naomba tuendelee sasa na swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum. Swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

Na. 72

#### Hitaji la Kiwanda cha Maziwa Makete

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING (K.n.y. MHE. NEEMA W. MGAYA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kiwanda cha maziwa Wilayani Makete?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri a Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega karibu kwa majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe una ng'ombe wa maziwa 19,759 na idadi kubwa ya ng'ombe hawa wapo katika Wilaya ya Makete ambapo wanakadiriwa kufikia 8,310.

Katika mwaka 2018/2019 uzalishaji wa maziwa kwa Mkoa wa Njombe ulifiki lita 8,846,496 zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 6,596,925,230/= na wastani wa bei ya maziwa ulikuwa kati ya shilingi 670/= hadi 1,000/= kwa lita moja. Mwaka 2018/2019 Wilaya ya Makete ilizalisha maziwa lita 1,241,550 zinazokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 1,241,550,000/= na kuifanya Wilaya hii kuwa ya tatu kwa uzalishaji wa maziwa katika Wilaya za Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wilaya ya Makete inazalisha lita 103,462.5 kwa siku moja. Kwa takwimu hizi ni wazi kwamba maziwa ni bidhaa muhimu kwa kuongeza kipato cha wananchi wa Wilaya ya Makete na Mkoa wa Njombe kiujuimla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe una kiwanda kimoja cha Maziwa cha Njolifa kilichopo Njombe Mjini chenye uwezo wa kusindika maziwa lita 20,000 kwa siku na mwaka 2018/2019 kilisindika lita 1,620,000. Ni wazi kwamba kiwanda hiki kina uwezo mdogo wa kusindika maziwa ukilinganisha na maziwa yanayozalishwa na wafugaji kwa Mkoa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kutambua umuhimu wa tasnia ya maziwa kwa wananchi wa Wilaya ya Makete na nchi kwa ujumla, Serikali ya Awamu ya Tano immeendelea kuhamasisha wawekezaji katika Wilaya ya Makete na eneo nzima la Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini. Kwa sasa kiwanda cha ASAS kipo katika hatua za mwisho za upanuzi wa kiwanda chake kipyा Wilayani Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Kituo cha Uwekezaji tunaendelea na kampeni ya kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya maziwa kwa eneo la ukanda huu ili kuweza kutumia maziwa yote yanayozalishwa Mkoani Njombe ikiwemo Wilaya ya Makete. Hivyo, Wizara inaendelea na jithada za kuhakikisha mwekezaji mahiri anapatikana ili kuhakikisha maziwa yote yanayozalishwa na Mkoa wa Njombe ikiwemo Wilaya ya Makete na maeneo yanayouzunguka Mkoa huu yanapata soko la uhakika kupitia kiwanda au viwanda vitakavyojengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Norman.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Makete tumekwenda pale na Waziri kutembelea kile kituo tukaona kwamba idadi ya ng'ombe wanaotakiwa kuwepo pale ni 4,000 lakini sasa hivi wako ng'ombe 750 tu. Ni Lini Serikali itapeleka ng'ombe wa kuzaliana Kitulo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa majibu yaliyokuwa yakiendelea Mheshimiwa Naibu Waziri na swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na Kituo cha Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namuunga mkono kabisa kwamba Kituo chetu cha Kitulo ndiyo Kituo pekee cha uzalishaji wa Ng'ombe wa maziwa bora hapa nchini kwetu, na ni kweli kabisa kwamba idadi ya Mifugo imepungua kwenye lile shamba letu; na kama yeye mwenyewe alivyo sema hivi karibuni nilikuwa kwenye ziara katika eneo hilo.

Nataka tu nimhakikishie kwamba tunakamilisha mipango ya kuhakikisha kwamba shamba letu hilo tunaliboresha upya kuanzia uoteshaji wa nyasi katika shamba lenyewe pamoja na miundombinu mingine iliyochakaa. Vilevile kuhakikisha kwamba ng'ombe wanarejeshwa mle, kwa maana ya kuongeza idadi ya ng'ombe, ili iendane na ukubwa wa eneo na mahitaji ya wananchi amba kwa sasa wanahitaji mitamba mingi sana kila sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tukuhakikishie kwamba ujio wangu ule ndiyo ilikuwa mipango ya kuanza kununua ng'ombe wengine na kujaza kwenye hilo shamba lakini na kuhakikisha kwamba mahitaji ya wananchi wa Tanzania wanaohitaji mitamba bora kutoka Kitulo wanaipata mitamba hiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Kiruswa halafu Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa swali la nyongeza Mkoa wa Njombe ni moja ya Mikoa yenye hali ya hewa nzuri ambayo inaruhusu ng'ombe wa maziwa kuweza kustawi na kuzalisha maziwa ya kutosha. Je, ni nini Mkakati wa Wizara kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Njombe amba wanapenda kufuga wanapata ng'ombe bora wa kisasa ili uzalishaji uongezekere na pia ili Viwanda viweze kupata malighafi za kutosha? Ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa Serikali katika kuhakikisha tunaongeza idadi ya ng'ombe katika Mkoa wa Njombe. Majibu ya msingi na majibu ya ziada yaliyojibiwa na Mheshimiwa Waziri yameeleza wazi juu ya Mkakati wa Serikali wa kuongeza idadi ya mitamba katika mashamba yetu ya Serikali likiwemo Shamba la Kitulo lililopo katika Mkoa huo wa Njombe; pia vilevile shamba letu la sao hill lililoko pale Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hii kwa pamoja, pamoja na mikakati mingine ya kuanzisha makambi ya uhimilishaji wa ng'ombe mikoani, amba tunaendelea nao hivi sasa katika maeneo mbalimbali ya hapa nchini ya kuongeza mbali ama breed za kisasa za ng'ombe watakaotuletea tija zaidi inayokwenda sambasamba na kutuhakikishia kufikia katika lengo la kuwa na ng'ombe wa maziwa wa kutosha nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa tuna takribani ng'ombe milioni moja wa maziwa wazuri; na mkakati wetu ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2021/2022 tuwe na jumla ya ng'ombe milioni nne watakao kuwa ng'ombe wazuri wa maziwa kwa ajili ya uzalishaji mkubwa wa maziwa na kuingiza katika viwanda vyetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli tayari? Haya! Tunaendelea sasa na Wizara hiyo hiyo Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa David Mathayo David Mbunge wa Same Magharibi.

Na. 73

**Ahadi ya Kujenga Malambo na Majosho Kata ya**

**Ruvu Same**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Serikali iliahidi katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kujenga malambo, majosho na kisima kirefu kwa ajili ya Wananchi wafugaji wa Kata ya Ruvu Jimbo la Same Magharibi?

Je, ni lini ahadi hiyo itakamilishwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mhe. Dkt. David Mathayo Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuitia bajeti yake pamoja na program mbalimbali imeendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya maji ya mifugo katika maeneo mengi ya ufugaji hapa nchini ili kupunguza tatizo la maji hasa wakati wa kiangazi kikali. Katika Mwaka huu wa Fedha 2019/2020 Wizara imetenga fedha Jumla ya shilingi 700,000,000 kwa ajili ya kujenga visima kumi na kukarabati mabwawa kumi katika mikoa kumi Tanzania Bara. Katika utekelezaji wa mpango huo, kisima kimoja kinatarajiwa kuchimbwa katika Wilaya ya Same, hususan Kata ya Ruvu ili wafugaji waweze kupata maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2019/2020 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati majosho 161 nchi nzima ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengine. Mpaka sasa, majosho 46 yamekamilika, majosho 95 ukarabati unaendelea na majosho 20 ukarabati bado haujaanza. Aidha Wizara imejenga joshu moja la kisasa Wilayani Bariadi. Pia Halmashauri mbalimbali zinakarabati majosho 288 na zinajenga majosho mapya 84. Kwa Halmashauri ya Same joshu moja linakarabatiwa na Wizara katika Kata ya Ruvu-Muungano na matatu yanakarabatiwa na Halmashauri yaliyopo kwenye vijiji vya Mwembe, Bangalala na Mkonga. Mikakati ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo inaendelea kadri fedha zinapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Napenda kuchukua fursa hii kutoa rai kwa halmashauri zote hapa nchini ikiwemo Halmashauri ya Same kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga, kukarabati na kuendeleza miundombinu ya mifugo katika maeneo yao kwa kutumia fedha zinazopatikana kutokana na makusanyo ama tozo za mifugo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Mathayo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini niwashukuru pia kwamba sasa wataanza kuchimba kisima kirefu kwa ajili ya wafugaji wa Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi hii ya Serikali ni ya mwaka 2012/2013 na mwaka 2015 wataalamu walikuja Kata ya Ruvu na kubainisha maeneo ya majosho na malambo pamoja na visima virefu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imeshakuwa ni muda mrefu na wafugaji wale wa Kata ya Ruvu wanahangaika sana kuhamisha mifugo huku na kule. Je, Serikali haioni kwamba kwa sasa na hasa kwenye bajeti hii inayokuja ya mwaka 2020/2021 wakatenga

fedha za kutosha ili waweze kukamilisha ahadi yao ambayo ilishakubalika mwaka 2012/2013 ili wananchi hao wa Ruvu waweze kupata hii huduma ya malambo na majosho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutembelea Wilaya ya Same na kuona maeneo ambayo yanahitaji miundombinu ya mifugo kusudi wafugaji wale waweze kupata miundombinu hiyo na mifugo iweze kupata huduma hiyo kama inavyotakiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa David Mathayo ambaye ni Waziri Mstaifu wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvu, na kwamba nijibu maswali yake mawili kama alivyouliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niko tayari kufanya ziara jimboni kwake mara tu baada ya Bunge hili kumalizika na kwenda kukutana na wafugaji wa maeneo hayo na kukagua miundombinu yao na kutafuta namna ya kuiboresha ili waweze kupata sehemu nzuri ya kunyweshea mifugo yao lakini pamoja na kuogeshea mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nakubaliana na yeye kwamba katika bajeti hii inayoanza tutaingiza mradi wa lambo katika jimbo lake; ambao umekuwa wa muda mrefu sana kama alivyoeleza mwenyewe, tangu yeye mwenyewe akiwa Waziri na mpaka leo hii ahadi hiyo haijatekelezwu. Sasa safari hii tutaitekeleza kwa kuweka bajeti kwenye mpango wetu wa Serikali ambao tutauanza hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma Mbunge wa Mtwara Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 74

#### Amani na Utulivu Katika Chaguzi Nchini

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Je, Serikali inahakikishaje amani na utulivu vinakuwepo katika chaguzi mbalimbali nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwafahamisha wananchi kuwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa amani na utulivu vinatamalaki nchini wakati wote bila kujali nyakati au majira mbalimbali katika mwaka. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama limejipanga vizuri kudhibiti vitendo mbalimbali vya uvunjaji wa sheria ikiwemo fujo au aina yejote ya ukosefu wa amani vinavyoweza kusababisha wananchi kushindwa kushiriki katika shughuli zao za kila siku, ikiwemo kushiriki katika michakato ya chaguzi mbalimbali zinazofanyika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia Jeshi la Polisi inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa askari wake wa ukakamavu, upelelezi na kuongeza vifaa vya kutenda kazi

ili kuwajengea uwezo na weledi mkubwa wa kuweza kuzuia na kukabiliana na vitendo kama hivyo vinavyojitokeza nyakati za uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; hivi sasa Manispaa ya Mtwara Mikindani kumekuwa na baadhi ya Viongozi wa vyama vyaa siasa wa wilaya na mkoa ambao wameweza kuratibu vikundi mbalimbali kwa ajili ya kufanya uhalifu kwenye uchaguzi unaotarajia kufanyika mwaka huu 2020. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je Serikali Mheshimiwa Waziri yuko tayari hivi sasa kuja Mtwara kuweza kuchukua ushahidi ambao nitampatia kwa mikono yangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Manispaa ya Mtwara Mikindani kuna baadhi ya viongozi wa vyama vyaa siasa wanachukua na kuwatumia baadhi ya askari polisi kwenda kuwafanya hujuma Wapinzani usiku saa nane, saa tisa na kuwagongea majumbani kwao na kuwakamata bila sababu yoyote ya msingi na kwenda kuwaweka ndani eti kwa sababu tu wanafanya kazi ya kunadi Chama cha Wananchi - CUF na vyama vingine vyaa Upinzani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari hivi sasa kuwachukulia hatua Askari wa aina hiyo wanaotumika kwa ajil ya Chama Tawala? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maftaha Nachuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ameuliza kama nipo tayari kwenda kuchukua ushahidil; nimuhakikishie kwamba niko tayari kufanya hivyo kama ushahidi huo ni kweli anao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ametoa tuhuma nzito kwa Jeshi letu la Polisi kwamba linashirikiana na vyama sijui chama gani. Mimi nimuhakikishie Mheshimiwa Maftaha na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba tunavyotambua na ilivyo kabisa, si tunavyotambua, na uhalisia ulivyo, Jeshi letu la Polisi kwa kiwango kikubwa wanajitahidi kufanya kazi zake kwa kufuata weledi, sheria na maadili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kuwa yeye Mheshimiwa Maftaha ambaye mimi ninamheshimu sana kama ni mionganii mwa viongozi wasio wengi sana makini wa upinzani anaweza kusema ana ushahidi wa jambo kama hilo wa tuhuma hizo nzito; imani yangu ni kwamba nitakapokuwa nimeambatana naye kama alivyoomba katika swali lake la msingi basi atatupatia ushahidi huo ili tuweze kuchukua hatua. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea swali la Mheshimiwa Zitto Ruyagwa Kabwe litaulizwa Mbunge wa Kigoma Mjini litaulizwa na Mheshimiwa Heche.

Na. 75

**Ukosefu wa Maafisa Uhamiaji Katika Balozi Zetu**

**MHE. JOHN W. HECHE (K.n.y MHE. KABWE Z. R. ZITTO)** aliuliza:-

Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanapata changamoto za huduma za uhamiaji kutokana na Balozi zetu takribani zote kutokuwa na Maafisa Uhamiaji.

Je, ni lini Serikali itapeleka Maafisa Uhamiaji kuhudumu kwenye Balozi zetu ili kutoa huduma bora kwa raia wa Tanzania kwenye nchi hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI,** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji inawajibika kuhakikisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanapata huduma bora za uhamiaji wanapofika kwenye Balozi zetu nje ya nchi. Maafisa Uhamiaji waliokuwa wanatoa huduma za uhamiaji katika Balozi zetu ama wamestaafu au wamemaliza muda wao wa kuhudumu katika Balozi walizokuwa na wamerejea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha huduma bora za uhamiaji zinaendelea kutolewa kwa raia wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi, tayari Serikali imewateua maafisa watano kutoka Idara ya uhamiaji ambao wamepatiwa mafunzo ya kuhudumu katika Balozi. Kwa sasa Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wako katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kuwapeleka Maafisa hao kwenda kuhudumu katika Balozi walizopangiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema Serikali imeteua maafisa watano; na tunajua kwa miaka mitano ya uongozi wa awamu hii maafisa wengi wamerejeshwa Tanzania na hivyo Balozi nyingi hazina maafisa kwa sababu ya hofu labda ambazo wanazijua ndani ya chama chenu. Sasa maafisa watano tu katika Balozi nyingi ambazo ziko kwenye nchi mbalimbali hamuoni kwamba mnawapatia Watanzania wanaoishi nje ya nchi matatizo ya kupata huduma ambayo ni ya kimsingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tarehe 31 mwezi wa kwanza mwaka huu Serikali ilisitisha matumizi ya passport za zamani; na tunajua Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanahitaji passport ambayo ndiyo inawapa uwezo wa kuishi huko wanakoishi na kufanya shughuli zao. Ni lini Serikali itahakikisha Watanzania wanaoishi huko wanapata huduma hii kwa haraka ili wasionekane kama wamekuwa-condemned kurudishwa huku kwa sababu hawana passport?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Heche kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuhakkishie kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina hofu, ni suala la utaratibu tu. Kwamba kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi, kwamba kwa kutambua upungufu huo wa Maafisa Uhamiaji ndiyo maana maafisa watano wako mbioni kupelekwa wakati wowote. Hata hivyo nataka nimhakkishie kwamba kutokuwa na Maafisa wa Uhamiaji katika kila Balozi hakumaanishi kwamba wananchi au wageni wanaotaka kupewa huduma hizo wanashindwa kupata; kwa sababu

kwanza hivi sasa hivi tuna Mfumo wa Uhamiaji Mtandao ambao nitauelezea kwa kifupi ili pamoja na mambo mengine utakuwa umeweza ku-cover lile swali lake la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Uhamiaji Mtandao ambao unahusisha uhamiaji kwa maana ya e-passport, e-visa, e-permit pamoja na e-gate umerahisisha sana kutoa huduma kwa wananchi kwani sasa haihitaji mwananchi kwenda moja kwa moja kwenye Ofisi zetu na badala yake anaweza kwenda kwenye mtandao tu na kujaza fomu zake na kuweza kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo maafisa ambao wapo katika Balozi zetu wameshapata *training* juu ya matumizi haya ya uhamiaji mtandao, na pale ambapo wananchi ama wageni wanapohitaji huduma hizo kwa maeneo ambayo hakuna Maafisa Uhamiaji basi Maafisa wa Mambo ya Nje waliopo katika Balozi zetu huwa wanatoa msaada kwa wale ambao wanahitaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelezo hayo kwa ufupi ni dhahiri kwamba uchache huo wa maafisa ambao ameuzungumzia Mheshimiwa Heche hauna madhara yoyote mpaka sasa hivi kwa huduma mbalimbali za raia na wageni ambao wanataka kuzipata katika Balozi zetu duniani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Kutokana na muda tunaendelea na Wizara ya Maji; Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti maalum sasa aulize swali lake.

Na. 76

#### **Hitaji la Visima Virefu vya Maji – Nkasi**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga visima virefu vya maji katika Wilaya ya Nkasi ili kutatua changamoto ya maji iliyopo?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maji majibu ya swali hilo.

Na. 76

#### **Hitaji la Visima Virefu vya Maji – Nkasi**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga visima virefu vya maji katika Wilaya ya Nkasi ili kutatua changamoto ya maji iliyopo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua tatizo la maji lililopo katika Wilaya ya Nkasi Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 imepanga kuchimba visima virefu 9 katika maeneo ya Masolo, Katogolo, Mpata, Miende, Itindi, Kacheche, Lyele, Mbwendi na Kakoma. Kiasi cha shilingi milioni 315 kimetengwa katika bajeti ya mwaka 2019/2020 kwa ajili

ya kazi hiyo. Hadi kufikia mwezi Disemba 2019, Visima 7 vimechimbwa katika vijiji vya Masolo, Katogolo, Mpata, Miende, Kanazi na Ipanda na kiasi cha shilingi milioni 220 kimetumika katika upimaji na uchimbaji wa visima hivyo ambavyo vitatumika kama vyanzo vya maji katika vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mrefu wa kutatua tatizo la maji katika Wilaya ya Nkasi, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imepanga kutumia zaidi ya bilioni 1.3 kwa kupitia Programu ya PforR kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Nkasi. Wizara imeshatuma fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji 6 Wilayani Nkasi ambapo miradi yote hiyo itatekelezwa kwa mfumo wa wataalam wa ndani (Force Account).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Nelsona Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Kiongozi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa kazi kubwa ya kuweza kumtua mama ndoo kichwani. Serikali hii imewaza kutuliza hata ndoa za wanawake wa Tanzania, wameweza kutulia kwa sababu maji yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza;

(i) Wilaya ya Nkasi ina takribani ya vijiji 35 wanaoishi pembezoni mwa Ziwa Tanganyika, na wanatumia maji ya ziwa Tanganyika ambayo yanawasababishia kupata magonjwa mbalimbali ikiwemo kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Sasa ni lini sasa Serikali itawajengea visima virefu ambavyo vitawasababisha wapate maji salama?

(ii) Wilaya ya Nkasi imegawanyika katika sehemu mbili, Nkasi Kusini na Nkasi Kaskazini. Naishuruku Serikali imeweza kujenga visima 9 ambavyo sasa hivi vinaendelea kujengwa, lakini bado Nkasi Kusini ambavyo havijajengwa visima takribani 7 ambavyo tuliomba kijiji cha Masolo, Kijiji cha Milindikwa, Malongwe, Sintali, Nkana na vijiji vingine bado havijachimbiwa visima.

Je, nili sasa Serikali itachimba visima hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amekuwa mpiganaji mkubwa hususan kwa kina mama wa Mkoa wake wa Rukwa. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji hatuta kuwa kikwazo kwa Mkoa wa Rukwa na Nkasi katika kuhakisisha wanapata maji. Ziara ya Mheshimiwa Waziri katika Jimbo la Nkasi kwa Mheshimiwa Kessy alilia sana pale Mheshimiwa Mbunge na tumetoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa katika mji wa Kilando pamoja na Namanyele zaidi ya milioni tano kwa ajili ya miradi ile mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepeata fedha za PforF zaidi ya bilioni nne kwa Mkoa wa Rukwa, tumepeleka bilioni 1.3 katika Wilaya ya Nkasi katika kuhakisisha tunakwenda kutatua tatizo la maji. Naomba Waheshimiwa Wabunge waende kusimamia miradi ile katika kuhakisisha wakinamama wanaendelea kutua na ndoo kichwani na ndoa zao zinaendelea kuimarika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana naamini majibu hayo yanaelekea kwenye mikakati ya Mikoa yote Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, sasa tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate Mbunge wa Tunduru Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 77

### Tatizo la Maji – Jimbo la Tunduru Kusini

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Jimbo la Tunduru Kusini lina changamoto ya maji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima virefu na vifupi katika kata ya Tuwemacho, Mchuluka, Mchoteka, Mbati, Marumba, Wenje, Nasomba, Namasakata na Lukumbule.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa maji naomba kujibu Swalii la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Jimbo la Tunduru Kusini lina jumla ya miradi mitano ya maji ya bomba kwenye vijiji 11. Miradi hiyo ipo kwenye Kata za Mbati, Nalasi, Namasakata, Misechela, Mtina, Ligoma, Mchesi na Lukumbule. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Maji *Help for Underserved Communities* imechimba visima 72 katika Kata za Tuwemacho, Marumba, Lukumbule Mbesa na Mtina. Visima hivyo vimefungwa pampu za mkono. Vilevile Wilaya ya Tunduru kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Maji *All Mother and Child Count* imechimba visima virefu katika kata za Mchuluka, Namasakata, Chiwana na Lukumbule. Visima hivyo vitatumika kujenga miradi ya maji ya bomba katika maeneo hayo. Tayari utekelezaji umeanza kwa kata ya Chiwana na Namasakata

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha huduma ya maji inakuwa ya uhakika katika Wilaya ya Tunduru, Serikali kuititia Wakala ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji ni imetenga na kutoa fedha katika bajeti ya mwaka 2019/2020 kiasi cha shilingi milioni 974 kwa ajili ya kujenga, kukarabati na kufanya upanuzi wa miradi ya maji katika vijiji mbalimbali vilivyopo wilaya hiyo vikiwemo vijiji vya Jimbo la Tunduru Kusini. Vijiji hivyo ni Mbesa, Airport, Nasomba, Namasakata, Chiwana, Semeni, Nalasi, Misechela, Angalia, Ligoma na Mchekeni. Aidha, Serikali imepanga kuchimba visima Virefu viwili katika vijiji vya Wenje na Likweso vilivyopo Jimbo la Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha kadri zinavyopatikana ili kuweza kujenga na kukarabati miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Jimbo la Tunduru Kusini ili wananchi wawzeze kunufaika na huduma ya majisafi na usafi wa mazingira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutembelea katika kijiji cha Mbesa aliahidi kisima kirefu amechimba, amekwenda kuangalia na sasa ameahidi kutoa milioni 200 kwa ajili ya kufanya ule mradi kukamilike vizuri. Vilevile tunawashukuru wafadhili wetu waliojenga visima 72 na wengine wamejenga visima 90 katika Jimbo la Tunduru Kusini. Na nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mradi wa Mbesa, mradi wa Lukumbuli ambao ulikamika miaka mitatu iliyopita na mradi wa wanalasa ambao ulikamilika zaidi miaka 9 iliyopita haufanyi kazi kutokana na tatizo la kutumia mafuta ya *diesel* ambayo wananchi wameshindwa kutumia.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufunga solar ili wananchi waweze kutumia kwa ukamilivu?

Kwa kuwa katika mradi wa Kijiji cha Mtina uliokamika mwaka moja uliopita umeshindwa kufanya kazi vizuri kutokana na panel solar zilizopo pale kutokutoshleza kusukuma maji kwa ajili ya kupeleka kwa wananchi.

Je, Serikali haioni haja yakuongeza solar panel katika mradi ule ili uweze kuhudumia wananchi wa Mtina ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kiukweli ni mionganini mwa Wabunge wanafanya kazi kubwa sana, na niseme hili ni baba lao kwa eneo la Tunduru Mungu akubariki sana. Lakini kikubwa ninachotaka kukisema watalamu wetu kwa maana ya WARUSA pamoja na wizara hawana kisingizio tena, utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha, tumeppata fedha kwa mikoa 17 zaidi ya bilioni 119. Hata katika Jimbo lako la Tunduru tumeshapeleka bilioni 1.3 hizi fedha ni kwa ajili ya kwenda kutatua changamoto za miradi ya maji. Ni mtake mhandishi wa maji wa Tunduru Kusini katika kuhakikisha anatumia changamoto hizi ili kukarabati na wananchi wako waweze kupata huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi sasa aulize swali lake.

Na. 78

#### Fidia kwa Wananchi Waliopisha Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma (Mara)

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fedha zao wananchi wa Musoma ambao maeneo yao yapo pembezoni mwa Uwanja wa Musoma na wameshafanyiwa tathmini ili kupisha upanuzi wa ujenzi wa uwanja huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** aliujibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma ambao uko katika hatua za awali za manunuzi ili kumpata Mkandarasi. Mchakato wa manunuzi unakwenda sambamba na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika na mradi huu wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahakikisha kwamba, wananchi wanaostahili kulipwa fidia wanalipwa kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi huu wa upanuzi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joyce Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba silizishwi na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Toka nimekuja katika Bunge hili nimeshazungumzia hili suala la uwanja wa ndege wa Mkoa wa Mara, mara kwa mara. Majibu ya Waziri ukizingatia Mkoa wa Mara una vivutio vingi sana vya utalii. Kwanza tuna mbuga, ya wanyama ya Serengeti, pia tuna kivutio cha Kumbukumbu ya Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni umuhimu wa kujenga uwanja ule au kuupanua uwanja ule ukawa uwanja ambao utaleta watalii wengi katika Mkoa wa Mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba comentiment ya Serikali. Je ni lini uwanja ule utakamilishwa?

**MWENYEKITI:** Umeshauliza mawili.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni moja.

**MWENYEKITI:** Mawili umeuliza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na malipo ya wananchi wale wananchi wanazunguka eneo lile na uwanja wa ndege zile nyumba zilishawekewa X muda mrefu sana. Takribani sasa hivi ni mwaka mmoja na nusu au miaka miwili. Wale wananchi wanaishi kwa wasiwasi hawajawahi kulipwa hata senti tano, mpaka imeshasababishia baadhi ya wananchi wameshakufa.

Je, serikali itawalipa lini wananchi wale ili waendelee kuwa na maisha yao bila wasiwasi kusema kwamba ni lini watalipwa. Kwa sababu wale wananchi hawakopesheki. Ahsante nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Joyce majibu mawili ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, ni kweli zoezi la kufanya ujezi wa uwanja huu tumekuwa tukiendelea nao kwa muda. Lakini Mheshimiwa Mbunge nikufahamishe kwamba hatua nzuri zimefanyika, kwa sababu pale awali wananchi ambao walikuwa imeonyesha watalipwa fidia walikuwa wapo wengi gharama ziliikuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuishukuru uongozi wa mkoa na mwandisi mkoa wa Mara. Kwamba kazi kubwa iliyofanyika kuendelea kutambua upya wananchi watakoahitajika kulipwa fidia na zoezi hili lilikamilishwa Mheshimiwa. Tumeokoa kama bilioni 10 hivi, hii ni kazi kubwa imefanyika.

Kwa hiyo, ninawapongeza sana lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge wananchi 135 watalipwa fidia kwa sababu tumeshawatambua baada ya kufanya mapitio wananchi hawa wanatoka katika Kata Nyasho, niwahakikishie wananchi 97 watalipwa, wananchi wa Kata ya Kamnyonge wananchi 38 watalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ime-indicate kwamba bilioni 4.319 zitalipwa kwa wananchi hawa. Kwa hiyo, wavute subra kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba ni lazima kwanza wananchi tuwalipe ili tuweze kupeleka huduma katika eneo hili.

Kama alivyosema mwenyewe anatambua record zinaonesha 95% ya matumizi ya uwanja ni wale watu wanaokuja kwa ajili ya utalii. Serikali inatambua hivyo na watalii wengi kutoka Kenya, kutoka Uganda wanatumia uwanja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua ndio maana Serikali imefanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba uwanja huu tunaupanua tunauweka ukae vizuri ili huduma iwe kubwa zaidi katika eneo hili. Kwa hiyo, tunakuomba uvute subra kazi nzuri Serikali ya Awamu ya Tano inafanya na uwanja huu tutakwenda kuujenga na utatumika kwa wananchi na watalii pia.

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 79

### **Barabara ya Likuyufusi - Mkenda**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu wa kilometra 124 inayounganisha Tanzania na Mozambique mpaka sasa bado haijajengwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini Serikali itapeleka pesa na kuanza ujenzi huo kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swalii hili namba 79.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS JOHN KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Likuyufusi – Mkenda yenye urefu wa kilometra 124 ni barabara muhimu kutokana na ukweli kwamba inaunganisha nchi mbili za Tanzania na Msumbiji na pia inahudumia wananchi wengine wa vijiji vya Mkenda/Mitomoni hadi Likuyufusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), ilifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii kwa kumtumia Mkandarasi Mshauri M/s Crown Tech. Consult (T) Ltd. wa Dar es Salaam ambaye alikamilisha kazi hiyo mwaka 2012. Baada ya kukamilika kwa usanifu huo, kulijitokeza ongezeko kubwa la matumizi katika barabara hiyo kutokana na kugundulika na kuanza kuchimbwa kwa makaa ya mawe katika eneo la Muhukuru pamoja na matarajio ya uwekezaji wa shamba la miwa na kiwanda cha sukari eneo la Nakawale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko hayo, Wizara yangu kupitia TANROADS inapitia upya usanifu wa awali ili kuzingatia mahitaji ya sasa. Kazi hiyo imeshaanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2020. Baada ya kukamilika kwa kazi hiyo, Serikali itajua gharama halisi za ujenzi na kuanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii katika suala la usanifu na upembuzi wakina sasa hivi limechukua miaka nane. Sasa swali langu ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu kiasi hiki kwa ajili ya kufanya tu usanifu na upembuzi wa kina?

(b) Barabara hii imebeba uzito mkubwa sana katika kuharakisha shughuli za kiuchumi ili tuweze kufikia uchumi wa kati itakapofika mwaka 2025. Lakini kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba upembuzi yakinifu unaendelea na usanifu mpaka inakapofika Juni, 2020 ninapata mashaka kwamba huenda hii barabara ikaendelea kuchelewa ziadi.

Je, Serikali haioni kwamba kutoleta maendeleo au kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo inapita katika kata zifuatazo zinazoendelea kujishughulikisha katika shughuli za uchumi ikiwa pamoja na makaa ya mawe yanayochimbwa huko? Lakini pia shamba kubwa la miwa linaloenda kuanzishwa huko. Na kata hizo ningependa nizitaje, ni kata ya Likuyufusi, Litapwasi, Ndogosi, Muhukulu lilayi na Muhukulu barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa serikali itakwenda kuanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu waziri majibu ya maswali haya ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu nitumie nafasi hii nishukuru kwa swali nzuri lakini niseme tu, eneo hili la Likuyufusi barabara hii ya Likuyufusi Mkenda ni barabara ambayo inagusa majimbo mawili; Jimbo la Peramiko kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, lakini pia inawahudumia kwa kiasi kikubwa wananchi wa jimbo la Nyasa. Ambapo kuna kazi kubwa imefanyika kwa sababu barabara hii ina wapunguzia adha wananchi wa kata hii ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa juhudini ambazo zinafanyika na kwa ushirikiano mkubwa kwa Mheshimiwa Jacqueline na Wabunge wa majimbo inayofanyika, barabara hii ipo katika ubora kwa kuzingatia mahitaji ambayo nimeyata. Tunatambua kwamba ili tuweze kujenga uchumi ni lazima miundombinu iwe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea na nimejionea namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge hawa akinamama, na niseme Wabunge wakinamama kazi nzuri wanafanya. Nimekwenda kule nimeona kule Mitomoni kuna MV Stella inasaidia wananchi wale kuvuka ili watumie barabara hii ambayo kwa kiasi kikubwa tumeiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga vizuri. Wakati harakati za kujenga barabara ya lami zinafanyika, tunazingatia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha barabara hii inakuwa bora. Yako maeneo ambayo tumeweka madaraja ya chuma, yako maeneo tumeelekeza ili wakati huu tunafanya harakati za kuhuisha kujua gharama halisi za ujenzi wa barabara za lami, barabara hii inakuwa bora na makaa ya mawe yanabebwa, hata mwekezaji anaendelea na harakati zake za uwekezaji wa kiwanda cha sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga vizuri, tutawa-support wananchi wa maeneo haya ya Peramiko, wananchi wa

Kata alizozitaja ili nao waende katika harakati; hatupendi tukifika uchumi wa kati wawe chini ya mstari ule wa wastani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tumejjipanga vizuri kwenda kuiboresha barabara hii. Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo; Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Manyanya, tumejjipanga vizuri, vuteni subira, muwe comfortable, tutaenda kujenga barabara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda Mkenda nimeona pia kuna soko zuri, nimeona wananchi wa kule Msumbiji wana mahitaji makubwa ya mahindi ambayo yanazalishwa upande wa Peramiko. Kwa hiyo, tunatambua umuhimu huo wa kufanya maboresho ili wananchi hawa wawewe kupata manufaa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo mazuri. Tunamalizia Wizara ya mwisho, Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia Mbunge wa Chemba sasa aulize swali lake.

Na. 80

### **Kodi kwa Makocha na Wachezaji wa Kigeni**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Je, Serikali imekusanya kiasi gani cha kodi kutoka kwa makocha na wachezaji wa kigeni wanaofanya kazi nchini katika mwaka wa fedha 2017/2018?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Suleimani Nkamia, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Kifungu cha 7; "kila mtu anayepata mapato yatokanayo na ajira ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawajibika kulipa kodi ya mapato kulingana na kipato chake."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, jumla ya shilingi milioni 1,733.6 zilikusanywa kama malipo ya kodi ya ajira kutoka kwa makocha na wachezaji wa kigeni wanaofanya kazi hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Suleiman Nkamia swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu, nina maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; malipo ya wachezaji na makocha wengi wa kigeni hapa Tanzania yanafanywa kiholela, hakuna mfumo rasmi:-

(a) Je, Serikali inatambuaje kwamba fulani kalipa na fulani hajalipa?

(b) Nchi zilizoendelea kama Uingereza, kodi ni jambo muhimu sana kwa wachezaji wa mpira wa miguu na hakuna kukwepa. Je, Serikali hapa Tanzania ina mkakati gani wa

kuhakikisha kwamba vilabu vya ligi daraja la Premier na ligi daraja la kwanza wanapopata ajira kwenye vilabu hivi wanalipa kodi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii lake la kwanza kujua nani kalipa na nani hajalipa kama nilivyosema, kulingana na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, kila mtu anayepata mapato ndani ya Taifa letu anastahili kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la mwajiri kwenda kutoa taarifa Mamlaka ya Mapato Tanzania ya waajiriwa wake alionao wanaotakiwa kulipa kodi hiyo. Kwa hiyo, niwatake tu timu zetu zote ambazo zinaajiri makocha na wachezaji kutoka nje ya nchi; kwenye mikataba yao, maana msingi wa kulipa kodi ya mapato na kodi ya ajira, kwanza kodi ya mapato ni lazima mlipaji yule awe ni mkazi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyofahamu, pia kwa kodi hii ya mapato, kila mgeni akifikisha zaidi ya miezi sita anahesabika ni *local resident* na anatakiwa alipe kodi hiyo na mwajiri wake, anatakiwa kutoa taarifa hiyo ili kodi hiyo iweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu kaka yangu kwamba waajiriwa wote wanatakiwa kulipa kodi hii kulingana na Sheria za Taifa letu zinavyoolekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii lake la pili kwamba wanalipa kiholela na wengine yawezekana wanalipwa fedha hizi mkononi; kama nilivyosema, ni jukumu la mwajiri kutoa taarifa ya nani analipwa nini ndani ya klabu yake ndani ya taasisi yake na ndani ya kampuni yake ili kodi zote zinazostahili kulipwa na hasa kodi ya mapato ambayo ni ngumu kulipika iweze kulipwa kama sheria zetu zinavyotakiwa kutekelezwa kwa vitendo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kukamilisha maswali majibu ya maswali yetu ya leo.

Sasa ni wakati wa matangazo. Naomba nitangaze wageni ambao wako Bungeni asubuhi hii. Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni Viongozi wa Asasi za Kiraia (Mazingira na Maendeleo) ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, Ndugu Ally Ngalema na Ndugu Abdallah Kawambwa. Karibuni sana wageni wetu. (Makofii)

Mgeni mwagine ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM Songea Mjini Ndugu Issa Kazumari, karibu sana Mwenyekiti wetu wa UVCCM Songea Mjini. (Makofii)

Wageni wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mbunge ambaye ni Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni Ndugu zake kutoka Pangani Mkoa wa Tanga, wakiongozwa na Ndugu Amina Hamis. Karibuni sana ndugu zetu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso kutoka Tanga.

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Mbunge na Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu

Florence King'uzza. Karibu sana ndugu yetu kutoka Dar es Salaam. (Makofii)

Wengine ni wageni 11 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge amba ni Wanakwaya Ebenezer kutoka Iringa Road Dodoma wakiongozwa na David Ngunji. Karibuni sana katika Bunge letu. (Makofii)

Wageni wengine ni wageni 50 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge amba ni Wanamaombi kutoka Mkao wa Dodoma. Karibuni sana katika Bunge letu. (Makofii)

Wengine ni wageni sita wa Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mbunge amba ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Loyce Lobozi. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. (Makofii)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab amba ni jamaa zake kutoka Netherland na Tanzania, Ndugu Paul Diruch na Ndugu Edward Lukaka. Karibuni sana katika Bunge letu. (Makofii)

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Josephine Gezabuke, Mbunge amba ni Viongozi wa UWT na wadogo zake kutoka Kasulu Mkao wa Kigoma, Ndugu Grace Mbwiliza, Ndugu Josephine Ntauheza na Ndugu Stella Japhet. Karibuni sana ndugu zetu. (Makofii)

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge ambaye ni Mtaalam wa Mifugo kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Deogratias Sosthenes. Karibu sana. (Makofii)

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa Mbunge ambaye ni Mkurugenzi wa Shule ya Awali na Msingi Orimb Engeneba kutoka Longido Mkao wa Arusha, Mchungaji Joseph Lemoya. Karibu sana mgeni wetu. (Makofii)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jitu Soni, Mbunge, ambaye ni ndugu yake kutoka Babati Mkao wa Manyara, Ndugu Akshei Odedra, karibu sana na ndugu yetu. (Makofii)

Wageni wengine ni walioko Bungeni kwa ajili ya mafunzo; kuna wanafunzi 70 na walimu wanne kutoka *Dar es Salaam Independent School (DIS)* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi wetu, mmepependeza kwa kweli, karibuni sana katika Bunge letu kwa ajili ya mafunzo pamoja na walimu wenu. Karibuni sana. (Makofii)

Katibu, tuendeleee.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE NA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA;**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA  
NA SHERIA;**

**NA**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
SHERIA NDOGO**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hakuna miongozo leo kutokana na kazi tuliyonazo mezani. Tunaendelea na Hoja za Kamati, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

**MBUNGE FULANI:** Una sura kama Bikira Maria, lakini roho!

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti unavunja kanuni.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba make. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Rweikiza karibu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utumie dakika zisizozidi 20 na Kamati zote zitazofuata zitatumia dakika hizo hizo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Spika tafadhali.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Chief Whip amesimama.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa 117 fasili ya 15 ya kanuni za Bunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chief Whip wa Kambi ya Upinzani, naomba ukae, utapata nafasi baadaye kuhusu mwongozo wako. Mwenyekiti naomba tuendelee.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuzingatie kanuni ya 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ziara za Ulagazi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; miradi ya i l i y o t e m b e l e w a      inaonekana      k a t i k a u k u r a s a      w a      p i l l i      w a      t a a r i f a h i i ;      p i l l i ,      uchambuzi wa Taarifa z a      Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais; tatu, kushiriki katika Semina za Ndani; nne, ziara za Ulagazi wa Miradi ya Ofisi ya Rais; na tano, Uchambuzi wa Muswada wa Sheria;

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi na Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati.

(a) Mradi wa Miji Mikakati ya Tanzania PSCP

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Majiji matano na Halmashauri za Manispaa tatu za Mtware Mikindani, Kigoma Ujiji na Illemela Mwanza na utagharimu jumla ya dola za Kimarekani 355.7. Halmashauri ya Jiji la Dodoma imepata jumla ya shilingi bilioni 178.44 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami kilomita 26.7,

stendi ya mabasi ya kisasa, soko la kisasa la Job Ndugai eneo la mapumziko (*Recreational Park*) la Chinangali, Kituo cha Maegesho ya Malori Nala na uwekaji wa taa za barabarani 625 zinazotumia umeme wa jua (*solar street lights*) ambapo ujenzi umefikia 82%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza Serikali kwa kutumia TSP kuboresha Jiji la Dodoma na inashauri miradi hiyo kusimamiwa na kuendeshwa kisasa kwa kupata wataalamu wenye sifa ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

Aidha nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa heshima aliyopewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ya soko jipya la Dodoma kuitwa jina lake. Hii ni heshima kubwa ambayo itafanya mchango wake katika Bunge hili la Tanzania la Mkoa wa Dodoma ikumbukwe katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TASAF imekuwa ikizingatia matumizi ya mfumo wa kiteknolojia wa habari ya mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli zake. Mifumo hiyo imekuwa ikiboreshwa katika awamu mbalimbali ili iweze kuongea na mifumo mingine ya Kitaifa. Miongoni mwa mifumo hiyo ni mfumo wa malipo kwa walengwa E'Payment System ambapo hutumika kuchakata malipo ya walengwa kwa kuandaa orodha ya malipo kwa ngazi zote hizi zinazohusika na mwakilishi wa kaya. Kupitia mfumo huu malipo kaya hutumwa moja kwa moja kwenye akaunti aidha ya simu au benki kwa mwakilishi wa kaya. Uzoefu umeonyesha kwamba 65% ya wanaolipwa hutumia mitandao ya simu na 5% ndiyo hutumia akaunti za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua hii na inashauri Serikali kuhakikisha mfumo unasambazwa na kutumika katika maeneo yote ya nchi kwa walengwa wa mpango kwani una ufanisi na uwazi wa kutosha. Malipo hufika kwa wakati na moja kwa moja kwa walengwa na hivyo kuokoa muda. Aidha, changamoto ya usajili wa laini za simu iondolewa ili kutokwamisha mfumo huu kutumika kwa walengwa wa ruzuku kwa kaya masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ichangie kikamilifu theluthi moja kwa mujibu wa makubaliano na wadau wengine wa mpango huu. Katika kipindi hiki cha miaka sita na nusu ya bajeti kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2019/2020 Serikali ilichangia shilingi bilioni 8.11 tu katika ya shilingi bilioni 70.01 zilizoidhinishwa Bunge hili. Kiasi hicho ni sawa na 11.58% tu na ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa DART unatekelezwa kwa awamu sita na utahusisha barabara zenye urefu wa kilomita 146. Awamu ya kwanza ilikamilika na kuanza kutoa huduma Mei, 2016 kwa kutumia Mto Huduma wa Mpito "interim service provider" ambaye amekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uchache wa mabasi kwani aliiingiza mabasi 140 kati ya 305 yaliyohitajika na kukosa mfumo wa uhakika wa tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua kadhaa ili kukabili changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuanza mchakato wa kumpata Mto Huduma Kamili ifikapo Julai mwaka huu. Hatua hiyo itasaidia kuongeza mabasi na kuboresha huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, wataalam wa DART, TAMISEMI na eGA wanashirikiana kutengenezamfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kukusanya mapato ambao utakamilika Machi, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza juhudhi hizo za Serikali na inaishauri Serikali kuhakikisha DART inapatia sheria mahususi, kwani kukosekana kwa sheria kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Masoko Kariakoo linakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na upungufu katika Sheria ya Shirika ambao unaathiri utendaji na uendeshaji, uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo kutokana na umri mkubwa, miaka 40 na zio la magari yanayoleta mazao katika Soko la Kariakoo kutokana na Sheria Ndogo za Manispaa ya Ilala na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri changamoto hizi zifanyiwe kazi ili kuwezesha shirika hili kuijendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kupata sheria bora ambayo itawezesha shirika kupeleka vitega uchumi zaidi na hivyo kuongeza wigo wa mapato. Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati umeelezwa katika ukurasa wa 5 - 46 katika taarifa hi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa:-

(1) Kiasi cha fedha kinachotengwa kwa TARURA ni kidogo sana ikilinganishwa na mtandao wa barabara inazohudumia kilomita 108,000;

(2) Mgao wa fedha kwa 30% ambapo TARURA inapata kutoka Mfuko wa Barabara (Road Fund) ni mdogo sana. inatakiwa uongezwe;

(3) Upungufu wa watumishi, uhaba wa ofisi na vitendea kazi unaathiri utendaji wa TARURA;

(4) Ukosefu wa sheria ndogo ndogo kwa lengo la kulinda na kuzuia uharibifu wa barabara zinazosimamiwa na TARURA unachangia matumizi ya barabara yasiyo sahihi;

(5) Matumizi ya *force account* katika ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini yanapunguza ghamama na hivyo kuokoa fedha nyingi. Hata hivyo, ukarabati huo usiposimamiwa na wataalam wahandisi wenge uwezo, unaweza kutekelezwa chini ya kiwango;

(6) Utamaduni wa kukarabati majengo na miundombinu ya Shule za Sekondari na Taasisi nyingine za Serikali, utawezesha majengo hayo na miundombinu mingine kudumu kwa muda mrefu;

(7) Miradi ya soko la kisasa stendi kuu ya mabasi, kituo cha mapumziko na kituo cha maegesho ya malori, inayotekelawa kupitia mipango miji ya kimkakati (PSP) italeta tija na thamani halisi ya fedha (*value for money*) iwapo itasimamiwa vizuri na kuendeshwa kitaalamu;

(8) Kupatikana kwa Mto Huduma Kamili (Service Provider) ambaye atakuwa na idadi ya mabasi ya kutosha kutasaidia kuboresha huduma ya usafiri kwa jiji la Dar es Salaam kupitia DART;

(9) Kukosekana kwa Sheria mahususi ya DART kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wakala huo. Aidha, Wakala umekosa kanuni za kusimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya miundombinu;

(10) Serikali itengeneze barabara ya Ihumwa – Hombolo (km 27) kwa kiwango cha lami ili kupunguza uharibifu wa vyombo vya usafiri unaosababishwa na ubovu wa barabara hiyo;

(11) Serikali iwezeshe chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kujenga uzo ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya chuo kutoka kwa wananchi wanaoishi jirani, na kuimarisha hali ya usalama;

(12) Sheria ya Shirika la Masoko Kariakoo ni ya siku nyingi, ikifanyiwa marekebisho itasaidia kuondoa upungufu uliopo ambao unakwamisha shirika hilo kutekeleza majukumu yakena kujiedesha kwa tija; na,

(13) Hatua ya Serikali kununua mashine za kukusanya mapato za kielektroniki (POS) 7227 na kuzigawa kwa halmashauri zote nchini kutasaidia kuimarisha ukusanyaji na udhibiti wa mapato.

**(b) Mheshimiwa Mwenyekiti,**

i. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hatua ya Serikali kuanzisha Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya (*District Revolving Fund*) kwa lengo la kusaidia halmashauri kutekeleza urasimishaji itafanikiwa iwapo fedha za kutosha zitatorewa na kusimamiwa vizuri.

ii. Hatua ya Halmashauri za wilaya chache (28) kumiiliki ajenda ya urasimishaji inayotekelizwa na MKURABITA inaonesha ni jinsi gani viongozi wa halmashauri nyingi nchini hawajaelewa vya kutosha umuhimu wa MKURABITA na hawana utashi wa kutekeleza mpango huo katika maeneo yao.

iii. Bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) inaathiri jitihada za kuongeza wigo ili kufikia maeneo mengi zaidi nchini.

iv. Hatua ya Taasisi ya Uongozi kushirikiana na viongozi wastaifu wa Kitaifa kuandika na kuchapisha vitabu vya wasifu (*autobiography*) wao ni jambo la kupongezwa kwani litasaidia kuhamasisha viongozi wengine kujitekeza na kuandika vitabu. Aidha, utaratibu huo utasaidia kuweka kumbukumbu za viongozi hao kwa vizazi vijavyo.

v. Iwapo mfumo wa malipo wa kielektroniki (e-payment system) utatumiwa kikamilifu na TASAF kufanya malipo ya ruzuku kwa kaya maskini, utaongeza tija kutokana na uwazi na kuchukua muda mfupi.

vi. Hatua ya Serikali kutochangia kikamilifu k a t i k a m p a n g o wa kunusuru kaya maskini kunafanya mpango kutegemea zaidi fedha za wahisani;

vii. TASAF itafikia asilimia 30 ya viji, mitaa na shehia ambazo hazijafikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini, itaondoa malalamiko kutoka kwa wananchi wa maeneo hayo.

viii. Hatua ya Serikali kuhamishia i l i y o k u w a Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) ilenge kuboresha na kusambaza huduma za mafunzo kwa njia ya mtandao badala ya kuzihafisha.

ix. Serikali iimarishe suala la usalama wa Serikali Mtandao ili kuzuia au kudhibiti uvamizi wowote unaoweza kukwamisha shughuli za Serikali zinazotekelizwa kwa njia ya mtandao; na,

x. Serikali iiwezeshe kifedha na kiutaalam Mamlaka ya Serikali Mtandao ili iende sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo; kwa kuwa TARURA inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi wa ofisi na vitendea kazi vingine; Kamati inalishauri Bunge lako tuku kuitaka Serikali Kutenga bajeti ya kutosha na kutoa fedha kikamilifu ili kuiwezesha TARURA kutimiza majukumu yake kikamilifu ya kuhudumia mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inaousimamia nchini. Mionganoni mwa njia za kuongeza fedha kwa TARURA ni kuongeza mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara (RF) kutoka asilimia 30 ya sasa hadi asilimia 50. Aidha, Kamati iliyopewa jukumu la kupendekeza kuhusu jambo hilo ni vyema ikalikamilisha haraka ili kuruhusu utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe Nchini na Matumizi ya Force Account

KWA KUWA; matumizi ya force account katika ukarabati konwe nchini yameonesha mafanikio makubwa kwa kupunguza gharama na hivyo kuokoa fedha nyingi; Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha taasisi za umma zinatumia utaratibu wa force account katika utekelezaji wa miradi ili kuokoa fedha za Serikali na kuzielekeza katika matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utamaduni wa Kufanya Ukarabati wa Mara kwa Mara. Kwa kuwa ubovu na uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo ya shule kongwe za sekondari za Serikali vimesababishwa na kukosekana kwa utamaduni wa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara. Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali na taasisi zake kujenga utamaduni wa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara katika miundombinu na majengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania. Kwa kuwa miradi ya m i j i y a k i m k a k a t i T a n z a n i a , vitega uchumi vyta Soko la Kisasa, Stendi Kuu ya Mabasi, Kituo cha Mapumziko na Kituo cha Maegesho ya Malori (Nala), inayotekelzewa kupitia Mpango wa Miji ya Kimkakati (TSCP) katika Jiji la Dodoma imegharimu fedha nyingi ambazo ni mkopo. Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa uongozi wa Jiji la Dodoma unaendesha vitega uchumi hivyo kwa ufanisi na faida kwa kuajiri na kuruhusu mtaalam mshauri atekelze majukumu yake ya kitaalam kwa mujibu wa makubaliano bila kuingiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam. Kwa kuwa tangu Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam ulipoanza kutoa huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam Mei, 2016 umekuwa ukitumia mtoe huduma wa mpito Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali iharakishe mchakato wa kupatikana kwa mtoe huduma kamili (service provider) ambaye atakuwa na idadi ya mabasi inayohitajika ili aweze kuboresha huduma ya usafiri katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kukosekana kwa Sheria Mahususi ya DART. Kwa kuwa Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) hauna sheria mahususi ya kusimamia utendaji wa majukumu yake; Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuiwezesha DART kupata sheria mahususi ili kusaidia kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo; Ubovu wa barabara ya Ihumwa – Hombolo. Kwa kuwa barabara ya Ihumwa – Hombolo (kilomita 27) ni mbovu sana; Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kupunguza uhari bifu wa vyombo vya usafiri kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kukosekana kwa Uzio Kuzunguka eneo la chuo. Kwa kuwa, hakuna uzio kuzunguka enel la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Kamati inalishauri Bunge kuitaka Seriki kaa kikiwezesha chuo hicho kujenga uzio kuzunguka maeneo yake ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu katika Sheria ya Shirika la Masoko Kariakoo. Kwa kuwa Sheria ya Shirika la Masoko ya Kariakoo ya mudaa mrefu, zaidi miiaka 40, na hiyo kuuwa na mapungufu mengi; Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuanza mchakato wa kuwasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya sheria hiyo ili kuliwezesha Shirika la Kariakoo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Kwa kuwa Serikali imeanzisha Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya kwa lengo la kusaidia halmashauri kutekeleza majukumu yake; Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali ihakikisha inatenga na kutoa fedha za kutosha za dhamana ili kuwezesha Halmashauri nyingi kukopa katika mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho. Ninapohitisha taarifa hii nikumbushe kidogo kuhusu dhana ya ugatuvi wa madaraka na upelekaji wa madaraka kwa wananchi (Devolution by Decentralization) ambayo msingi wake ni Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Leo sote tu mashahidi kwamba wananchi kwa kushirikiana na Serikali wanavyoshiriki katika shughuli za maendeleo kama ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, shule za msingi na sekondari, miradi ya maji, n.k kwa kuchangia nguvu zao na fedha. Ni kutokana na manthiki hiyo Kamati inashauri Serikali kuendelea kuunga mkono juhudhi za wananchi kwa kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka katika halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheeshimiwa George Huruma Mkuchika, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Selement Said Jafo (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb) na Naibu Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, nawashukuru watendaji wote wa ofisi ya Bunge kwa ushirikiano waliotupatia katika kamati hii. Kwa namna ya pekee nawashukuru sana kwa moyo wa dhati wajumbe wa Kamati hii ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wao walionipatia katika kipindi cha mwaka mmoja tunaombalizia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai na watumishi walioko chini yake kwa msaada waliotupatika katika kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. JACKLINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA  
MITAA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.1 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Taarifa hii inaelezea shughuli mbalimbali zilizotekelawa na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ikitimiza majukumu ya kikanuni ya kuvisimamia na kuishauri Serikali.

**1.2 Majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inasimamia shughuli za Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Kanuni, 2016 kinaeleza kuwa majukumu ya Kamati hii yatakuwa: -

- a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais;
- c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

**1.3 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

- a) Vikao na Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais ili kufahamu Muundo na Majukumu na shughuli zinazotekelawa;
- b) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kiutendaji kutoka Ofisi ya Rais;
- c) Ugaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo

Ia Januari, 2016; na

d) Mafunzo na Semina za kuwajenglea uwezo (capacity building) Wajumbe wa Kamati.

Lengo la kutumia mbinu hizo tofauti ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujelimisha kwa kina kuhusu nyanja ambazo wamepewajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

#### **1.4 Shughuli zilizotekeliza na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia ipasavyo masharti ya kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

##### **1.3.1 Ziara za Ulagazi wa Miradi ya Maendeleo 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilifanya ziara za ukagazi Miradi ya Maendeleo inayotekeliza na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Miradi iliyohusika ni ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 na inatekeleza katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kama ifuatavyo: -

###### **i) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

- Miradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP);
- Wakala wa Barabara za Mijini na Vijiji (TARURA); na
- Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Vijana Wenye Ulemavu (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri)

###### **ii) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala**

- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); na
- Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).

##### **1.3.2 Kuchambua Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, katika kutekeleza jukumu la kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwamwaka wa fedha 2018/2019.

Uchambuzi huo ulilenga kuiwawezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

### 1.3.3 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, ili kutekeleza jukumu la kikanuni ambalo chimbuko lake ni katiba [[libara ya 63 (2)]], la kuismamia na kuishauri Serikali. Hoja mbalimbali zilibiliwa kutokana na mijadala ya taarifa hizo na ufanuzi wake unapatikana katika sehemu ya pilii ya taarifa hii.

### 1.3.4 Kushiriki katika Semina za Ndani

**Mheshimiwa Spika**, Wajumbe wa Kamati ya Utawala walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali zilizoandalisha na Ofisi ya Bunge (Legislative Support Programme), Wizara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais (TASAF, Uongozi Institute, Wakala wa Serikali Mtandao - eGA) pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Kamati. Miongoni mwa taasisi hizo ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto - UNICEF, Wadau wa Kituo cha Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa - CDC kutoka Chuo Kikuu cha Maryland Baltimore cha nchini Marekani. Lengo la Semina hizo ilikuwa kuwaongeza uelewa Wajumbe wa Kamati katika nyanja mbalimbali pamoja na kuwakumbusha kuhusu wajibu na majukumu ya Kibunge ambayo wanayatekeleza katika kuismamia na kuishauri Serikali.

### 1.3.5 Ziara za Ukaguzi wa Shughuli za Ofisi ya Rais

**Mhehimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua shughuli mbalimbali zinazotekeliza na Ofisi ya Rais, kuitia Taasisi na Idara zake. Msingi wa ziara hizi ni kuwapa Wajumbe wa Kamati fursa ya kujiridhisha kuhusiana na utekelezaji ulifanyika katika maeneo mbalimbali ambayo Taarifa zake ziliwasilishwa na Serikali kwenye Kamati kabla ya ziara hizo.

### 1.3.6 Uchambuzi wa Muswada wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipewa jukumu la kuchambua Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019 (The e-Government Authority Act, 2019) ambao ulilenga kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.

## SEHEMU YA PILI

### 2.1 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI 2.2 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya taarifa inaelezea kwa ufasaha majukumu yaliyotekeliza na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika kwa kuanisha Wizara, Taasisi na Idara iliyohusika na kuonesha mafanikio na changamoto. Aidha, ili kufafanua zaidi na kuongeza uelewa katika baadhi ya maeneo ya uchambuzi wa matokeo, sehemu hii itatumia takwimu na **vielelezo/michoro**.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 Kamati iilikutana na kutembelea Ofisi ya Rais kama ifuatavyo:

#### 2.2.1 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

- a) Mikoa Ishirini na Sita (26) ya Tanzania Bara;
- b) Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA);

- c) Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART);
- d) Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) – Hombolo;
- e) Shirika la Masoko Kariakoo (KMC); na
- f) Shirika la Elimu Kibaha (KEC).

#### 2.2.2 **Ofisi ya Rais, Menejimet ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

- a) Wakala wa Serikali Mtandao (eGA)
- b) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
- c) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC);
- d) Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TaGLA);
- e) Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- f) Wakala wa Ndege za Serikali; na
- g) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayochambuliwa katika sehemu hii kuhusu Wizara, Taasisi na Idara zilizoanishwa hapo juu yamegawanyika kama maeneo yafuatavyo: -

- a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- b) Uchambuzi wa Bajeti;
- c) Taarifa za Utekelezaji;
- d) Ziara za ukaguzi wa shughuli za kiutendaji; na
- e) Uchambuzi wa Miswada.

#### 2.3 **Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati**

##### 2.2.1 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, jukumu hili hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati ilitembelea na kukagua miradi iliyotengewa na kuidhinishiwa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo inatekelezwa na Ofisi ya Rais, katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Ukaguzi huo ulilenga kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujiridhisha iwapo utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na thamani halisi ya fedha "value for money" iliyotolewa. Aidha, Wajumbe wangeongeza ulewa na hivyo kuishauri vyema Serikali wakati wa uchambuzi wa bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata. Ifuatayo ni baadhi ya miradi iliyokaguliwa na Kamati: -

##### a) **Mpango wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kuitia Kifungu 1009 "Infrastructure Development Division" chini ya Fungu 56 – Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mradi huu unagharamiwa na mkopo kutoka Benki ya Dunia na ruzuku kutoka Serikali ya Denmark tangu mwaka wa fedha 2010/2011 na utaendelea hadi mwaka 2020/2021 kwa thamani ya **Dola za Marekani millioni 355.7**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Manispaa ya Mtwara Mikindani ambako unaotekeliza chini ya Kifungu 8091, Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara.

Mradi unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya huduma za miji na uimarishaji wa mifumo ya Halmashauri katika kutoa huduma bora kwa jamii. Barabara zenye urefu wa kilomita 15.78 zimejengwa kwa kiwango cha lami kwa jumla ya **shilingi bilioni 24.01**. Barabara hizo ni Bandari (kilomita 2.75), Zambia (kilomita 3.75), Mikindani (kilomita 1.9), Chuno (kilomita 5.78) na Kunambi (kilomita 1.6).

Aidha, ujenzi wa dampo la kisasa na vizimba 25 vya kukusanya taka, pamoja na ununuzi wa mitambo na vifaa vya kusafirishia taka kutoka kwenye vizimba hadi dampo viligharimu jumla ya **shilingi bilioni 4.96**.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufanisi katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miradi hiyo, Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipata nyongeza ya **shilingi bilioni 8.8** ili kujenga mifereji ya maji yenye urefu wa kilimita 7.4 maegesho ya magari katika dampo, mizani ya kupimia taka na uwekaji wa taa za nishati ya juu katika barabara ya Chuno.

Aidha, **shilingi bilioni 21.68** zitatumika kujenga barabara (kilomita 4.1), mfereje wa kupeleka maji baharini (kilomita 3.4), kuboresha maeneo ya wazi, maduka makubwa, stendi ya daladala ya Mikindani, ujenzi wa soko la kisasa la Chuno, kazi zitakazotekeliza na Mkandarasi M/s Jiangxi Geo Engineering Group kutoka China.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania umekuwa na faida nyingi ikiwa ni pamoja na; kuongeza kilomita 18.8 za mtandao wa barabara za lami, kukuza uchumi kwani taa za barabarani zimevezesha wananchi kufanya biashara nyakati za usiku; kuboresha usafi wa mji kwa kuzoa taka na kuzeleka dampo la kisasa na hivyo kusaidia kudhibiti magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu na mengineyo.

Licha ya mafanikio yaliyoshuhudiwa na kamati, zipo changamoto kadhaa ambazo zinaweza kuzorotesha utekelezaji wa mpango huu. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa stendi ya daladala ya Mikindani kutokana na kutokamilika kwa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliohama ili kupisha mradi, na kasi ndogo ya ujenzi wa barabara kutokana na msimu wa mvua.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inakamilisha zoezi la fidia kwa haraka ili wananchi wanaohusika waweze kupisha ujenzi uendelee kwa haraka.

#### b). Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA)

**Mheshimiwa Spika**, wakala huu ambao ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 ulianza kutelezea majukumu yake mwaka 2017 na unahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 108,946 nchi nzima. TARURA inafanya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijijini na mijini pamoja na madaraja ili kuwezesha barabara kupitika muda wote.

Inatarajiwa kuwa utendaji wa TARURA utachangia kuina shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kuboresha barabara katika maeneo muhimu ya viwanda, machimbo ya madini na kilimo.

Ili kujidisha na utekelezaji wa shughuli za TARURA Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Mkoani Lindi ambapo Wakala inahudumia barabara zenyet urefu wa kilomita 693.1. Kamati ilikagua barabara ya Nyengendi (1 km) inayojengwa kwa kiwango cha lami ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyengendi - Mnara-Rutamba yenyet urefu wa kilomita 48, na kipande cha Nyangao kituo cha Mabasi - Nyangao Hospital (0.8 km) ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyangao - Namupa- Mihima yenyet urefu wa kilomita 23.2

Ujenzi wa barabara hizo unatekelezwa na Nyumbani Construction Company Ltd kwa gharama ya **shilingi milioni 531.93** na umefikia wastani wa asilimia 38.5. Kukamilika kwa kipande cha barabara ya Nyengendi - Mnara - Rutamba kutarafisha huduma za usafiri kutoka barabara kuu ya Lindi - Mtwara kwenda eneo la Rondo ambako kuna Msitu wa Hifadhi ya Taifa na hivyo kuchochea shughuli za utali.

Aidha, kukamilika kwa kipande cha Nyangao kituo cha Mabasi - Nyangao Hospitali kutarafisha usafiri kwa wakazi wa kata ya Nyangao na Namupa, kutoka barabara kuu ya Lindi - Masasi kwenda Hospitali teule ya wilaya (Nyangao - DDH) kupata huduma za matibabu

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa shughuli za TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi umesaidia kuboresha huduma ya usafiri kwa wananchi kutoka barabara kuu ya Lindi - Masasi kwenda katika Hospitali Teule ya Wilaya (Nyangao DDH). Aidha, kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami kutaongeza thamani ya ardhi katika kata sita ambazo maeneo yake yako jirani na barabara hizo.

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ya matengenezo ya barabara ikinganishwa na mahitaji halisi, ukosefu wa usafiri wa uhakika wa kuwezesha kuafuafilia na kusimamia ujenzi wa barabara na upungufu wa Wataalam wa ujenzi (wahandisi).

Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya TARURA na kuajiri Wataalam wa ujenzi wanaohitajika katika Halmashauri ya Lindi ili kuwezesha utekelezaji na usimamizi thabiti wa miradi ya miundombinu ya barabara inayotekelizwa na TARURA).

**(c) Mradi Na.4946 – Local Government Authority Own Source Projects ‘Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu’**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ultengewa jumla ya **shilingi bilioni 3.01** na kutekelezwa chini ya Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara. Kupitia mradi huu Wanawake, Vijana na wenyewe Ulemavu huwezesha kiuchumi kwa kupatiwa mafunzo na mitaji kutokana na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nichini. Hadi Desemba, 2018 jumla ya Vikundi 1,213 kutoka makundi hayo, vilikuwa vimenufaika na kiasi hicho cha fedha kilichotengwa. Kamati ilitembelea Vikundi vitatu ambavyo ni kikundi cha Wanawake cha Tunalekane; kikundi cha Vijana cha Tuvamo na kikundi cha wenyewe Ulemavu cha Waajibu.

**i. Kikundi cha Wanawake cha Tunalekane (Tunalekane Women Group)**

**Mheshimiwa Spika**, kikundi hiki chenye wanachama watano (5) kilanzishwa mwaka 2012 na kinajishughulisha na kutoa mafunzo ya utengenezaji wa sabuni za maji

na vipande, mafuta ya mgando na batiki kwa wajasiriamali wengine. Aidha, kinafuga kuku, kupika vyakula kwenye sherehe na kuza vifaa vya utengenezaji wa sabuni na batiki.

Tangu kuanzishwa kikundi hiki kimeishapata mikopo yenyе thamani ya **shilingi milioni 12** kwa awamu tatu na kupokea mafunzo ya ujasiriamali kutoka Manispaa ya Mtwara Mikindani, ambavyo vimewezesha wanakundi kujkwamua kiuchumi wao pamoja na familia zao. Aidha, kikundi kimeweza kutoa mafunzo kwa wajasiriamali zaidi ya 670 katika mikoa ya Mbeya na Mtwara.

Kupitia kipato wanachopata, wanakundi hao wamemudu kusomesha watoto, kupata mahitaji ya nyumbani na pia mtaji kwa kila mwanachama ili kuendesha shughuli za kiuchumi nje ya kikundi. Kikundi cha Vijana cha Tuvamo (Tuvamo Group)

**Mheshimiwa Spika**, kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2016 na vijana watano (5) wa kiume walioamua kuanzisha shughuli ya kutengeneza na kuza samani, kukarabati majengo (upauaji, kufunga jipsum) na kukopeshana fedha kwa hiyari.

Kikundi kilianza kwa mtaji wa **shilingi milioni 2** na hadi Kamati inafanya ziara mtaji ulikuwa umefikia **shilingi milioni 14** baada ya kupata mkopo mwaka 2018 kupitia Mfuko wa kuwezesha kiuchumi, Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu.

Kupitia miradi hii kikundi kimeweza kutoa ajira kwa vijana wanne (4) amba ni mafundi; kuongeza uzalishaji wa samani na hivyo kukuza kipato cha kila mwanakundi sambamba na kuchangia mapato ya Serikali kwa kulipa kodi.

#### **ii. Kikundi cha Watu wenyе Ulemavu cha Wajibu (Wajibu Disabled Group)**

**Mheshimiwa Spika**, kikundi hiki ambacho kinaundwa na watu wenyе ulemavu watano (5) wanaume watatu na wanawake wawili, kilianzishwa mwaka 2018 ili kujishughulisha na uchomeleaji (welding), ushonaji (tailoring) na biashara ndogondogo sokoni.

Kikundi kilianza shughuli zake na mtaji wa **shilingi milioni 4.7** uliotokana na mkopo usio na riba kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani. Kamati ili potembelea kikundi hicho tayari kilikuwa kimerejesha asilimia 12 ya mkopo huo na kimejipanga kurejesha fedha yote ndani ya wakati uliopangwa.

Shughuli za kikundi zimevezesha wanachama wake kujimudu kiuchumi kwa kupata mahitaji muhimu ya chakula, matibabu, mavazi na kusaidia kuondoa hali ya unyanyapaa kwa wanachama kutokana na Ulemavu walio nao.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia ukaguzi wa mradi huu katika Manispaa ya Mtwara Mikindani Kamati ilibaini mafanikio na changamoto kadhaa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ajira kwa Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu amba ni wanachama wa vikundi vilivyotembelewa, na ongezeko la mapato ya manispaa kutokana na ulipaji wa kodi stahiki.

Aidha, kumekuwa changamoto za kukosa soko la uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa na vikundi kama vile samani, na batiki, na kukosekana kwa elimu ya ujasiriamali. Kamati imeshauri Serikali kutumia Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Wanawake, vijana na watu wenyе ulemavu kabla ya kuwapatia mikopo ya kuanzisha shughuli za kiuchumi.

d) **Mradi Na. 4921 – Mpango wa Kurasimisha Rasimiali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, mpango huu unatekelezwa chini ya kifungu 1003 "Policy and

"Planning" cha fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. MKURABITA inaandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshajji wa biashara unaotambulika kisheria ambao huwezesha wananchi wanyonge kurasimisha ardhi na biashara wanazomiliki.

Kamati ilifanya ziara katika Halmashauri ya Nachingwea na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Mbondo, Nahimba na Nakalonji ambako jumla ya mashamba 2,328 yameweza kupimwa na Hati za Haki miliki za kimila 1,341 kuandaliwa. Aidha, MKURABITA imewezesha vijiji 104 kati ya 127 katika halmashauri hiyo kupima mipaka yake na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi hadi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, mionganini mwa mafanikio yaliyobainika kutokana na zoezi la urasimishajji ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi na mipaka ya miliki katika vijiji husika; Wanawake kupata fursa ya ama kumiliki Hati za haki miliki ya ardhi peke yao au kwa kushirikiana na wenza wao; na maeneo kuongezeka thamani kwa ardhi ya wananchi katika maeneneo yaliyorasimishwa.

Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na ufinyu wa bajeti na ukosefu wa wataalamu wa kuandaa na kusajili Hati za haki Miliki za Kimila, jambo linaloathiri kasi ya urasimishajji wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutatua changamoto hizo Kamati inashauri Serikali kuongenza bajeti ya MKURABITA na wataalamu wa kuandaa na kusajili hati za haki miliki za kimila ili kuwezesha zoezi la urasimishajji katika maeneo mengine ya Halmashauri ya Nachingwea.

**e) Mradi Na.6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF) – Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ultengewa **shilingi bilioni 74.36** na ulipangwa kutekelezwa chini ya kifungu 1003 "administration and human resource management" cha Fungu 30 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. TASAF inatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, na uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji ambayo inasaidia kaya maskini kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini wa kipato. Hadi sasa takribani kaya maskini zaidi ya **milioni 1** zenye jumla ya Watanzania **milioni 5** zimeandikishwa kunufaika na mpango.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujidhisha kuhusu utekelezaji wa mpango huu, Kamati ilitembelea Kijiji cha Namela kilichopo katika Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara ambacho ni mionganini mwa vijiji 99 vinavyonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini katika wilaya hiyo. Kijiji hiki kina jumla ya Kaya 117 zinazonufaika na mpango huu ambazo zilikuwa zimepokea ruzuku ya **shilingi milioni 109.99** kutokana na awamu 30 za uhawilishajji tangu kuanza kwa mpango huo Julai – Agosti,2014 hadi Januari – Februari,2019.

Aidha, TASAF imewezesha kijiji cha Namela kutekeleza miradi ya utoaji wa ajira za muda kwa kaya zote 117 za walengwa kwa kugharamia mradi wa upandaji wa mikoko katika eneo la ufukwe wa bahari ya Hindi lenye ukubwa wa ekari 4 kwa gharama ya **shilingi milioni 14.46** na ujenzi wa kisima cha pete kwa gharama ya **shilingi milioni 14.89**. Jumla ya **shilingi milioni 7.12** zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na ongezeko la mahudhurio ya watoto shulenii hasa wanaotoka katika kaya za walengwa tofauti na awali; walengwa wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, ufugaji, kilimo, na biashara na hivyo kuboresha

maisha ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wananchi kukosa uelewa kuhusu utekelezaji wa mpangowa ruzuku kwa kaya maskini jambo ambalo limeibua malalamiko kutoka kwa kaya ambazo hazijaingizwa kwenye mpango.

Kamati ilishauri Serikali kuwajengea uelewa wa kutosha wananchi kuhusu utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, pamoja na kuhakikisha kaya zenye sifa zinaingizwa kwenye mpango.

#### f) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika**, chuo kilanzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali, Agosti, 2000 kwa sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili, Chuo cha Watumishi wa Serikali (Civil Service Training Centre) kilichokuwa Dar es Salaam na Chuo cha Uhazili Tabora (Tabora Secretarial College). Uanzishwaji wa chuo hiki ulilenga kusaidia maboresho katika Utumishi wa Umma ili kuleta tija katika utoaji wa huduma.

Tangu kuanzishwa kwake chuo kimeweza kuongeza matawi hadi kufikia sita ambayo ni Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Mbeya, Tabora na Tanga.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo, Kamati ilitembelea Kampasi ya Mtwara na kubaini mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na kutoa wahifimu 8,560 katika fani mbalimbali tangu mwaka 2009, kupata usajili kamili kutoka Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundsi Tanzania (NACTE), kumiilki viwanja viwili katika eneo la Shangani na kupunguza watumishi wa mikataba kutoka asilimia 76 hadi asilimia 41.

Pamoja hayo mafanikio hayo bado kuna changamoto kadhaa ambazo ni pamoja na uhaba wa mabweni jambo linalozua ongezekola udahili wa wanafunzi, upungufu wa vitabu 200 na uchakavu wa majengo ambaa unahatarisha usalama wa watumiaji.

Kamati imeshauri Serikali kujenga Mabweni ya kutosha ili kuongeza udahili wa wanafunzi na kukarabati majengo yaliyochakaa ili kuepusha madhara yanayoweza kujitekeza iwapo uchakavu utaachwa kuendelea.

#### 2.2.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kukamilisha zoezi la ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilijelekeza katika uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais ili kuzingatia Kanuni ya 98 (2), pamoja na kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Bajeti ya Ofisi ya Rais inahusisha Mafungu 28 kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Mafungu 8 kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Uchambuzi ulijikita katika kupitia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Vikao vya Uchambuzi wa Bajeti vilifanyika kama ifuatavyo: -

#### 2.2.3 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa bajeti katika Ofisi hii ulihusisha mafungu yafuatayo: -

- 1) Fungu 56 – Ofisi ya Rais – TAMISEMI
- 2) Fungu 2 - Tume ya Utumishi wa Wadilimu (TSC)
- 3) Fungu 70 – Mkoa wa Arusha
- 4) Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya
- 5) Fungu 79 – Mkoa wa Morogoro
- 6) Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam
- 7) Fungu 63 – Mkoa wa Geita
- 8) Fungu 90 – Mkoa wa Songwe
- 9) Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa
- 10) Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara
- 11) Fungu 81- Mkoa wa Mwanza
- 12) Fungu 84 – Mkoa wa Singida
- 13) Fungu 85 – Mkoa wa Tabora
- 14) Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro
- 15) Fungu 71 – Mkoa wa Pwani
- 16) Fungu 36 – Mkoa wa Katavi
- 17) Fungu 73 – Mkoa wa Iringa
- 18) Fungu 87 – Mkoa wa Kagera
- 19) Fungu 54 – Mkoa wa Njombe
- 20) Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma
- 21) Fungu 76 – Mkoa wa Lindi
- 22) Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu
- 23) Fungu 95 – Mkoa wa Manyara
- 24) Fungu 77 – Mkoa wa Mara
- 25) Fungu 72- Mkoa wa Dodoma
- 26) Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma
- 27) Fungu 83 – Mkoa w Shinyanga
- 28) Fungu 86 – Mkoa wa Tanga

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikani wa fedha za matumizi kutoka Hazina kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa

#### **(i) Ukusanyaji Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imekusanya **shilingi bilioni 9.85** sawa na asilimia 44 tu ya lengo la kukusanya **shilingi bilioni 22.64** katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Kamati ilielezwa kwamba makusanyo hafifu ya maduhuli yamechangiwa na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) kushindwa kupata **shilingi bilioni 1.2** ilizotarajia kutoka Benki ya CRDB; baadhi ya halmashauri kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; na Mauzo hafifu ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa na asilimia 43.7 iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Ingawa kiwango kilichokusanywa kiko chini ya asilimia 70 iliyopaswa kufikiwa hadi katika robo ya tatu, bado ni kikubwa kwani malengo yaliyowekwa yalikuwa makubwa zaidi ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha uliotangulia.

Aidha, uchambuzi umebaini kwamba, makusanyo yamekuwa yakiongezeka katika

kipindi cha miaka mitatu ya fedha (2016/17, 2017/18 na 2018/19). Kwa mtazamo wa Kamati ilikuwa vigumu kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kipindi kilichokuwa kimesalia, na hivyo kutishia kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mikoa na Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 makusanyo yaliikuwa ni **shilingi bilioni 735.73**, sawa na wastani wa asilimia 69, kiwango ambacho kinapaswa kuwa kimefikiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa bajeti. Bado Halmashauri zimeendelea kuwa na makusanyo makubwa ikilinganishwa na mikoa na makao makuu (Fungu 56) na taasisi zake.

#### (ii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa umebaini kwamba fedha zinazotolewa zimeendelea kupungua kwa mwaka wa tatu mfululizo; mwaka wa fedha 2016/17 (asilimia 57), mwaka wa fedha 2017/18 (asilimia 53) na mwaka wa fedha 2018/19 (asilimia 45.2).

Aidha, fedha zinazotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (cash flow plan) uliowekwa; fedha za matumizi ya kawaida zinazotolewa kwa wingi ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na fedha hazitolewi kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Ofisi hii.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 181.73** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 45.2** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mwenendo huo unaonesha kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 53 iliyopatikana katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2019 ofisi hiyo na taasisi zake ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 21.75** sawa na asilimia 50.6 ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 18.4 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/18.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi bilioni 159.98** sawa na asilimia 44.5 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2018/19 ziliidhinishiwa **shilingi trilioni 5.89** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 3.94** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi bilioni 580.2** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni **1.37** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa zimepokelewa kwa asilimia 57, wakati fedha za maendeleo zilikuwa zimepokelewa kwa asilimia 38.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini kwamba kwa wastani upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa Ofisi ya

Rais - TAMISEMI na Taasisi zake katika mwaka wa fedha 2018/19 ulikuwa ni **asilimia 47.55**, kwango ambacho kimepungua sana ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 60.5** katika miaka miwili ya fedha iliyopita (2016/17 na 2017/18).

Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, badala ya upatikanaji wa fedha kuongezeka ili kufikia lengo la angalau asilimia 25 kwa kilarobo katika mwaka fedha, sasa wastani umeshuka hadi kufikia asilimia 15.85 kwa robo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uchambuzi umebaini kwamba, wastani wa upatikanaji wa fedha ulikuwa ni kwa asilimia 47.5. Aidha, bado fedha za matumizi ya kawaida zimeendelea kupatikana kwa kwango cha juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Hii inaashiria kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaendelea kususua kutokana na fedha kucheleweshwa na kutolewa kwa kiasi kidogo.

### **(iii) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, imezingatia maouni na ushauri wa Kamati kwa kwango cha kuridhisha, jambo ambalo limesaidia kutatua changamoto zilizobainishwa, na hivyo kuboresha huduma za msingi kwa maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanya kazi maoni na ushauri kwa baadhi ya maeneo yaliyosalia ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na: -

(a) Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria utakaowezesha kusimamia kikamilifu asilimia kumi (10) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu. Sheria hiyo ilitungwa kuititia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 iliyofanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 37 A, na sheria hiyo ilianza kutumika Julai, 2018;

(b) Halmashauri ziendelee kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imebuni miradi ya kimkakati ili kuziwezesha Halmashauri kuongeza mapato ya ndani. Hadi kufikia Februari, 2019 Halmashauri 30 zilikuwa zimekidihi vigezo vya miradi 38 ambayo ilidhinishiwa **shilingi bilioni 268.4**;

**Mheshimiwa Spika**, licha ya baadhi ya maoni kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na: -

i. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu fedha za asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri na kuzipeleka kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe ulemavu. Aidha, Halmashauri ziandae na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na idadi ya vikundi vilivyopokea pesa, na kusimamia urejeshajji wa fedha hizo; na

ii. Serikali iendelee kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma katika halmashauri nchini ambayo yalijengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Serikali ilidhinisha **shilingi trilioni 1.36** kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini hadi Desemba, 2018 ni asilimia 38 tu ya fedha hizo ndiyo ilikuwa imetolewa. Hii inaashiria kwamba, ukamilishaji wa miradi ikiwa ni pamoja na maboma utaendelea kususua.

**iv.) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi triliioni 6.21**. Kati ya fedha hizo, **shilingi triliioni 4.52** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **shilingi triliioni 1.69** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida **shilingi triliioni 3.81** sawa na asilimia 61.33 ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, na **shilingi bilioni 707.95** sawa na asilimia 11.40 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya maendeleo imechukua asilimia 27.27 ya bajeti yote ya Ofisi hii. **Jedwali Na. 01** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Jedwali Na. 01** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Mgawanyo wa Bajeti	Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020	Asilimia ya Makadirio (%)
OC	707,951,000,000	11.40
Mishahara	3,807,104,425,000	61.33
Maendeleo	1, 692, 937, 354,769	27.27
<b>Jumla</b>	<b>6, 207,992, 779,769</b>	<b>100</b>

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2019/2020)

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa makusanyo ilikadiriwa kuwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zitakusanya jumla ya **Shilingi bilioni 802.16**. Mapato hayo yameongezeka kwa **shilingi bilioni 43.79** sawa na asilimia 6 ikilinganishwa na makusanyo ya **shilingi bilioni 758.36** katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Ongezeko hilo lilitarajiwa kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa takribani **shilingi bilioni 29.89** sawa na asilimia 4.1 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika mwaka wa fedha uliomalizika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipongeza hatua za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kufidia pengo la vyanzo vilivyo chukuliwa na Serikali Kuu, na kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, kwani kumekuwa na tija kubwa. Kwa ujumla wake bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilipungua kwa **shilingi bilioni 374.95** sawa na asilimia 5.69 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, Kamati ilibaini upungufu wa asilimia 5.92 kutoka **shilingi triliioni 1.79** kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi **shilingi triliioni 1.69** katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Uchambuzi ulibaini kwamba, upungufu huo wa bajeti ya jumla na ile ya maendeleo ulitarajiwa kubadili kabisa mwelekeo wa bajeti kwa ofisi hii ambayo iliongezeka kwa wastani wa asilimia 9 katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo

(2016/17 hadi 2018/19).

Aidha, katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 uchambuzi ulibaini kwamba, wakati bajeti ya Taifa ikiongezeka kwa asilimia

1.93 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19, bajeti ya TAMISEMI katika kipindi hicho ilipungua kwa asilimia 5.69.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni sawa na asilimia 18.74 ya bajeti ya Taifa, uwiano ambao umeendelea kupungua katika kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka mwaka wa fedha 2015/16 ambapo uwiano ulikuwa ni asilimia 24.

**Mheshimiwa Spika**, inashangaza kwamba licha ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kusimamia seka nyingi katika ngazi za mamlaka za Serikali za Mitaa, bajeti yake imepungua, na uwiano wa bajeti hii ikilinganishwa na bajeti ya Taifa umeendelea kupungua kwa mwaka wa nne mfululizo.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iendelee kuimarisha mfumo wa kuwahudumia wananchi ambao ndiyo msingi wa madaraka yote ya Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977. Njia madhubuti ya kuimarisha mfumo huo ni kupeleka kikamilifu fedha za kutosha (kuongeza bajeti) kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanya.

## 2.2.4 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utawala Bora, Kamati ilifanya uchambuzi wa mafungu yafuatayo: -

1. Fungu 20 – Ikulu;
2. Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
3. Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
4. Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
5. Fungu 67 – Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
6. Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma;
7. Fungu 09 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma; na
8. Fungu 04 – Idara ya kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

### (i) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi kilichotolewa na Hazina. Aidha, mtiririko wa fedha haukuwa mzuri kwani fedha ilikuwa inatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (cash flow plan) ulioandaliwa. Uchambuzi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi bilioni 374.7**, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 60.03 ya Fedha yote iliyoidhinishwa.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa Fedha kwa mwaka 2018/2019 na mwaka 2017/2018 na kubaini kuwa kiasi hicho cha fedha kilipungua kwa takribani **shilingi bilioni 43** sawa na asilimia

10.31 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambacho ilikuwa ni **shilingi bilioni 417.7**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 ofisi hii na Mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 82.05** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na **asilimia 46.87** ya fedha iliyodhinishwa. Kiasi hicho kilipungua kwa asilimia 60.19 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambacho ilikuwa ni **shilingi bilioni 206.72**. Kamati imebaini kwamba, ingawa mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukufikia lengo linalohitajika, uliimarika ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliotangulia. Kwa wastani upatikanaji wa fedha ilikuwa ni asilimia 65.03 ya fedha zote zilizoidhinishwa, wakati katika mwaka uliotangulia ilikuwa ni asilimia 50.37. Aidha, kasumba ya fedha za matumizi ya kawaida kupatikana kwa wingi kuliko fedha za maendeleo imeendelea kutamalaki.

**(ii) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilizingatia kikamilifu baadhi ya maoni ya Kamati, na ilikuwa inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwani kuhusu: -

- (a) Serikali kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi ambapo iliweza kuidhinisha asilimia 81 ya nafasi za uteuzi;
- (b) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu (Sheria, Kanuni na Miongozo) na hivyo kuepusha migongano isyo ya lazima. Mafunzo yalitolewa kwa wakurugenzi wa serikali za mitaa, wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa na wilaya; na
- (c) Benki na Taasisi za fedha zielimishwe kuhusu hadhi ya Hati za Haki Miliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, ambapo baadhi ya benki na taasisi za fedha zimeanza kukubali hati hizo baada ya kuelimishwa. Aidha, wananchi zaidi ya 500 wametumia hati hizo kukopa **shilingi bilioni 4.9** kutoka Benki za CRDB, NMB, PSPF na Agricultural Inputs Trust Fund; na
- (d) Kutambua na kuandikisha Kaya maskini katika maeneo ya Viji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo maandalizi ya awamu ya pili ya utekelezaji
- (a) wa TASAF III yako katika hatua za mwisho na maeneo yote hayo yatafikiwa.

**(iii) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Mheshimiwa Spika**, ili iweze kutekeleza malengo yaliyokusudiwa

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, iliomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 683.51**. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 483.66** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi bilioni 199.87** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, bajeti iliyombwa kuidhinishwa katika mwaka huu iliongezeka kwa **shilingi bilioni 14.43** sawa na asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyodhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ilikuwa **shilingi bilioni 669.09**. Ongezeko hilo la fedha lilbadili mwenendo wa bajeti ya ofisi hii kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/18 na 2018/19) ambapo bajeti ilikuwa ikipungua.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi ulibaini ongezeko la **shilingi bilioni 3.89** sawa na asilimia 1.99 ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi bilioni 195.97** zilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19. Uchambuzi zaidi ulibaini

kwamba licha ya ongezeko hilo, bajeti ya maendeleo kwa mwaka huu ilikuwa ni takribani asilimia 51.12 tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/2018.


**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi ulilengwa kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ufanuzi wa uchambuzi huo umetekelizwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

(a) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni **shilingi bilioni 683** ni sawa na asilimia 2.06 tu ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2019/20 ni **shilingi trillioni 33.1**

(b) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ulionesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 1.93, ikililinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/19; ilihali bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilionezeka kwa asilimia 2.16 ikililinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19;


(c) Mpango wa Maendeleo ya Taifa ulionesha ongezeko la asilimia 2.0 katika fedha za maendeleo, ambazo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2019/20, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliongezeka kwa asilimia 1.99 ikililinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01 na Na. 02** kama ifuatavyo:-

Figure 1 Chati Na. 01: Bajeti ya Taifa kwa ajili ya mishahara, Matumizi ya Kawaida, Maendeleo na deni la taifa kwa Mwaka 2019/20



**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020

**Figure 2 Chati Na. 02: Bajeti ya OR-UUB kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengine na Maendeleo kwa Mwaka 2019/20**



**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa fedha 2019/2020

#### 2.2.5 Kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza jukumu hili kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 7 (1) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Taarifa hii itahusisha uchambuzi wa taarifa za utekelezaji za baadhi ya taasisi.

(a) **Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, mkakati huu unalenga kurejesha shule kongwe katika ubora wake baada ya miundombinu yake kuchakaa na kuharibika kwa kiwango kikubwa. Mkakati huu ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 na unagharamiwa na Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Program For Results – EPSR).

Jumla ya shule 89 kongwe zitakarabatiwa kwa awamu kwa kuhusisha vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, ofisi za walimu, majiko, mifumo ya maji safi na taka, mifumo ya umeme na TEHAMA. Awamu ya kwanza yenye shule 45 utekelezaji wake ulianza mwaka wa fedha 2016/2017 na kugharimu **shilingi bilioni 54.85**.

Aidha, utekelezaji wa awamu ya pili yenye shule 19 ulianza Mei, 2019 kwa gharama

ya **shilingi bilioni 16.85** ambapo utaratibu wa force account unatumika na ukarabati uko katika hatua mbalimbali. Vilevile, maandalizi kwa ajili ya ukarabati kwa shule zilizosalia yameanza kufanyika kwa hatua za upembuzi yakinifu (conditional survey) na inakadirwa kwamba, utagharimu **shilingi bilioni 16.46**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuzikarabati shule kongwe nchini kwa lengo la kurejesha ubora wa awali ambaa pia unaleta mazingira bora ya kazi kwa walimu na ya kujifunzia kwa wanafunzi. Jambo hili linarejesha heshima ya shule za Serikali na kuongeza ari ya utendaji kwa Walimu.

Aidha, Kamati inapongeza hatua ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuanza mchakato wa kuacha na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika ukarabati wa baadhi ya shule kwani ameshindwa kuzingatia kikamilifu masharti ya mikataba aliyoasaini ili kutekeleza ujenzi au ukarabati.

Vilevile, Kamati inashauri Serikali kujenga mazingira ya kukarabati shule hizo mara kwa mara, na kutunga sheria ndogo ndogo zitasaidia kulinda mazingira na miundombinu ya shule hizo ili kuepusha uharibifu na uchakavu kutokea bila kushughulikiwa.

#### (b) **Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unagharamiwa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Duniya na fedha za ruzuku kutoka Serikali ya Denimark na utekelezaji wake uko katika awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza iliyotekeliza kwa miaka miaka mitano (2010/2011 hadi 2015/2016). Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Majiji Tano na Halmashauri za Manispaa tatu za Mtwara/ Mikindani, Kigoma/Ujiji Kigoma na Illemela, na utagharimu jumla ya **dola za marekani milioni 355.7**.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma ikiwa mionganoni mwa wanufaika wa mradi huu imeweza kujenga barabara za lami yenye urefu wa kilometa 42.29, Dampo la kisasa (Landfill) katika kijiji cha Chidaya, ununuzi wa makontena 61 ya kubeba taka ngumu, mfereji mkubwa wa maji ya mvua (storm water Drain) wenyewe urefu wa kilometa 7.64 na ukarabati wa Ofisi ya Mhandisi na ukarabati wa karakana ya Jiji. Kazi zote zilitekelezwa kwa gherama ya **shilingi bilioni 47.47**

**Mheshimiwa Spika**, ufanisi wa utekelezaji wa mradi huu umewezesha Halmashauri ya Jiji la Dodoma kupata nyongeza ya mkopo mara mbili (first and second additional financing) ya **shilingi bilioni 88.8** ambazo zimetumika kukamilisha kazi za awamu ya kwanza, na pia kujenga barabara za lami kilometa 26.7, stendi ya mabasi ya kisasa, Soko la Kisasa la Job Ndugai, eneo la mapumziko (recreational park) la Chinangali, kituo cha maegesho ya malori Nala, na uwekaji wa taa za barabarani 925 zinazotumia umeme wa juu (solar street lights), ambapo ujenzi umefikia asilimia 82.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia TSCP kuboresha Jiji la Dodoma kwa ujenzi wa miundombinu hiyo ambayo ni mwanzo mzuri wa kufanya jiji hili kuwa la kisasa, na kuwezesha wananchi kupata huduma bora za kijamii na kiuchumi. Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ihakikisha Halmashauri ya Jiji la Dodoma inatafuta waendeshaji wenyewe sifa katika Stendi ya Mabasi, Soko, Kituo cha Mapumziko cha Chinangali, na Kituo cha kuegesha Malori cha Nala, ili kuhakikisha thamani ya pesa zilizotumika katika uwekezaji huo inapatikana.

Aidha, nitumie fursa hii kukupongeza Mheshimiwa Spika, kwa heshima uliyopewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, ya Soko jipya la Dodoma kuitwa kwa jina lako. Hii ni heshima kubwa, ambayo itafanya mchango wako katika Bunge la Tanzania na Mkoa wa Dodoma

ikumbukwe katika historia ya nchi yetu.

**(c ) Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute)**

**Mheshimiwa Spika**, taasisi imeendelea na kusimamia malengo ya kuwa kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika ikianzia na Tanzania, Ukanda wa Mashariki na hatimaye Bara lote la Afrika. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

Taasisi hii kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichopo Helsinki, Finland imeendelea kutekeleza Programu ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi ambayo inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati na kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine.

Tangu kuanza kwa mafunzo hayo, Watumishi waandamizi 33 kutoka Wizarani, Taasisi na Mashirika ya Umma wameweza kushiriki na ambapo wamepata ujuzi wa masuala ya Uongozi wa matokeo, ubunifu na kuandaa Mpango Mkakati na namna ya kuutekeleza. Aidha, taasisi imeendesha kozi mbili (2) kwa Viongozi Waandamizi 36 kutoka Sekretarieti ya Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu masuala ya uongozi, uongozi binafsi na akili hisia kwa lengo la kui marisha utendaji wao.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi iliandaa na kuendesha vipindi vitano (5) vya majadiliano na Marais Wastaafu, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania; Mheshimiwa Ernest Bai Koroma wa Sierra Leone; Mheshimiwa Hery Rajaonarimampianina wa Madagasca; na Viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu kupitia runinga, tovuti ya Taasisi ya Uongozi na mitandao ya kijamii. Msingi wa vipindi hicho ambavyo vilrushwa kote barani Afrika ilikuwa kubailishana taarifa, maarifa na uzoefu wa kiuongozi.

Aidha, taasisi ya Uongozi imekuwa ikishirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa ya UNU-WIDER iliyopo Finland kufanya tafiti kuhusu uchumi wa viwanda, uchumi mpana, fedha, usimamizi wa mikopo endelevu pamoja na maeneo mengine, ambapo hadi sasa wamekamilisha tafiti 13.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hii imeweza kuandika na kuchapisha kitabu kinachoeleza maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamini William Mkapa ambacho kilizinduliwa mwaka jana, na inaendelea na maandalizi ya kitabu kwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi huku ikiendelea kuhamasisha viongozi wengine wastaafu kuandaa na kuchapisha vitabu kwa kushirikiana na taasisi hii.

Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu ikiwezekana wa kisheria ambaou utawataka viongozi wa ngazi ya uandamizi k u h u d h u r i a mafunzo yanayotolewa na taasisi hii kwa lengo la kujengewa uwezo au kuongezewa weledi katika masuala ya kiuongozi kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao.

**(d) Wakala wa Ndege za Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Ndege za Serikali ilianzishwa mwaka 2002 kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245. Awali ilikuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi na ilipohamishiwa Ofisi ya Rais, tangu tarehe Aprili, 2018.

Pamoja na kusimamia huduma za usafiri wa ndege kwa viongozi wakuu wa kitaifa, Wakala unaratibu ununuzi wa ndege mpya za Serikali na kuzikodisha kwa kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili ziweze kutumika kibiashara. Hadi sasa Wakala inamili ki ndege 10 ambazo zimegawanyika katika makundi mawili

(2), ndege nne (4) ambazo zinatumika kwa safari za Viongozi wakuu wa kitaifa na ndege sita (6) ambazo zimezokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

Aidha, wakala imeweza kuwapeleka mafunzoni wanahewa 19 kwa aiji ya kupata mafunzo ya kisheria kwa kuzingatia sheria, kanuni na utaratibu zinazoratibiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ili waweeze kuhuisha leseni zao.

Kamati inapongeza mafanikio ambayo Wakala imeyapata katika kipindi hiki cha awamu ya tano hasa kwa kununua ndege na kuzikodisha kwa Kampuni ya ATCL, jambo ambalo limewezesha shirika hilo kurejea angani na hivyo kuitangaza nchi yetu kimataifa.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ijenge utamaduni wa kulipa madeni yanayotokana na kukodisha ndege ili kuiwezesha Wakala kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi na hivyo kutoa huduma bora.

#### **(e) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika, tangu ulipoanzishwa mwaka 2000** mfuko huu umetekelizwa katika awamu tatu tofauti. Katika awamu ya kwanza (2000 – 2005) iliyohusisha maeneo 42 (halmashauri za Tanzania Bara, na Unguja na Pemba) jumla ya **shilingi bilioni 72** zilizumika kuwashudumia wananchi kupitia miradi mbalimbali ya afya, maji, miundombinu na elimu.

Kutokana na mafanikio yaliyopatikana, Serikali iliamua kuanzisha huduma za mfuko huo katika halmashauri zote 124 za wakati huo Tanzania Bara, pamoja na Unguja na Pemba kwa kuanzisha awamu ya pili (TASAF II) iliyotekelizwa kuanzia mwaka 2005 hadi 2013 kwa gharama ya **shilingi bilioni 430**.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanza kutekelezwa kwa TASAF Awamu ya Tatu mwaka 2013 ambayo inahusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu walengwa zaidi ya milioni moja katika Vijji/Mitaa/Shehia 9,968 wanufaika na zaidi ya **shilingi bilioni 706** zimetumika.

Utekelezaji wa mpango huu umeweza zaidi ya asilimia 95 ya watoto walio chini ya miaka 5 kutoka kaya za walengwa kuhudhuria kliniki, na zaidi ya asilimia 97 ya watoto wanaotoka kaya za walengwa kuhudhuria shuleni. Mahudhurio hayo kliniki na shuleni ni dalili njema ya kujenga nguvu kazi yenye afya bora na uelewa mzuri katika vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanza kutekelezwa kwa TASAF III jumla ya miradi 122 ya miundombinu yenye thamani ya **shilingi bilioni 4** inatekelezwa katika Halmashauri 13 za Mikoa ya Arusha na Njombe na tayari wavezeshajii katika ngazi ya Halmashauri na wajumbe wa kamati wamepatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa miradi katika maeneo yao.

Aidha, TASAF imekuwa ikizingatia matumizi ya Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli zake. Mifumo hiyo imekuwa ikiboreshwu katika awamu mbalimbali ili iweze kuongea na mifumo mingine ya kitaifa. Miogoni mwa mifumo hiyo ni Mfumo wa Kutambua na Kuandikisha Walengwa ambao ni dodoso la kielektroniki linalopokea taarifa kutoka ngazi ya jamii na kuzichakata ili kupata kaya zinazostahili kuandikishwa kwenye mpango wa kunufaika na ruzuku. Majaribio yameishafanyika katika Halmashauri za Siha, Mtwara Vijiji na Nanyamba Mji.

Mfumo mwingine ni Mfumo wa Malipo kwa Walengwa (e-payment system) ambao

hutumika kuchakata malipo ya walengwa kwa kuanda orodha ya malipo kwa ngazi zote zinazohusika na mwakilishi wa kaya. Mfumo huu unatekelezwa kwa majaribio katika maeneo ya utekelezaji kumi na sita (16) nchini ambapo **kaya 55, 350** zilikuwa zimelipwa kwa njia ya kielektroniki. Kupitia utaratibu huu malipo ya kaya hutumwa moja kwa moja kwenye akaunti aidha ya simu au benki ya mwakilishi wa kaya. Uzoefu umeonesha kwamba asilimia 95 ya wanaolipwa hutumia mitandao ya simu, na asilimia 5 tu ndiyo hutumia akaunti za benki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza hatua hii na inashauri Serikali kuhakikisha mfumo unasambazwa na kutumika katika maeneo yote ya nchi kwa walengwa wa mpango, kwani una ufanisi na uwazi wa kutosha, malipo hufika kwa wakati na moja kwa moja kwa walengwa na hivyo kuokoa muda.

Ni ushauri wa kamati kwamba, Serikali ihakikishe inaondoa changamoto ya usajili wa line za simu ili kutokwamisha mfumo huu kutumika kwa walengwa wa ruzuku kwa kaya maskini. Ni wazi kwamba, iwapo walengwa wengi watashindwa kusajili line za simu kwa kukosa vitambulisho vya NIDA, mfumo huu hautaweza kutumika kwa kiasi kikubwa kama inavyotarajiwa.

Aidha, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kupata mkopo nafuu wa **shilingi triliioni 1.035** (Dola za Marekani milioni 450) kwa ajili ya utekelezaji wa sehemu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini katika awamu ya tatu ya TASAF (TASAF III) kwenye Halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar kuanzia mwaka 2019 hadi 2023.

Ni matumaini ya Kamati kwamba, Serikali itahakikisha kuna usimamizi mzuri wa fedha hizi na kaya zote zenyeh sifa ambazo hazikuwa kwenye mpango katika awamu zilizopita zitaingizwa kwenye mpango ili kila mwenye sifa aweze kunufai ka.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kutokana na Serikali kutochangia kikamilifu theluthi moja (1/3) kwa mujibu wa makubaliano na wadau wengine wa mpango huu.

Kwa mfano katika kipindi cha miaka sita na nusu ya bajeti kuanzia 2013/2014 – 2019/2020 (Januari, 2020) Serikali illichangia **shilingi bilioni 8.11** tu kati ya **shilingi bilioni 70.01** zilizoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho sawa na takribani asilimia 11.58 tu ni kidogo sana. Mchanganuo zaidi wa uchangiaji wa Serikali umefafanuliwa zaidi kupitia jedwali **Na. 2** hapa chini.

#### **MCHANGO WA SERIKALI KATIKA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI MWAKA WA FEDHA 2013/2014 HADI 2019/2020 - JANUARI 2020**

<b>Mwaka wa Fedha</b>	<b>Bajeti Iliyoidhinishwa</b>	<b>Kiasi Kilichotolewa</b>	<b>Kiasi kilichobaki</b>
2013/2014	18,500,000,000	3,000,000,000	15,500,000,000
2014/2015	14,000,000,000	0	14,000,000,000
2015/2016	14,000,000,000	600,000,000	13,400,000,000
2016/2017	14,000,000,000	0	14,000,000,000
2017/2018	3,000,000,000	750,000,000	2,250,000,000
2018/2019	3,000,000,000	3,000,000,000	0
2019/2020	3,514,206,000	757,102,800	2,757,103,200
<b>JUMLA</b>	<b>70,014,206,000</b>	<b>8,107,102,800</b>	<b>61,907,103,200</b>

**Jedwali Na. 02**

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinaonesha kwamba, mpango wa kunusuru kaya maskini kwa takribani asilimia 89 umekuwa ukigharamiwa na fedha za mkopo na msaada kutoka kwa wahisani, jambo linaloleta wasiwasi kama unaweza kuendelea

iwapo wahisani watajiondoa.

Kamati inaendelea kushauri juu ya Serikali kutathmini ushiriki wake katika mpango huu na kutoa mchango wake wa fedha kikamilifu ili kujenga utamaduni na kuandaa mazingira ya kugharamia mpango huu kwa fedha za ndani iwapo wahisani watajiondoa au watafikia ukomo katika kuchangia. Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) ulianzishwa kwa lengo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo madlum ya muda mfupi kwa kutumia Teknoloja ya Habari na Mawasiliano. Serikali iliamua kuuanganisha Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) na Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) Juni, 2019 jambo linaloufanya wakala kuwa sehemu ya Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).

Miongoni mwa shughuli zilizokuwa zikitekelezwa na wakala ambazo sasa zitatekelezwa na TPSC ni pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali kwa njia ya midahalo na kwa njia ya Mtandao wa Video katika maeneo ya Uongozi na Menejimenti, Utawala Bora, Maadili, Afya na stadi za Utendaji ambazo zaidi ya washiriki 957 wamenufaika.

Aidha, kumekuwa na ushirikiano baina ya wakala na wadau wa ndani na nje katika kutoa huduma kutohana na mahitaji ya wadau. Wadau wapya ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu Huria (OUT) walijunga ili kushirikiana na TaGLA na kupata elimu kuhusu manufaa ya kutumia tehma na kufanya mikutano kwa njia mtandao wa video (video conference).

Wadau wengine ni pamoja na NIMRI, Shirika la Posta Tanzania, African Legal Support Facility (ALSF), DAWASA na Wizara ya Mawasiliano.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, hatua ya Serikali kuunganisha TaGLA na TPSC isihafifishe kazi zilizokuwa zikitekelezwa na wakala huo, badala yake kazi hizo ziboreshwe na kutekelezwa sambamba na utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania.

#### **f) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika,** MKURABITA imekuwa ikiendelea kutekeleza mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria. Mpango huu umewezesha wananchi wanyonge kurasimisha mali ardhi na biashara na kuzigeuza kuwa nyenzo ya kupambana na kuijkwamu dhidi ya umasikini.

Ili kufanikisha zoezi la urasimishaji nchini, MKURABITA inawajengea uwezo watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wizara za kiseka kwa upande wa Zanzibar, kwa kuwapatia mafunzo ili waendeleze urasimishaji katika maeneo yao.

Licha ya umuhimu wake, mpango huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ya maendeleo, na hata ile inayotengwa fedha zimekuwa zikitolewa kwa kiwango kisichoridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudzi za Serikali za kuanzisha mfuko endelevu wa Urasimishaji katika Wilaya (District Revolving Fund) ili kuwezesha zoezi la urasimishaji kuijendesha kupitia mfuko huo, ambapo imeweka **shilingi milioni 243** katika benki ya NMB kama dhamana ya mfuko huo. Aidha, tayarî majaribio yanafanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Hamlimashauri ya Mji Njombe kwa Halmashauri hizo kukopa **shilingi milioni 100** kutoka mfuko huo

kwa ajili ya urasimishaji.

Hata hivyo, ni mtazamo wa Kamati kwamba kiasi kilichotengwa ni kidogo sana ikilinganishwa na halmashauri 185 zilizopo nchini ambazo urasimishaji unahitajika. Aidha, kumekuwa na changamoto kwa Halmashauri nyingi kutoona umuhimu wa zoezi la urasimishaji na hivyo kushindwa kutenga fedha za kuratibu zoezi hilo, na kutoshirikiana na waratibu wa MKURABITA. Takwimu zinaonesha hadi sasa ni Halmashauri 28 sawa na asilimia 15 ya halmashauri zote nchini (185) ambazo zimeweza kumiliki ajenda ya urasimishaji na kuweza kupima mashamba.

**Mheshimiwa Spika**, hii ni ishara kwamba juhudzi zaidi zinahitajika ili kuhakikisha halmashauri zote nchini zinatambua umuhimu wa MKURABITA na kuweza kumiliki agenda ya urasimishaji ambayo utekelezaji wake utanufaisha wananchi na mamlaka za Serikali za mitaa kwa kuondoa migogoro ya umiliki wa ardhi, na kukuza uchumi wa wananchi ambaa utasaidia kuongeza mapate ya Serikali.

#### (h) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART).

**Mheshimiwa Spika**, Wakala huu ulianzishwa mwaka 2007 kwa Tangazo la Serikali Na. 120 ili kusimamia utekelezaji wa mfumo wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam kwa ufanisi na hivyo kupunguza msongamano ambaa ni kero kubwa.

Mradi wa DART utatekelezwa kwa awamu sita na utahusisha barabara zenyet urefu wa kilomita 146. Awamu ya kwanza iikamilika na kuanza kutoa huduma Mei, 2016 kwa kutumia Mto Huduma wa Mpito "interim service provider" ambae amekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uchache wa mabasi kwani alilingiza nchini mabasi 140 katika ya 305 yanayohitajika, na kukosa mfumo wa uhakika wa tiketi.

Serikali imechukua hatua kadhaa ili kukabilii changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuanza mchakato wa kumpata Mto Huduma Kamilii ifikapo Julai mwaka huu. Hatua hiyo itasaidia kuongeza mabasi na kuboresha huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, wataalam wa DART, TAMISEMI na eGA wanashirikiana kutengeneza mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kukusanya hauli ambaa utakamilika Machi, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudzi hizo za Serikali. Hata hivyo, inapenda kushauri Serikali kuhakikisha DART inapata sheria mahususi, kwani kukosekana kwake kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala, ikiwa ni pamoja kukosa kanuni ambazo zingesaidia usimamizi na udhibiti wa matumizi mabaya ya miundombinu ya wakala.

#### (i) Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo

**Mheshimiwa Spika**, chuo hiki ambacho kilianzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Bunge Na. 26 ya mwaka 1994 kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kushauri katika masuala mbalimbali yanayohusiana na uendeshaji wa Serikali za Mitaa.

Chuo kilianza kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada na kuanzia mwaka wa 2019/2020 kimeanzisha Shahada (Bachelor Degree) ya Utawala na Menejimenti katika Serikali za Mitaa. Aidha, chuo hiki kimekuwa kikiandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa viongozi wa ngazi mbalimbali wa kiasasa na watendaji katika Serikali za Mitaa. Mionganoni mwa viongozi hao ni Madiwani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ufanisi unaopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, chuo kimekuwa kikibiliwa na changamoto kubwa ya ubovu wa barabara ya lhumwa - Hombolo (km 27) ambao unasababisha uharibifu wa vyombo vya usafiri na hivyo kusababisha gharama kubwa katika matengenezo. Aidha, kukosekana kwa uzio kuzunguka maeneo ya chuo kimekuwa kukisababisha wananchi wanaoishi maeneo ya jirani kuingia katika maeneo ya chuo jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa mali za chuo na wanafunzi. Ni ushauri wa Kamati kwamba, changamoto hizo zitatuliwe ili kukiwezesha chuo kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na kuwezesha Wanafunzi kusoma katika hali ya utulivu.

#### (j) Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC)

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 36 ya Mwaka 1974 ili mionganini mwa mambo mengine, liweze kusimamia na kuendesha Soko Kuu pamoja na masoko mengine yatakayowekwa chini yake, kujenga masoko mengine katika Jiji la Dar es Salaam na kusimamia uendeshaji wake.

Shirika hilo ambalo lipo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI lina wanahisa wawili ambao ni Hal mashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Hisa asilimia 51) na Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali Kuu (Hisa asilimia 49), linamiliki mali zenyenye thamani ya **shilingi bilioni 56**. Aidha, mbalii na Soko Kuu la Kariakoo Shirika lina maeneo mengine Tabata Bima na Mbezi Beach (Makonde).

Pamoja na shirika kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio, limekuwa likibiliwa na changamoto kadhaa ambazo ni pamoja; na upungufu katika Sheria ya Shirika ambao unaathiri utendaji na uendeshaji, uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo kutokana na umri mkubwa (miaka 40), na zuio la magari yanayoleta mazao katika Soko la Kariakoo kutokana na Sheria Ndogo za Manispaa ya Ilala na Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri changamoto hizi kufanyiwa kazi ili kuwezesha shirika hili kujendesha kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kupata sheria bora ambayo itawezesha shirika kuwekeza vitega uchumi zaidi na hivyo kuongeza wigo wa mapato.

#### 2.2.6 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

**(a) Maadhimisho ya Mkataba wa Haki za Watoto na Vijana Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na

Shirika la Taifa la Watoto (UNICEF) kwa lengo la kuwakumbusha Wajumbe kuhusu haki za watoto. Semina ilisisitiza kuhusu namna ambavyo kundi hili (watoto) muhimu katika jamii lina haki zinazopaswa kuzingatiwa na kulindwa na makundi mengine katika jamii.

Aidha, Wajumbe waliaswa kutumia nafasi yao ya uwakilishi na jukumu la kutunga sheria kuhakikisha wanaishawishi jamii kuhusu umuhimu wa kutambua, kuzingatia na kulinda haki za watoto. Mionganini mwa haki hizo ni kuishi, kuperdwa, kusilikizwa, kupata huduma muhimu za elimu, afya na lishe.

Wajumbe wa Kamati walikumbushwa kwamba, iwapo watatekeleza kikamilifu jukumu la kutunga sheria kwa jicho la kumlinda mtoto ni wazi watasaidia kupunguza au kuondoa kabisa wimbi la watoto wa mitaani ambao huishi katika mazingira magumu, na hivyo kujenga vizazi bora kwa manufaa ya taifa letu.

**(b) Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute)**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) kwa ajili ya kuwajengea uelewa Wajumbe wa Kamati juu ya uongozi binafsi (personal leadership); pamoja na uongozi na wajibu wa kiongozi kwenye dola.

Semina ilieleza maana ya kiongozi, sifa za kiongozi bora na mwenendo ambao kiongozi anapaswa kuonesha katika taasisi anayoiongoza na pia katika jamii inayomzunguka. Aidha, Wajumbe wa Kamati waliaswa kuepuka kujingiza katika mwenendo na kutenda mambo ambayo yanaweza kuwashushia hadhi katika jamii.

Wajumbe walishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuweka utaratibu wa kisheria ambao utawezesha viongozi wanaoteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali na jamii, kuhudhuria mafunzo yanayotolewa na taasisi ya Uongozi kabla ya kuanza kutumikia nyadhifa walizopewa.

**2.2.7 Ziara za Ukaguzi wa Miradi**

**Utekelezaji wa Mradi wa Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project) katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Miji ya Kimkakati (Tanzania Strategic Cities Project) unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Duni, katika Halmashauri za Maji Matano (5) ya Mwanza, Tanga, Arusha, Mbeya na Dodoma; na katika halmashauri za manispaa tatu (3) ambazo ni Mtwara/Mikindani, Kigoma/Ujiji na Illemela. Mradi una lenga kuimarisha na kuboresha huduma za msingi katika jamii ambazo ni pamoja na:-

(a) Kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara, madampo ya kisasa, masoko, stendi za mabasi, vituo ya magari na mizigo, mifereji ya maji ya mvua, sehemu za mapumziko na vizimba vya kuhifadhi taka; na

(b) Kujenga uwezo wa taasisi katika kutoa huduma hususan katika kujenga misingi ya uchumi wa wananchi, kuwezesha utekelezaji wa uendelezaji wa mipango miji, kuimarisha ukusanyaji wa taka ngumu na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri.

Katika Jiji la Dodoma Mradi huu unatekeleza ujenzi wa soko la kisasa na stendi kuu ya mabasi katika eneo la Nzuguni; eneo la mapumziko (recreational area) katika eneo la Chinangali, dampo la taka katika Kijji cha Chidaya, kituo cha maegesho ya malori eneo la Nala na ujenzi wa kilomita 68.36 za barabara za lami. Miradi yote hiyo inakadiriwa kuwa na thamani ya takribani **shilingi bilioni 178.44**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi ya ujenzi wa stendi kuu ya mabasi na soko la kisasa katika eneo la Nzuguni ambayo utekelezaji wake ulikuwa katika hatua za mwisho kabla hajiazinduliwa rasmi na kuanza kutoa huduma.

Mradi wa ujenzi wa Stendi Kuu ya Mabasi unatekelezwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 60, kwa gharama ya **shilingi bilioni 24.03**. Inatarajiwaa kuwa stendi hiyo itakuwa na uwezo wa kuhudumia mabasi 100 yanayoshusha na kupakia abria kwa wakati mmoja, maegesho ya mabasi 150, magari binafsi 600 na taxi 250 kwa wakati mmoja, na jengo la abiria (waiting lounge) lenye uwezo wa kubeba abiria 6,000 kwa wakati mmoja watakaokuwa wamekaa. Aidha, kutakuwa na jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria 80 wenye hadhi

maalum (VIP Lounge), vizimba vya biashara 60, migahawa na maduka kwa ajili ya kutoa huduma kwa abiria. Inaaminika stendi hii itakapokamiliika itakuwa kubwa na ya kisasa kuliko stendi za mabasi zote katika eneo la Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa soko la kisasa, mradi huu unatekelezwa katika eneo lenye ukubwa wa ekari 27 kwa gharama ya **shilingi bilioni 14.65**. soko hili ambalo limepewaji jina la "**Soko la Ndugai**" litakuwa na uwezo wa kuhudumia Wafanyabiashara 400 wa jumla na rejareja, kuegesha malori 30 wakati wa kupakia na kushusha mizigo kwa wakati mmoja, kuegesha magari mengine 600 kwa wakattimoja, vizimba 172 vya biashara za bidhaa za mashambani, machinjio ya kisasa, maduka, na maeneo ya kupangisha wafanyabiashara wa bidhaa za viwandani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua madhubuti ambazo Serikali inazichukua ili kubadilisha sura ya Jiji la Dodoma kwa uboreshaji wa miundombini. Hatua hiyo itarahisisha huduma za usafiri, uuzaaji na ununuzi wa biadha na mifumo ya maji, na itaboresha madhari ya Jiji la Dodoma kwa kulifanya liwe na hadhi ya Mji Mkuu wa Serikali, na mionganoni mwa maji ya kisasa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla.

## 2.2.8 Muswada wa Sheria

**Mheshimiwa Spika**, uileta Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao wa Mwaka 2019 (The e-Government Act, 2019) kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ili iweze kuufanya kazi.

Muswada huu ulipendekeza kutungwa kwa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli za Serikali Mtandao. Aidha, mamlaka hii itachukua nafasi ya iliyokuwa Wakala wa Serikali Mtandao (e-Government Agency) ambayo ilianzhishwa mwaka 2012 chini ya Sheria ya Wakala za Serikali, Na. 3 ya Mwaka 1977, Sura 245 na Kanunizake.

Kamati ilitimiza wajibu wake wa kushughulikia Muswada huo kati ya Tarehe 21 hadi 26 Agosti, 2019 ambapo ilifanya uchambuzi wa kitaalam ulioboresha Muswada huo kwa kuzingatia maelezo na hoja zilizowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, kuhusu vifungu vya Muswada, hoja za Wadau mbalimbali na kufanya tathmini na kuandaa maoni ambayo yalilisa idia Bunge kutunga Sheria ya Serikali Mtandao iliyokidhi viwango.

**Mheshimiwa Spika**, kutungwa kwa sheria hii kuliwezesha nchi yetu kuondokana na Wakala wa Serikali Mtandao ambayo ilitekeleza zaidi jukumu la ushauri badala ya usimamizi. Hivyo, kuwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ni kuwa na chombo cha kisheria ambacho kitahakikisha Sera, Sheria, Kanuni Viwango na miongozo kuhusu Serikali Mtandao vinazingatiwa kikamilifu katika taasisi za umma kwa lengo la kurahisisha matumizi ya Serikali Mtandao katika kuongeza ufanisi na ubora wa huduma za Serikali zinazotolewa kuitia mfumo huu.

Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha usalama wa Serikali Mtandao unazingatiwa kwa kiwango cha juu kwani ni eneo muhimu sana na iwapo litavamiwa linaweza kukwamisha shughuli zote za Serikali zinazotekeliza kwa njia ya mtandao. Aidha, mamlaka iwezeshe kifedha na kiufundi ili iweze kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanayotokea duniani.

## SEHEMU YA TATU

### 3.1 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelawa katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake. Maoni hayo ni haya yafuatayo: -

#### (a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

- i. Kiasi cha wa fedha kinachotengwa kwa TARURA ni kidogo sana ikililinganishwa na mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inazozihudumia;
- ii. Mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambaao TARURA inaupata kutoka Mfuko wa Barabara (RF) ni mdogo hivyo unapaswa kuongezwa;
- iii. Upungufu wa watumishi, uhaba wa ofisi na vitendea kazi unaathiri utendaji wa TARURA;
- iv. Iwapo Ukosefu wa sheria ndogo ndogo kwa lengo la kulinda na kuzuia uharibifu wa barabara zinazosimamiwa na TARURA kunachangia matumizi yasiyo sahihi ya barabara;
- v. Matumizi ya force account katika ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari nchini yanapunguza ghamama na hivyo kuokoa fedha nyngi. Hata hivyo, ukarabati huo usiposimamiwa na wataalam (Wahandisi) unaweza kutekelezwa chini ya kiwango;
- vi. Utamaduni wa kukarabati majengo na miundombinu ya Shule za Sekondari na taasisi nyagine za Serikali utawezesha majengo na miundombinu hiyo kudumu kwa muda mrefu;
- vii. Miradi ya Soko la Kisasa, Stendi Kuu ya Mabasi, Kituo cha Mapumziko na Kituo cha Maegesho ya Malori inayotekelawa kupitia Mpango wa Miij ya Kimkakati (TSCP), italeta tija na thamani halisi ya fedha "value for money" iwapo itasimamiwa vizuri na kuendeshwa kitaalam;
- viii. Kupatikana kwa Mto Huduma Kamili (Service Provider) ambaye atakuwa na idadi ya mabasi inayohitajika kutasaidia kuboresha huduma ya usafiri kwa jiji la Dar es Salaam kupitia DART;
- ix. Kukosekana kwa Sheria mahususi ya DART kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Wakala huo. Aidha, Wakala umekosa kanuni za kusimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya miundombinu;
- x. Serikali itengeneze barabara ya Ihumwa – Hombolo (km 27) kwa kiwango cha lami ili kupunguza uharibifu wa vyombo vya usafiri unaosababishwa na ubovu wa barabara hiyo;
- xi. Serikali iwezeshe chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo kujenga uzo ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya chuo kutoka kwa wananchi wanaoishi jirani, na kuimarisha hali ya usalama;
- xii. Sheria ya Shirika la Masoko Kariakoo ni ya siku nyngi, ikifanyiwa marekebisho itasaidia kuondoa upungufu uliopo ambaao unakwamisha shirika hilo kutekeleza majukumu yake na kuijendesha kwa tija; na
- xiii. Hatua ya Serikali kununua mashine za kukusanya mapato za kielektroniki (POS)

7227 na kuzigawa kwa halmashauri zote nchini kutasaidia kuimarisha ukusanyaji na udhibiti wa mapato;

**(b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

(i) Hatua ya Serikali kuanzisha Mfuko Endelevu wa Urasimishajji wa Wilaya (*District Revolving Fund*) kwa lengo la kusaidia halmashauri kutekeleza urasimishajji itafanikiwa iwapo fedha za kutosha zitatalewa na kusimamiwa vizuri;

(ii) Bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) inaathiri jithada za kuongeza wigo ili kufikia maeneo mengi zaidi nchini;

(iii) Hatua ya Halmashauri za wilaya chache (28) kumi liki ajenda ya urasimishajji inayotekelizwa na MKURABITA

inaonesha ni jinsi gani viongozi wa halmashauri nyinginchi hawajaelewa vya kutosha umuhimu wa MKURABITA au hawana utashi wa kutekeleza mpango huo katika maeneo yao;

(iv) Hatua ya Taasisi ya Uongozi kushirikiana na Viongozi Wastaafu wa Kitaifa kuandika na kuchapisha vitabu vya wasifu (*autobiography*) wao, ni jambo la kupongezwa kwani litasaidia kuhamasisha viongozi wengine kujitekeza na kuandika vitabu. Aidha, utaratibu huo utasaidia kuweka kumbukumbu za viongozi hao kwa vizazi vijavyo;

(v) Iwapo mfumo wa malipo wa kielektroniki (e-payment system) utatumia kikamilifu na TASAF kufanya malipo ya ruzuku kwa kaya maskini, utaongeza tija kutokana na uwazi na kuchukua muda mfupi;

(vi) Hatua ya Serikali kutochangia kikamilifu katika mpango wa kunusuru kaya maskini kunafanya mpango kutegemea zaidi fedha za wahisani;

(vii) Iwapo TASAF itafikia asilimia 30 ya viji, mitaa na shehia ambazo hazijafikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini, itaondoa malalamiko kutoka kwa wananchi wa maeneo hayo;

(viii) Hatua ya Serikali kuhamishia iliyokuwa Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtando (TaGLA) katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), ilenge kuboresha na kusambaaza huduma za mafunzo kwa njia ya mtando badala ya kuzihafifisha;

(ix) Serikali iimarishe suala la usalama wa Serikali Mtando ili kuzuia au kudhibiti uvamizi wowote unaoweza kukwamisha shughuli za Serikali zinazotekelizwa kwa njia ya mtando; na

(x) Serikali iiwezeshe kifedha na kiutaalam Mamlaka ya Serikali Mtando ili iende sambamba na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano duniani.

### 3.4 Mapendeleko

#### 3.2.1 Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (TARURA)

**KWA KUWA,** TARURA inakabiliwa na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi, ofisi na vitendea kazi vingine;

**NA KWA KUWA;** halii hiyo inaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya TARURA na hivyo kusababisha ishindwe kutekeleza kikamilifu matengenezo ya miundombinu ya barabara inazosimamia;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali: -

i. Kutenga bajeti ya kutosha na kutoa fedha kikamilifu ili kuiwezesha TARURA kutimiza majukumu yake kikamilifu ya kuhudumia mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inaousimamia nchini. Miongoni mwa njia za kuongeza fedha kwa TARURA ni kuongeza mgawo wa fedha za Mfuko wa Barabara (RF) kutoka asilimia 30 ya sasa hadi asilimia 50. Aidha, Kamati iliyopewa jukumu la kupendekeza kuhusu jambo hilo ni vyema ikalikamilisha haraka ili kuruhusu utekelezaji; na

ii. Kuendelea kuiwezesha TARURA kupata ofisi katika maeneo mbalimbali ya nchi, magari na vitendea kazi vingine pamoja na watumishi ili kupunguza uhaba uliopo

### 3.2.2 **Mkakati wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari**

#### 3.2.2.1 **Matumizi ya Force Account**

**KWA KUWA**; matumizi ya force account katika ukarabati wa baadhi ya miundombinu na majengo ya Shule Kongwe za Sekondari nchini yameonesha mafanikio makubwa kwa kupunguza gharama na hivyo kuokoa fedha nyangi;

**KWA KUWA**, bado baadhi ya taasi za umma hazijsiona umuhimu wa kutumia utaratibu huu wa force account katika utekelezaji wa miradi yake na badala yake kuendelea kutumia kandarasi ambazo gharama yake ni kubwa;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha taasi za umma zinatumia utaratibu wa force account katika utekelezaji wa miradi ili kuokoa fedha na kuzielekeza katika matumizi mengine. Aidha, Serikali ihakikisha kunakuwa na usimamizi wa kitaalamu katika miradi inayotekelwa kwa force account ili kuhakikisha inazingatia viwango vya ubora vinavyotakiwa.

#### 3.2.2.2 **Utamaduni wa kufanya ukarabati wa mara kwa mara**

**KWA KUWA**, ubovu na uchakavu wa miundombinu yakiwemo majengo ya shule kongwe za sekondari za Serikali vimesababishwa na kukosekana kwa utamaduni wa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo ya ubovu na uchakavu imesababisha Serikali kutumia fedha nyangi kwa ajili ya matengenezo na ukarabati ili kurejesha miundombinu hiyo katika ubora unaotakiwa;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali na taasi zake kujenga utamaduni wa kufanya matengenezo na ukarabati wa mara kwa mara katika miundombinu na majengo yake, ili kuepusha ubovu na uchakavu ambao ukarabati wake hugharimu fedha nyangi ambazo zingetekeliza shughuli nyagine.

#### 3.2.3 **Miradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP)**

**KWA KUWA**, miradi ya vitega uchumi vya Soko la Kisasa, Stendi Kuu ya Mabasi, Kituo cha Mapumziko na Kituo cha Maegesho ya Malori, inayotekelwa kupitia Mpango wa Miji ya Kimkakati (TSCP), katika Jiji la Dodoma imegharimu fedha nyangi ambazo ni mkopo;

**NA KWA KUWA**, miradi hiyo inahitaji kusimamiwa vizuri ili iwe na tija kwa kutoa huduma iliyokusudiwa kwa jamii, kuonesha thamani halisi ya fedha "value for money"

na kuzalisha fedha ambazo zitachangia kulipo mkopo na kufanya maendeleo mengine;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha Uongozi wa Jiji la Dodoma unaendesha vitega uchumi hivyo kwa ufanisi na faida kwa kuajiri na kuruhusu Mtaalam Mshauri atekelze majukumu yake ya kitaalam kwa mujibu wa makubaliano bila kuingiliwa;

### 3.2.4 Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)

#### 3.2.4.1 Kukosekana kwa Mto Huduma Kamili

**KWA KUWA,** tangu Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam ulipoanza kutoa huduma ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam Mei, 2016 umekuwa ukitimia Mto Huduma wa Mpito "Interim service provider";

**NA KWA KUWA,** mto huduma huyo ameshindwa kutoa huduma kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na uchache wa mabasi (140 kati ya 305 yanayohitajika) aliyonayo, pamoja na kukosa mfumo madhubuti wa ukusanyaji nauli;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali iharakishe mchakato wa kupatikana kwa Mto Huduma Kamili (Service Provider) ambaye atakuwa na idadi ya mabasi inayohitajika ili aweze kuboresha huduma ya usafiri katika jiji la Dar es Salaam na hivyo kuwapunguzia wananchi adha ya msongamano wanayoipata;

#### 3.2.4.2 Kukosekana kwa Sheria mahususi ya DART

**KWA KUWA,** Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) hauna sheria mahususi ya kusimamia utendaji na utekelezaji wa majukumu yake;

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa sheria hiyo mahususi kunaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala, ikiwa ni pamoja na kukosa kanuni za kusimamia na kudhibiti matumizi mabaya ya miundombinu yake;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuiwezesha DART kupata sheria mahususi ambayo itasaidia kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya wakala. Aidha, sheria hiyo itawezesha kutungwa kwa Kanuni za DART ili kusimamia na kudhibiti uvamizi na matumizi mabaya ya miundombinu ya wakala.

### 3.2.5 Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) Hombolo

#### 3.2.5.1 Ubovu wa barabara ya Ihumwa – Hombolo

**KWA KUWA,** barabara ya Ihumwa – Hombolo (kilomita 27) ni mbovu sana;

**NA KWA KUWA,** ubovu huo unasababisha uharibifu na uchakavu wa vyombo vyaa usafiri vyaa chuo na wafanyakazi wa chuo na hivyo kugharimu fedha nyingi katika matengenezo;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kupunguza uharibifu wa vyombo vyaa usafiri unaosababishwa na ubovu wa barabara hiyo.

### 3.2.5.2 Kukosekana kwa uzio kuzunguka eneo la chuo

**KWA KUWA**, hakuna uzio kuzunguka enel la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inaweza kuchangia maeneo ya chuo kuvamiwa na wananchi wanaishi jirani na chuo na kuhatarisha usalama wa wanafunzi na malii za chuo na wanafunzi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukiwezesha chuo hicho kujenga uzio kuzunguka maeneo yake ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

### 3.2.6 Upungufu katika Sheria ya Shirika la Masoko Kariakoo

**KWA KUWA**, Sheria ya Shirika la Masoko ya Kariakoo ni ya siku nyingi (tangu mwaka 1974) na hivyo kubainika kuwa na upungufu mwingi;

**NA KWA KUWA**, upungufu huo unaathiri utendaji na utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo na kukwamisha uwekezaji wa vitega uchumi;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuanza mchakato wa kuwasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya sheria hiyo ili kuliwezesha Shirika la Kariakoo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuijendesha kwa tija kulingana na mazingira ya kisasa.

### 3.2.7 Mpango wa Kurasimisha Rasiliimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

#### 3.2.7.1 Kuanzishwa kwa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya (District Revolving Fund)

**KWA KUWA**, Serikali imanzisha Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya (District Revolving Fund) kwa lengo la kusaidia halmashauri kutekeleza urasimishaji kwa kuchangia ghama;

**NA KWA KUWA**, ufanisi wa utekelezaji wa mfuko huo utategemea fedha ambazo Serikali itaweka katika benki kama dhamana ya mikopo kwa halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya k u t e k e l e z a zoezi la urasimishaji;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali ihakikishe inatenga na kutoa fedha za kutosha za dhamana ili kuwezesha Halmashauri nyngi kukopa katika mfuko huo na kutekeleza zoezi la urasimishaji kwa ufanisi;

#### 3.2.7.2 Bajeti finyu inayotengwa na Serikali

**KWA KUWA**, bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Rasiliimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) inaatirii jitihada za kuongeza wigo ili kufikia maeneo mengi zaidi nchini;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inasababisha wananchi wa maeneo mengi kutofikiwa na MKURABITA na hivyo kukosa fursa ya kurasi misha ardhi na biashara zao;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo ya MKURABITA ili kuwezesha zoezi la urasimishaji kuwfikia wananchi wengi na kuwapa fursa ya kurasi misha ardhi na biashara zao na kuzitumia kujikwamua kiu chumi.

#### 3.2.7.3 Halmashauri chache kumiliki ajenda ya urasimishaji

**KWA KUWA**, Halmashauri 28 (sawa na asilimia 15) ndiyo zimepokea na kumiliki ajenda ya urasimishaji wa ardhi na biashara inayotekeliza na MKURABITA;

**NA KWA KUWA**, hatua hiyo inaashiria ni jinsi gani viongozi wa halmashauri nyingi nchini ama hawajaelewa vya kutosha umuhimu wa MKURABITA au hawana utashi wa kutekeleza mpango huo katika maeneo yao;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuweka mkakati wa makusudi wa kisheria utaohakikisha halmashauri zote nchini zinamiliki ajenda ya urasimishaji ili kuwezesha wananchi wa maeneo yao kutumia fursa hiyo kurasi misha ardhi na biashara zao na hivyo kujikwamua kiuchumi.

### 3.2.8 Usalama wa Serikali Mtandao

**KWA KUWA**, Serikali imeendelea kuhimiza na kujikita katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utekelezaji wa shughuli zake na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuanzisha Mamlaka ya Serikali Mtandao;

**NA KWA KUWA**, kutokana na umuhimu wake eneo hilo linaweza kuvamiwa na wadukuzi na wahalifu wa kimtandao na hivyo kuathiri au kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali, utoaji wa huduma kwa wananchi na pia upotevu wa rasimili fedha, taarifa muhimu na muda;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha inaimarisha usalama wa Serikali Mtandao ili kuzuia au kudhibiti uvamizi wowote unaoweza kukwamisha Serikali kutekeleza shughuli zake kwa njia ya mtandao pamoja na kuwashudumia wananchi.

Aidha, Serikali ihakikishe inaiwezesha kifedha na kiutaalam Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ili iende sambamba na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Duniani.

#### 3.2.8.1 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Mfumo wa malipo ya kielektroniki (e-payment)

**KWA KUWA**, TASAF imeanza majaribio ya malipo ya ruzuku kwa kaya masikini kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (e-paymanet) katika maeneo ya utekelezaji 16;

**NA KWA KUWA**, majaribio hayo yameonesha mafanikio makubwa kwa ufanisi, uwazi, malipo kufika kwa wakati na kwenda moja kwa moja kwa walengwa;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuhakikisha TASAF inakamilisha maandalizi na kuanza kutumia mfumo huo kufanya malipo kwa walengwa wote wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini nchini.

#### 3.2.8.2 Maeneo ambayo hayajafikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini

**KWA KUWA**, asilimia 30 ya maeneo (vijiji/mitaa/shehia 5,693) nchini haikuungizwa kwenye awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini,

**NA KWA KUWA**, hali hiyo inawanyima walengwa kati ya **355,000 – 426,000** wenye sifa katika maeneo hayo fursa ya kunufaika na mpango huo ili waweze kupunguza kiwango cha umaskini kutokana na shughuli za kiuchumi,

**KWA HIYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali itumie kikamilifu mkopo wa riba nafuu wa **shilingi trillioni 1.035** iliopata kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa sehemu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini na kuzifika Halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na wilaya zote za Zanzibar, na hivyo kuwapawananchi wote wenye sifa fursa ya kunufaika.

### 3.2.8.3 Mchango wa Serikali katika Mpango wa kunusuru Kaya maskini

**KWA KUWA**, katika kipindi cha miaka sita na nusu ya bajeti kuanzia 2013/2014 hadi 2019/2020 (Januari 2020) Serikali iliweza kuchangia **shilingi bilioni 8.11** tu katи ya **shilingi bilioni 70.01** zilizoidhinishwa na Bunge;

**NA KWA KUWA**, kiasi hicho sawa na asilimia 11.58 ya fedha iliyoidhinishwa ni kidogo sana na hakifiki theluthi moja (1/3) inayopaswa kuchangiwa na Serikali na hivyo kuufanya mpango wa kunusuru kaya maskini kutegemea zaidi fedha za mkopo na msaada kutoka kwa wahisani;

**HIVYO BASI**, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuzingatia makubaliano ya uchangiaji katika mpango huo ambayo ni theluthi moja (1/3) kwa Serikali na 2/3 kwa wahisani.

## SEHEMU YA NNE

### 4.1 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, ninapohitisha taarifa hii nikumbushe kidogo kuhusu dhana ya ugatuzi wa madaraka au upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*Devolution by Decentralization - D by D*) ambayo msingi wake ni Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Utekelezaji wa dhana hiyo ya kikatiba kupitia sera iliyotungwa mwaka 1998 umesaidia kusogezwa kwa huduma karibu na wananchi, na kuwashirikisha katika kutathmini, kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali kwa manufaa yao. Leo sote tu mashahidi kwa namna wananchi kwa kushirikiana na Serikali wanavyoshiriki katika shughuli za maendeleo kama ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, shule za msingi na sekondari, miradi ya maji, n.k kwa kuchangia nguvu zao na fedha.

**Mheshimiwa Spika**, ni kutokana na manthiki hiyo Kamati inashauri Serikali kuendelea kuunga mkono juhudzi za Wananchi kwa kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka kikamilifu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudzi wanazonesha katika kuchangia miradi ya kijamii na maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. George Huruma Mkuchika, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mhe. Seleman Said Jafo (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara (Mb) na Naibu Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, nawashukuru watendaji wote wa ofisi ya Rais – TAMISEMI waki ongozwa

na Mhandisi Joseph Nyamuhanga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Dkt. Laurian Ndumbaru, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee niwashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, natambua na kuthamini mchango wao adhimu na kujtoa kwao kikamilifu katika kuhakikisha Kamati yetu inatekeleza wajibu wake kikamilifu. Iwapo wajumbe wasingejitoa kikamilifu na kwa weledi kushirikiana nasi viongozi wa kamati, ni hakika ufanisi usingepatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kamati katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Kwa heshima kubwa ningetamani kuwataja majina yao, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
4. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb
7. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb
8. Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb
9. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, Mb
10. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb
11. Mhe. Venance Methusela Mwamoto, Mb
12. Mhe. Anna Joram Gidanya, Mb
13. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
14. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
15. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
16. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
17. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
18. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
19. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
20. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
21. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
22. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
23. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
24. Mhe. Mansoor Hilan Shaniff, Mb
25. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanalby Mohamedali Raza, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote cha ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Pia, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, na Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerald Magili.

Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Eunike Shiri, wakisaidiwa na Ndg. Modesta Kipiko, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelizwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hiso, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**Jasson S. Rweikiza**  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA**  
**SERIKALI ZA MITAA**  
4 FEBRUARI, 2020

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za mitaa; hoja imeungwa mkono.

#### MWONGOZO WA SPIKA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nimepata ki-memo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba CHADEMA tuna nafasi mbili CUF wana nafasi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti unajua leo tunakamati tatu, na kamati zote ni muhimu, na Waheshimiwa Wabunge wana haki ya kupata fursa ya kuchangia. Natambua unaweza ukasema mmetoa muda mchache kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge kiti chako kina nafasi ya kuongeza muda wa ziada mpaka pale shughuli za Bunge zitakapo kamilika. Hatuwezi kuwanyima Wabunge hasa wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoa maoni yao kwa Kamati muhimu za leo za Katiba na Sheria, Sheria Ndogo, Kamati ya Utawala inayohusu utawala bora mambo ya serikali ya mtaa kwa sababu ya kisingizio cha muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimesema na una jukumu la kuongeza muda; tunaomba mwongozo wako, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ipewe nafasi za nyongeza hili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini, tumetoka kuwa tunajadili kamati mbili upande wa CHADEMA tunapata nafasi mbili CUF wanapata nafasi ya ziada. Leo tunajadili kamati tatu mnatoa CUF nafasi moja CHADEMA nafasi mbili. Tunaomba mwongozo wako haki itendeke kama inavyotendeka kwa kambi ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther umeeleweka naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge ratibu zetu za Bunge zinaenda kwa mujibu wa utaratibu, kwa siku ya leo kwa ratiba ilivyo nafasi za CHADEMA ni mbili na CUF ni moja kwahiyko kama manataka kuongea zaidi mgawane dakika kazi itakwenda tuendelee na mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria karibu.

**MHE MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni taarifa yangu ya mwisho kwa Bunge hili la kumi na moja, taarifa ya mwaka ya mwisho, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeneweza kusimama mbele ya Bunge lako hili

Tukufu ukizingatia kwamba hiki ni kipindi changu cha pili kama mwenyekiti wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge katika Bunge hili la kumi na moja. Nawashukuru wapiga kura wangu wa jumbo la rufiji kwa kuendelea kuwa na imani kubwa na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha taarifa hii kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo na Majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6 (2) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ni mionganini mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta, ambayo, imepewa jukumu la kusimamia Wizara nne ambazo ni: Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shughuli Zilizotekeleza na Kamati; Kutembea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Katika kutekeleza kanuni 98(1) kanuni za Bunge mnamo mwezi Machi, 2019 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa mahakama nchini katika mikoa ya Mbeya Njombe, Manyara na Arusha.

Aidha kwa kibali chako Kamati ilifanya ziara maalumu kwa ajili ya kutembelea na kukagua ujenzi wa Mahakama kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utekelezaji wa ziara hizo pamoja na maswali yaliyobainika pamoja na maoni ya Kamati ni kama yaliyvoainishwa na Kamati katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Miswada ya Sheria. Katika kipindi cha Februari, 2019 hadi januari, 2020 kamati hii ilishughulikia jumla ya miswada ya sheria mitano iliyofanywa marekebisho katika jumla ya sheria 51 zinazohusu sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Muswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) ya Mwaka 2019 [*The written laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2019*]; ambaao ulifanya marekebisho katika sheria nane ili kuondoa upungufu ambaao ulibainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa taasisi inayosimamia utekelezaji wa sheria hizo. Orodha ya sheria hizo ni kama ilivyoainishwa katika taarifa hii.

b) Muswada ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.4) ya Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2019*]; ambaao ulifanya marekebisho katika sheria ya kumi na moja ili kuondoa upungufu ambaao ulibainika wakati wa utekelezaji wa sheria hizo. Orodha ya sheria hizo ni kama ilivyoainishwa kwenye taarifa hii.

c) Muswada wa Sheria ya marekebisho mbalimbali (Na. 5) ya Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.5) Bill, 2019*] ambaao ulifanya marekebisho katika sheria saba ili kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yilibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika sheria husika. Orodha ya sheria hizo ni kama zilivyoainishwa kwenye taarifa hii.

d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 7) ya Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.7) Art, 2019*] ambaao ulifanya marekebisho katika sheria ya kumi na moja ili kuondoa mapungufu mbalimbala ambayo

yilibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika sheria husika. Orodha ya sheria hizo ni kama zilivyoainishwa kwenye taarifa hii.

e) Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 8) ya Mwaka 2019 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Arts, (No. 8), 2019*] ambao ulifanya marekebisho katika sheria kumi na nne ili ziendane na mabadiliko ya wakati kutatua changamoto mbalimbali iliyojiteza wakati wa utekelezaji wa sheria hizo. Orodha ya sheria hizo ni kama zilivyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako hili Tukufu kuwa Kamati ilitegeleza wajibu wake wa kikanuni kwa uaminifu weledi na ufanisi mkubwa katika kulisaidia Bunge kutunga Sheria Jumuhishi kupitia muswada husika. Aidha, Kamati inajivunia kuwa sehemu ya mabadiliko makubwa ya kisheria hapa nchini yanayoendelea kutekelezwa na Serikali ya awamu ya tano kwa maendeleo ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupokea na Kujadili Taarifa ya Utekelezaji. Katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020 Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili taarifa nane za utekelezaji wa majukumu ya wizara inayosimamia pamoja na taasisi zake ambazo taarifa sita ziliwasilishwa na taasisi zilizochini ya ofisi ya Waziri Mkuu, na taarifa mbili kutoka taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama zilivyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa mwenyekiti, baada ya kujadili taarifa hizo kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yalifanuliwa kwa kina katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa za Wizara Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Kifungu 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge mwezi Machi, 2019 Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti na Wizara zilizosimamia kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kufanya ulinganisho na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Matokeo ya uchambuzi yaliyofanywa na Kamati yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati. Kamati ilibaini baadhi ya changamoto zilizoikibili ofisi ya Waziri Mkuu kwenye uratibu usimamizi wa wa masuala ya uwekezaji nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ni kukosekana kwa ushirikiano wa uratibu mionganoni mwa taasisi za Serikali. Hii inatokana na kukosekana kwa mipango na mikakati madhubuti inayoshabihiana kati ya Sekta zinazohusika, hali ambayo imeleta mitazamo tofauti mionganoni mwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi;

(ii) Ni ucheleweshaji wa huduma kwa wawekezaji kama vile vibali na leseni katika baadhi ya wizara na taasisi za Serikali kwa sababu ya ukosefu wa mfumo wa TEHAMA katika kuhakikisha utoaji maamuzi na mawasiliano;

(iii) Upungufu wa maeneo yenye miundombinu muhimu na wezeshi katika ngazi za halmashauri na wilaya na mikoa nchini. Hali hii imebainika kuathiri miradi ya sekta za kilimo, uchimbaji wa madini, viwanda na utalii ambayo iko mbali na maeneo yenye miundombinu;

(iv) Ugumu katika upatikanaji na umilikishwaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hali hii imebainika kusababishwa na utaratibu na uhaulishwaji wa ardhi kuchukua muda mrefu, kutoka ardhi ya kijiji kuwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji;

(v) Muingiliano wa Taasisi za Udhibiti wa Biashara na Tozo za Leseni na Vibali kwa sababu ya wingi wa taasisi za udhibiti wa biashara. Hali hii imechangia kuongeza ghamama za uendeshaji wa shughuli za uwekezaji hapa nchini;

(vi) Uwepo wa urasimu wa utoaji wa huduma, hali hii imesababishwa na baadhi ya watumishi wa taasisi za Serikali katika kuwahudumia wawekezaji kwa kushindwa kutoa huduma bora za haraka ikiwemo na ucheleweshaji maamuzi ya uwekezaji;

(vii) Ushiriki mdogo wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati inayotekelizwa hapa nchini. Hali hii inathibitishwa na ushiriki mdogo wa makampuni ya kitanzania katika miradi mbalimbali ya kimantiki inayoendelea kutekelezwa hapa nchini.

(viii) Uelewa tofauti kuhusu dhana na fursa za uvezeshaji wananchi kiuchumi kutokana na ufinyu wa elimu kuhusu fursa na jinsi ya ushiriki wa watanzania kwenye hizo fursa;

(ix) Mikoa na wilaya kushindwa kuratibu ipasavyo majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi husika na hivyo kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuchelewesha uwekezaji katika maeneo hayo;

(x) Kukosekana kwa matawi ya Tanzania Private Sector Foundation (TPSF) katika ngazi za mikoa na wilaya, hali ambayo husababisha shughuli nydingi za uratibu wa sekta binafsi kukasimiwa kwa TCCIA ambayo huweka maslahi yake mbele kuliko maslahi ya Sekta binafsi kwa kujumuisha wafanyabiashara ambao siyo wanachama wa TCCIA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kibali cha Mheshimiwa Spika tarehe 24 Januari, 2020 kamati ilifanya ziara ya kikazi Mkoani wa Iringa kwa ajili ya kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa programu ya kitaifa ya Usajili wa Vizazi na Vifo inayoratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria kuititia RITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejionea na imejidhihirishia utekelezaji wa programu hiyo muhimu kwa kubaini ongezeko kubwa la usajili wa watoto chini ya miaka mitano kwa kuwapatia vyeti vya kuzaliwa hapo hapo kwa haraka na pasipo upungufu wowote. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuheshimu umuhimu wa haki za mtoto wa kitanzania kupatiwa cheti cha kuzaliwa kama haki yake ya msingi itakayomuwezesha kufikia fursa mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, kamati inaipongeza na kulishukuru Shirika la UNICEF kwa kuwezesha utekelezaji wa programu hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kuwa, Serikali ijpange ili kupanua programu hiyo kutoka mikoa kumi na tano inayopata huduma hiyo hadi nchini ili watoto wetu wapate haki hiyo muhimu kwa ustawi wa maisha yao kama watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati; Ofisi ya Waziri Mkuu Uratibu Masuala ya Uwekezaji katika mikoa na wilaya. Kwa kuwa imebainika kuwepo kwa mikoa na wilaya zilizoshindwa kuratibu ipasavyo katika ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi husika, na kwa kuwa mikoa na wilaya kushindwa kuratibu majadiliano ya masuala ya biashara na uwekezaji inachelewesha na kukwamisha jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano kuchochaea uwekezaji wa viwanda kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Hivyo basi, kamati inaishauri Serikali kuanza kutekeleza mwongozo wa majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi ya mikoa na wilaya ili kutatua changamoto hiyo na kuchochaea uwekezaji katika ngazi za mikoa na wilaya nchini. hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, TPSF inakuwa na ofisi zake katika ngazi za mikoa na wilaya ili kuharakisha uratibu wake.

Kwa kuwa, masuala ya uwekezaji nchini yanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiusimamizi na kiuratibu mionganoni mwa taasisi husika za Serikali kama zilivyoainishwa na kamati kwa kupitia uchambuzi wa taarifa mbalimbali za Serikali,

Na Kwa Kuwa, changamoto hizo zinasababishwa na mfumo uliopo wa kitaasisi na kisheria unaoweza kuathiri mwenendo wa uwekezaji katika sekta mbalimbali na hivyo kukwamisha mipango ya Serikali kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Hivyo basi, Kamati inashauri kuwa Serikali ihakikishe inaongeza Vituo vya pamoja vya Usimamizi na Uratibu (One Stop Centers) kwenye maeneo mbalimbali ya kimkakati, ili kuziwezesha taasisi zote husika kuratibu kwa pamoja masuala ya uwekezaji kwa urahisi zaidi na kupunguza urasimu usiyo wa lazima ambao unaweza kukatisha tamaa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki mdogo kwa watanzania katika miradi ya kimkakati. Imebainika kuwa, Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) linakabiliwa na changamoto ya ushiriki mdogo wa wananchi katika miradi ya kimkakati ukilinganisha na ushiriki wa wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Na Kwa kuwa, ushiriki mdogo wa Wananchi kwenye miradi ya kimkakati unaweza kuathiri maendeleo ya nchi hapo baadaye kwa kuhamishia nje rasilimali za nchi kupitia wawekezaji kutoka nje ya nchi;

Hivyo basi, kamati inashauri Serikali kuwa, ihakikishe Baraza la Taifa la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi linashirikiana na taasisi za elimu pamoja na wadau wa maendeleo katika kuyajengea uwezo makampuni ya Kitanzania ili yaweze kushiriki katika miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa na Serikali hapa nchini. Aidha, baraza hilo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali liendelee kutoa elimu kuhusu fursa zilizopo na jinsi ya kuzifikia kupitia maonyesho mbalimbali na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa ofisi ya TIC.

Kwa kuwa, imebainika kuwa Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (TIC) kinakabiliwa na ufinyu wa ofisi kutokana na ongezeko la mahitaji ya nchi kwa sasa, ikiwemo upungufu wa rasilimali watu.

Na Kwa Kuwa, bila kituo hiki kupatiwa miundombinu wezesheji ya ofisi yenye kujitosheleza pamoja na wafanyakazi wakutosha inaweza kuathiri utekelezaji wa mipango ya utekelezaji kwa upande wa Serikali.

Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuwa TIC iwezesheji ili ianze na kukamilisha jengo la Jijini Dodoma lenye uwezo wa kutekeleza majukumu yake chini ya mfumo wa One Stop Centre, kwa kuwa na ofisi yenye kujumuisha ofisi zote zinazohusika katika masuala yote ya uwekezaji ili kuiwezesha ofisi hiyo kuwa na mazingira wezeshi ya kurahisisha uratibu wa masuala ya uwekezaji hapa nchini kwa kushirikiana na taasisi nydingine za Serikali kwa ufanisi zaidi. Hii ni pamoja na kuajiri wafanyakazi wa kutosha kwa kuzingatia vipaumbele vya kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Kamati imebaini uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuwa ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya vijana hapa nchini kutokana na uratibu mzuri unaotekeliza na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na Kwa Kuwa, uwepo kwa mahitaji makubwa ya vijana zaidi ya uwezo wa mfuko kunaweza kusababisha fursa hiyo isiwafikie vijana wengi.

Hivyo basi, kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya yafuatayo:-

(a) Kuona umuhimu wa kuongea Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili Mfuko huo uweze kuwafikia vijana wengi zaidi kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kudhihirisha uwezo mkubwa katika uratibu wa mfuko huo;

(b) Ongezeko hilo la Bajeti liwezeshe Serikali kupanua uwigo wa wanufaika wa Mfuko wa Vijana kwa kuanza kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali ya vijana yaliyosajiliwa na yenye mipango ya miradi yenye lengo la kuongeza ajira (CBO) na makampuni yaliyosajiliwa kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya kati na mikubwa ya kutoa ajira nyingi kwa vijana;

(c) Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane kwa ukaribu zaidi na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambao ndio yenye dhamana na halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kila halmashauri inawajibika kuratibu fedha zilizotolewa na Mfuko wa Vijana pamoja na asilimia 4% za fedha za halmashauri kwa kusimamia utekelezaji wa miradhi hiyo na marejesho yake kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa utoaji haki nchini. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata haki sawa mbele ya vyombo stahiki vya sheria na haki hiyo inatolewa kwa wakati.

Na Kwa kuwa, usimamizi wa utoaji haki nchini unategemea sana ufanisi wa taasisi husika zenye dhamana hiyo;

Hivyo basi, kamati inashauri taasisi husika zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza masuala ya msingi yafuatayo:-

(a) Mahakama iendelee kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wake iliyojiwekea wa kuhakikisha kila Hakimu au Jaji anayeshughulikia kikamilifu idadi ya mashauri husika kwa muda husika ili kuongeza imani ya wananchi kwa chombo hiki cha utoaji wa haki nchini;

(b) Serikali iendelee kuboresha Bajeti ya Fungu 55 la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 16 la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 19 la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Fungu 35 la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Serikali ione umuhimu wa kuboresha mazingira ya rasilimali watu chini, chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara na Vitengo vyote vya sheria kwenye taasisi zote za Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kutokana na mabadiliko makubwa ya mfumo wa kisheria yaliyotekeliza hivi karibuni kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati. Bunge lina dhamana kubwa ya kusimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya Mwaka 1977. Na kwa kuwa katika kutimiza jukumu hili Bunge hutumia kamati zake ambazo hutoa ushauri, mapendekezo na maelekezo mbalimbali kwa Serikali kuititia Wizara na Taasisi zake, hivyo kamati inaishauri Serikali kuititia wizara na taasisi zake kuendelea kupokea na kutekeleza ushauri na mapendekezo mbalimbali ya kamati na kutoa taarifa ya utekelezaji wa ushauri na mapendekezo hayo kila inapotakiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioutoa kwa kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi chake cha mwaka mmoja uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa wizara na taasisi ambazo kamati inasimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Kama walivyotambulia kwenye taarifa hii napenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Prof. Adelardus Kilangi na Watendaji wake wote kwa ushirikiano wao mkubwa kwa kamati pale walipohitajika kufika mbele ya kamati kwa ajili ya kuwasilisha hoja za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa wadau wa taasisi mbalimbali ambazo zimeshirikiana na kamati wakati wa kutekeleza majukumu katika kipindi chote cha Februari 2019 hadi Januari 2020 kama zilivyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza kufanikisha majukumu ya kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba majina yao yote yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao wa kufanikisha shughuli za kamati chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi ambao ni Ndugu Michael Chikokoto na Ndugu Gerald Sengano, Katibu wa Kamati Ndugu Stanslaus Kagisa na Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi ya kamati.

Aidha, nawashukuru Washauri wa Masuala ya Sheria Bungeni kwa namna bora walivyoshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. Ninaomba taarifa yangu yote yenyewe kurasa 46 iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa hoja, Baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizoteklezwa na Kamati yangu ya Katiba na Sheria, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya kamati naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee, kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli zilizoteklezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofij*)

**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA KATIBA NA  
SHERIA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI 2019 HADI JANUARI 2020 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

[Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**  
**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya

Mwaka, kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari 2020. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na ubora unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta ikiwemo Kamati ya Katiba na Sheria zina wajibu wa kuwasilisha Taarifa za Mwaka za shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari 2020 na imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo:-

- a) **Sehemu ya Kwanza** inatoa Maeleo ya Jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelawa;
- b) **Sehemu ya Pili** inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- c) **Sehemu ya Tatu** inabainisha maoni na mapendeleko ya Kamati; na,
- d) **Sehemu ya Nne** ni hitimisho la taarifa.

### 1.2 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 6 (2) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ni mionganini mwa Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta, ambayo, imepewa jukumu la kusimamia Wizara Tatoo ambazo ni:-

- a) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano),
- b) Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, ambapo kwa sasa inajumuisha pia masuala ya Uwekezaji; na
- c) Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati hii ni:-

- a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### 1.3 Njia na mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Ibara ya 96 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati za Kudumu za Bunge ni Mawakala wa Bunge na hivyo hutekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge. Kamati za Kudumu za Bunge huliwakilisha Bunge katika kuvisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zenyet kujidhi matakwa ya Katiba na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Njia hizo ni:-

- i) Vikao vya uchambuzi wa Bajeti za Serikali kwa Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.
- ii) Vikao vya kushughulikia Miswada ya Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) pamoja na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- iii) Kupokea maoni ya Wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge;
- iv) Ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoishia kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ili kujiridhisha kuhusu hatua za utekelezaji na ufanisi wake, kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotengwa na kupokelewa na Taasisi husika;
- v) Kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na
- vi) Kufanya ziara mbalimbali za kikazi kujionea hali hali ya utekelezaji wa baadhi ya Sheria, pamoja na Programu ili kuwataka Mawaziri wafafanue na kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyohitaji ufanuzi;
- vii) Kupata mafunzo ya Mradi wa LSP II na Mafunzo mengine mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbali za Serikali na Asasi za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge.

#### **1.4 Shughuli zilizotekeliza:**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

##### **1.4.1 Kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;**

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayozitaka Kamati za Bunge za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilitembelea na kukagua Miradi mbalimbali ya maendeleo ilio chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

##### **1.4.2 Kuchambua Miswada ya Sheria;**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 84 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati hii ilishughulikia Jumla ya Miswada ya Sheria Mitano (5) iliyofanya marekebisho katika Jumla ya Sheria Hamsini na Moja (51) zinazohusu Sekta mbalimbali kama ifuatavyo:-

##### **a) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) Wa Mwaka 2019 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2019,**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Nane (8) zifuatazo:  
i) Sheria ya Makampuni (Sura 212) (The Companies Act, (Cap. 212))

ii) Sheria ya Haki Miliki (Sura 218) (The Copyright And Neighbouring Rights Act, (Cap. 218));

- iii) Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (Sura 230) (*The Films And Stage Plays Act*, (Cap. 230);
- iv) Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali (Sura 56) (*The Non-Governmental Organizations Act*, (Cap. 56));
- v) Sheria ya Vyama vyta Kijamii (Sura 337) (*The Societies Act*, (Cap. 337));
- vi) Sheria ya Takwimu (Sura 351) (*Statistics Act*, (Cap. 351));
- vii) Sheria ya Uwakala wa Meli (Sura 415) (*Tanzania Shipping Agencies Act*, (Cap. 415)); na
- viii) Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini (Sura 318) (*The Trustee's Incorporation Act*, (Cap. 318)).

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulikusudia kufanya marekebisho katika Sheria Nane (8) zilizoainishwa ili kuondoa upungufu ambao ulibainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sheria hizo.

**b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) Wa Mwaka 2019 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.4) Bill, 2019;**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Kumi na Moja (11) ili kuondoa upungufu ambao ulibainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Orodha ya Sheria Kumi na Moja (11) zilizofanyiwa Marekebisho katika Muswada huu ni hizi zifuatazo:-

- i) Sheria ya Mawakili, Sura 341,
- ii) Sheria ya Usajili wa Viazi na Vifo, Sura 108,
- iii) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura 20,
- iv) Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura 368,
- v) Sheria Mashauri dhidi ya Serikali, Sura 5,
- vi) Sheria za Mahakama ya Mahakimu Wakazi, Sura 11,
- vii) Sheria ya Taifa ya Mashitaka, Sura 430,
- viii) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329,
- ix) Sheria ya Mapato yatokanayo na Uharifu, Sura 256,
- x) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268, na
- xi) Sheria ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Sura 66.

**c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.5 wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2019];**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria Saba (7) zifuatazo:

- i) Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura 306,
- ii) Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Milipuko, Sura 223,
- iii) Sheria ya Baraza la Taifa la Sanaa, Sura 204,
- iv) Sheria ya Baraza la Mithani Tanzania, Sura 107,
- v) Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, Sura 61,
- vi) Sheria ya Viwango, Sura 130, na
- vii) Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura 283.

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya marekebisho ya Sheria hizo ni kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yalibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria husika.

**d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 7 wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.7) Act, 2019]:**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulifanya marekebisho katika Sheria kumi na moja (11) zifuatazo:-

- i) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156 [*The Animal Diseases Act, (CAP. 156)*];
- ii) Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 [*The Animal Welfare Act, (CAP. 154)*];

- iii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 [*The Bank of Tanzania Act, (CAP. 197)*];

- iv) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura ya 134 [*The Government Loans, Guarantees and Grants Act, CAP. 134*];

- v) Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa VVU na UKIMWI, Sura ya 431 (*The HIV and AIDS Prevention and Control Act (CAP. 431)*);

- vi) Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182 [*The Industrial and Consumer Chemicals (Management and Control) Act, (CAP 182)*];

- vii) Sheria ya ya Madini, Sura ya 123 [*The Mining Act, (CAP. 123)*];

- viii) Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa, Sura ya 419 [*The National Ledears' Funerals Act, (CAP. 419)*];

- ix) Sheria ya Bandari, Sura ya 166 [*The Ports Act, (CAP. 166)*];

- x) Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 [*The Prevention of Terrorism Act), (CAP.19)*]; na

- xi) Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu, Sura ya 36 [*The Registration and Identification of Persons Act, (CAP. 36)*].

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya marekebisho ya Sheria hizo ni kuondoa mapungufu mbalimbali ambayo yalibainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria husika.

**e) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 8 wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Act, 2019]:**

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umeshughulikiwa katika Mkutano wa Kumi na Nne (18) wa Bunge, na umefanya marekebisho katika Sheria Kumi na Nne (14) ili ziendane na mabadiliko ya wakati na kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo. Orodha ya Sheria zilizofanyiwa Marekebisho katika Muswada huu ni hizi zifuatazo:-

- i) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20);

- ii) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai(Sura ya 33);

- iii) Sheria ya Maziwa,(Sura ya 262);

- iv) Sheria ya Wakala wa Serikali,(Sura 245);

- v) Sheria ya Uvuvi(Sura ya 279);

- vi) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Dhidi ya Serikali(Sura ya 5);

- vii) Sheria ya Mtoto (Sura ya 13);

- viii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura ya 287);

- ix) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Sura ya 288);

- x) Sheria ya Tasnia ya Nyama, (Sura ya 421);
- xi) Sheria ya Kanuni za Adhabu, (Sura ya 16);
- xii) Sheria ya Usimamizi wa Mirathi (Sura ya 352);
- xiii) Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, (Sura ya 307); na
- xiv) Sheria ya Usajili wa Wadhamini (Sura 318).

#### **1.4.3 Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara;**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kifungu cha 6(2)(a) na(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(d) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Februari 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea na kujadili Taarifa Nane (8) za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazosimamia pamoja na Taasisi zake, ambapo, Taarifa Sita (6) ziliwasilishwa na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taarifa mbili (2) kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, kama ifuatavyo:-

##### **a) Taarifa Sita (6) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu:-**

- (i) Muundo na Majukumu ya Ofisi hiyo kwa kuzingatia Majukumu ya Uwekezaji yaliyoongezwa.
- (ii) Muundo na Majukumu ya Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC);
- (iii) Muundo na Majukumu ya Baraza la Taifa la Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC);
- (iv) Muundo na Majukumu ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC);
- (v) Mafanikio na Changamoto katika kutekeleza Programu ya Uendelezaji Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na Huduma za Kifedha Vijiji; na
- (vi) Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokonayo na Taarifa ya Mwaka ya Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019.

##### **b) Taarifa Mbili (2) kutoka Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu:-**

- (i) Mafanikio na Changamoto katika Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu; na
- (ii) Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokonayo na Taarifa ya Mwaka ya Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(c) cha Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

#### **1.4.4 Uchambuzi wa Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazosimamia kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezewa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI;

#### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari 2020, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayotolewa Taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuiwezesha Kamati, Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa.

#### 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyobainishwa na Kamati kama ifuatavyo:-

##### 2.2.1 Yatokanayo na Taarifa za Utendaji wa Taasisi za Serikali;

###### i) **Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Muundo na Majukumu ya Ofisi hiyo kwa kuzingatia Majukumu ya Uwekezaji yaliyoongezwa.**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 25 Oktoba, 2019 ilianisha kuwa, kuanzia mwezi Aprili, 2019 baada ya Mhe.Rais kuidhinisha Muundo mpya wa Ofisi ya Waziri Mkuu, aliongezea Ofisi hiyo jukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya uwekezaji nchini.

Kwahiyo, masuala ya Uwekezaji yanasmamiwa kuitia Idara ya Maendeleo ya Uwekezaji, ambapo majukumu yake yametokana na kuunganishwa kwa majukumu yaliyokuwa yakitekeleza na Idara ya Uwekezaji iliyokuwa Wizara ya Viwanda na Biashara na baadhi ya Majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Uvezeshaji Wananchi yanayohusu uratibu wa mazingira ya biashara na uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, majukumu ya Idara hii ni kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mapitio ya Sera, Mikakati, Mipango, Programu na Sheria ya Uwekezaji nchini, pamoja na kusimamia maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridishwa na hatua nzuri za uratibu na usimamizi wa masuala ya Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwasababu mafanikio yanaonekana katika Sekta mbalimbali nchini.

Hata hivyo, Kamati ilibaini baadhi ya changamoto zinazoikabili Ofisi ya Waziri Mkuu, kwenye uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Kukosekana kwa ushirikiano wa uratibu mionganoni mwa taasisi za Serikali. Hii inatokana na kukosekana kwa mipango na mikakati madhubuti inayoshabihiana kati ya Sekta zinazohusika, hali ambayo imeleta mitazamo tofauti mionganoni mwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi;

ii) Ucheleweshaji wa huduma kwa wawekezaji kama vile vibali na leseni katika baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali, kwasababu ya ukosefu wa mfumo wa TEHAMA katika kurahisisha utoaji maamuzi na mawasiliano;

- iii) Upungufu wa Maeneo yenyne Miundombinu muhimu na wezeshi katika ngazi za Halmashauri za Wilaya na Mikoa nchini. Hali hii imebainika kuathiri miradi ya Sekta za Kilimo, Uchimbaji wa madini, viwanda na utalii ambayo iko mbali na maeneo yenyne miundombinu;
- iv) Ugumu katika upatikanaji na umilikishwaji wa Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji. Hali hii imebainika kusababishwa na taratibu za uhaulishaji wa ardhi kuchukua muda mrefu, kutoka ardhi ya kijiji kuwa ardhi kwaajili ya uwekezaji;
- v) Muingiliano wa Taasisi za Udhibiti wa Biashara na Tozo za Leseni na Vibali kwasababu ya wingi wa taasisi za udhibiti wa biashara. Hali hii imeabinika kuongeza ghamra za uendeshaji wa shughuli za uwekezaji nchini;

**Mhesimiwa Spika**, baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, ilitoa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika mapendekezo kwenye taarifa hii (**SEHEMU YA TATU**).

**ii) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Muundo na Majukumu ya Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC);**

**Mhesimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 24 Oktoba, 2019, ni kuwa, lengo la kuanzishwa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania ni kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwekezaji, kama ambavyo majukumu yake yameainishwa chini ya Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997(The Tanzania Investment Act, 1997). Majukumu hayo ni pamoja na kuwa taasisi ya msingi ya Serikali kwa ajili ya kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha, kufanikisha na kuishauri Serikali kuhusu Sera na masuala yanayohusu Uwekezaji.

**Mhesimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na Kituo cha Uwekezaji nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Kitengo cha Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Center), Kuongezeka kwa Mitaji ya Uwekezaji kutoka nje (FDI), Kuongezeka kwa miradi inayomilikiwa na wawekezaji wa ndani kufikia aslimia 48 ukilinganisha na idadi ya miradi inayomilikiwa na wawekezaji kutoka nje asilimia 27 na miradi ya ubia asilimia 25, na Uanzishaji wa Kamati ya Taifa ya Uvezeshaji Uwekezaji (National Investment Facilitation Committee) inayoundwa na wakuu wa Taasisi zinazotoa vibali na leseni mbalimbali kwa wawekezaji.

**Mhesimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, kulibainika pia baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi, katika sekta nzima ya uwekezaji kama ilivyoainishwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, zipo baadhi ya changamoto ambazo zilibainika kukabili Kituo cha Uwekezaji kwa upekee. Changamoto hizo ni pamoja na :-

- i) Kuwepo kwa ugumu katika kuandaa 'Unit Titles' kutoka kwenye 'Derivative Rights' zinazomilikiwa na wawekezaji wa kigeni wanaowekeza katika ujenzi wa nyumba za kuuza, kutokana na Sheria iliyopo kutotoa fursa hiyo ambayo hutolewa na Kituo cha Uwekezaji.
- ii) Uwepo wa urasimu katika Utoaji wa Huduma.Hali hii inasababishwa na baadhi ya Watumishi wa Taasisi za Serikali katika kuwashudumia Wawekezaji kwa kushindwa kutoa huduma bora za haraka, ikiwemo na ucheleweshaji maamuzi ya uwekezaji.
- iii) Upungufu wa Rasilimali fedha pamoja na Rasilimali watu katika Kituo cha Uwekezaji, hali ambayo inaathiri ufanisi wa Kituo hicho.Hii ni pamoja na ufinyu wa Ofisi ukilinganisha na ukubwa wa Majukumu ya kituo hicho.

**Mhesimiwa Spika**, baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, ilitoa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika mapendekezo kwenye taarifa hii (**SEHEMU YA TATU**).

**iii) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Muundo na Majukumu ya Baraza la Taifa la Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC);**

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limeundwa chii ya Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004, ambayo inalipa Baraza jukumu la msingi la kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004, kupitia Kamati mbalimbali za kiuratibu.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 23 Oktoba, 2019, Kamati ilibaini kuwepo kwa mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na Baraza hili kuanzia mwaka 2007 hadi 2019.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya mafanikio hayo, ni pamoja na Utoaji wa dhamana ya Mikopo kwa Wananchi yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 13.81**. Hatua hii, imewezesha **Watanzania 14,000** kutoka Mikoa 13 kuanzisha biashara mpya na kuboresha shughuli zao za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, pia Kamati ilibaini uwepo wa mwamko mkubwa wa Wananchi kujunga na vikundi vya kiuchumi ambapo zaidi ya **Wananchi Milioni 10** kupitia **vikundi 400,000** vya kiuchumi wanajishughulisha katika maeneo mbalimbali ya kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, kulibainika changamoto mbalimbali zinazolikabili Baraza katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya Changamoto hizo ni:-

i) Ushiriki mdogo wa Watanzania kwenye miradi ya kimkakati inayotekelzwa hapa nchini. Hali hii inathibitishwa na ushiriki mdogo wa Makapuni ya kitanzia katika Miradi mbalimbali ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa hapa nchini; na

ii) Uelewa tofauti kuhusu dhana na fursa za uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kutohuna na ufinyu wa Elimu kuhusu fursa na jinsi ya ushiriki wa watanzania kwenye hizo fursa..

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, ilitaa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika mapendekezo kwenye taarifa hii (**SEHEMU YA TATU**).

iv) **Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Muundo na Majukumu ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC);**

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ni jukwaa la majadiliano kati ya sekta ya umma na Sekta binafsi, lillioanzishwa kwa Waraka wa Rais Na.1 wa Mwaka 2001 na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na.39 la tarehe 28 Septemba, 2001.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Baraza la Biashara limeundwa kuwezesha majadiliano ya mara kwa mara kwaajili ya kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake. Hii ni pamoja na kushawishi na kuwezesha kufanyika kwa tafiti za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera za kibiashara, kiuchumi na kijamii hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Baraza hili ni nguzo muhimu katika kuunganisha wadau wote muhimu wa kijamii na kiuchumi na lina muundo unaoliwezesha kuzifikia Wilaya na Mikoa yote nchini kupitia Kamati zake za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini mafanikio yaliyofikiwa na Baraza la Taifa la Biashara, yaliyotokana na majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi pamoja na kufikiwa kwa maazimio mbalimbali ambayo utekelezaji wake umesaidia kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuandaliwa kwa Mpango wa kuboresha Mazingira ya biashara nchini (*Blue Print*), ikiwa ni utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Tano wa Maazimio ya Mkutano wa 7 wa Baraza la Taifa la Biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Pia Kamati ilibaini uboreshaji wa huduma za bandari na mipakani, utoaji wa misamaha ya adhabu na riba (Tax Amnesty) kwa asilimia 100, kuwatambua wajasiriamali wasio rasmi, kuanzisha kitengo cha Local Content, kuandaliwa kwa mwongozo wa majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika Ngazi ya Mikoa na Wilaya, uanzishwaji wa vituo vya biashara vya pamoja (One Business Centres-OsBC), pamoja na kupunguzwa na kuondolewa kwa kodi na tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa Wafanyabiashara na Wawekezaji, kama vile tozo za OSHA.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kubaini mafanikio yaliyofikiwa na Baraza husika, pia ilibaini kuwepo kwa baadhi ya changamoto zinazolikabili shirika hilo. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

- i) Mikoa na Wilaya kushindwa kuratibu ipasavyo majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi katika ngazi husika, na hivyo kusababisha malalamiko mengi kutoka kwa Wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuchelewesa uwekezaji katika maeneo hayo; na
- ii) Kukosekana kwa matawi ya TPSF katika ngazi za Mikoa na Wilaya, hali ambayo husababisha shughuli nyingi za uratibu wa sekta binafsi kukasimiwa kwa TCCIA, ambayo huweka maslahi yake mbele kuliko maslahi ya Sekta binafsi kwa kujumuisha wafanyabiashara amba siyo wanachama wa TCCIA.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, ilitoa ushauri kwa Serikali kama iliyooainishwa katika mapendekezo kwenye taarifa hii (**SEHEMU YA TATU.**)

v) **Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Mafanikio na Changamoto katika kutekeleza Programu ya Uendelezaji Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini;**

**Mheshimiwa Spika**, Programu ya Miundombinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini(MIVARF) ni programu ya miaka saba ambayo utekelezaji wake ulianza mwaka 2011 na ilipangwa kukamilika mwezi machi 2018 lakini kutohana na kuchelewa kuanza, programu iliongezwa muda wa miaka miwili na hivyo itakamilika mwezi machi 2020.

**Mhesi miwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, utekelezaji wa MIVARF unachangia katika uwekezaji katika Kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa Mitaji, kuboresha miundombinu kwa ajili Kilimo ili kufanikisha upatikanaji wa pembejeo na masoko ya mazao ya kilimo na kuchochaea ukuaji wa Viwanda ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Programu hii unalenga kuongeza kipato na uhakika wa chakula kwa kaya zenyе kipato chini hususan katika maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Serikali iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 28 Oktoba, 2019 iliajisha kuwa, walengwa wa Programu hii ni Halmashauri 62 za Tanzania Bara na Wilaya 10 za Zanzibar amba ni wakulima wadogo wadogo, wavuvi, wafugaji na wafanyakazi za mikono(artisans), wajasiriamali wadogo wadogo vijijini na wafanyabiashara vijijini, Asasi ndogo ndogo za kifedha zenyе kutoa huduma vijijini, vyama vya Msingi vya Ushirika vya Vijijini vyenye kujihusisha na usindikaji wa mazao na masoko ya mazao vijijini pamoja na Wanawake kwa kila kundi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia Septemba, 2019 Programu imeweza kuzifikia jumla ya Kaya 1,441,399 na kukarabati jumla ya kilometa 1,078.6 za Barabara za vijijini, ujenzi wa masoo 16, ujenzi wa maghala 29 na kukarabati 5 pamoja na kutoa ruzuku kwa maghala 64 ili yawenze kutekeleza mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani.

**Mheshimiwa Spika**, pia ilibainika kuwa, hadi Septemba, 2019 jumla ya **shilingi Bilioni 282.16** zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika utekelezaji wa programu ya MIVARF, pia kulibainika baadhi ya changamoto mbalimbali zilizoibuka wakati wa utekelezaji wa programu hiyo, kama ifuatavyo:-

i) Halmashauri za Wilaya 23 bado hazijakamilisha malipo ya mchango wa asilimia 5 kwa wakandarasi katika uboreshaji wa miundombini.Deni hilo ni **Shilingi milioni 478,636,681.7**,

ii) Utawala dhaifu wa asasi za ushirika kutokana na usimamizi hafifu uliosababisha wanachama kupoteza amana zao na kupoteza imani katika vyama vyao vya ushirika, na

iii) Matumizi madogo ya kilimo cha kisasa katika kupunguza kilimo cha mkono chenye kuongeza gharama za uzalishaji na kupunguza kipato cha wakulima wa kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kubaini changamoto hizo, ilitoa ushauri kwa Serikali kama ilivyoainishwa katika mapendekezo kwenye taarifa hii (**SEHEMU YA TATU**).

vi) **Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokonayo na Taarifa ya Mwaka ya Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa 15 wa Bunge, ulioanza tarehe 29 Januari hadi 9 Februari, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge iliwasilisha Jumla ya Mapendekezo matatu (3) kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu yaliyoazimiwa na Bunge ili yafanyiwe utekelezaji na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 22 Oktoba, 2019 Kamati ilipokea taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa Maazimio husika kama ilivyoolekezwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio hayo yameainishwa kwenye **Azimio NA 14.1,14.2 na 14.3**, katika Kitabu cha Majumuisho ya Maazimio ya Bunge cha Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Mwezi Februari, 2019. Maazimio hayo yalikuwa kama ifuatavyo:-

i) Kuitaka Serikali kuongeza usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa lengo la kuimarisha SACCOS zilizopo na kudhibiti SACCOS hewa ambazo hukopeshwa na kupotea na fedha za Serikali;

ii) Kuitaka Serikali kupanua wigo wa wanufaika wa Mfuko wa Vijana kwa kutoa Mikopo kwa makundi mbalimbali ya Vijana nje ya SACCOS, na

iii) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge, kuandaa ziara ya kikazi kwa Kamati kutembelea na kukagua Vikundi/SACCOS za vijana ili kujionea hali halisi na kuishauri Serikali ipasavo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu imetekeliza Maazimio yote matatu kama yaliyoazimiwa na Bunge, kwa ufanisi mkubwa. Utekelezaji huo umethibitishwa na Kamati siyo tu kwa kupitia taarifa za Serikali bali kwa Kamati kutembelea baadhi ya Wilaya ili kujionea hali hali ya utekelezaji wa maazimio hayo, na Kamati imejionea na kujiridhisha pasipo shaka kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maana ya Mawaziri wote, wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe, pamoja watendaji wote wa Ofisi hiyo, ni wasikiu katika upokea maazimio ya Bunge pamoja na maelekezo ya Kamati na kuyafanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kwa Wizara na taasisi nyingine za Serikali kuiga mfano mzuri uliodhahirishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

vii) **Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Mafanikio na Changamoto katika Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu;**  
**Mheshimiwa Spika**, kwa kibali chako, tarehe 24 Januari, 2020 Kamati ilifanya ziara ya kikazi Mkoani Iringa kwa ajili ya kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Usajili wa Vizazi na Vifo, inayoratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria kuititia RITA.

**Mheshimiwa Spika**, kamati imejionea na imeridhishwa na utekelezaji wa Programu hiyo muhimu kwa kubaini ongezeko kubwa la usajili wa watoto chini ya miaka mitano kwa kuwapatia Vyeti nya kuzaliwa hapo hapo kwa haraka na pasipo usumbufu wowote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuheshimu umuhimu wa haki za mtoto wa Kitanzania kupatiwa cheti cha kuzaliwa kama haki yake ya msingi itakayomuwezesha kuzifikia fursa mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Kamati inalipongeza na kulishukuru Shirika la UNICEF kwa kuwezesha utekelezaji wa Programu hiyo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, Serikali ijipange ili kupanua programu hiyo kutoka mikoa Kumi na Tano inayopata huduma hiyo kwa sasa hadi Mikoa yote ili Watoto wetu wapate haki hiyo muhimu kwa ustawi wa maisha yao kama Watanzania.

viii) **Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yatokonayo na Taarifa ya Mwaka ya Kamati kwa kipindi cha Januari 2018 hadi Januari, 2019.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa 15 wa Bunge, ulioanza tarehe 29 Januari hadi 9 Februari, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge iliwasilisha Jumla ya Mapendekezo saba (7) kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria yaliyoazimiwa na Bunge ili yafanyiwe utekelezaji na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio hayo yameainishwa katika **Azimio Na 14.4** kwenye Kitabu cha Majumuisho ya Maazimio ya Bunge cha Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Mwezi Februari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 31 Oktoba, 2019 Kamati ilipokea taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Maazimio husika kama ilivyoelekezwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake imetekeliza Maazimio yote Saba (7) kama yaliyoazimiwa na Bunge, kwa ufanisi mkubwa. Hivyo, Kamati inaipongeza Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa kuiga mfano mzuri wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika kutekeleza Maazimio ya Bunge pamoja na maelekezo ya Kamati.

## 2.2.2 Uchambuzi wa Miswada ya Sheria;

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Miswada Mitano (5), ambayo ilizifanyia marekebisho jumla ya Sheria (51) zilizochambuliwa na kujadiliwa na Kamati na hatimaye kuitishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoainishwa katika sehemu ya kwanza ya taaarifa hii, kwa ujumla, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Miswada hii ilikusudia kufanya marekebisho katika Sheria Hamsini na Moja (51) kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, ili Sheria hizo ziendane na mabadiliko ya wakati na kutatua changamoto mbalimbali zilizobainika katika Sekta husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilitekeleza wajibu wake wa kikanuni kwa uaminifu, weledi na ufanisi mkubwa katika kulisaidia Bunge kutunga Sheria jumuishi kuititia Miswada husika. Aidha, Kamati inajivunia kuwa sehemu ya

Mabadiliko makubwa ya Kisheria nchini yanayoendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano, kwa maendeleo ya Taifa letu.

### **2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mnamo mwezi Machi, 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Mbeya, Njombe, Manyara na Arusha. Aidha, kwa kibali chako, Kamati ilifanya ziara maalum kwa ajili ya kutembelea na kukagua Ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara ambao umezingatia matumizi ya TEHAMA. Aidha, Kamati iliridhidhishwa na ukarabati wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya ambao pia umezingatia matumizi ya TEHAMA katika usikilizaji wa mashauri pamoja na utunzaji wa Kumbukumbu za Mahakama hiyo. Hivyo, Kamati inaipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuanza kuzingatia matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mahakama nchini, kwa kuwa mfumo huo, utarahisisha utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukaguzi wa Miradi husika, pia Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo juu ya ujenzi wa Mahakama 35 nchini, kwa mgawanyo ufutao:-

- a) Mahakama Kuu Tatu (3),
- b) Mahakama za Hakimu Mkazi Sita (6),
- c) Mahakama za Wilaya Kumi na Nne (14), na
- d) Mahakama za Mwanzo Kumi na Mbili (12)

**Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha mazingira ya utoaji haki nchini ikiwemo kupunguza usumbufu kwa baadhi ya Wananchi kutembea Kilomita nyingi kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine ili kufuata haki ya Mahakama katika mashauri mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia, ilipokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Mahakama ya Tanzania kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021 wa Maendeleo ya Miundombinu kuhusu Ukarabati na Ujenzi wa Mahakama mbalimbali katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mikoa na Kitaifa pamoja na Nyumba za Makazi ya Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama nchini. Mpango huu pamoja na mambo mengine unalenga kuiwezesha Mahakama nchini kupunguza kwa kiasi kikubwa au kuondokana kabisa na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo ya muhimili huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, endapo Mpango huu wa miaka Mitano (5) utatekelezwa kwa wakati, utaiwezesha Mahakama kujenga Jengo la Makao Makuu na Mahakama ya Rufani Jijini Dodoma, Majengo ya Mahakama Kuu katika Mikoa Kumi na Mbili (12), Majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi Kumi na Saba (17), Mahakama za Wilaya Mia Moja na Nne (104) na Mahakama za Mwanzo Mia Moja (100), Nyumba za Majaji Kumi na Moja (11) na Nyumba za Mahakimu na Watumishi wengine Kumi (10).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na Mpango huu kwa kuwa unalenga kuongeza upatikanaji wa haki kwa Wananchi, na pia umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ziliombewa na kuidhinishiwa **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nane Tisini na Moja, Laki Tano Tisini na Nane Elfu, Mia Tatu na Mbili (7,891,598,302/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 iliongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Blioni 6.27** ongezeko ambalo ni sawa na **asilimia 4.64%** ya Bajeti ilioidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko hilo lilizingatia mahitaji ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutokana na vipaumbele vilivyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hii ni pamoja na kuongeza bajeti ya Fungu 19; Ofisi mpya ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwemo bajeti ya Maendeleo kwa lengo la kuiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake ndani na nje ya nchi kwa ufanisi zaidi, ikiwemo kuimarisha Nguvu kazi ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na uwepo wa Ofisi hiyo sambamba na utendaji wake wa kazi kwa sasa, ambao umeiwezesha Serikali kushinda kesi muhimu za madai ndani na nje ya nchi, na hivyo kurejesha heshima ya nchi kwa viwango vinavyoridhisha na kwa uzalendo mkubwa.

#### 2.2.4 Ufinyu na ukomo wa Bajeti kwa Taasisi ambazo Kamati inazisimamia

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa Mafungu 14 ya Wizara na Taasisi inazosimamia kama ifuatavyo:-

##### a) Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)-FUNGU 26 na 31

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ultazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2018 na kiwango ambacho kilikuwa kimepokelewa hadi Machi 2019 katika Robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi huu pia ultazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 **Fungu 26** la Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais lilitengewa **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Nne Themanini na Tano, Laki Tisa Tisini na Moja Elfu Mia Tano Sabini na Nane na Senti Tano (6,485,991,578.05/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja na Milioni Hamsini na Tatu, Laki Sita Sitini na Sita Elfu (1,053,666,000/=)** ilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne Thelathini na Mbili, Laki Tatu Ishirini na Tano Elfu, Mia Tano Sabini na Nane na Senti Tano (5,432,325,578.05/=)** ilikuwa ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2018 hadi mwezi Machi 2019, **Jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tano Sabini na Mbili, Laki Nane na Kumi Elfu, Mia Tano Sabini na Nane na Senti Tano(4,572, 810,578,.05)**, zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kiasi hicho cha Fedha kilichopokelewa ni sawa na **asilimia 70.5%** ya Bajeti ilioidhinishwa na Bunge katika **Fungu 26**.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 **Fungu 31** la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla lilitengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Milioni Mbili, Themanini na Mbili Elfu, Mia**

**Tano Ishirini na Tatu na Senti Ishirini na Nane (10,002,082, 523.28/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Ofisi hiyo ilipokeea **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tano Thelathini na Saba, Laki Saba Tisini na Tano Elfu na Tatu na Senti Ishirini na Nane (5,537,795,003.28)** sawa na **asilimia 55.4%** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati, hatua ambayo iliisaidia Ofisi Binafsi ya Makamu Rais-Muungano kutekeleza Majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mafungu yote (**Fungu 26 na Fungu 31**).

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (**Fungu 26**) iliomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nane Hamsini na Tano na Tisini na Tatu Elfu (7,855,093,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Ishirini, Laki Moja Ishirini na Nane Elfu (1,120,128,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Saba Thelathini na Nne, Laki Tisa Sitini na Tano Elfu (6,734,965,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Bajeti ya **Fungu 26** iliongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Sitini na Tisa, Laki Moja na Moja Elfu, Mia Nne Ishirini na Mbili (1,369,101,422)** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 21.11%** ya Bajeti ya **Fungu 26** kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Ongezeko hili lilitokana na mahitaji halisi ya Ofisi hiyo hususan gharama za utocaji huduma kwa Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Makamu wa Rais (**Fungu 31**) iliomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Hamsini na Saba, Laki Tano Sabini na Tano Elfu, Mia Tano Sitini (5,357,575,560/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Thelathini na Moja, Laki Sita Ishirini na Nne Elfu (1,931,624,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nne Ishirini na Tano, Laki Tisa Hamsini na Moja Elfu, Mia Tano Sitini, (3,425,951,560/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa **Fungu 31** iliongezeka kwa **asilimia 4.5%** ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na uanzishwaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

**b) Ofisi ya Waziri Mkuu;**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina **Mafungu 6 ya bajeti** kama ifuatavyo;

- i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkoo,
- ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkoo,
- iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
- iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
- v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na

**vi) Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Sita, Laki Tatu Themanini na Tisa Elfu, Mia Sita Tisini na Nane (66,166,389,698/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili, Laki Tano Sabini na Mbili Elfu, Mia Tano Tisini na Nne (19,200,572,594/=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Moja Thelathini na Sita, Laki Tatu Hamsini na Moja Elfu na Hamsini na Tatu (23,136,351,053=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Laki Nne Sitini na Sita Elfu na Hamsini na Moja (23,829,466,051=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari 2019 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Tano Ishirini na Nane na Ishirini na Nane Elfu, Mia Tatu Sabini na Saba (37,528,028,377/=)** sawa na **asilimia 58%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambao kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ultengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Tano (15,000,000,000/=)**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa na upatikanaji wa Fedha za kutekeleza Mradi huo, kwani kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Ofisi ya Waziri Mkuu ilipokea kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili (12,000,000,000/) sawa na asilimia 80%** ya Bajeti ya Mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**c) Wizara ya Katiba na Sheria;**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 .

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tano, Milioni Mia Saba Ishirini na Sita, Laki Saba Sitini na Tatu Elfu (145,726,763,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Saba, Milioni Mia Moja Sabini na Tatu, Laki Mbili Tisini na Tatu (77,173,293,000)** zilikuwa ni za Mishahara na **Shilingi Bilioni Sitini na Nane, Milioni Mia Tano Hamsini na Tatu, Laki Nne Sabini Elfu(68,553,470,000)** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Februari 2019 Wizara na Taasisi zake zilipokea **Jumla ya Shilingi Bilioni Themanini na Saba, Milioni Mia Tano Sitini na Tatu, Laki Mbili Kumi na Nne Elfu, Mia Nne Arobaini na Tano (87,563,214,445)** sawa na **asilimia 46%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi ulionyesha kuwepo kwa mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Matumizi Mengineyo kwa kuwa hadi kufika Mwezi Februari, 2019 **jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Tisa, Laki Tisa Hamsini na Nane Elfu, Mia Tisa Themanini na Mbili (36,169,958,982)** sawa na **asilimia 51%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi mengineyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ilidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini na Nne, Milioni Mia Saba Sitini na Saba, Laki Mbili Kumi na Tisa Elfu (44,767,219,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita Milioni Mia Saba Sitini na Saba, Laki Mbili Kumi na Tisa Elfu (26, 767,219,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Februari, 2019 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nane Themanini na Tisa, Laki Moja Ishirini Elfu na Tisini na Tano (12,889,120,095/=) sawa na asilimia 29 %** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Saba (7,000,000,000/=)** sawa na **asilimia 38.9%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani. Aidha, fedha za Nje zilizopokelewa hadi Mwezi Februari, 2019 ni **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nane Themanini na Tisa, Laki Moja Ishirini Elfu na Tisini na Tano (5,889,120,095/=)** sawa na **asilimia 22** ya fedha za nje zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Saba, Milioni Mia Mbili Themanini na Tatu, Laki Tano Sitini na Tano Elfu, (47, 283, 565,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Moja, Laki Tisa Themanini na Nne Elfu (25, 231,984,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, Milioni Hamsini na Moja, Laki Tano Themanini Moja Elfu (22,051,581,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

## 2.2.5 Semina na Mafunzo

**Mheshimiwa Spika**, katika Kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari 2020, Kamati ilipatiwa Semina na mafunzo kutoka Taasisi na Asasi mbalimbali za Kiraia kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge, kwa ajili ya kuijengea Kamati uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria hususan masuala ya msingi katika hatua za Uchambuzi wa Miswada. Taasisi ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-

- a) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa *Legislative Support Program (LSP II)*;
- b) Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA);
- c) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- d) Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS);

Aidha, Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu walitoa mafunzo ya Semina mbalimbali kuhusu masuala mbalimbali ya kisera, kisheria, Muundo na Majukumu ya Ofisi hiyo kwa kuzingatia majukumu mapya ya Uwekezaji yaliyoongezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe wamejengewa uwezo na uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kisera na kisheria na hivyo kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuishauri Serikali ipasavyo.

## 2.2.6 Mazingira wezeshi ya Vijana

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari 2020, chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilitembelea Miradi mbalimbali ya Vijana katika Wilaya za Iringa

Mjini na Morogoro kwa lengo la kujonea hali halisi ya utekelezaji wa Miradi hiyo, yenyewe kufadhliliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa kwa jinsi ambavyo vijana wananaufaika na ufadhili wa mfuko huo kupitia vikundi mbalimbali vya uzalishaji. Hata hivyo, ilibaini changamoto mbalimbali za usimamizi wa miradi hiyo kwa upande wa Halmashauri (TAMISEMI).

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI

#### 3.1 Ofisi ya Waziri Mkuu;

##### a) Uratibu wa Masuala ya Uwekezaji katika Mikoa na Wilaya;

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA**, imebainika kuwepo kwa Mikoa na Wilaya zilizoshindwa kuratibu ipasavyo katika ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi katika ngazi husika,

**NA KWA KUWA**, Mikoa na Wilaya kushindwa kuratibu majadiliano ya masuala ya biashara na uwekezaji inachelewesha na kukwamisha jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuchochaea uwekezaji wa Viwanda kuelekea uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025;

**HIVYO BASI**; Kamati inashauri Serikali kuanza kutekeleza Mwongozo wa Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi ya Mikoa na Wilaya ili kutatua changamoto hiyo na kuchochaea uwekezaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya nchini. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa, TPSF inakuwa na Ofisi zake katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili kurahisisha uratibu.

**Mheshimiwa Spika**,

**b) KWA KUWA**, masuala ya uwekezaji nchini yanakabiliwa na changamoto mbalimbali za kiusimamizi na kiuratibu mionganini mwa taasisi husika za Serikali, kama zilivyoainishwa na Kamati kupitia uchambuzi wa taarifa mbalimbali za Serikali,

**NA KWA KUWA**, changamoto hizo zinasababishwa na mfumo uliopo wa kitaasisi na kisheria unaoweza kuathiri mwenendo wa uwekezaji katika sekta mbalimbali na hivyo kukwamisha mipango ya Serikali kuelekea Uchumi wa Kati ifikapo Mwaka 2025,

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaongeza Vituo vya pamoja vya Usimamizi na Uratibu (One Stop Centers) kwenye maeneo mbalimbali ya kimkakati, ili kuziwezesha Taasisi zote husika kuratibu kwa pamoja masuala ya uwekezaji kwa urahisi zaidi na kupunguza urasimu usiyo wa lazima, ambao unaweza kukatisha tamaa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

##### c) Ushiriki Mdogo wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati;

**Mheshimiwa Spika**,

**KWA KUWA**, imebainika kuwa, Baraza la Uwezesajji wananchi Kiuchumi (NEEC) linakabiliwa na changamoto ya ushiriki mdogo wa Wananchi katika Miradi ya Kimkakati ukilinganisha na ushiriki wa Wawekezaji kutoka nje ya nchi;

**NA KWAKUWA**, ushiriki mdogo wa Wananchi kwenye miradi ya Kimkakati unaweza kuathiri maendeleo ya nchi hapo baadaye kwa kuhamishia nje rasilimali za nchi kupitia wawekezaji kutoka nje ya nchi;

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuwa, ihakikishe Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linashirikiana na taasisi za Elimu pamoja na Wadau wa maendeleo katika kuyajengea uwezo Makampuni ya Kitanzania ili yaweeze kushiriki kwenye Miradi mikubwa ya Kimkakati, inayoendelea kutekelezwa na Serikali hapa nchini. Aidha, Baraza hilo kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali liendelee kutoa elimu kuhusu fursa zilizopo na jinsi ya kuzifikia kupitia maonyesho balimbali na vyombo vya habari.

**d) Ufinyu wa Ofisi ya TIC;**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, imebainika kuwa, Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (TIC) kinakabiliwa na ufinyu wa Ofisi kutokana na ongezeko la mahitaji ya nchi kwa sasa, ikiwemo upungufu wa rasilimali watu,

**NA KWA KUWA**, bila kituo hiki kupatiwa miundombinu wezesheji ya Ofisi yenye kujitosheleza pamoja na Wafanyakazi wakutosha, inaweza kuathiri utekelezaji wa Mipango ya Uwekezaji kwa upande wa Serikali,

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Serikali kuwa, TIC iwezeshwe ili ianze na kukamilisha Jengo lake Jijini Dodoma lenye uwezo wa kutekeleza majukumu yake chini ya Mfumo wa One Stop Centre, kwa kuwa na ofisi yenye kujumuisha Ofisi zote zinazohusika katika masuala yote ya Uwekezaji, ili kuiwezesha Ofisi hiyo kuwa na mazingira wezeshi ya kurahisisha uratibu wa masuala ya uwekezaji hapa nchini, kwa kushirikiana na taasisi nyngine za Serikali, kwa ufanisi zaidi. Hii ni pamoja na kuajiri Wafanyakazi wa kutosha kwa kuzingatia vipaumbele vya Kituo hicho.

**e) Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana;**

**Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA**, Kamati imebaini uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kuwa ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya Vijana nchini kutokana na uratibu mzuri unaotekeliza na Ofisi ya Waziri Mkuu,

**NA KWA KUWA**, kuwepo kwa mahitaji makubwa ya Vijana zaidi ya uwezo wa Mfuko kunaweza kusababisha fursa hiyo isiwafikie Vijana wengi nchini,

**HIVYO BASI**, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya yafuatayo:-

a) Kuona umuhimu wa kuongea Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili Mfuko huo uweze kuwafikia Vijana wengi zaidi kutokana na Ofisi ya Waziri Mkuu kudhihirisha uwezo mkubwa katika uratibu wa mfuko huo;

b) Ongezeko hilo la Bajeti liiwezeshe Serikali kupanua uwigo wa wanufaika wa Mfuko wa Vijana kwa kuanza kutoa Mikopo kwa makundi mbalimbali ya Vijana yaliyosajiliwa na yenye mipango ya miradi yenye lengo la kuongeza ajira, CBOs na Makampuni yaliyosajiliwa kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya Kati na Mikubwa ya kutoa ajira nyngi kwa Vijana, na

c) Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane kwa ukaribu zaidi na Ofisi ya Rais –TAMISEMI ambao ndiyo wenye dhamana na Halmashauri kwa lengo la kuhakikisha kila Halmashauri inawajibika kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko wa Vijana pamoja na **asilimia 4%** za Fedha za Halmashauri, kwa kusimamia utekelezaji wa Miradhi hiyo na marejesho yake kwa wakati.

### 3.2 Usimamizi wa utoaji haki nchini;

#### **Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA:** ni jukumu la Serikali kuhakikisha kila mwananchi anapata haki sawa mbele ya vyombo stahiki vya Sheria na haki hiyo inatolewa kwa wakati,

**NA KWA KUWA:** usimamizi wa utoaji wa haki nchini unategemea sana ufanisi wa Taasisi husika zenyenye dhamana hiyo;

**HIVYO BASI:** Kamati inashauri Taasisi husika zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kutekeleza masuala ya msingi yafuatayo:-

a) Mahakama iendeleee kutekeleza kwa ufanisi utaratibu wake ilijojiwekea wa kuhakikisha kila Hakimu na Jajii anashughulikia na kukamilisha idadi ya Mashauri husika kwa muda husika ili kuongeza imani ya Wananchi kwa chombo hiki cha utoaji wa haki nchini,

b) Serikali iendeleee kuboresha Bajeti ya Fungu 55 la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 16 la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 19 la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Fungu 35 la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, na

c) Serikali ione umuhimu wa kuboresha mazingira ya Rasilimali watu chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara na Vitengo vyote vya Sheria kwenye taasisi zote za Serikali pamoja na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kutokana na mabadiliko makubwa ya mfumo wa Kisheria yaliyotekelwa hivi karibuni kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Ufanisi katika mwenendo wa Bajeti za Serikali;

#### **Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA:** Kamati imebaini kuwa, kumekuwepo ongezeka la upatikanaji wa Fedha za ndani ukilinganisha na upatikanaji usioridhisha wa Fedha za Nje, katika mwenendo wa Bajeti ya Serikali,

**NA KWA KUWA:** hatua hii ya kutumia fedha za ndani kuendeshea mipango ya nchi inapunguza utegemezi wa kiuchumi na ni ya uhakika zaidi,

**HIVYO BASI:** Kamati inashauri kuwa:-

a) Serikali iendeleee kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika;

b) Serikali kupitia vyombo husika, ibuni vyanzo vipyta vya mapato vyenye uhakika na endelevu, na

c) Elimu ya kulipa Kodi iendeleee kutolewa kwa Wananchi ili kila Mtanzania aone umuhimu wa kulipa kodi kwa Maendeleo endelevu ya Taifa letu.

### 3.4 Semina na mafunzo kwa Kamati

#### **Mheshimiwa Spika,**

**KWA KUWA:** Programu ya utekelezaji wa Mradi wa LSP (II) chini ya UNDP, imekuwa msaada mkubwa sana katika kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati hii kuhusu masuala mbalimba katika uchambuzi wa Miswada ya Sheria,

**NA KWA KUWA**, Kamati hii ina jukumu la Kuchambua na kujadili Miswada mingi ya Sheria za Marekebisho ya Sheria mbalimbali ambazo zinagusa Sekta mbalimbali nchini,

**NA KWA KUWA**; bado mafunzo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge na Sekretarieti ili kupanua wigo wa uelewa katika mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao;

**HIVYO BASI**; Kamati inashauri Ofisi Bunge kuona umuhimu wa kuendelea kupanua utekelezaji wa **Mradi wa LSP (II)** katika Bunge la Kumi na Mbili kwa kuendelea kuwajengea Uwezo Wabunge Wapya na Sekretarieti kuhusu masuala ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Sheria Ndogo, Mikataba na Itifaki za Kimataifa pamoja na Uchambuzi wa Bajeti za Serikali, kwa lengo la kuongeza weledi kwa Wajumbe na Sekretarieti zake kwa Kamati zitakazoundwa katika Bunge la Kumi na Mbili (12).

Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mradi huu wa LSP uwe endelevu kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo yenye tija kwa kuongeza ufanisi zaidi kwa Wabunge na Sekretarieti yake katika kusimamia utendaji wa Serikali na Taasisi zake.

### 3.5 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**:

**KWA KUWA**, Bunge lina dhamana kubwa ya kusimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

**NA KWA KUWA**, katika kutimiza jukumu hili Bunge hutumia Kamati zake ambazo hutoa ushauri, Mapendekezo na maelekezo mbalimbali kwa Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake;

**HIVYO BASI**; Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake kuendelea kupokea na kutekeleza ushauri na mapendekezo mbalimbali ya Kamati na kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri na mapendekezo hayo kila inapotakiwa kufanya hivyo.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

#### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Mwaka Mmoja uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja Uliopita. Shukrani za Pekee ziwaendee Mawaziri waliohudumu chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2019, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe.Balozi Dkt.Augustine P.Mahiga (Mb), Manaibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. Antony Mavunde (Mb) na Mhe. Ikupa Alex (Mb), Mhe. Mussa Ramadhan Sima (Mb) Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hizi.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe.Prof. Adelardus Kilangi, kwa ushirikiano wake mkubwa katika Kamati pale alipohitajika kufika

mbele ya Kamati kwa ajili ya kuwasilisha hoja za Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya Kisheria.

Aidha, Kamati inawashukuru sana Wanasheria wote na Waandishi wa Sheria chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada mbalimbali. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Washauri wa Masuala ya Sheria Bungeni (CPLC) kwa namna bora walivyoshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye kamati ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza Majukumu katika kipindi cha Januari 2019 hadi Januari 2020. Kwa uchache naomba kuwataja Wadau wafuatao:-

- i) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) chini ya Mradi wake wa *Legislative Support Program (UNDP - LSP)*;
- ii) Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG),
- iii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre*)-LHRC,
- iv) Stallion Attorneys,
- v) Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (*Tanganyika Law society*)-TLS,
- vi) Tanzania Women Lawyers Association-TAWLA
- vii) TWAZEZA
- viii) Jukwaa la Katiba Tanzania(JUKATA),
- ix) *Tanzania Network of Legal Aid Providers-TANLAP*,
- x) Shirikisho la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), na
- xi) Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dodoma

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. **Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo:**

1. Mhe. Mohamed Omari Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – **Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline K. Ngonyani Msongozi, Mb- Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omari Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Suzan Kolimba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, chini ya Uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Wasaidizi ambao ni Ndg. Michael Chikokoto na Ndg. Gerald Sengano Magili, Katibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagisa, Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima, kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina Shughuli zilizoteklezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu shughuli ilizozitekeleza kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii .

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa Hoja.

Mohamed Ommary Mchengerwa, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

4 FEBRUARI, 2020

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Andrew John Chenge. Karibu! Makamu Mwenyekiti! Karibu Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti. (Makofii)

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge na kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inahusu majukumu ya uchambuzi wa Sheria Ndogo yaliyoteklezwa na kamati katika kipindi cha kuanzia Februari 2019 hadi Januari 2020. Naomba muhtasari huu ninaousoma uwe sehemu ya taarifa nzima ambayo imewasilishwa kwa utaratibu wa kawaida na isomeke kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imeanisha ufanuzi kuhusu njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya kamati, utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Tano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, taarifa imebainisha matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba pamoja na maoni ya mapendekezo ya Kamati kuhusu Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya kamati na msingi wa utekelezaji wake. Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinabainisha majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kuwa ni kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Malengo ya masharti haya kikanuni kulipatia Bunge mamlaka ya kuhibiti utungaji wa Sheria Ndogo kwa vyombo vingine ambavyo Bunge lako limekasimu kwake mamlaka ya kutunga sheria kwa mujibu wa Ibara ya 97(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kama ilivyofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia zinazotumika kutekeleza majukumu ya kamati. Baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali

sheria hiyo inatakiwa kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita ya Vikao vya Bunge katika mkutano husika. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa Kifungu cha 38(1) cha tafsiri ya sheria. Matakwa haya ya sheria yanatiliwa nguvu kupitia Kanuni ya 37(2) cha Kanuni za Kudumu za Bunge kama inavyosomeka na nanukuu, "Nakala za matoleo yote ya gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita zitawasilishwa Bungeni na Waziri" mwisho wa kunukuu. Baada ya hatua hiyo Bunge linakuwa na fursa ya kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa na mamlaka inayopatikana katika Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020. Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba, Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo mia nane tisini na saba (897) ikilinganishwa na Sheria Ndogo mia saba na nne (704) zilizowasilishwa katika kipindi cha mwaka 2018 hadi mwaka 2019. Hivyo, kwa mwaka 2019 hadi mwaka 2020 kumekuwa na ongezeko la Sheria Ndogo mia moja tisini na tatu (193) ambazo ni sawa na asilimia 22.6 ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba katika hatua hii taarifa hii irekebishwe isomeke hii asilimia 22.6 kama ambavyo nimeisoma sasa badala ya asilimia 44 kama ambavyo iko kwenye taarifa mama ambayo iko kwenye mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo kamati imebaini jumla ya Sheria Ndogo 73 kati hizi sheria 897 ambazo ni sawa na asilimia 8.13 badala ya asilimia 44 kama ambavyo nimesema ifanyiwe marejeo ambazo zilikuwa na dosari mbalimbali ambapo kamati ilitoa maoni na mapendekezo ili kuondoa dosari hizo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara zilizoguswa katika uchambuzi huu ilikuwa ni pamoja na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Uchambuzi Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba. Katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa, kamati ilibaini kuwepo na dosari mbalimbali na zifuatazo ni baadhi yake. Kwanza Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyininge za nchi lakini pia Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika majedwali, Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria; Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu na baadhi ya Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia (unreasonable provisions). (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika mchakato mzima wa utungaji wa Sheria Ndogo ambazo zimechangia uwepo wa dosari zilizoainishwa katika Sheria Ndogo na ambazo tulizifanyiwa uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache tu naomba kuzisoma baadhi ya changamoto kama ifuatavyo:-

(i) Uchache wa Wanasheria wenye taaluma ya uandishi wa sheria katika wizara, taasisi na mamlaka za Serikali na hata Serikali za Mitaa, uhaba wa wataalamu hao unasababisha sheria ndogo nyingi kufika katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiwa tayari zina dosari ambazo zinaweza zisibainike kirahisi na mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali kwa sababu naye siyo tu kwamba ana wataalamu wachache lakini pia ana kazi nyingi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, baadhi ya mamlaka zilizokasimiwa kutunga sheria zimekuwa zikitunga sheria ndogo na wakati mwingine zikipoka mamlaka ya vyombo vingine vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi na jambo hili tunaomba sana Serikali iendelee kulifanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu baadhi ya Wizara kutumia mwanya wa mamlaka iliopewa; na nasema tu, kwa jinsi ambavyo tumeona uchambuzi na katika kutekeleza huu mfumo wa utungaji wetu wa sheria ndogo wakati mwingine baadhi ya Wizara zinajisahau na kutotimiza masharti ya msingi wa utungaji wa sheria. Tumekuwa tukishauri mara kadhaa tunapokutana na Wizara hizi kuzingatia misingi ya utungaji wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge Serikali imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo 196 na uchambuzi wa Kamati ulibainika kuwa Sheria Ndogo 14 tu ndizo ziliikuwa na hoja mbalimbali za kiuchambuzi. Hapa kwa kweli tunaipongeza Serikali kwa sababu mzigo ulikuwa mkubwa, lakini sheria chache ndiyo zilioneekana zina hitilafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Ndogo hizo ziliikuwa chini ya Wizara zifuatazo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano p a m o j a n a Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa Sheria Ndogo, Kkamati yetu pamoja na Wizara tulikutana kwa pamoja na kimsingi Serikali iliwasilishwa na mapendekezo, ushauri na maoni ya Kamati. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizo zimeendelea kuratibu kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na mawasiliano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na kufanya mawasiliano na Halmashauri husika ambazo sheria ndogo zake zilibainika kuwa na kasoro mbalimbali ili kurekebisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge hasa tarehe 3 Aprili, 2019 Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo 174 ambapo uchambuzi wa Kamati ulibainika kuwa Sheria Ndogo 22 ziliikuwa na dosari. Tulizifanya kazi, lakini pia baada ya kushauriana na Serikali, Serikali iliindhia maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kamati yetu ilipata fursa ya kukutana na wadau mbalimbali, lakni kama nilivyo sema, taarifa yetu isomwe kwa ujumla wake na tumeainisha pia baadhi ya wadau ambao tulikutana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Mkutano wa Kumi na Saba. Taarifa hii pia inahusisha uchambuzi wa Sheria Ndogo

zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba na uchambuzi ambao tumeufanya pia umebainisha dosari kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba niwasilishe kwa niaba ya Kamati yetu uchambuzi wa Sheria hizo Ndogo ambazo tumezibaini katika Mkutano wa Kumi na Saba na kuelezea maeneo ambayo tuliyaona yana upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita, mnamo tarehe 6 Septemba, 2019 katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Serikali ilivasilisha Mezani jumla ya Sheria Ndogo 361 kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika sheria hizo na kimsingi tulizibaini zilikuwa Sheria Ndogo 27 na tumezibainisha katika jedwali letu la uchambuzi. Mara nydingi dosari zilibainika katika maeneo yafuatayo: Moja, sheria ndogo zimeweka masharti yanayokwenda kinyume na sheria mama na sheria nydingine za nchi kutokizingatia misingi ya uandishi wa sheria ndogo, kuweka masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake na makosa ya uandishi katika majedwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilikutana na Wizara zote zilizoguswa katika uchambuzi wetu na kimsingi Serikali iliridhia maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 12 Novemba, 2019 katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge Serikali ilivasilisha Mezani jumla ya Sheria Ndogo 166 kwa mujibu wa kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kikisomwa pamoja na kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo 10 ambazo ndio zilikuwa zimekidhi uhitaji wa uchambuzi wa Kamati yetu, lakini pia kama nilivyo sema jedwali letu linaonesha kwa yale ambayo tuliybaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuonesha dosari hizo, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilikutana na Wizara zote zilizoguswa na uchambuzi wa sheria hizo ndogo zilizochambuliwa katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge ambapo Wizara hizo zilikubaliana na hoja zote na kuahidi kuanza mchakato wa kurekebisha ili kuondoa kasoro zilizobainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Maoni ya jumla, Kamati inashauri kuwa, ni vema Kanuni za The Microfinance (Community Microfinance Groups) Regulations, 2019 zilizotanangaza kupitia Government Notice 678 zikawekewa masharti mepesi ambayo utekelezaji wake hautaleta changamoto kwa watumiaji wake ambao wengi wao ni wananchi wa vipato vyachini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapendekeza kwamba Kanuni za The Microfinance Regulations, ya mwaka 2019 iliyochapishwa kwenye Government Gazette kupitia chapisho Na. 678 zitafsiriwe kwa Kiswahili. Pia majedwali yaliyoambatishwa yawekwe kwenye lugha nyepesi itakayosaidia wananchi kuelewa ili kupunguza changamoto kwa walengwa wa Kanuni hizi ambao wengi wao hawana elimu wala ujuzi kwa kiwango amba chuo penginie mtu ange tarajia kwa masuala yanayohusiana na feedha. Kwa hiyo, tunashauri sana Serikali izingatia ushauri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kanuni za The Microfinance Regulations za mwaka 2019 zilizochapishwa kupitia Government Notice 678 zirejje tafsiri ya Community Microfinance Groups iliyotolewa katika sheria mama ya The Microfinance Act ambayo imewe ka wazi makundi yanayoguswa na pia kuweka exceptions kwa makundi yasiyoguswa na kanuni hizi.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia kuondoa changamoto kwa watumiaji wa kanuni hizi katika kufahamu aina za shughuli za vikundi vinavyoguswa na kanuni hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebaini kwamba Wizara ya Fedha na Mipango tunashauri kwamba itoe miongozo kwa Halmashauri zote ambazo ndizo zimekasimiwa jukumu la usimamizi wa *Community Microfinance Groups*. Miongozo hiyo iainishe mambo muhimu kama vile wajibu wa Halmashauri kwa vikundi hivyo, namna ambavyo vikundi hivyo vitakavyolelewa ikiwa ni pamoja na kupewa elimu ya masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kamati inashauri inashauri Serikali kufanya mapitio ya sheria ndogo zote zilizowasilishwa Bungeni tangu Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, ambazo zimebainika kuwa na dosari ili kuondoa dosari hizo na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali kufikia Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, taarifa yetu ina mambo mengi kuelezea yote haya. Kuhusu maoni na mapendekezo kwa Serikali kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yameandalowiwa kwa muhtasar kuzingatia matokeo ya uchambuzi ulifanywa na Kamati katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Saba. Yamefafanuliwa katika jedwali letu ambalo linaambatana na taarifa tuliyowasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Kamati yetu yako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dosari ya uandishi wa majedwali ikilinganishwa na vifungu vya sheria:-

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi:-

KWA KUWA, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi;

NA KWA KUWA, kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi;

NA KWA KUWA, kukinzana huko kunaharamisha Kanuni husika kwa kwango ilichokinzana na Sheria Mama;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Wizara zinazohusika, zifanyiwe marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama au na Sheria nyingine za nchi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria.

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kwamba baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi;

NA KWA KUWA, dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwneyekiti, kuhusu masharti yasiyokuwa na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini:-

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati, imebainika kuwepo kwa dosari zinazoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia;

NA KWA KUWA, kwa dosari hizo zinaweza kupelekea kuwepo ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na Sheria Ndogo husika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasio na uhalisia zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukiuka misingi ya haki za binadamu:-

KWA KUWA, katika uchambuzi wa Kamati imebainika Sheria Ndogo kuwa na dosari ya kuweka kifungu kinachokiuka misingi ya haki za binadamu;

NA KWA KUWA, kwa dosari hizo zinaweza kupelekea kuminya haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na vyombo vyenye Mamlaka ya kutoa maamuzi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambayo Sheria Ndogo yake imebainika kuwa na dosari za kuweka kifungu kinachokiuka misingi ya haki za binadamu, ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani za dhati kwako binafsi na kwa Bunge lako Tukufu pia Wenye viti wenzio, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kiongozi wetu Mkuu wa Mhimili Mheshimiwa Spika mwenyewe kwa kutupa nafasi ya kuwasilisha taarifa hizi sisi Kamati ya Sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaamini kwamba maoni na ushauri wa Kamati kuititia taarifa hii umeongeza tija kwa kuweza kuisaidia Serikali kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo zilizochambuliwa na hatimaye kutolewa na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa niaba ya Mwenyekiti wetu kwa kazi kubwa tunayoifanya kwa pamoja kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa na Serikali katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba na hatimaye kufanikisha taarifa hii kuwasilishwa hapa leo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nimshukuru pia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemaru pamoja na wasaidizi wake pia Waheshimiwa Manaibu Waziri kwa kuendelea kuweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha mezani magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho

vyake kwa wakati. Pia uratibu mzuri wa uwasilishaji wa jedwali la uchambuzi kwa Wizara husika ambazo sheria ndogo zake zimebainika kuwa na dosari. Hali hii kwa muda wote imekuwa ikiwezesha Kamati yetu kufanya majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Manaibu wote wa Wizara mbalimbali pamoja na Watendaji wa Wizara hizo, Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Wizara husika mara nyingi kwa kufika mbele ya Kamati yetu na kujibu hoja zinazoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati hii kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo huwa tunakumbusha siku zote, Kamati ya Sheria Ndogo inaongozwa na Mtemi Andrew Chenge. Huyu ni mtaalamu, mbobeju wa sheria. Taifa hili linaendelea kumtegemea na kufaidi uweledi wake. Sisi Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo tunafaidi zaidi kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Tunaendelea kumpongeza sana kwa kazi kubwa anazofanya kutulea, kutusaidia kutuongoza katika kutekeleza majukumu yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunawashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaopati Kamati yetu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Kamati Ndugu Michael Chikokoto akisaidiwa na Ndugu Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Mkuta Masoli, Ndugu Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndugu Paul Chima, mzee wa kazi huyu kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelzwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufanua matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

### **TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

#### **SEHEMU YA KWANZA**

##### **1.0 UTANGULIZI**

###### **1.1 Maelezo ya awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inahusu majukumu ya uchambuzi wa Sheria Ndogo yaliyotekelzwa na Kamati katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

Taarifa hii imeanisha utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Aidha, Taarifa imebainisha matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali

zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge pamoja na Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Sheria Ndogo hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii vilevile inafafanua kuhusu njia mbalimbali zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati sanjari na mapendekezo ya Kamati kuhusu namna bora ambavyo Bunge linaweza kuisimamia Serikali katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo.

### 1.2 Majukumu ya Kamati na Msingi wa Utekelezaji Wake

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kinabainisha majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kuwa ni kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

Malengo ya masharti haya ya kikanuni ni kulipatia Bunge Mamlaka ya Udhibiti wa Utungaji wa Sheria Ndogo kwa vyombo vingine (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ambavyo Bunge limekasimu kwake mamlaka ya kutunga Sheria kwa mujibu wa Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya **1 (The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002)** imeweka masharti maalum yanayotoa mamlaka kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Msingi huu unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoshauri na kuisimamia Serikali. Hii pia ni kwa sababu Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania. Shughuli hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- a) Kilimo cha mazao ya biashara na chakula;
- b) Ufugaji;
- c) Uvuvi;
- d) Biashara za mama lishe;
- e) Vicoba;
- f) Biashara ya usafiri wa "bodaboda";
- g) Uchimbaji wa madini; na
- h) Utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

### 1.3 Njia Zinazotumika Kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria hiyo inatakiwa kuwasilishwa Bungeni (*laid before the National Assembly*) ndani ya siku sita (6) ya Vikao vya Bunge (*six sitting days*) katika Mkutano husika. Utaratibu huu ni kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1).

Matakwa haya ya Sheria yanapewa nguvu kupitia Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayosomeka kama ifuatavyo:-

**"37. - (2) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri ..."**

Baada ya hatua hiyo, Bunge linakuwa na fursa ya kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa mamlaka inayopatikana katika Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo ambazo hutangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni ni kama zifuatazo:-

- a) Amri (Orders);
- b) Matamko (Proclamations);
- c) Kanuni za Taasisi (Rules);
- d) Kanuni za Mahakama (Rules of Court);
- e) Kanuni za Wizara (Regulations);
- f) Matangazo ya Serikali (Notices);
- g) Sheria Ndogo za Halmashauri (By - Laws); na
- h) Hati Idhini (Instruments).

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hizi hutungwa na vyombo mbalimbali vya Serikali ambavyo vimekasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejivekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-

- a) Kuandaa Orodha ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika kila Mkutano wa Bunge;
- b) Kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa;
- c) Kuandaa Jedwali la Uchambuzi wa Kamati (*Matrix*) linalobainisha matokeo ya Uchambuzi wa Kamati na kuliwasilisha Serikalini ili iandae majibu ya hoja zilizoibuliwa kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni;
- d) Kukutana na Wizara husika (*relevant Ministries*) ili kupokea majibu ya Serikali kutokana na Uchambuzi wa Kamati;
- e) Kuwasilisha Bungeni Taarifa Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo uliofanywa na Kamati na kutoa maoni na mapendekezo ili Bunge liridhie kwa Azimio la Bunge (*Parliamentary Resolution*) kwa ajili ya Utekelezaji wa Serikali;
- f) Kusikiliza Maoni ya Wadau;na
- g) Kufanya mafunzo na semina kuhusiana na Mchakato wa Utungaji wa Sheria Ndogo na namna ya uchambuzi wa Sheria Ndogo.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KATIKA KIPINDI FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020

CHA KUANZIA

#### 2.1 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge

**Mheshimiwa Spika**, katika Kipindi cha kuanzia Februari 2019 hadi Januari 2020 katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo Mia Nane Tisini na Saba (897) ikilinganishwa na Sheria Ndogo Mia Saba na Nne (704) zilizowasilishwa katika kipindi cha Mwaka 2018 – 2019, hivyo kwa mwaka 2019 – 2020 kumekuwa na ongezeko la Sheria Ndogo Mia Moja Tisini na Tatu (193) ambazo ni zaidi ya asilimia 27.4 ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa 2018 - 2019.

Katika kutekeleza jukumu la uchambuzi wa Sheria Ndogo Kamati imebaini jumla ya Sheria Ndogo Sabini na Tatu (73) kati ya Mia Nane Tisini na Saba (897), ni sawa na asilimia 44 zilikuwa na dosari mbalimbali, ambapo Kamati ilitoa Maoni na Mapendekezo ili kuondoa dosari hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo ni Kamati ya Sekta Mtambuka, Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa na dosari au masharti yake kuhitaji ufanuzi wa kina kuhusu maudhui yake, ziligusa Wizara zifuatazo:-

- a) Ofisi ya Waziri Mkuu;
- b) Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira;
- c) Ofisi ya Rais (TAMISEMI);
- d) Wizara ya Fedha na Mipango;
- e) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
- f) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
- g) Wizara ya Mifugo na Uvuu;
- h) Wizara ya Nishati;
- i) Wizara ya Madini;
- j) Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; na
- k) Wizara ya Katiba na Sheria.

#### 2.1.1 **Matokeo ya Uchambuzi Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Saba wa Bunge.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa, Kamati ilibaini kuwepo na dosari mbalimbali na zifuatazo ni baadhi yake:-

- a) Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi;
- b) Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu);
- c) Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria (*Drafting Principles*);
- d) Sheria Ndogo kukiuka misingi ya haki za binadamu; na
- e) Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia (*unreasonable provisions*).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika Mchakato mzima wa Utungaji wa Sheria Ndogo ambazo zinachangia uwepo wa dosari zilizoainishwa katika Sheria Ndogo zilifanyiwa uchambuzi. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- a) Uchache wa wanasheria wenyewe taaluma ya uandishi wa sheria (*legislative drafters*) katika Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uhaba wa wataalamu hao unasababisha Sheria Ndogo nyingi kufika katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali zikiwa tayari zina dosari ambazo zinaweza zisibainike kirahisi na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (*Chief Parliamentary Draftsman*) kwa sababu naye siyo tu kwamba ana wataalamu wachache, lakini pia ana kazi nyingi.
- b) Baadhi ya Wizara kutumia mwanya wa mamlaka waliyopewa na Bunge ya kutunga Sheria Ndogo kwa kuweka masharti ambayo aidha yalikataliwa au kupingwa na Kamati za Kudumu za Bunge wakati wa uchambuzi wa Muswada wa Sheria inayotoa madaraka (*Principal Act*). Kwa kufanya hivyo, Kamati ya Sheria Ndogo imekuwa na jukumu kubwa la kushughulikia dosari za masharti yaliyomo ndani ya Sheria Ndogo ambayo yangeweza kupatiwa uhalali kwa kuyaweka masharti hayo katika Sheria Mama.

c) Baadhi ya Mamlaka zilizokasimiwa Mamlaka ya Kutunga Sheria Ndogo, zimekuwa zikitunga Sheria Ndogo zinazopoka Mamlaka ya vyombo vingine vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria za Nchi ya kusimamia Mamlaka hizo. Mfano baadhi ya Kanuni za Wizara kuwa na vifungu ambavyo utekelezaji wake unaingiliana Mamlaka ya Mahakama. Pili Kanuni kuweka majukumu kwa Waziri anayosimamia na ambayo yanaingiliana na Mamlaka ya Waziri mwagine.

## 2.2 **Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge Serikali imetekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

### 2.2.1 **Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo Mia Moja Tisini na Sita (196) ambapo baada ya uchambuzi wa Kamati ilibainika kuwa jumla ya Sheria Ndogo Kumi na Nne (14) tu ndizo ziliwa na hoja mbalimbali za kiuchambuzi.

Sheria Ndogo hizo ziliwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ilikuwa na Sheria Ndogo Tano (5) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi Kumi na Saba (17); Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilikuwa na Sheria Ndogo Tatu (3) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi Nane (8); na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilikuwa na Sheria Ndogo Sita (6) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi Nane (8).

#### **Mheshimiwa Spika,**

kwa maana ya kulitaarifu Bunge lako tukufu naomba nionyeshe baadhi ya dosari zilioibuliwa na Kamati na baada ya majadiliano na Serikali ambapo ilikubaliana na hoja hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano katika uchambuzi Sheria Ndogo ya **The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Inquiry), Regulations 2018** ambazo zimetungwa chini Sheria ya **The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017**, Kamati ilibaini kuwa **Kanuni ya 3(1)** ilikuwa inakwenda kinyume na Sheria Mama na Sheria nyingine za Nchi, ambapo ilikuwa inaweka utaratibu usio wa lazima kwa malalamiko dhidi ya daktari kuwasilishwa kwa Msajili wa Baraza la Madaktari. **Kanuni ya 3(1)** ilitumia neno “**May**” ambalo kwa mujibu wa **Kifungu cha 53(1)** cha Sheria ya Tafisiri ya Sheria, iwapo neno hilo litatumika linaondoa ulazima wa kufuata utaratibu huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kuwa utaratibu unaowekwa na Kanuni hii ulikuwa Kinyume na **Kifungu cha 41** Sheria Mama **The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017** ambacho kinaweka sharti la lazima la kuwasilishwa malalamiko kwa Msajili kabla ya kufikishwa katika Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo kwa kuwa, Kamati iliona kuwa **Kanuni ya 3(1)** inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1)** cha Sheria ya Tafisiri ya Sheria Sura ya 1 (*Intepretation of Laws Act*) ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vya Sheria Mama vinavyoianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Tafisiri ya Sheria, Kanuni hiyo ya **Kanuni ya 3(1)** ilikuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana na Sheria ya **The Medical, Dental and Allied Health Professionals Act Na. 11 of 2017**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Kamati ilibaini kutofuatwa kwa utaratibu wa uandishi katika Kanuni ya **The Civil Aviation (Security) Regulation 2018** iliyotungwa chini ya Sheria ya **The Civil Aviation Act (Sura 80)**. Kanuni ya 102 (3) inaweka tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Kanuni hizi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia utaratibu mzuri wa uandishi wa Sheria, tafsiri za maneno yaliyotumika mara kwa mara katika Sheria hupaswa kuwekwa katika Kifungu mahsusini kinachotoa tafsiri ya maneno.

Hivyo basi, Kamati ilielekeza tafsiri ya maneno iliyowekwa katika **Kanuni ya 102 (3)** kuwekwa katika **Kanuni ya 4** ya Kanuni hizi kwa lengo la kuzingatia utaratibu mzuri wa uandishi wa sheria ambao pia unarahisisha usomaji mzuri wa Kanuni hizi.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa awali katika Taarifa hii kuwa, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Moja ya Sheria hizo ni **Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, 2018**, ambazo zimetungwa chini **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura 287)**. Kamati ilibaini kuwa na makosa ya uandishi katika rejea za Kanuni zinazoanzisha majedwali.

Kwa mfano, Jedwali la Sheria Ndogo hizi lilitajwa kuanzishwa chini ya **Kifungu 32** cha Sheria Ndogo hizi. Kamati ilibaini rejea sahihi iliyopaswa kuwekwa katika Jedwali hili ni **Kifungu cha 31** ambacho ndiyo chenye maudhui ya sahihi ya Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa Sheria Ndogo, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili Kupokea majibu kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge.

Katika Majadiliano hayo na Kamati, Wizara hizo ziliwasilisha majibu yao ambapo zilikubaliana na hoja za kiuchambuzi thelathini na Tatu (33) zilizoibuliwa na Kamati kutokana na uchambuzi wa Sheria Ndogo Kumi na Nne (14).

Wizara hizo zimeendelea na utaratibu wa kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na mawasiliano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, pamoja na kufanya Mwasiliano na Halmashauri husika ambazo Sheria Ndogo zake zilibainika kuwa na kasoro mbalimbali.

## 2.2.2 **Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge mnamo tarehe 3 Aprili, 2019 Serikali iliwasilisha Bungeni jumla ya Sheria Ndogo Mia Moja Sabini na Nne (174) ambapo baada ya uchambuzi wa Kamati ilibainika kuwa jumla ya Sheria Ndogo Ishirini na Mbili (22) tu ndizo zilikuwa na hoja mbalimbali za kiuchambuzi.

Sheria Ndogo hizo zilikuwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ambayo ilikuwa na Sheria Ndogo Kumi na Moja (11) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi Kumi na Nane (18), Wizara ya Fedha na Mipango ilikuwa na Sheria Ndogo Mbili (2) iliyokuwa na hoja ya kiuchambuzi Tatu (3), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilikuwa na Sheria Ndogo Moja (1) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi Mbili (2) Wizara ya Nishati ilikuwa na Sheria Ndogo Mbili (2) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi Kumi na Moja (11), Wizara ya Madini ilikuwa na Sheria Ndogo Tatu (3) zilizokuwa na hoja za kiuchambuzi kumi na mbili (12), na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilikuwa na Sheria Ndogo Tatu (3) zilizokuwa hoja za kiuchambuzi Nane (8).

**Mheshimiwa Spika**, kwa maana ya kulitaarifu Bunge lako tukufu naomba kuonesha baadhi ya dosari zilizoibuliwa katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge ulibaini uwepo wa Sheria Ndogo zenyenye maudhui yanayokwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo iliyobainika kuwa na dosari ni **Sheria Ndogo za (Ada za Vibali vya Burudani) za Halmashauri ya Jiji la Tanga, 2019** iliyo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kamati ilibaini kwamba Sheria Ndogo hizi zilifanya rejea ya kuanzishwa chini ya **Sura 290 ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa** wakati zina kichwa kinachosomeka **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)**, ambayo ni **Sura 288**.

**Mheshimiwa Spika**, utungaji wa Sheria Ndogo yoyote hutokana na Sheria Mama, hivyo utaratibu wa uandishi wake ni lazima ufanye rejea sahihi ya Jina la Sheria Mama pamoja na Kifungu kinachotoa Mamlaka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo husika (*enabling provision*). Hivyo basi, Kamati iliona kuwa Sheria Ndogo imekiuka Sheria Mama kwa kurejea Jina tofauti la Sheria inayopianzisha.

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya ukiukwaji wa Sheria Mama pia ilibainika katika Sheria Ndogo za **The Petroleum (Natural Gas) (Regulatory Accounting and Reporting Standards) Rules 2019** ambazo zimetungwa chini ya **The Petroleum Act (Sura 392)** zilizo chini ya Wizara ya Nishati.

Kamati ilibaini **Kanuni ya 13 (2)** ya Kanuni hizi zinaweka faini ya **Shilingi Milioni Kumi** au kifungo kisichopungua miaka miwili au vyote (faini na kifungo) kwa kosa la kumzuia Afisa wa EWURA kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kuwa, adhabu hii ni tofauti na ile inayocainishwa katika **Kifungu cha 234 (a) cha Sheria ya Petroli, 2015** ambacho kinataja kuwa, mtu ye yeyote atakayetenda kosa la kumzuia Afisa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Ishirini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote (faini na kifungo).

**Mheshimiwa Spika**, hivyo kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni ya **Kanuni ya 13 (2)** inakuwa ni batili kwa kiwango inachokinzana na **Kifungu cha 234 (a) cha Sheria ya Petroli, 2015**.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, baada ya kukamilika kwa uchambuzi wa Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili Kupokea majibu kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge. Katika Majadiliano hayo na Kamati, Wizara hizo ziliwasilisha majibu yao ambapo zilikubaliana na hoja za kiuchambuzi hamsini na nne (54) zilizoibuliwa. Wizara hizo zimeendelea na utaratibu wa kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, pamoja na Halmashauri husika ambazo Sheria Ndogo zake zilibainika kuwa na kasoro mbalimbali.

## 2.3 Mikutano ya Kamati na Wadau

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari 2019 hadi Januari, 2020 Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau mbalimbali wanaoguswa na Sheria Ndogo zinazochambuliwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau wa sekta mbalimbali za afya kutoka Chama cha Madaktari na **Tanzania Dental Society Association (TDSA), TAMSA, Association of Medical Practitioners Tanzania (AMEPTA) na Association of Physiotherapists (APTA)**, lengo la kukutana na wadau lilikua ni kupata uelewa na maoni yao kuhusu utekelezaji wa Sheria Ndogo **The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Internship), Regulations 2018, The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Fees and Charges), Regulations 2018, The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Inquiry), Regulations 2018; na The Medical, Dental and Allied Health Professionals (Continuing Professional Development), Regulations 2018** ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge.

Aidha, Kamati ilipata fursa ya kukutana na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Tanzania Bus Owners Association) na kujadiliana kuhusu Kanuni zilizotengenezwa chini ya Sheria ya The **Land Transport Regulatory Authority Act, No. 2019** na Kanuni zilizotengenezwa chini ya Sheria ya Transport Licencing Act.

#### 2.4 **Uchambuzi wa Miswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2019] na Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 (The Arbitration Bill, 2020)**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2019 hadi Januari, 2020 Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo ilifanya uchambuzi wa Miswada Miwili ya Sheria.

Mnamo tarehe 4 Septemba, 2019, wakati wa Kikao cha Pili cha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.6 wa Mwaka 2019 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2019] ulisomwa mara ya kwanza Bungeni. Baada ya hapo, Mheshimiwa Spika alizingatia masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati iliujadili Muswada huo uliopendekeza kufanya marekebisho katika katika Sheria Tisa ukiwa na Ibara Mia Moja (100). Aidha, mnamo tarehe 12 Septemba, 2019 Kamati iliandaa Maoni na Ushauri wa Kamati na kuwasilisha Bungeni kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile mnamo tarehe 28 Januari, 2020, wakati wa Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge, **Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 (The Arbitration Bill, 2020)** ulisomwa mara ya kwanza Bungeni. Baada ya hapo, Mheshimiwa Spika alizingatia masharti ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kuupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Kamati inaendelea na taratibu za uchambuzi wa Muswada huo ambao taarifa yake itawasilishwa kwa mujibu ya Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge.

#### 2.5 **Semina/Mafunzo Mbalimbali**

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Februari 2019 hadi Januari 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ilipata fursa ya kushiriki katika kwa lengo la kujengewa katika maeneo mbalimbali. Semina hizo zilijikita katika maeneo yafutayo:-

- a) Masuala ya Kupambana na Madawa ya Kulevyा;
- b) Kanuni mbalimbali zinazohusu sekta ya Madini;
- c) Dhana Kuu ya Jinsia na Uchambuzi wa mfumo wa dhana ya kijinsia katika fikra ya kinadharia na vitendo;
- d) Mfumo wa kisheria na kisera kuhusu masuala ya jinsia na jinsi ya kuhusisha masuala ya jinsia katika shughuli/kazi za msingi za Bunge;
- e) Uchambuzi wa Mapitio ya Bajeti;

- f) Kanuni za vyombo vya usafirishaji;
- g) Masuala yanayohusu watu wenyewe Ulemavu; na
- h) Maliasili.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikiri kuwa kupertia Semina hizo Wajumbe wa Kamati walipata uelewa mkubwa zaidi katika maeneo mbalimbali, hivyo kurahisisha katika utekelezaji wa jukumu la Uchambuzi wa Sheria Ndodo.

### SEHEMU YA TATU

#### 3.0 **Uchambuzi wa Sheria Ndodo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii pia inahusisha uchambuzi wa Sheria Ndodo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita na Kumi na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge. Uchambuzi wa Sheria Ndodo hizo pia umetekelezwa na Kamati katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, hata hivyo taarifa zake hazikuwasilishwa Bungeni kama ilivyokuwa kwa Sheria Ndodo zilizowasilishwa Mezani katika Mkutano wa Nne na Mkutano wa Kumi na Tano, ambazo taarifa yake iliwasilishwa Bungeni mnamo tarehe 13 Septemba, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ridhaa yako naomba niwasilishe uchambuzi wa Sheria Ndodo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi Sita na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge ili Bunge liweze kuazimia maoni na mapendelekezo ya Kamati.

#### 3.1 **Uchambuzi wa Sheria Ndodo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 6 Septemba, 2019 katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani jumla ya Sheria Ndodo **Mia Tatu Sitini na Moja (361)** kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Sheria Ndodo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

- a) Sheria Ndodo za Halmashauri (*By-Laws*) -97;
- b) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 31;
- c) Kanuni za Taasisi (*Rules*) - 7;
- d) Amri (*Orders*) – 182;
- e) Matangazo (*Notices*) – 41; na
- f) Proclamations – 3.

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo wa Sheria Ndodo ulioainishwa, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndodo Ishirini na Saba (27). Baada ya Uchambuzi wa Kanuni hizo Kamati imetoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha maudhui ya Kanuni hizo kama inavyonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** lililoambatishwa. Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, baadhi ya dosari zilizobainika katika Kanuni hizo ni kama ifuatavyo:-

##### **a) Sheria Ndodo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndodo zilizotungwa na Wizara (*Regulations*) zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria

Nyingine za Nchi. **Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria** ambacho kinabainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote haipaswi kukinzana na masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya **The Explosives (Manufacturing) Regulations, 2019 (GN. Na. 422)**, ambazo zimetungwa chini Sheria ya **The Explosives Act Cap. 45** na kubaini kuwa **Kanuni ya 15** inataoa adhabu kwa mtu atakayevunja masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi kuwa ikiwa ni mtu, basi itakuwa ni faini isiyozidi milioni ishirini au kifungo kisochozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja. Ikiwa aliyejukua masharti ya Kanuni hii ni Kampuni, adhabu yake ni faini isiyopungua milioni hamsini.

Kamati iliona kwamba masharti yanayowekwa kwa mujibu wa Kanuni hiyo ni kinyume na Adhabu hizi ni Kinyume na **Kifungu cha 7(2)** cha Sheria Mama, kinachoweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka saba au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo. Aidha Sheria Mama haijaweka adhabu kwa kuzingatia suala la mtu au kampuni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa, **Kanuni ya 15** ya Kanuni hizi inaenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika **Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 (Interpretation of Laws Act)** ambacho kinaelekeza kwamba, Sheria Ndogo haipaswi kwenda kinyume na vifungu vyta Sheria Mama inayioianzisha au Sheria yoyote ya Nchi. Hivyo kwa mantiki ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kanuni hiyo ni batili kwa kiwango inachokinzana na Sheria ya Mama.

**b) Sheria Ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa Sheria (Drafting Principles)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo ya **The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2019 (GN. Na. 382)** zilizoanzishwa chini ya Sheria ya **The Electricity Act Cap.131**.

Katika uchambuzi huo Kamati imebaini dosari za uandishi ambapo **Kanuni ya 17** inaelekeza kuwa mfano wa Cheti baada ya kukamilisha **Installation Work** kinaonekana katika **Jedwali la Nne** la Sheria Ndogo hii, hata hivyo **Jedwali** halijaonesha Cheti hicho, hali inayoleta changamoto ya kufahamu juu ya yale yanayopaswa kuwepo katika cheti hicho.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilibaini kutozingatiwa kwa utaratibu wa uandishi katika Sheria Ndogo ya **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, 2019 (GN. Na. 530)** iliyotungwa chini ya **Sheria ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290)**.

Kamati ilibaini kuwa, Sheria Ndogo ina makosa ya kutokuweka namba za vifungu vidogo katika maelezo yanayofuata mara baada ya **Kifungu cha 5(5)**. Kukosekana kwa nambari za vifungu katika maneno hayo kunayafanya maandishi haya kukosa nguvu ya Kisheria na pia itapelekea changamoto wakati wa kufanya rejea.

**c) Masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia katika utekelezaji wake ni **The Anti- Money Laundering (Electronic Funds Transfer and Cash Transaction Reporting) Regulations, 2019 (GN. Na. 420)** ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya **The Anti – Money Laundering Act Cap. 423**.

Uchambuzi umebaini kuwa **Kanuni ya 13** inaipa **Financial Intelligence Unit (FIU)** nguvu ya kuwawekea vikwazo vyta kiutawala **reporting persons** ikiwemo kusitisha leseni za biashara, kusitisha baadhi ya shughuli za kibiashara, kutoza faini isiyopungua shilingi milioni moja na

isiyozidi milioni tano kwa siku na kwa kuzingatia siku ambazo makosa yamefanyika kwa kumsimamisha au kumuondoa kazini mfanyakazi wa taasisi husika aliyeshindwa kutoa taarifa za miamala ya fedha inayopaswa kutolewa taarifa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa Masharti ya **Kanuni ya 13** hayana uhalisia kwa kuwa utekelezaji wake hauwekezani, kwa kuwa masharti hayo yanatekelezwa na mamlaka nyingine kwa mujibu wa Sheria za Nchi. Mfano suala la kumuondoa kazini mfanyakazi wa Taasisi iliyoshindwa kuwasilisha tarifa za miamala za fedha, kimsingi haliwezi kutekelezwa na FIU badala yake linaweza kutekelezwa na mwajiri wa mfanyakazi wa Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini **Sheria Ndogo za (Ada na vibali vya Shughuli za Kiutamaduni) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, 2019 (G.N Na. 532)** zilizotungwa chini ya **Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Sura ya 290)** zimeweka masharti yasiyo na uhalisia.

**Kifungu cha 4** kinatoa sharti kwamba, Mtu yejote hatoruhusiwa kuendesha shughuli yoyote ya kiutamaduni ndani ya eneo la Halmashauri bila ya kupata kibali kutoka Halmashauri. Hii inatokana na **Kifungu cha 3** kinachotoa tafsiri ya maneno mbalimbali ambacho kimetafsiri shughuli za kiutamaduni kuwa ni pamoja na mikusanyiko ya msiba.

Kamati inaona kwamba, masharti haya hayana uhalisia katika utekelezaji wake kwa kuwa yatapelekea shughuli za mikusanyiko ya msiba kulazimika kuomba kibali cha kukusanyika pasipo kuzingatia ukweli kwamba shughuli za msiba pindi zinapotokea watu hukusanyika pasipo kuhitaji kibali kwa kuzingatia mila na desturi za kitanzania.

d) **Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)**

**Mheshimiwa Spika**, makosa ya kiuandishi yamebainika katika Sheria Ndogo za **(Ushuru na Uendeshaji wa Soko la Samaki Feri - Magogoni) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (G.N. Na. 603)**, ambazo zimetungwa chini Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura ya 290).

Katika uchambuzi uliofanyika, Kamati imebaini dosari katika rejea za Kanuni zinazoanzisha majedwali. Kwa mfano, Jedwali la Nne kuhusu kufifilisha kosa limerejea kuanzhishwa chini ya Kifungu cha 33 ambacho hakipo katika Sheria Ndogo hizi na kubaini kuwa Kifungu sahihi kinachohusu kufifilisha kosa ni kifungu cha 32.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati pia ulibaini pia Sheria Ndogo za **Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, 2019 (GN.Na. 239)** kuna mapungufu katika mpangilio wa Majedwali, ambapo inatoka Jedwali la Tatu na kwenda Jedwali la Sita, wakati Sheria haina Jedwali la Nne na Tano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa, ni vema uandishi wa Majedwali katika sheria uzingatie kurejea Kanuni sahihi zinazoanzisha majedwali husika, kwa kuwa Majedwali ni sehemu ya Sheria kwa lengo la kufafanua zaidi masharti ya utekelezaji wa Kanuni mbalimbali katika Sheria Ndogo. Hivyo kwa kutorejea vifungu sahihi sio tu inaondoa maana ya masharti ya Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinacho tambua Majedwali kuwa ni sehemu ya sheria, bali pia dosari hizo zinaleta changamoto katika usomaji mzuri wa sheria husika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ilikutana na Wizara zote zilizoguswa na uchambuzi wa Sheria Ndogo ishirini na saba (27) zilizowasilishwa katika Mkutano wa kumi na Sita wa Bunge, ambapo Wizara hizo zilikubaliana na hoja zote na kuahidi kuanza mchakato wa marekebisho ili kuondoa kasoro zilizobainika.

### 3.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Saba Bunge

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 12 Novemba, 2019 katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani jumla ya Sheria Ndogo **Mia Moja Sitini na Sita (166)** kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Sheria Ndogo hizo zimegawanyika katika makundi yafuatayo:-

- a) Sheria Ndogo za Halmashauri (By- Laws) – 31;
- b) Kanuni za Wizara (Regulations) -16;
- c) Amri (Orders) – 57; na
- d) Matangazo (Notices) – 62.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kubaini dosari mbalimbali katika Sheria Ndogo Kumi (10), ambapo imetoa Maoni na Mapendekezo kwa lengo la kuboresha maudhui ya Sheria hizo kama inavyoonekana katika **JEDWALI LA UCHAMBUZI** liiloambatishwa. Kwa ajili ya kulitaarifu Bunge kuhusu uchambuzi uliofanyika, naomba kuainisha baadhi ya dosari kama ifuatavyo:-

#### a) Sheria Ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo zilizotungwa na Wizara (Regulations) zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria Nyingine za Nchi. Mfano wa Sheria hizo ni **The Meat Industry (Inspection of Meat Industry Stakeholders Activities) Regulations, 2019 (GN. Na. 739/2019)** ambazo zimetungwa chini Sheria ya **The Meat Industry Act (Sura ya 421)**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, **Kanuni ya 17** inaweka adhabu tofauti na iliyoinishwa chini ya Sheria Mama, kwamba iwapo mtu akipatikana na hati ya kumzuia Mkaguzi kutekeleza majukumu yake, atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisochopungua miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja. Wakati **Kifungu cha 32** cha Sheria Mama kimeweka adhabu kwa kosa hilohilo kuwa ni faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichoziidie miezi sita au vyote kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, adhabu inayowekwa na Kanuni hizi ni kinyume na masharti ya **Kifungu cha 36 (1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ambacho kinabainisha kwamba, Sheria Ndogo yoyote haipaswi kukinzana masharti ya Sheria ya Bunge inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote.

#### b) Sheria Ndogo kuwa na makosa ya uandishi katika Majedwali (Kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu)

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati pia ulibaini Sheria Baadhi ya Sheria Ndogo kuwa na doasri katika majedwali na vifungu vinavyoanzisha Majedwali husika. Moja ya Sheria Ndogo zenye dosari hizo ni **The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2019 (GN Na. 676)** ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya **The Environmental Management (Act Sura 191)**.

Kamati ilibaini kuwa Jedwali la Nne limefanya rejea ya **Kanuni ya 16(1)** ambayo si rejea sahihi kwa kuwa, **Kanuni ya 16(1)** inaaniszisha **Jedwali la Tano**. **Kamati iliono kwamba**, Kanuni sahihi zinazoanzisha Jedwali la Nne ni **12(1) na 28**.

**c) Masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini uwepo wa Sheria Ndogo zilizo na masharti yasiyokuwa na uhalisia kwa kuzingatia utakelezaji wake. Masharti haya yamebainika katika **Sheria Ndogo za The Microfinance (Community Microfinance Groups) Regulations, 2019** zilizotungwa chini ya **The Microfinance Act**, (Sura ya 407).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa **Kanuni ya 4(2)** inaweka sharti kwamba, *Community Microfinance Groups* inaweza kuanzishwa na watu kuanzia kumi hadi hamsini. Aidha, Kanuni hii inazuia watu zaidi ya hamsini kuanzisha *Community Microfinance Groups*.

Kamati ina maoni kwamba, ukomo wa juu uliowekwa na Sheria Ndogo hizi unakosa uhalisia kwa kuwa vikundi vingi vina wanachama zaidi ya hamsini, hivyo sharti la kuweka ukomo wa wanachama hamsini linaweza kuleta changamoto ya vikundi vingi kuvunjika ili kuendana na sharti hilo. Aidha, sharti hilo linazuia watu wengi zaidi walio katika malengo yanayofanana kujunga katika *Community Microfinance Groups*.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ilikutana na Wizara zote zilizoguswa na uchambuzi wa Sheria Ndogo kumi (10) zilizo wasilishwa katika Mkutano wa kumi na Saba wa Bunge, ambapo Wizara hizo zilikubaliana na hoja zote na kuahidi kuanza mchakato wa marekebisho ili kuondoa kasoro zilizobainika.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**4.1 Maoni ya Jumla**

a) Kamati inashauri kuwa, ni vema Kanuni za *The Microfinance (Community Microfinance Groups) Regulations, 2019* (GN. 678) zikawekewa masharti mepesi ambayo utekelezaji wake hautaleta changamoto kwa watumiaji wake ambao wengi wao ni wananchi wa vipato vyta chini.

b) Kanuni za *The Microfinance (Community Microfinance Groups) Regulations, 2019* (GN. 678) zitafsiriwe kwa Kiswahili. Pia majedwali yaliyoambatishwa yawekwe kwenye lugha nyepesi itakayosaidia wananchi kuelewa ili kupunguza changamoto kwa walengwa wa Kanuni hizi ambao wengi wao hawana elimu wala ujuzi wa masuala yanayohusiana na fedha.

c) Kanuni za *The Microfinance (Community Microfinance Groups) Regulations, 2019* (GN. 678) zirejee tafsiri ya *Community Microfinance Groups* iliyotolewa Sheria Mama ya *The Microfinance Act*, (Sura ya 407) ambayo imeweka wazi makundi yanayoguswa na pia kuweka exceptions kwa makundi yasiyoguswa na Kanuni hizi. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kuondoa changamoto kwa watumiaji wa Kanuni hizi katika kufahamu aina za shughuli za vikundi zinazoguswa na Kanuni hizi.

d) Kwamba, Wizara ya Fedha na Mipango itoe Miongozo kwa Halmashauri ambazo ndizo zimekasimiwa jukumu la usimamizi wa *Community Microfinance Groups*. Miongozo hiyo, iainishe mambo muhimu kama vile wajibu wa Halmashauri kwa Vikundi hivyo, namna ambavyo vikundi hivyo vitakavyolelewa ikiwa ni pamoja na kupewa elimu ya masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa fedha.

e) Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa Bungeni tangu Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na

Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge ambazo zimebainika kuwa na dosari, ili kuondoa dosari hizo na kuzitangaza katika Gazeti la Serikali kufikia Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge.

f) Kamati inashauri Mamlaka zinazopewa jukumu la kutunga Sheria Ndogo zishirikishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika hatua za uandaaji wa Sheria Ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

g) Kamati inaishauri Serikali iendelee na programu za utoaji wa mafunzo ya uandishi wa sheria kwa Maafisa Sheria. Mafunzo hayo yatasaidi kupunguza makosa ya uandishi katika Sheria Ndogo kabla ya Sheria Ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

h) Kamati inashauri kuwa, Mamlaka au Taasisi zilizokasimiwa Mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo zishirikishe wadau katika hatua za awali za uandaaji wa Sheria Ndogo. Lengo ni kupunguza au kuondoa changamoto mbalimbali ambazo zinaweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo husika.

#### 4.2 **Maoni na Mapendekezo kwa Serikali Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge;**

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo haya yameandalowiwa kwa muhtsari kuzingatia matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Saba Bunge na yamefafanuliwa kwa kirefu katika Jedwali la Uchambuzi ambalo limeambatishwa na Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

##### 4.2.1 **Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria**

**KWA KUWA**, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali katika majedwali kuhusu vifungu vinavyoanzisha majedwali husika;

**NA KWA KUWA**, kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba Majedwali ni sehemu ya Sheria;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifaniwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

##### 4.2.2 **Kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.**

**KWA KUWA**, baadhi ya Sheria Ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi;

**NA KWA KUWA**, kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Sheria Ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi;

**NA KWA KUWA**, kukinzana huko kunaharamisha Kanuni husika kwa kiwango ilichokinzana na Sheria Mama;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, zifanye marekebisho katika Sheria Ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama au na Sheria nyingine za nchi.

##### 4.2.3 **Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria (Drafting Principles)**

**KWA KUWA**, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kwamba baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari mbalimbali za kiuandishi;

**NA KWA KUWA**, dosari hizo zimesababisha mantiki na madhumuni yaliyokusudiwa katika vifungu husika kutofikiwa na hivyo kuleta changamoto katika utekelezaji wake;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

#### 4.2.4 **Masharti yasiyo na uhalisia ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini.**

**KWA KUWA**, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwepo kwa dosari zinazoweka vifungu vyenye masharti yasiyo na uhalisia;

**NA KWA KUWA**, kwa dosari hizo zinaweza kupelekea kuwepo ugumu katika utekelezaji wake na hivyo kukandamiza wanaolengwa na Sheria Ndogo husika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika vifungu vyenye masharti yasio na uhalisia zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

#### 4.2.5 **Kukiuka Misingi ya Haki za Binadamu**

**KWA KUWA**, katika uchambuzi wa Kamati imebainika Sheria Ndogo kuwa na dosari ya kuweka kifungu kinachokiuka misingi ya haki za binadamu;

**NA KWA KUWA**, kwa dosari hizo zinaweza kupelekea kuminya haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuvi yaliyotolewa na vyombo vyenye Mamlaka ya kutoa maamuvi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Wizara ambayo Sheria Ndogo yake imebainika kuwa na dosari za kuweka kifungu kinachokiuka misingi ya haki za binadamu, ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

### SEHEMU YA TANO

#### 5.0 **HITIMISHO**

##### 5.1 **Shukrani**

**Mhesimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa Taarifa hii ya Mwaka 2019 – 2020 ni ya mwisho katika uhai wa Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa za Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Kimsingi Taarifa hizo ziliweka wazi dosari mbalimbali zilizobainika katika Sheria Ndogo zilizochambuliwa na Kamati kwa kipindi cha Mwaka huu na miaka iliyopita.

Hivyo tunaamini kwamba, Maoni na Ushauri wa Kamati kupitia Taarifa hizo kumeongeza tija kwa kuweza kuisaidia Serikali kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo zilizochambuliwa na hatimaye kutolewa na Maoni na Ushauri wa Kamati.

**Mhesimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne, Mkutano wa Kumi na Tano, Mkutano wa Kumi na Sita na Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge na hatimaye kufanikisha Taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

- |                                      |              |
|--------------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Andrew John Chenge, Mb -     | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. William Mganga Ngeleja, Mb - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb -    | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Khamis Mtumwa Ali, Mb -      | Mjumbe       |
| 5. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb -    | Mjumbe       |

6. Mhe. Mlinga Goodluck Asaph, Mb -	Mjumbe
7. Mhe. John John Mnyika, Mb -	Mjumbe
8. Mhe. Halima James Mdee, Mb -	Mjumbe
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb -	Mjumbe
10. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mb -	Mjumbe
11. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb -	Mjumbe
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb -	Mjumbe
13. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb -	Mjumbe
14. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb -	Mjumbe
15. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb -	Mjumbe
16. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb -	Mjumbe
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb -	Mjumbe
18. Mhe. Mary Deo Muro, Mb -	Mjumbe
19. Mhe. Easther Lukago Midimu, Mb -	Mjumbe
20. Mhe. Catherine Nyakao Ruge, Mb -	Mjumbe
21. January Yusuf Makamba, Mb -	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Jenista Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (Sheria Ndogo) kwa wakati, pia uratibu mzuri wa uwasilishaji wa Jedwali la Uchambuzi kwa Wizara husika ambazo Sheria Ndogo zake zimebainika kuwa na dosari. Hali hii kwa muda wote imekuwa ikiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Wizara mbalimbali pamoja na Watendaji wa Wizara hizo, kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizoijiteza katika Sheria Ndogo.

Kwa heshima na taadhima naomba nitambue Wizara hizo kama ifuatavyo:-

1. Ofisi ya Waziri Mkuu;
2. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
3. Wizara ya Maji na Umwagiliaji;
4. Ofisi ya Rais (TAMISEMI);
5. Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira;
6. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
7. Wizara ya Fedha na Mipango;
8. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
9. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji;
10. Wizara ya Mifugo na Uvuvu;
11. Wizara ya Nishati;
12. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;
13. Wizara ya Kilimo;
14. Wizara ya Katiba na Sheria; na
15. Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaopatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Kamati Ndg. Michael Chikokoto akisaidiwa na Ndg. Gerald Magili Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg.

Stanslaus Kagisa wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 5.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelawa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufafanua matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili, na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Andrew J. Chenge

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGUE YA SHERIA NDOGO**

4 Februari, 2020

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa William Ngeleja kwa taarifa hiyo; na hoja imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Sasa tunaanza na uchangiaji wetu. Tunaanza na Mheshimiwa Lolesia, Bukwimba baadaye Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika taarifa hizi za Kamati. Kwanza nianze kipekee kabisa kuwapongeza Wenyeviti wote pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi kwa kazi kubwa ambayo imefanyika. Kusema ukweli mmechambua vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita zaidi katika Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu shughuli zake za utekelezaji katika mwaka uliopita. Kabla sijaanza, nitoe kabisa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu tulikuwa na changamoto kubwa sana katika upande wa Sekta ya Afya lakini Serikali kupitia Mheshimiwa Rais ameweza kutupatia hospitali ambayo itajengwa katika eneo la Mji Mdogo Katoro, pia ni hospitali ambayo ni ya Umoja pamoja na Uselesele. Hii yote ni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Serikali za Mitaa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kwa kweli Serikali inafanya mambo makubwa sana hasa katika Serikali za Mitaa. Wote tumeshuhudia jinsi ambavyo mambo mengi yamefanyika. Siku za nyuma ilikuwa ni changamoto kubwa sana katika Sekta ya Afya, lakini kwa kweli kwa sasa hivi tunaona jinsi ambavyo Serikali inafanya mambo makubwa sana kupitia TAMISEMI. Tumeona katika Sekta ya Afya lakini pia katika Aekta ya Elimu Serikali imeendelea kutekeleza mambo mengi kwa kushirikiana na wananchi. Yote haya nina kila sababu ya kuweza kushukuru na kuipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nilitaka kulizungumza hapa ni suala kubwa kuhusu barabara ambazo ziko chini ya TARURA. Kamati imezungumzia vizuri sana katika ukurasa wa tisa wa taarifa hasa ya Kamati ya Utawala wa Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa barabara kupitia TARURA. Ni kweli kwamba barabara za TARURA zina changamoto kubwa sana na nilikuwa ninaomba kama ambavyo Kamati imeshauri, kwamba kutokana na ufinyu wa bajeti kwa bajeti zilizopita na mwaka huu tumeshuhudia kwamba kuna mvua nyingi sana ambazo zinaendelea Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali katika bajeti ijayo kama ambavyo Kamati imesema kwamba waangalie uwezekano mkubwa wa kuweza kuongeza bajeti hasa katika TARURA ili kuweza kushughulikia barabara ambazo imekuwa ni changamoto kubwa sana. Tukiangalia kila sehemu katika nchi yetu ya Tanzania mvua zinanyesha kwa wingi lakini pia barabara hazipitiki kwa kiasi kikubwa, madaraja yamebomeka. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali sasa pengine iangalie sana suala hili la TARURA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia, nami pia nikiangalia kwenye Jimbo langu ninaona kabisa kwamba bajeti za TARURA zinakuwa ni kidogo barabara za TARURA ni nyingi, lakini bajeti inayotengwa ni kidogo. Kwa hiyo, kama Mbunge nilikuwa naishauri Serikali iangalie suala hili kwa sababu barabara ndiyo kiungo kikubwa katika maendeleo ya jamii katika maeneo yetu ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona jinsi ambavyo mwananchi hawesi kusafiri kutoka point moja kwenda point nyingine. Kama barabara haipo kwa kweli changamoto inakuwa ni kubwa. Kwa hiyo, naomba sana kama ambavyo Kamati imesema, tuombe TARURA iongeze bajeti ya kutosha ili kuweza kuboresha barabara za mijini na vijijini ili hatimaye tuweze kuona utekelezaji na uboreshaji wa huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika upande wa TAMISEMI tumeshuhudia jinsi ambavyo Serikali inajenga Hospitali na Vituo vya Afya vilivyoboreshw; tunaipongeza sana. Nilikuwa naomba sasa katika bajeti ijayo pengine Serikali iangalie umuhimu wa kuongeza watumishi katika sekta hasa ya Afya ambapo tuna upungufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika sehemu mbalimbali Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wanalamikia kwamba kuna upungufu mkubwa wa watumishi, ikiwemo pia kwenye halmashauri yangu kwakweli kuna upungufu mkubwa sana ambapo wanahitajika zaidi ya watumishi 200 katika Seta ya Afya.

Kwa hiyo nilikuwa ninaomba pengine Serikali kwa kuwa imeboresha zaidi katika miundombinu hasa kwa kujenga vituo vya afya na hospitali, nilikuwa naomba katika bajeti zizajo iangalie uwezekano wa kuangalia suala zima la kuhakikisha watumishi wanapatikana wa kutosha ili sasa tuweze kuhakikisha kwamba huduma sasa inaboreshw vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki wananchi wanahuduria kliniki au kwenye vituo vya afya, lakini kwa sababu ya wingi wa watu unakuta watumishi wanakuwa wachache, na hatimaye kunakuwa na changamoto kubwa sana katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Serikali imeboresha kwa kiasi kikubwa, imeongeza dawa za kutosha; na ukiuliza hata sasahivi vijijini watu wanafurahia sana huduma kwa kiasi kikubwa. Juzi nilikuwa napigwi simu naambiwa hata ukienda katika hospitali ya Rufaa ya Wilaya na hata ile ya Mkoa tumeshuhudia kwamba wazee wametengewa sehemu maalum kwa ajili ya kupewa huduma. Kwa kweli huduma zimeboreshwa vizuri, lakini tu ni mpungufu madogo hasa katika upungufu wa watumishi katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pamoja na sekta ya afya, napenda tu kuomba mimi binafsi kwenye jimbo langu tumeshuhuda Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwamba kila halmashauri ihamie kwenye maeneo yao ya utawala. Sisi katika halmashauri yetu, ofisi yetu ya halmashauri imehamia Nzela, ambako kidogo ni mbali kiasi kwamba baadhi ya wananchi ndani ya halmashauri wanapata shida kubwa sana katika kuzifikia huduma hizi katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitumie fursa hii kuiomba Serikali pia iangalie changamoto hizi. Najua inazifanya kazi, lakini naomba sasa iharakishe jambo hili, ipitie hizi halmashauri ambazo zimefanya maamuzi ya kuhamia kwenye maeneo yao ya utawala kuangalia kama kuna changamoto ili hatimaye kuweza kuzirekebisha.

Nilipokuwa jimboni kwakweli maeneo mengi hasa vijiji watu wamekuwa wakiniulizia sana kuhusu suala hili, hasa la kuhamishiwa Halmashauri Nzela; ambako sasahivi zaidi ya kilometra 100 wananchi wanahangaika kwenda kufuata huduma. Hili pengine pia limechangia hata mapato kushuka, kwa sababu wengine wanajuliza niende kweli, nikaandikiwe kibali Nzela kule halafu nije nilipe mapato. Kwa hiyo kumekuwepo pia changamoto kubwa sana katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimepata nafasi nilikuwa naomba tu Serikali iweze kuliangalia suala hili hasa kwangu kwa sababu watu wengi sana wanapata changamoto, kama ilivyofanya katika Halmashauri ya Lindi, Mkoa wa Lindi pamoja na Mkoa wa Morogoro, iweze kufanya marekebisho basi na kwenye mikoa baadhi kama halmashauri yangu ya Geita basi Serikali iangalie itusaidie, itupatие halmashauri mpya. Kama hakuna uwezekano huo basi Serikali iangalie namna utaratibu mzuri ili wananchi waweze kupata huduma kwa karibu kwa sababu lengo la Serikali ni kuona kwamba wananchi wanapata huduma kwa karibu zaidi kuliko kwenda kufuata huduma mbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja kwa ajili ya Kamati hizi. Najua mambo mengi mazuri yamezungumzwa, nikiamini kwamba Serikali inasikiliza na kuweza kuyafanya kazi yaliyobakia. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. Tunaendelea na Mheshimiwa Pauline Gekul, baadaye Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Godbless Lema wajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ambayo iko mbele yetu, na ninaomba nitangulie kuunga mkono hoja kwa asilimia 100, lakini pia niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote pamoja na Wajumbe ambao wametuletea taarifa hii ambayo imefanyiwa kazi kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba bado saa chache, Chama chetu Chama Cha Mapinduzi kuadhimisha miaka 43 ya kuzaliwa, naomba niendelee kuitakia kheri katika kuongoz anchi yetu na taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia mambo matano. Naomba niishauri Serikali yangu mambo matano ambayo nafikiri kwamba yanaweza yakwasaidia wananchi wetu, na nitachangia zaidi TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza niipongeze Serikali na TAMISEMI kufikia makusanyo ya zaidi ya asilimia 69 katika halmashauri zetu. Naamini halmashauri zetu zinajitahidi kukusanya. Niishauri Serikali yangu kwamba pamoja na makusanyo haya kuna sababu ya kukaa na wakurugenzi wetu ili kuangalia vyanzo vingine vya kuwasaidia zaidi waendelee kukusanya. Lakini kama tutawashauri, ni vizuri sasa TAMISEMI pia tukae na wakurugenzi tuhakikishe zile asilimia 40 za maendeleo zinapelekwa katika miradi ya maendeleo. Nasema hili kwa sababu tukikusanya tusipopeleka kwenye miradi ya maendeleo tukaiachia Serikali kuu iwe inapeleka fedha za kukamilisha maboma ya madarasa na zahanati nafikiri Serikali Kuu itazidiwa. Kwa hiyo pamoja na kazi nzuri hii inayofanywa ya kukusanya fedha hizi, lakini sasa zirudi kukamilisha maboma na zahanati ambazo wananchi wamezinyanya zimebakia tu *finishing*. Kwa hiyo naamini Serikali, hili mtaliangalia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo natamani sana niishauri Serikali. Hali za barabara zetu si nzuri sana; niombe, ifikie muda sasa wa Serikali yetu kufanya maamuzi ya dhati kwa TARURA kupewa asilimia 50 kuliko ambavyo sasa ni asilimia 30. Tunaombaa Serikali yetu iangalie hili. Sasa hivi TARURA wako site pamoja na hii hali ambayo si nzuri ya mafuriko; wamekuwa wakihangaika kutafuta moram na kuziba madaraja ambayo yamekatika. Ukweli ni kwamba kwa hizi asilimia 30 TARURA haitaweza kusaidia barabara hizi nydingi ambazo zimekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaelekea kwenye wakati wa bajeti. Tunaombaa Serikali iangalie gawio la 70 kwa 30, hizi asilimia zikirekebishwa naamini TARURA watafanya kazi nzuri; na hata sasa wanafanya kazi nzuri kwa asilimia 30; lakini Bunge hili tukiwasaidia TARURA wakapewa hata asilimia 30 itasaidia sana kukarabati barabara zetu. Niiombe Wizara ya TAMISEMI, sasahivi TARURA wameshaleta maoteo ya uharibifu ambaa umefanyika huko kwenye barabara katika mitaa yetu, na Wizara ya Ujenzi na TARURA Taifa pia wanasema pia sasa TAMISEMI wao wameshapokea. Niiombe Serikali yangu response ya haraka sana kwa sababu katika mafuriko haya ambayo yanatokea, wananchi wameathirika, hawapiti na wanafunzi wanakwenda shule. Kwa hiyo TAMISEMI mtusaidie upesi kwamba sasa yale maoteo mliyoletewa mnaweza mkatupatia majibu lini ili wananchi kule kazi ziendelee na wanafunzi waendelee kwenda shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine la tatu ambalo nilifikiri kwamba niishauri Serikali ni suala la miradi ya kimkakati. Serikali yetu imefanya mambo mazuri sana. Niwashukuru, Mji wa Babati ni miongoni mwa miji ambayo tulipatiwa fedha za World Bank kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na timu yako naamini si halmashauri zote wamefikisha zile kilometra 10, mfano sisi ni kilometra 10, lakini kwenye zile kilometra 10 tumetekeleza kilometra 8.2 bado 1.8. Tunaomba sasa fedha zile ziweze kufika mapema ili zile kilometra 10 ambazo ilikuwa ndiyo azma yetu tuweze kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, Serikali yetu iliomba tipeleke tena miradi ya kimkakati kuitia TAMISEMI kwenda Wizara ya Fedha. kwa taarifa ambazo ninazo kama ile miradi sasa haijaanza na imesimamishwa baadhi, sisi Mji wa Babati tulileta mradi wa kimkakati katika halmashauri yetu, mradi wa stendi kuu ya mabasi Babati. Tunaomba sasa tupate majibu ya haraka tuweze kujua kwamba ule mradi wa stendi unaanza lini itatusaidia sana kwa sababu pia ni hitaji letu katika mkoa wetu na halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa ambaa wamechaguliwa hivi karibuni. Nipongeze sana Chama Cha Mapinduzi kwa kushinda kwa asilimia 99. Niiombe sasa TAMISEMI kuitia waurugenzi, wahakikishe wenyeviti wetu hawa wanapatiwa semina. Wenyeviti hawa ndiyo wanaokaa na wananchi muda wote, wenyeviti hawa ndiyo wanaotatua kero mbalimbali za wananchi muda wote. TAMISEMI sasa tunaomba halmashauri zetu zielekezwe kwa sababu hao wenyeviti tukiwaacha wakafanya kazi bila kupata mafunzo inaweza ikawawia vigumu. Kwa hiyo kote nchini mafunzo haya tuiombe TAMISEMI wasimamie ndani ya muda mfupi waweze kupewa mafunzo wenyeviti na wajumbe hao wa Serikali ambaa wamechaguliwa. Halmashauri wanaweza wakasema kwamba hawana fedha za kutosha lakini haop watu ni watu muhimu sana. Kwa hiyo niiombe Serikali yetu itoe kauli juu ya mafunzo ya Wenyeviti hao ambaa wameweza kuchaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo siku ya leo ningependa kuishauri Serikali yangu ni suala la TASAF. Fedha hizi zinasimamiwa vizuri katika halmashauri zetu na zinatoka kwa wakati; kwanza niwapongeze hili linafanyika lakini niombe sasa, si wazee wote au si kaya zote maskini zile zimeweza kuingia kwenye mpango. Kwanza niombe iharakishe suala zima la wale ambaa hawajaingia na wanaingia katika bajeti na mpango wa mwaka

huu na kuendelea huu mchakato ukamilishwe haraka ili wale wazee ambaa walikuwa wamesubiri kwa muda mrefu waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri pia kwa upendo kabisa kuhusu wazee wa Taifa letu. Niombi Serikali yangu tena wafikirie kuwaingiza wazee katika asilimia 10 za mkopo unaotolewa kwenye halmashauri zetu. Tumefanikiwa kwa vijana, akina mama na walemavu. Wazee hawa tukiwatengea asilimia mbili kama ambavyo tumetenga kwa walemavu, tukatenga kwa vijana na akina mama wazee hawa na wao wapate hilo dirisha naamini watafanya kazi na pia Watazalisha wataendelea kupata mitaji na wataendelea kuhudumia familia zao, kwa sababu si wazee wote ambaa wanashindwa kufanya kazi. Umri wa mzee ni kuanzia miaka 60 na kuendelea; haimaanishi kwamba ukiwa mzee hauwezi kufanya kazi. Kama tumeweza kuwa-consider akina mama na vijana na walemavu, niombi Serikali yangu kwa moyo wa dhati wazee sasa katika bajeti hii tunayoelekea waweze kupewa kwa sababu waliomba pension kwa muda mrefu lakini sasa kwa sababu hatukuwatimizia hili, tukiwaweka kwenye dirisha la mkopo wa halmashauri usiokuwa na riba itatusaidia sana kuondoa kero kwa wazee wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mambo yangu matano nimemaliza. Naunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul, tunaendelea na Mheshimiwa Ruth Mollel, dakika tano na atafuatiwa Mheshimiwa Godbless Lema, dakika tano halifu Mheshimiwa Vedastus Ngombale ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ambayo imewekwa hapo mezani. Katika taarifa zote nilizosoma hakuna mahali katika Taarifa ya Utawala Bora na Utumishi ambayo imezungumzia group kubwa ambalo ni muhimu sana la watumishi wa Serikali, rasiliimaliwatu. Kwa miaka mingi, minne sasa hawajawahi kuongezewa mshahara, na hili jambo nimeshalisema sijui mara ngapi katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa Serikali ikaweka katika bajeti ijayo mishahara kwa ajili ya kuwaongezea watumishi ambaa hali zao ni mbaya na wanahitaji kuboresha maisha yao na kuendesha familia zao. Itengwe bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko pia suala la uhuru wa kutoa maoni. Awamu hii uhuru wa kutoa maoni umeminywa sana, ukitoa maoni yoyote ya kuikosoa Serikali, unatekwa au unapotezwa au unauawa au unafunguliwa kesi ya uchochezi. Wengine wamenyang'anywa *passports* zao. Mfano mzuri ni yule Chief Executive wa TWAKEZA alinyang'anywa *passport*, Mheshimiwa baba Askofu wa Kagera Niwemugizi, yeye pia alizungumza tu kuhusu Katiba mpya akanyang'anywa *passport* yake na mpaka leo ninapozungumza hajarudishiwa *passport* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ni pamoja na kumwambia huyu Askofu kama *passport* yake hairudishiwa kwa sababu gani na lini atarudishiwa *passport* yake maana ni kama sasa yupo kwenye *house arrest*. Hawezi kutoka nje ya nchi kwenda kwenye shughuli zake, hawezi kufanya chochote. Kwa hiyo ninaomba Serikali imueleze yule Bishop kama yeye si raia arudishwe kule alikotoka au arejeshewe pasi yake ya kusafiria. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye eneo lingine la utakatishaji fedha. hii dhana ya utakatishaji fedha imekuwa ni ngumu sana na imekuwa na uonevu mkubwa sana. Watu wanawekwa ndani kwa *money laundering*, wanakaa miaka, upelelezi unaendelea. Ni kwa nini TAKUKURU inapeleka hizi kesi kwa DPP ilhali haijamaliza upelelezi?

Mimi naishauri Serikali, upelelezi ukamilike kabla ya kupeleka hizi kesi kwa DPP badala ya kuwanyima watu haki zao na kuwaweka rumande mwaka nenda mwaka rudi. Hii ni sawa na kuwa kama kifungo kwa saabu hakuna kitu chochote unachowenza kufanya ila ni kukaa ndani. Kwa hiyo upelelezi ukamilike ndipo watu wapelekwe Mahakamani, kesi zao ziende vizuri, kama ni kuhukumiwa wahukumiwe, kama hawana makosa warudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunao mfano mzuri Zanzibar, wenzetu ukienda kesi zote zinadhaminika, ukienda unawekwa ndani, ikifika miezi tisa upelelezi haujakamilika, unapata dhamana unatoka na kesi inaendelea. Kama una kosa unafungwa na kama huna kosa unaachiwa. Kwa hiyo tuna mfano mzuri ambaa tunaweza kuiga kwa wenzetu wa Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninazungumzia suala la mahusiano. Suala la mahusiano ni kama hii issue iliyotokea Mambo ya Ndani; tunaona Waziri Lugola ametumbuliwa lakini ninajiliza mimi kama Katibu Mkuu Mstaafu inawezekanaje Waziri atuhumiwe lakini Katibu Mkuu ambaye ndiye Afisa Masuhuli, yeye ndiye anasimamia mikataba, yeye ndiye anayesimamia kila kitu katika Wizara, inakuwaje? Ikanipa tafakari kubwa sana. Kwamba inawezekana Makatibu Wakuu na Mawaziri pengine hawapati semina ya kutosha kujua majukumu yao, majukumu ya Waziri ni yapi, majukumu ya Katibu Mkuu ni yapi; na inawezekana pia, naona Waziri wa Utumishi hayupo; kwamba je, Mawaziri wanapewa ile red book waweze kuzisoma na kuzielewa? Mimi sina hakika kama Mawaziri wote wamepewa ile red book, Mheshimiwa Jenista, wapewe red book wajue majukumu yao.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel subiri kuna taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe Taarifa Mheshimiwa Ruth Mollel. Kwanza taratibu zote za utendaji kazi wa Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa Katiba, kwenye Baraza la Mawaziri la Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, zote zimefuatwa na kila instrument imeeleza kazi za Mheshimiwa Waziri na kila jambo ambalo Mheshimiwa Waziri anatakiwa kuwa nalo katika kutekeleza wajibu wake, vifaa, documents na zana zote za kiutendaji kila Waziri anazo, tuko full nondo hapa na kila mtu ana kila kitu!. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tu naomba niendelee kumwambia dada Ruth, yeye aendelee kutushauri katika muundo wa utendaji kazi wetu na namna ya kufanya kazi lakini asiwe na mashaka. Rais wetu anatusimamia vizuri na sisi tunatekeleza wajibu wetu kama inavyotakiwa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth Mollel nafikiri umeelewa hayo ambayo ulikuwa unamuambia Mheshimiwa Jenista. Endelea Mheshimiwa Ruth.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyosema Mheshimiwa Jenista ni sahihi basi liko tatizo; na kama liko tatizo litafutwe ni tatizo gani linalosababisha huu mtafaruku katika Wizara. Kwa sababu haiwezekani kuwe na mtafuruku kati ya Waziri na Katibu Mkuu kama hizo instrument zote zipo, basi iko shida na hiyo shida itafutwe ili itafutiwe dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala pia ambalo linahusu TAMISEMI na ul mradi wa DART. Ule mradi wa DART ofisi zile kila mara kunapokuwa na mafuriko maji yanajaa, na unajiuliza ingekuwa ni nyumba za watu binafsi sasahivi zingebomolewa na zikaondolewa; na hali hii inahatarisha usalama wa raia na pia usalama wa nchi yenyewe. Ni kwa nini sasa katika bajeti ijayo hizi ofisi za DART pale Jangwani zisiondolewe kwa sababu zipo katika

mkondo wa maji na kila mara kumekuwa maji yanajaa mabasi yanasimama hayawezi kuyahudumia wananchi wakati wananchi wanahitaji huduma? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho mimi nasema hivi kwamba Serikali iliyopo madarakani ni ya wananchi, ni wananchi ndio tumeiweka Serikali madarakani. Kwa hiyo Serikali inawajibika kwa wannachi, maana sisi ndio tumeiweka madarakani. Kwa hiyo tunapotoa maoni yetu. Tunapoikosoa Serikali, tunaisaidia Serikali iweze kwenda katika namna inayopaswa na kuboresha huduma na kutuhudumia inavyopaswa kwa kodi zetu ambazo zinakatwa kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo muhimu sana, tujue kwamba hata Serikali inapofanya kazi vizuri inatimiza wajibu wake kwa wananchi na kwamba hawatupi msaada, sio msaada ni wajibu wa Serikali. na hiyo inatumika kwa kutumia kodi zetu sisi wenywewe. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi/Vigelegele)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ruth, tunaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema dakika 5 baadaye Mheshimiwa Vedasto, na Mheshimiwa Mussa Mbarouk wajiandae.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza niulize swalii moja, hivi nyie Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema unamuuliza nani?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakuuliza wewe...

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti haulizwi swalii, Mwenyekiti anasikiliza michango...

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia.

**MWENYEKITI:** Haya changia.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema hivi sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunapoishauri Serikali hatuishauri kwa sababu tuna chuki, tunaishauri kwa sababu hii ni nchi yetu. Sasa mara nydingi unaona unapoishauri Serikali kwenye mambo *critical* watu wanasimama kuomba miongozo na utaratibu, hatupo hapa ku-shine, tupo hapa kulisiaidia Taifa. Ninyi mna-shine, ninyi ndio mna Serikali, ni Mawaziri tusikilizeni sisi tuwaambie muende mkafanyie kazi haya mambo. Hii nchi ikiharibika, inaharibika yote kama ambavyo mafuriko yakija hayachagui CHADEMA, CCM wala CUJF. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno utawala bora linachukuliwa kirahisi sana, leo Taifa hili imefika mahali mtu hajatiwa hatiani na mahakama, anpata msamaha kama mtuhumiwa, yaani mimi napelikwa mahakamani leo, ninawekwa jela miaka mitano, ninaitwa nimetakatisha fedha halafu baadaye unatangazwa msamaha kwamba anayetaka kuomba msamaha aje; sijatiwa hatiani na mahakama kuitwa mwizi nasamehewa kitu gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamkamata mtu mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu, wanne; mimi mwenywewe ukiniweka ndani kama familia yangu haipo *stable*, mke wangu na wazazi wangu watasema omnia msamaha, kubali makosa uza nyumba ukae nje kuna

maisha mengine zaidi ya haya. Kuna watu wanaomba msamaha leo si kwa sababu ya hatia, ni kwa sababu familia zao zimechoka kuona watu wakiwa ndani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utawala bora tunaouongelea sio wa kwetu, kimsingi waliopo jela wengi ni wakwenu tukiongelea kwa mambo ya itikadi. Utawala bora tunaouongelea leo ni kulinda maslahi ya kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uchaguzi mwaka huu, pengine asilimia ndogo sana ya Wabunge watarudi. Kwa namna kesi ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi zinavyoendeshwa sasa, kila mtu hapa ana-*qualify* kuwa mtuhumiwa na kwenda jela. Mimi nimekwenda magereza kuna watu wana M-Pesa 900,000 wamepewa utakatishaji fedha wapo magereza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utawala bora sio kujenga barabara na kununua ndege, utawala bora ni kutengeneza misingi ya haki ambayo inadumisha utu katika Taifa hili. Mimi leo ukinipa barabara kilometra milioni moja Jimboni kwangu lakini ukamchukua mtu mnyonge maskini ukamuweka jela, huyu mnyonge kutoka jela ina maana kwangu kuliko barabara; utu ni wa msingi kuliko vitu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyosema utawala bora wa haki, tunataka Bunge liwe huru, mahakama ziwe huru na Serikali iwe huru. Tunapopingana na Serikali hatupingani kwa sababu tunamchukia Rais. Na hakuna mtu anasema kila kitu anachofanya Rais ni kibaya lakini nyie sio malaika na ndio maana mnapata usingizi na mnakufa, kwa vile sio malaika mkubali mshauriwe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hali ni mbaya, tunakwenda kwenye uchangazi Mkuu mwaka 2020. Tumeona matamko huko nje ya UVCCM, matamko yanayotamkwa vijana wa UVCCM nikitamka mimi asubuhi saa 4, saa 6 nipo magereza na bila dhamana. Badala ya Serikali kuchukulia hatua matamko makali kama haya, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi anasema ninawaonya vijana wa UVCCM. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihudhuria kesi za mauaji ya Rwanda Arusha, watu wote walioitiwa hatiani ni kwa sababu ya matamko. Tulinde Taifa hili kwa upendo, tulinde Taifa hili kwa kuonana sisi ni watu wema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukikaa kantini Wabunge wanakaa kwa caucus, wanaogopa hata kukaa na sisi wakati wa Jakaya mafumuana humu ndani, mkitoka nje jioni mnakwenda mnakunywa chai na juice; hiyo ndio ilikuwa siasa, leo siasa imeshindikana. Polisi ndio wanasaidia kuumiza watu; yakija maswali hapa mnakata. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitagombania Ubunge mwaka 2020 kesho kutwa, sigombanii kwa sababu nitashinda ama nitashindwa, nagombania kuweka alama ya kwamba wakati demokrasia inapita kwenye majoribu, sikuogopa nilisimama imara nikapigana hii vita. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wote mnaweza mkarudi kwa sababu uchaguzi wenu hauamuliwi na kura, unaamuliwa na bunduki lakini nawaambia mnachojenga katika Taifa hili ni kitu kibaya sana kwa vizazi vinavyokuja. Ni bora Mungu awape hekima leo muone mnachokifanya. Utawala bora leo Mawaziri hawana *confidence* na ndio maana hakuna innovation. **[Maneno Hayo Hapo Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi ya Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwepo na uwezo...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema confidence ya Mawaziri subiri sasa, haya Mheshimiwa Jenista.

### KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye utaratibu na hilo la confidence ya Mawaziri wala sina shaka, nchi inatuona tuna confidence na tunafanya kazi ya kutosha. Kwa hiyo, hayo ni mawazo ya Mheshimiwa Lema. Mimi nakwenda kwenye suala la kiutaratibu, la confidence wala sitazungumza kwa sababu taifa linatuona confidence yetu na Rais wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala la utaratibu, Mheshimiwa Lema amesema hapa na jambo hili hatuwezi kuliacha kwamba ushindi ambao umekuwa ukipatikana kwenye chaguzi ndani ya nchi hizi umeamuliwa na mtutu wa bunduki. Jambo hili kwa mujibu wa taratibu, Kanuni ya 61(1)(a) jambo ambalo Mbunge hana uhakika nalo na si la ukweli hatakiwi kulisema Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua chaguzi zote zinaendeshwa kwa misingi ya sheria na Katiba.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaad!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri kwa sababu Kanuni ya 63 inanitaka mimi ni-prove hiki ninachokizungumza, kifungu cha 44 cha Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kimesema kama kuna mtu ameona uchaguzi katika eneo lake haukuwa haki na halali, ana uwezo wa kwenda ndani ya siku 30...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaad!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Nisikilizeni basi...

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, endelea. Waheshimiwa tutulizane basi amalize. Mheshimiwa Jenista naomba uendelee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 44 cha Kanuni za Uchaguzi kwa mfano kwenye Serikali za Mitaa tulizomaliza juzi kimeeleza wazi ndani ya siku 30 kama mtu ana ushahidi uchaguzi haukuwa halali aende akashitaki...

**WABUNGE FULANI:** Na weweee!

**WABUNGE FULANI:** Huyoooo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujapata hiyo kesi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jenista. Naomba tutulizane basi, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Utaratibu ni hivi ndio ukweli wenyewe; Tanzania kama nchi haijawahi kupata ushindi wa aina yoyote kwa mtutu wa bunduki.

**WABUNGE FULANI:** Eeeeeee!

**MWENYEKITI:** Sio hivyo sasa mnakwenda mbali hebu subirini. Tanzania kama nchi haikuwahi kupata sifa hiyo, kama kuna maeneo yametokea hayakufanywa kwa usahihi, sheria zipo hilo ndio lilirozungumzwa. Mheshimiwa Lema tumalize hapo, kama umekusudia nchi nzima kwa maana ya Tanzania naomba ufute hiyo kauli.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushauri. Mheshimiwa Jenista kwa jinsi unavyopenda Uwaziri siku ukitumbuliwa unaweza ukafa baada siku mbili kwa sababu huwezi ku-defend kila jambo eti kwa sababu uonekane, kuna saa ku-chill ni wisdom, una-chill tu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua haya mambo tunaongea unafahamu na ni hivi, hatufanyi ili kuwa Mbunge; nimeshakuwa Mbunge awamu mbili, hatufanyi mimi kuwa Mbunge. Tunaposema utawala bora katika Tume huru ya Uchaguzi, naomba niongezee muda tafadhalii sana...

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema utawala bora ulenge katika Tume huru ya Uchaguzi sio tume ya kuisaidia CHADEMA, tume ya ku-harmonize future ya Taifa hili. Kwamba kusiwepo na mashaka, ni hatari sana watu kufikiria eti huwa mnaiba kura. Hilo tu lenyewe ni hatari yaani tu kufikiria kwamba huwa mnaiba kura ni hatari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha muhimu ni nini, ili kuwa na future nzuri, wananchi wanatakiwa wawe na imani na uchaguzi, wananchi wakiondoa imani na uchaguzi, watatafuta alternative. Haya mambo yanahusu wajukuu na watoto zenu, wewe utakuwa mzee ama utakuwa umetumbuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili suala lizingatiwe, sasa tukisema tuanze kuleta ushahidi hapa Pompeo mwenyewe amesema...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Pompeo amesema kwani hamuona Wamarekani wamesema nyie...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo.

Nimwabie tu Mheshimiwa Lema kwamba humu ndani sisi Mawaziri tunapofanya kazi tunaendelea kulinda heshima na hadhi ya Serikali. Haya maneno ya kutumbuliwa ama kutokutumbuliwa hayatukatishi tamaa, sisi tunaendelea kupambana. Kwa hiyo, kwetu hiyo sio hoja na Mheshimiwa Lema wala asifikiri atanitoa kwenye hoja kwa kunitishia kutumbuliwa, huo utashi utani... (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye mwongozo bado ninaendelea kusitiza kwamba Ibara ya 74(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinaitamka Tume

ya Uchaguzi kwamba ni idara huru. Ibara ya 11 na ya 12 inaeleza mipaka ya Tume ya Uchaguzi kutokuingiliwa na chama wala taasisi yoyote.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba hapa suala la kiutaratibu kwamba hatuwezi kama Ibara tu ya Katiba inaonesha uhuru wa vyombo tulivyonavyo, hawesi Mbunge humu akaendelea kusimama akadai kwamba uchaguzi tunaoshinda kwenye nchi yetu unatumia mtutu wa bunduki, haiwezekani. (Makofii)

**WABUNGE FULANI:** Hivyo hivyo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize kwamba ni lazima jambo hilo

liondolewe kwenye hansard vinginevyo hatuwezi kumaliza kikao hiki kwamba nchi hii inashinda kwa kutumia...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa ngoja nimalize moja halafu tutaendelea na lingine...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Taarifa kwa Jenista

**MWENYEKITI:** Aah! Hakuna taarifa kwa Jenista, hakuna taarifa kwa Mheshimiwa Jenista. Mheshimiwa Heche naomba ukae chini...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hebu tutulizane, Waheshimiwa Wabunge naomba tutulizane. Mnapoteza muda wa kuchangia mambo muhimu, kote nasema naomba mtulizane. Ikiwa kama tunahisi kwamba Katiba inasema ipo sahihi na Katiba lazima wote tunaiamini na ndio tunaapa kwa Katiba hapa. Ikiwa Katiba inasema kwamba tume ni huru na imepewa mamlaka kamili kama kuna Katiba imevunjwa pahala tunajua taratibu zipo wapi, kama hamkwenda mtulie mynyamze mnasema kitu ambacho sicho.

Mheshimiwa Lema nilikwambia pale mwanzo kwamba nchi hii haikuwahi kupata ushindi kwa mtutu wa bunduki kwa maana ya Tanzania. Kwa hiyo, ili umalizie vizuri mchangano wako naomba hiyo kauli uifute na kama hujaifuta nitaondosha kwenye hansard.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chief Whip naomba utulivu, kwa hilo naomba utulie amalizie kuchangia Mheshimiwa Lema.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Lema amalize kuchangia...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ni haki kama aliyokuwa nayo Jenista Mhagama upande wa Serikali, nijibu mwongozo wa Mwenyeekiti.

**MWENYEKITI:** Naomba amalize Mheshimiwa Lema halafu utazungumza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Mwenyeekiti  
(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Mwenyeekiti, nina haki kama aliyokuwa nayo Mheshimiwa Jenista Muhagama upande wa Serikali Chief Whip. Mwongozo wa Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo

**MWENYEKITI:** Naomba amalize Mheshimiwa Lema nitakupa ruhusa, muache Mheshimiwa Lema amalize.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MWENYEKITI:** Nakupa nusu dakika umalizie Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa hiyo, nusu dakika ni wewe bora uiondoe kwenye hansad ila mimi siwezi kufuta ukweli. Ni sawasawa na kuanza kujisachi kama mimi ni mwanamke ama ni mwanaume. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** uchaguzi sio huru kwa hiyo kama unaiondoa kwenye hansard hakuna shida lakini mimi siwezi kufuta.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Hapana, Mheshimiwa Lema nakwambia hivi kwamba kauli uliyozungumza si kauli sahihi, hata ukienda kwenye Kamati ya Maadili utatuhumiwa kwa kosa lako. Tanzania haikuwahi kupata ushindi kwa mtutu wa bunduki, kwa hiyo naomba ufute hiyo kauli...

**MBUNGE FULANI:** Hataki

**MBUNGE FULANI:** Atoke nje, atoke nje.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Tulishinda kesi ya uchaguzi Ndalambo kule Mombasa na mahakama ilisema polisi walitumia silaha kutangaza...

**MWENYEKITI:** Hiyo sio Tanzania, ni sehemu ndogo sana. Kwa hiyo, naomba hiyo iondoke nimeshaiondoa kwenye hansard. Malizia mchango wako, haya umeshamaliza basi ukae chini.

**MWENYEKITI:** Tayari, Mheshimiwa Lema naomba tumalize hapo basi...

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Nimemaliza?

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini tumalize basi, Mheshimiwa Chief Whip haya sema mwongozo wako.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kwa mujibu wa kanuni zetu na Katiba...

**MBUNGE FULANI:** kanuni ipi?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mbunge ana haki ya kutoa maoni yake...

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ipi?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokifanya Mheshimiwa Godbless Lema ni kutoa maoni yake. Inawezekana upande wa Chama Cha Mapinduzi wasijue uchungu tunaopitia sisi kwenye uchaguzi. Unapozungumzia eneo alilolisema Lema ni Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda kwenye uchaguzi wa Siha, polisi walikuwa wanabandika matokeo sio tume... (Makofij)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni.

**MWENYEKITI:** Nimeshakuelewa

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kwa hiyo, tupo hapa kuchangia kwa matakwa ya Mheshimiwa Jenista...

**MWENYEKITI:** Nimekuelewa naomba ukae chini. Waheshimiwa Wabunge kanuni hizo hizo ambazo umetumia wewe ambazo zinampa uhuru Mbunge kuzungumza au kuchangia/kutoa maoni yake, ni kanuni hizohizo zinatutaka tuzungumze kwa lugha inayokubalika ndani ya Bunge. Kwa hiyo, hilo limemalizika na limekwisha nawaomba tuendelee kuchangia kwa namna ambayo Bunge linahitaji kuchangiwa.

Mheshimiwa Vedasto Ngombale dakika tano halafu Mheshimiwa Mussa Mbarouk dakika tano.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kusema chochote katika michango ya kamati hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kusema kwamba yapo malalamiko kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na nilitarajia kwamba kwenye taarifa ya kamati basi kuna chochote kingesemwa ili basi kuweka hiki kitu sawasawa. Kwa hiyo, nitake kwamba Serikali ifanyie hili suala kazi, wananchi wanalamika sana juu ya namna ambavyo uchaguzi umeendeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo ningependa niseme ni kwamba...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba mtulizane, naomba mna mjadala mwininge upande huu.

**MHE. VEDASTUS E. NGOMBALE:** ...zipo Halmashauri ambazo mpaka leo bado hazijapeleka michango ya makato kwa malipo ya Waheshimiwa Madiwani na Serikali isipokuwa makini tutaenda kwenye kumaliza wakati wetu, kwa baadhi ya halmashauri nyingine watashindwa kulipa viinua mgongo vya Waheshimiwa Madiwani. Kwa hiyo, ni

jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba kila halmashauri inapeka hiyo michango ili basi Waheshimiwa Madiwani waweze kupata stahiki zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la TASAF. Ripoti ya Kamati inaonesha kwamba wafadhilli wanatoa fedha lakini Serikali imeonesha kusuasua kutotoa pesa sawa sawa. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuitaka Serikali ichangie ipasavyo ili basi michango hii iende kwa zile kaya masikini ziendelee kupata kama ilivyokuwa katika utaratibu wa kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la TARURA. TARURA inafanya kazi nzuri na mwaka huu mvua ni nyigi, kwa hiyo barabara nyigi zimeharibika. Kwa hiyo, naiomba Serikali ikubali ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa kuongeza asilimia ya mgawanyo. Kwa kupendekeza, TARURA ipate sasa asilimia 40 ili iweze kushughulikia ipasavyo barabara za mijini na vijiji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha sheria ya asilimia 10 ya mapato ya ndani iende kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Zipo Halmashauri zimeanza kutopeleka hizo asilimia 10 kama zinavyotakiwa na sheria na hivyo kuanza kuzalisha madeni. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuzitaka Halmashauri zote zipeleke ipasavyo hizo asilimia 10 ili basi michango ile iende sawa sawa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hii asilimia mbili inayokwenda kwa watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wana chagamoto; ukisema waandae makundi ili wakopeshe, wengine wanakosa haki. Kwa mfano, mtu mwenye ulemavu wa akili unamweka katika kundi gani? Napendekeza kwamba watu wenye ulemavu wa aina hiyo, basi wazazi wao washirikishwe kwenye makundi hayo ili basi nao waweze kupata stahiki zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo bado inaonekana kuna uwezekano mkubwa kwamba asilimia mbili inayotakiwa kwenda kwa watu wenye ulemavu isiende kwao kwa sababu vikundi vinavyotengenezwa vya watu wenye ulemavu ni vichache sana. Serikali iangalie utaratibu mwingine wa kuweza kuangalia namna gani itawapatia hizi fedha watu wenye ulemavu, ikiwezekana waangalie pia mahitaji yale muhimu ya watu wenye ulemavu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nashauri Serikali sasa ilette Muswada wa Sheria kama ilivyozungumzwa kwenye Taarifa ya Kamati kwa ajili ya kusaidia Shirika la Masoko la Kariakoo lifanye kazi sawa sawa. Shirika hili ni la siku nyigi lakini inaonekana lina upungufu wa sheria na linashindwa kufanya kazi yake sawa sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie suala la pale Jimboni kwangu, Njinjo. Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Kilwa na hasa Jimbo la Kilwa Kaskazini tumepatwa na kadhia ya mafuriko, hali ni mbaya sana. Ninavyozungumza, zaidi ya watu 26 wamepoteza maisha ikiwemo watu saba wa familia moja na watu sita wa familia nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza, katika zile Kata mbili kuna shule nne zimeharibiwa kabisa. Nachukua nafasi hii kuomba wenzangu wa TAMISEMI washirikiane na watu wa maafa wa Waziri Mkuu waangalie namna gani ya kuwasaidia wale watu. Isitoshe kwamba zaidi ya watu 10,000 wamekosa makazi na hivyo kulazimika kupewa viwanja kwa ajili ya kupata makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeshughulikia tatizo hili. Naiomba huko ambako wananchi wanakwenda kupewa viwanja, basi Serikali ihakikishe haraka iwezekanavyo inapeleka huduma muhimu

ikiwepo shule, miundombinu ya barabara, umeme na maji ili wale wananchi waweze kuishi maisha kama walivyokuwa wanaishi mwanzoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwaomba Jumuiya za Kimataifa, asasi za kiraia, watu mbalimbali kuchangia watu walioathirika na mafuriko. Ikupendeze, hata Bunge lako Tukufu, ikiwezekana, ikikupendeza basi nalo lichangie waathirika wa mafuriko katika Wilaya ya Kilwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kutoa pole kwa waathirika wote ambaeo wamekutwa na kadhia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk, baadaye atafuata Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na tukawezesha kuendelea na shughuli zetu za Bunge kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la TAMISEMI. Kwenye TAMISEMI kuna jambo ambalo limetokea katika jiji letu, hususan katika Halmashauri yetu ya Jiji la Tanga. Kuna Madiwani wamehama kutoka chama kimoja kwenda chama kingine. Ufahamu wangu unanielekeza kwamba moja ya sababu za kupoteza Udiwani ni ikiwa Diwani atahama kutoka chama chake alichochaguliwa nacho kwenda chama kingine; ikiwa Diwani atafungwa zaidi ya miezi sita; na labda akifanya biashara na Halmashauri bila kutangaza interest. Hizo ni baadhi ya sifa za kupoteza Udiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wamehama chama kutoka CUF kwenda Chama cha Mapinduzi, lakini cha kushangaza sasa, sheria haifuatwi. Madiwani wale bado wanaingia katika vikao vya Madiwani, wanalipwa posho na wanalipwa pesa ya mwisho wa mwezi na wanapitisha mpaka bajeti. Sasa je, wakitokea wasamaria wema, wakaenda wakafungua kesi kwamba bajeti hiyo iliyopitishwa siyo halali, si ina maana tutawaathiri wananchi wa Tanga? Kwa sababu itabidi Halmashauri isimamishwe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kuishauri Serikali. Hili jambo siyo mara ya kwanza. Kipindi cha nyuma kutoka mwaka 2014 kuja 2015 yupo Diwani alifanya mchezo huo huo na akatangazwa na Mkurugenzi kwamba ataendelea kuwa Diwani mpaka mwisho wa kipindi utakapofika na atapewa kiinua mgongo. Sasa najiuliza, sisi hapa kwa imani zetu tunaapishwa hapa...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Tunaapishwa, tunashikishwa misaafu Waislamu, Wakristo wanashikishwa Biblia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa, taarifa. Mheshimiwa Susan Lyimo.

## TAARIFA

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hata Manispaa ya Kinondoni mwaka 2019 Diwani aliyekuwa Viti Maalum kuititia CHADEMA amehamia CCM, lakini cha ajabu kwenye kikao kilichofuata akawa ni Diwani wa Chama cha Mapinduzi wakati tunajua majina huwa yanaenda Tume.

Sasa tunajiuliza Tume ilipata wapi jina la huyu Diwani wa CHADEMA wakampa na hakuna uchaguzi?

**MBUNGE FULANI:** Hee!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa, taarifa hiyo.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii nimeipokea kwa mikono miwili. Nataka niseme kwamba, narudia tena; Wabunge wote humu ndani kila mtu ana imani yake ya dini. Tunapoapishwa kushika vitabu vya Mwenyezi Mungu, halafu kumbe tunamdhihaki Mwenyezi Mungu kwamba tutaiheshimu, kuitii na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano pamoja na sheria zake, kumbe sisi ni waongo. Tunafikiri Mwenyezi Mungu atatuchukulia hatua gani kwa mambo... (Makofsi)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mwacheni amalizie. Malizia Mheshimiwa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, wale Madiwani kwa sababu wameshapoteza sifa kwa mujibu wa sheria na Katiba, basi wasihudhurie vikao vya Halmashauri na wasilipwe posho wala wasilipwe kiinua mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulisema ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kuna mikoa mitano ilitangazwa isifanye uchaguzi wa Serikali za Mitaa kabisa, ukiwemo Mkoa wetu wa Tanga. Athari yake imeanza kujitokeza. Jana wakati tunaangalia taarifa ya habari huu Mkoa wa Dodoma, kipo kijiji wamemkataa Mwenyekiti, wanasema sio chaguo letu.

Sasa je, hatuoni kwamba tunakwenda kuitia hasara Serikali? Kama wananchi wamemkataa ina maana pale lazima uchaguzi urudiwe. Je, likifanyika jambo hilo nchi nzima itakuaje? (Makofsi)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ikibidi uchaguzi wote wa Serikali za Mitaa urudiwe, tutende haki tuwape Watanzania haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowataka.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Waitara, nusu dakika.

Haya, Mheshimiwa Waitara.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Haya, sema taarifa yako Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee au nisiendelee?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ...utaratibu wa kumkataa Mwenyekiti wa Mtaa unajulikana...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Niendelee au nisiendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, zungumza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:** Kama kuna watu walihamasishwa kwenda kwenye mkutano...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara sema.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwamba utaratibu wa kumkataa Mwenyekiti unajulikana. Moja, kama kuna mtu ana tuhuma za Mwenyekiti ataandika, atawasilisha malalamiko yake...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, double standards. Taarifa hiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ...ataenda kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya atakuja kuitisha mkutano ndani ya muda wa siku saba. Yule mtuhumiwa, kama mnakataa Mwenyekiti wa Mtaa, maana yake atasomewa tuhuma zake naye atajibu na baadaye Mkutano Mkuu utapiga kura ya kutokuwa na imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mkutano umeitwa, watu wamehamasishwa wakasema kwamba wamemkataa Mwenyekiti, utaratibu huo haupo. Huu ndiyo utaratibu wa kawaida, lazima tuhuma ziwepo. Kwa hiyo, kama kuna watu wana hoja, watafuata utaratibu ambao kisheria upo pale ili waweze kuchukua hatua dhidi ya mwenyekiti yule.

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Waitara. Taarifa hiyo Mheshimiwa Mussa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:** Vinginevyo waliomkataa watatangaziwa kwamba huyu ni Mwenyekiti halali na aendelee na kazi zake kama kawaida.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi taarifa yake siipokei.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, hebu tusikilizane. Taarifa zinakwenda kwa utaratibu. Siyo kila mtu tu anatoa taarifa hata hajasema chochote.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa, malizia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake mimi siipokei, lakini tu niseme kwamba majibu ya taarifa anayonipa...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** ...ni kwamba waliharibu uchaguzi makusudi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka, nimeshawapa kwa utaratibu. Nimempa Mheshimiwa Susan, nimempa Mheshimiwa Waitara. Nyamaza ili aendelee amalize.

Mheshimiwa Mussa, naomba umalizie.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ina maana kwa maelezo ya Mheshimiwa Waitara wameharibu makusudi ili wananchi waje waandike barua sasa za kuomba eti ifanyike mikutano ya hadhara halafu waangalie asilimia. Huo siyo utaratibu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashawishi Wabunge wenzangu, hasa wa Upinzani, tutakaporudi kwenye Majimbo yetu tuwahamasisheni wananchi wawakatae Wenyeviti wote waliopita bila kipingwa. Nami nawaambia, kama uchaguzi utafanyika haki bin haki, bila ya dhuluma, hakuna Mwenyekiti hata mmoja wa CCM atakayepatikana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufanyeni haki, tuwaache wananchi wachague Wenyeviti wanaowataka. Sasa hivi Wenyeviti hawajulikani na wengine wameanza kulalamika kwamba tumepewa nafasi ambazo wananchi hawatutambui. Huu siyo utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa, umefahamika. Tuendelee na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MBUNGE FULANI:** Walisusa wenywewe.

**MBUNGE FULANI:** Hata Rais walikuwa hawamtambui, wameanza kumtambua.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa wanaoongea bila ya ruhusa nitawatoa nje sasa hivi. Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehemu, mwangi wa utukufu kwa kunipa uzima ili nami niweze kusimama hapa leo kuweza kuchangia Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala la utawala bora. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli; nampongeza Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan; nampongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa utendaji mzuri wa kazi unaozingatia suala la utawala bora. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu ya Rais tangu amekuwa Rais toka mwaka 2015, pamoja na kazi nyingi sana alizofanya za kuhakikisha kwamba

Tanzania yetu inaendelea kupaa kiuchumi, leo hii nitataja baadhi tu ya mambo ambayo ameyafanya. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kusimamia kwa makini kabisa suala la rushwa; matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za Taifa; amesimamia suala la kuondoa watumishi hewa; na ametoa elimu bure. Mpaka sasa tangu elimu bure imeanza kutolewa ni fedha zaidi ya shilingi trillioni moja ambazo zimetumika. Hongera sana Mheshimiwa Rais. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha mikopo ya elimu ya juu. Hakuna malalamiko wala maandamano. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais amesimamia ujenzi wa Stiegler's Gorge; zaidi ya pesa trillioni sita zimetolewa; amesimamia vizuri miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu; amesimamia suala la Vituo vya Afya kuhakikisha kwamba anatoa fedha vituo 352 vinajengwa; ndege nane zinanunuliwa; hospitali 67 mpya; na hospitali za mikoa tano. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameendelea kutekeleza majukumu yake. Amekubalika ndani ya nchi, nje ya nchi na Bara zima la Afrika. Ndiyo maana amepata nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Nchi zote 16 za SADC. Tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wetu. Haya ni baadhi tu ya mambo machache ambayo Mheshimiwa Rais amefanya. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la utawala bora, sijakusudia kuchoma sindano lakini kwa sababu nasikia sauti za wanawake wenzangu wanachoma choma sasa naenda kuchoma sindano. Tunapozungumzia suala la utawala bora ni vizuri pia tukaangalia hata kwenye vyama vyetu, hali ikoje? Kweli tuko kwenye misingi ya utawala bora au tunapiga kelele tu kwa upande wa pili wakati sisi wenye hatuko vizuri kwenye suala la utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye Chama ambacho ni cha Demokrasia na Maendeleo. Chama hiki ukiangalia katika uchaguzi uliopita...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Tulieni mpate elimu kidogo. Katika uchaguzi uliopita, viongozi wote waandamizi wa chama hicho wamewekwa kwa maana ya udini; ni Wakristo watupu. Pia, ukienda katika hoja hiyo hiyo, ukiangalia katika Kanda ya Arusha kuna bwana mmoja anaitwa Ali Bananga...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...aligombea nafasi na akaenguliwa. Huo ni ubaguzi wa hali ya juu. Pia ukienda...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...kwa Mheshimiwa Sumaye, alifanyiwa kampeni ya kupigwa kura za hapana. Huo ni ubaguzi wa hali ya juu sana. Vile vile ukienda kwa suala la Mheshimiwa Joseph Selasini aliondolewa kwenye nafasi ya Chief Whip kimtindomtindo tu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Sasa suala la utawala bora hapa likoje? Tunapozungumzia suala la utawala bora, suala la utawala bora likoje?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii...

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba tunapozungumzia suala la utawala bora katika huko huko...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...upande huo huo wanaopiga kelele kuna ndoa za jinsia moja. Sasa unapozungumzia...

**MBUNGE FULANI:** Choma sindano, choma sindano.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Au unapofanya vitendo vyta ya ndoa ya jinsia moja...

**MBUNGE FULANI:** Rudia hiyo ya jinsia moja hiyo!

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sehemu ya utawaa bora?

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaskia hiyo ya ndoa. hiyo ya ndoa hiyo!

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Hii sio sehemu ya utawala bora...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Ndoa za jinsia moja upande huo siyo sehemu ya maadili. Siyo sehemu ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Afrika...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za Afrika, Tanzania imetajwa kwamba ni nchi ambayo inathamini na kujali suala la utawala bora. Imeshika nafasi ya juu kabisa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...na ndiyo maana wamejitokeza baadhi ya wanasiwa wanakwenda kuropokaropoka hata nje ya nchi, akiwepo Mheshimiwa Zitto Kabwe, akiwepo Mheshimiwa Tundu Lissu na wengine wengi. Akina Mheshimiwa Lema hawa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nzungumzie suala la TRA.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti una double standards.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Naomba nzungumzie suala la TRA.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, malizia dakika moja.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia. tunapozungumzia suala la utawala bora tujiangalie na sisi.

**MBUNGE FULANI:** Majambazi wako kule, akina Lema.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Majambazi wako upande huo! Ndoa za jinsia moja ziko upande huo! Hii siyo sehemu ya utawala bora. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline, umemaliza muda wako.

Mheshimiwa Jacqueline, muda wako umekwisha, ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Wataweza kweli!

**WABUNGE FULANI:** Aah, wapi!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yenu. Ni haki yenu, lakini naomba sana tuelewane. Naomba nimalizie kabla sijasitisha Bunge, nirudie tena; kauli ya Mheshimiwa Lema naiondoa kwenye Hansard kwa sababu nchi hii haijawahi kupata ushindi kwa mtutu wa bunduki.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila utaratibu)

**MWENYEKITI:** Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirudia)

**MWENYEKITI:** Katibu!

**NDG.RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE NA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA;**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA;**

**NA**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

(Majadiliano Yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Mwanne Mchemba baadaye Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwweza siku hii ya leo kuwa na afya njema na kupata muda wa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Kwanza naunga mkono maoni ya Kamati na nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii kwa uwasilishaji wake mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia, pia nianze na pongezi. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya lakini pia kuzilea ofisi hizi mbili za TAMISEMI na Utumishi na Utawala bora. Wizara hizi mbili kuwa chini ya Mhehsimiwa Rais kuna mafanikio makubwa, pia wateule wake, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Utumishi, kazi wanazofanya kwa kweli wanamuwalisha vizuri sana Mheshimiwa Rais. Pia Manaibu Waziri wa Wizara zote mbili wanafanya kazi nzuri za kusaidia kwenye Wizara hizi, vilevile Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, niwapongeze sana kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo pia kuna mambo ambayo sisi kama Kamati tulikuwa tumeridhika na Wizara zote mbili kwa wao kukubali maoni ya Kamati. Asilimia kubwa ya mafanikio haya yametokana na maoni ya Kamati yetu. Tuwapongeze Wizara chini ya Mawaziri hawa kukubali ushauri wa Kamati, kwa kweli niwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jafo; hivi karibuni tu, siku mbili zilizopita TAMISEMI walikuwa na kongamano au taarifa ya utekelezaji wa miradi ambayo Serikai ilitoa fedha na miradi hiyo imefanikiwa kwa asilimia 88 mpaka hivi sasa. Kwa hiyo ni imani yangu kwamba ifikapo Juni, kwa fedha hizi zitakazotengwa na zile zilizotengwa nina imani kubwa sana miradi yote itakuwa imekamilika, na sina shaka usimamizi ambao tunao kwenye Wizara hii mambo yote yatakwenda kama tulikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Waziri wa Fedha na Wizara yake na Naibu wake kwa kupeleka fedha TAMISEMI kwa asilimia zaidi ya asilimia 75. Kwanini ninasema hivyo; ni kwamba miradi mingi ya afya imetekelizwa vizuri sana, yote hii ni kutokana na usimamizi mzuri pamoja na umakini katika makusanyo ya fedha ambayo yameweza kuweka rekodi ya pekee kwa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tukizungumzia vifo vyta mama na mtoto vimepungua kwa sababu zahanati na vituo vyta afya vimesogea kartibu. Jana nilikuwa nasikia Mheshimiwa Kiula anasema kwake tayari wameshafanya oparetions za mama

mjamzito na wakaokoa mtoto. Sasa kwa hilo nimeona nisisitize kwamba TAMISEMI sasa siyo TAMISEMI ile, TAMISEMI inapaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nilitaka kusisitiza kwenye Kamati ni kwamba tuna mabasi ya mwendokasi, na kuna wakala ambaye anatarajia kupewa, au tender kutangazwa. Ningeshauri TAMISEMI wajitahidi kwanza Sheria iwe po kabla ya kuplewa mkataba, kwa sababu bila sheria tutarudi tena kusema mikataba mibovu na kadhalika. Kwa hiyo la kwanza niishauri TAMISEMI ihakikishe kwamba sheria inaletwa hapa na inapitishwa ili mambo yawewe kuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasahivi wanasema kwamba mabasi mengi yako pale, wakati wamvua wanapata shida. Hata hivyo, baada ya sisi kufuatilia kwa sababu tayari Kamati yetu ilitembelea kwenye maeneo; si kweli yale mabasi ni mabasi ambayo yalishaharibika. Hata hivyo Kamati yetu iliwashauri kwamba ni vizuri yakaondolewa kwenye eneo ili watu wasijue na wasielewe kwamba ni kila siku mabasi yanjaa maji; si kweli. Ni mabasi ambayo kweli wakati ule maji yalikuwa yanjaa, lakini sasahivi yaliyobaki ni yale ambayo huwezi kuyatengeneza na huwezi kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niende harakaharaka, ni suala zima la miundombinu. Kwakweli niipongeze sana TARURA inafanya kazi katika mazingira magumu kwa sababu haina fedha na haina tegemeo. Hizi Wizara mbili zote zina malalamiko Wizara ya Miundombinu wanasema kwamba fedha hiyo haiwatoshi na TARURA wanasema haiwatoshi. Mimi ningeshauri, hizi Wizara zingekaa pamoja, zikae pamoja zitulee nini kinachowezu kufanyika ili Sheria ya TANROADS ibadilishwe ya na TARURA waweze kupata fedha. Kama TARURA wangepata asilimia 40 kazi nzuri wangefanya kwa sababu tumetembelea miradi, wanajitahidi sana pamoja na kwamba hawana fedha. Tatizo kubwa ni kwamba kwa hali ya mvua ya sasahivi kuna matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niende harakaharaka kwa sababu nina Wizara mbili; Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI tukuombe sana kwa bajeti hii; madeni ya Madiwani ambayo wanadaiwa hatutaki tena kwenye bajeti yetu tuje tukutane nayo. tunataka ikifika wakati wa bajeti ya mwaka huu madeni yote kama ulivyoagiza yale yamekwisha kwa sababu Madiwani wanafanya kazi ngumu, wanakopwa vikao hawalipwi na wana madeni. Kwa hiyo hili suala kwenye Kamati hatutaki tena lirudiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, niombe pia kuhusu Shirika la Kariakoo Sheria ile imepitwa na wakati, ni ya tangu mwaka 1974. Wakati ule kulikuwa na watu wachache, sasa Kariakoo si ile ya mwaka 74 iletwe Sheria ifanyiwe marekebisho, lakini kwa upande wa TASAF mpaka hivi leo karibuni walengwa kwa asilimia 30 hawajapatiwa fedha. Sasa, kwa kuwa tunaingia wkenye awamu nyingine ni vizuri asilimia 30 ikamilishwe ili walengwa wote waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niende harakaharaka, ni kuhusu suala la MKURABITA. Suala la MKURABITA ni tatizo kubwa tumetembelea kwenye Ofisi zao, lakini kwa bahati mbaya hati mpaka leo hazijachukuliwa. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge hawa Wabunge wawahamasishe wananchi ambao hati zao ziko kwenye Ofisi wakachukue ili wajue maana ya kwenda kukopea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ningeomba kwa ridhaa yako kwamba wakala wa mafunzo kwa njia ya mtandao TAGLA, lengo la TAGLA kuanzishwa ni kuwawezesha watumishi wa Serikali au watumishi wa umma kwenda kujifunza na hatimaye kutumia mfumo huu wa mtandao ambao sasahivi upo. Kwa hiyo nimwombe Waziri mwenye dhamana ya utumishi ahakikishe kwamba anatoa waraka kwenye halmashauri kuhakikisha watumishi wanapata haki zao na wanakwenda kujifunza haya mafunzo ili kutumia posisvizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono.(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwanne Mcemba nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Jitu Soni, lakini sijamuona tuendelea na Mheshimiwa Joram Hongoli baadaye Mheshimiwa Joel Mwaka ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, lakini nashukuru pia kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye hizi taarifa zote za hizi Wizara. Nianze kuwapongeza sana Wenyevit na Wajumbe wa Kamati za Wizara zote, Wizara ya TAMISEMI, Katiba na Sheria lakini pia na Sheria Ndogo kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya na wakaleta taarifa nzuri ambayo wametusomea hapa wametuletea hapa, nawapongeza sana. Pongezi kwa namna ya pekee Mawaziri wa Wizara hizi zote mbili, hasa nikianza na Waziri wa TAMISEMI na Manaibu Waziri wote wawili na watendaji wake wote, lakini pia na Watendaji wa Wizara nyingine na Mawaziri wa Wizara hizi zote nyingine ambazo taarifa zao zimewasilishwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia kwenye upande wa TARURA, Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini. Kama ilivyoeleza kwenye taarifa imeoneshwa vizuri sana kwamba TARURA wanashughulikia barabara zenye urefu wa kilometra 108,946. Hizi ni barabara nyingi sana, na hizi barabara ni zile ambazo zimesajiliwa lakini bado kuna barabara nyingi ambazo hazijasajiliwa, nazo pia kwa namna moja au nyingine pengine wanashughulikia nazo, lakini ukiangalia kwenye bajeti yetu bado TARURA wanapewa fedha kidogo sana kama walivyoeleza wenzangu. Sasahivi wanapewa kwenye bajeti asilimia 30 na asilimia 70 inaenda kwa TANROAD, mimi, kama walivyosema wenzangu, nilikuwa napenda nipayendekeze kwamba angalau wangeweza kuongezewa ikafika asilimia 45 hivi ili barabara nyingi hizi zinazoenda huku Vijiji ambako ndiko asilimia 80 ya wananchi wanashughulika na kilimo, ili waweze kusafirisha mazao yao vizuri ni lazima barabara za huko ziwe nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kupitia barabara hizo barabara tutaweza kukuza uchumi wetu; na ukiangalia mapato mengi halmashauri nyingi hasa za Vijiji zinategemea sana hizi barabara. Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa kwamba kuna baadhi ya halmashauri hazilipi Madiwani, ni kwa sababu tu hawapati mapato ya kutosha na inawezekana kinachochangiwa wasipate mapato ya kutosha ni kutokana na kwamba barabara ikifika misimu ya mvua kama hii sasahivi mizigo haiwezi kusafiri. Kwa hiyo maana yake mapato yale ambayo wanatakiwa kukusanya kupitia hizi barabara hawawezi kuyapata; kwa hiyo na hatimaye shughuli nyingi za maendeleo, lakini shughuli nyingi pia za halmashauri zinakwama kwa sababu barabara hizi hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua mfano kwangu mimi kwenye Jimbo langu mimi kwenye Jimbo langu Jimbo la Lupembe asilimia 80 ya mapato linategemea hizi barabara za vijiji, na miezi kama hii ambapo mvua zinanyesha nyingi barabara hizi zote hazipitiki. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri mkikaa kwenye Baraza lenu mpitishie hili kwamba angalau TARUARA wapewe hela za kutosha. Wakipata asilimia zaidi ya 40 hivi itakuwa nzuri na barabara nyingi zitaweza kuboreshwa na hatimaye uchumi wa halmashauri utakuwa na mapato yataongezeka na hatima yake miradi mingi ya maendeleo itatekelezwa kwa sababu vyanzo vya mapato vinaweza kupatikana kirahisi, pia mizigo inaweza kusafiri kirahisi kutoka vijiji kwenda mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichangie kuhusu mpango wa kurasimisha, biashara na rasilimali mbalimbali ikiwemo ardhi, nyumba na biashara. Mimi niongelee kidogo juu ya upande wa ardhi na makazi. Tunaushukuru sana, Serikali kwa kuanzisha mpango huu, na unaendelea vizuri na tunaona ardhi zinarasimishwa zinakuwa na thamani. Ilivyokuwa kabla ya mpango huu ardhi nyingi maeneo mengi ilikuwa haina thamani kwa sababu zilikuwa hazijarasimishwa; lakini pia na makazi tunajua watu wengi wamejenga kwenye viwanja ambavyo hazijapimwa, lakini Serikali imeendelea kurasimisha kupitia MKURABITA ili ardhi hizi

au nyumba hizo ziweze kutambulika na hatimaye ziweze kupata hati. Lakini tuna changamoto kubwa sana changamoto ya Maafisa Ardhi, pia na Maafisa Mipango Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya halmashauri hususan halmashauri za vijijini nyingi hazina wataalam wa ardhi, hazina Maafisa Ardhi Wateule na Maafisa Mipango Miji. Halmashauri ya kwangu, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe nayo ni mionganoni mwa halmashauri ambayo muda mrefu haina Afisa Ardhi Mteule na pia haina mtaalam wa mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunashindwa hata kupanga mipango ya ardhi, tunashindwa hata kupima na kutoa hati imekuwa ni vigumu kwa sababu hatuna wataalam. Kwa hiyo tuombe sana, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo tusaidie tuweze kupata Afisa Mteule pamoja na mtaalam wa mipango miji ili nasi tuweze kupata wataalam ambao watatusaidia kutoa hati pamoja na kurasisimisha ardhi na makazi. Vilevile tuweze kupanga miji ili tuweze kupata vyanzo vingine vya mapato na wakati huo huo miji yetu iweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu kukamilisha maboma. Tunashukuru sana Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma kama vile majengo ya afya na majengo ya elimu. Kwenye halmashauri yetu sisi bahati mbaya hatukupata pesa ya upande wa afya, kwa maana ya vituo vya afya, lakini niishukuru sana Wizara ya TAMISEMI mmetupatia milioni 200 kwa ajili kujenga kituo cha afya kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kuitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri mtusaidie tuweze kuongezewa fedha, tukipata angalau milioni 400 tuweze kukamilisha hicho kituo cha afya, na ikiwezekana mtupatие tupate vituo viwili kama zilivyo halmashauri lingine ambazo zimepata sisi tulikosa tumepata mwishoni hizo milioni 200; basi mtuongezee tuweze kukamilisha ujenzi wa vituo vyetu vya afya na maboma mengine ambayo yapo kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwahiyio naamini kwamba tukifanya hivyo tutakuwa tumeboresha sana na watu wengi watapata hii huduma ya afya kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto kubwa pia katika uboreshaji wa hivi vituo vya afya na kwenye upande wa elimu. Sasahivi tuna changamoto kubwa ya wataalam, wahudumu wa afya na walimu, hasa walimu wa shule za msingi kwenye elimu. Niombe sana Wizara iajiri walimu wa kutosha ili tuweze kuhakikisha kwamba shule zetu zinapelekewa walimu wa shule za msingi. Kuna baadhi ya shule zina walimu watatu na nyingine zina walimu wanne; kwa hiyo hili ni tatizo kubwa. Hatuwezi kutegemea kuwe na ubora wa elimu kama walimu wanaofundisha ni wanne. Kuna shule ambayo nilisoma mimi Mheshimiwa Waziri inaitwa Shule ya Msingi Kanikelele ina walimu sita tu na wanafunzi wako mia saba na kitu leo hii.(Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, tukiongeza ajira za walimu tutasaidia halmashauri nyingi ziweze kupata walimu na hatimaye watoto wetu waweze kupata elimu bora. Kwa hiyo ilivyo sasahivi watoto wengi wanashindwa kupata elimu bora kwa sababu walimu mashulenii hawapo. Kwa hiyo niombe sana katika mpango wetu katika bajeti hii tujikite kabisa kuajiri walimu, lakini pia tujikite kuajiri wataalam wa afya ili vituo vyetu vya afya ambavyo tumevianzisha viweze kupata watalam, pia na shule zetu hizi ziweze kupata walimu ili watoto wetu waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka nichangie kidogo juu ya mikopo ya walemau; wenzangu wameeleza pia; lakini niseme kwamba kwenye upande wa hasa ile asilimia mbili; niombe, kuna wale walemau ambao wao wenye hawana, mmoja amesema hapa kuhusu wale wenye utindio wa ubongo au wengine wana ulemavu ambao hauwawezeshi hata kufanya shughuli yoyote; tuwapatie basi wazazi wao ili waweze kuingizwa kwenye kikundi ili nao wahesabike na ili waweze kupata hii mikopo. Hii ni kwa

sababu ilivyo sasahivi inataka mlemavu mwenyewe aweze kuwepo kwenye kundi. hii itawatenga baadhi ya walemavu watashindwa kupata mikopo kwa sababu hawatakuwa na uwezo wa kuingia kwenye kundi. Sasa tukitumia wazazi ama walezi wao wataweza kunufaika na hiyo mikopo ambayo inatolewa na halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa nafasi na naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli, tunaendelea na Mheshimiwa Joel Mwaka, baadaye Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Lucia Mlowe wajiandae.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuwa mmoja kati ya wachangajiaj wanaochangia katika Taarifa za Kamati zetu tatu ambazo zimewasilisha Taarifa zao leo; Kamati ya TAMISEMI, Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwapongeze sana waliowasilisha Taarifa hizi, wameziwasilisha kwa makini na zimeandaliwa kwa ubora, zimeeleweka na tunawaunga mkono na tunawapongeza kwa kazi kubwa wanazozifanya kwenye Kamati zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ili iweze kuendelea inahitaji kuwa na amani, nchi ili iwe na amani inahitaji kuwe na Utawala Bora, ili kuwe na Utawala Bora tunahitaji sana kuwa na Sheria nzuri. Sheria nzuri zitagemea na wakati, kuna Sheria zilikuwa nzuri miaka ya nyuma lakini kadri tunavyokwenda mbele inabidi zibadilike ziende na wakati. Kuna Sheria ambazo sasa tunazo zinatusaidia ni nzuri sana lakini huko mbele tunakokwenda zitatakiwa zibadilike ili ziende na wakati na ndiyo maana tuna hizi Kamati kuzipitia Sheria zetu kwa wakati tofauti tofauti ili kuja na Sheria muafaka kwa wakati muafaka tulionao. Kamati zetu za Katiba na Sheria pamoja na Sheria Ndogo wanaifanya hiyo kazi kwa vizuri sana, nawapongeza sana. (Makofii)

Mhesheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala zima la Uraia pacha; uraia pacha kwa wakati tulionao, ninaomba sana Serikali iuangalie kwa karibu. Naziomba Kamati zetu hizi husika hasa Kamati ya Katiba na Sheria iangalie kuingiza na kuifanya nchi yetu iwe na Uraia Pacha. Tunapozungumzia maendeleo, maendeleo lazima yawe shirikishi, tunaposema maendeleo shirikishi maana yake tunashirikiana sote wananchi tulio ndani ya Nchi na walio nje ya nchi. Kwahiyio, tunapoondoa hii Sheria inakua haipo kwetu, tunaacha kuwashirikisha kwa karibu kabisa Ndugu zetu ambao wanaishi nje ya Nchi. Kwa hiyo, naomba sana Kamati husika ziliangalie jambo la uraia pacha iwe ni Sheria inayokubalika hapa Tanzania pia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri Jafo na Manaibu wake wote wawili na Wizara nzima kwa ujumla, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuchika, Makamu wake pamoja na Wizara nzima kwa ushirikiano mkubwa ambao wametuonyesha sisi Wajumbe wa Kamati ya TAMISEMI. Tumeshirikiana nao vizuri katika kuwashauri, katika kuwaeleza na tunashukuru kwa kweli wamekuwa wasikivu sana. Serikali hii ni sikivu kupitia kwa Mawaziri wetu hao katika kuyatekeleza yale ambayo Kamati inawashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la MKURABITA; amelizungumza mwenzangu hapa jirani lkwa kipfupi. MKURABITA wakati unaanzishwa kwa maana ya kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge ili ziweze kuwasaidia katika maisha yao. Amezungumza kwa uzuri kabisa kwamba watu wengi na sisi tumepata nafasi kama Kamati, tumeonanu watu wakikabidhiwa Hati za Kimila katika mpango mzima wa MKURABITA ili ziweze kuwasaidia wao kujinyanyua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme bado kuna Mabenki yanasurya kuzitambua Hati hizi za Kimila katika kuwasaidia wananchi kujiletea maendeleo. Niombe sana Mheshimiwa

Mkuchika na Wizara yako hebu mliangalie hili kwa karibu sana. Mabenki ambayo bado yanayosumbua yapewe maelekezo ili wananchi waweze kufaidika na mali zao walizonazo. Maeneo fulani tumejenga mpaka vituo vya biashara lakini vinaonekana havifanyikazi kwa sababu watu wa kwenda pale na kufanya hizo biashara hawapo kwa sababu hawana fedha kwahiyo naomba sana mliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili; ameongea Makamu wangu Mwenyekiti hapa madeni ya Madiwani. Halmashauri nyingi Madiwani wanazidai halmashauri hawajalipwa fedha. Hivi tunavyoolekea mwisho Madiwani hawajui nini cha kufanya lakini tumshukuru sana Mheshimiwa Jafo ulizungumza kwa umakini na kwa ukali sana wakati tupo kwenye kikao cha Kamati, umetoa maelekezo. Naomba maelekezo hayo uyakazie ili kwa kweli tufikapo mwezi wa sita tusingumzie tena madeni ya Madiwani kwenye halmashauri zetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie kwa uchache kuhusu barabara; kweli barabara zipo, mvua zimenesha na barabara zinaharibika tena kwa sabbau ya mvua. Niombi sana TARURA wajitahidi sana, waweze kuzirudisha barabara zetu katika hali ya kupitika ili mawasiliano yaendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache hayo, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia 100 Kamati zote hizi tatu, ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joel Mwaka. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni baadaye Mheshimiwa Lucy Mlowe na Mheshimiwa Upendo Peneza wajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kunipa fursa ya kuchangia leo lakini nitumie fursa hii kwa kuzipongeza Kamati zote tatu kwa kuwasilisha report ya Mwaka ambayo imeeleweka vizuri sana na tumeona maoni yao na tunaunga mkono kwa asilimia kubwa maoni yao waliyotoa lakini kuna baadhi ya meneo ningependa kuchangia ili tuweze kuboresha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; nilikuwa naomba Kamati ya Sheria Ndogo lakini pia Kamati ya Sheria wakati wanapofanya mapitio katika Sheria mbalimbali kwa sababu sasa tunatumia teknolojia basi wawe wanawenza kuweka na Bunge liangalie utaratibu wa sisi kupata hizo Sheria mbalimbali wanazopitia kwa sababu kipindi wao wanapitia Sheria hizo na Kanuni na sisi tuko kwenye Kamati zingine tunafanya shughuli zingine. Lakini kama kuna eneo ambalo ninahitaji kuja kuchangia basi niweze kujua ni lini itakuwa ni sehemu ya kupatia taarifa vizuri niweze kupitia hizo Sheria lakini ombi langu moja na nimekuwa nikilisema mara nyingi Bungeni; Sheria zote ziwe online ambazo ziko updated, Sheria na Kanuni. Leo tukitaka kufanya marejeo yoyote hizi Sheria ni ngumu kuzipata na nyingi haziko updated kwenda na wakati lakini pia Kanuni mbalimbali pia zote ziwe updated, ziwe online ili iwe rahisi kwetu sisi kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na moja katika mifano naweza kutoa; kipindi nimehangai kauleta hapa Sheria ile na kuleta kwenye Kanuni, suala la force account tulichukua miaka minne kwa sababu kupata tu nyaraka zile mbalimbali hazikuwepo. Nimshukuru Mheshimiwa Chenge kama siyo yeye, bado hili jambo la force account ingekuwa bado ni ndoto kwetu na yeye amesaidia kutoa kwenye archive yake zile document na leo sifa kubwa ya mafanikio ya Serikali yetu ni kwa kutumia force account.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lingine ni suala la upande wa uwekezaji kwa Waziri wa Uwekezaji pamoja na timu yake; wanafanya kazi kubwa na nzuri lakini bado naona kuna Sheria mbalimbali ambazo zinawapa ugumu wa kufanyakazi. Leo siyo kweli kwamba ni one stop center, bado changamoto ziko nyingi. Leo vibali vingi ambavyo viko

pia *TIC*, kwa kupata tu vibali vile vya muwekezaji wa class A hatuzungumzii yule mfanyakazi ni nani lakini yule wa Class A tu bado inasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu amewekeza ana jengo lake lina thamani labda ya ghorofa 10 lakini baada ya miaka miili au mitatu kupata ile Class A anahangaika kupata ile permit ya *labor*, bado aende kule kupata resident permit sasa mngeunganisha na ingekuwa rahisi kwamba mtu amewekeza hivi yule ukimnyima permit, hiyo mali yake inakwenda kwa nani? Lakini mbali na hilo, kuna biashara nyingine nyingi tu ambazo zimeendelea kufungwa na zimeendelea kudorora kutokana na watu kunyimwa vibali.

Leo kwa mfano; kwenye sekta ya *hotel*; unapomnyima mpishi wa aina mbalimbali kama ni Mchina au kama ni M-mexico unapowanyima vibali na wale watu wanakwenda kula pale kutokana na aina ya yule mtu kufanya hiyo kazi, unapomnyima kibali leo chakula kinapikwa na Jitu ambaye hajui kupika chakula Kichina kweli ni jina tu la Kichina lakini ile ladha na nini haipo. Tuangalie kwamba wale wakiwepo biashara kiasi gani inaongezeka na tunayo mifano mingi tunaweza kuwapa biashara zilizofungwa, kudorora kabisa kwa ajili ya watu kunyimwa vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *TIC* inasema vile vibali vitano vya mwanzo yaani hamtamuhoji yule Muwekezaji kwa sababu hata akileta Ndugu yake, amemleta pale ili asimamie kwa ajili ya imani na kuwa na uaminifu na yule Mtu. Sasa tunapoanza kuhoji mambo mengine ya kwamba je, hiyo kazi inaweza kufanya na Mtanzania na haiwezi kufanya kwenye uaminifu hakuna cha Utanzania hata mimi na Ndugu yangu wote Watanzania hatuaminiani kwa hiyo inaweza kuwa Mtu mwingine ambae ninamuamini anaweza kuwa anasimamia ile mali kuliko Ndugu yangu ambae anaweza kunirusha sasa ni vizuri haya mambo tuyaangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huko zamani kwenye incentives kulikuwa na mambo mengi leo hayo yote hayapatikani. Kwa mfano; tukitaka kuwekeza kwenye sekta ya kilimo na ndio hiyo katrika kila mchangu wangu hapa naise mea. Leo sekta ya kilimo bidhaa yake yote siyo veritable kwa hiyo sisi tukitaka exemption kwenye capital goods hatuwezi kupata hata tukiwa kwenye *TIC* hatuwezi kupata kwa sababu VAT on deferment bidhaa zetu hazipo veritable kwa hiyo tunanyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ya pili; unaambiwa ni lazima VAT kiwango kile kiwe ni milioni 10 na kuendelea. Milioni 10 ina maana ile bidhaa ni zaidi ya milioni 50 sasa capital goods kwa Watanzania ambao wanaanzisha viwanda vidogo vidogo kama haikufika hiyo milioni 10. Je, hawana haki ya kupata hiyo VAT on deferment hata kama bidhaa yao iko veritable? Kwahiyo, Sheria hizo zinafanya watu wengi wanaona kama *TIC* ni sehemu tu nydingine ya kupata vibali vingine vingi zaidi. Ni vizuri lengo la kuanzisha *TIC*, lengo la kuanzisha Wizara ya Uwekezaji ni kuangalia mahali tuwe na one stop center na sisi tukisema mbali na *TIC*, local content ni wangapi wamewekeza Watanzania *TIC*? Ni vizuri pia Watanzania wa kawaida wajue fursa zilizopo ili na sisi wengine ambao ni Watanzania tupate hizo fursa kuitia hizo incentives za *TIC* na tuweze kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine naomba nichangie kwa upoande wa Serikali za Mitaa, kwa upande wa TARURA; ni vizuri tungeendelea namna ya kuongeza bajeti ya TARURA lakini pia Waziri akae, TARURA ni agency inayojitegemea pamoja na TANROADS lakini matatizo mengi tunayoyapata barabarani sasa hivi katika barabara za vijijini ni matokeo ya athari za kujengwa kwa barabara za TANROADS.

Sasa ni vizuri wale wawili wakae kwa pamoja ili waweze kutatua na kusaidia katika kuboresha amzingira mbalimbali huko chini lakini TARURA mngejerhusu kazi nyingi angalau isiyozid milioni 200 zifanywe kwa mfumo wa force account. Force account leo hii barabara inayopangiwa milioni 30 au 40 huko kijijini itachongwa kilometra mbili au tatu, Morum wataweka mita 500 na labda kujenga culvert moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia force account tunaweza kutengeneza Kilometa 10 yote ilijojazwa vizuri kwasababu kukodisha mitambo yote kwa siku moja haizidi milioni tisa. Sasa tukienda kwa mfumo huo kwa force account, barabara nydingi amabzo ni za milioni 30 tutaweza kutengeneza sehemu kubwa na hasa kipindi hiki ambayo karibu barabara zote zimeharibiwa na mvua, kwa kutumia force account tutaweza kutengeneza barabara nydingi zaidi huko vijijini kwa hiyo, nilikuwa naomba muiruhusu TARURA kwa kipindi hiki iweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo lingine ni vizuri suala la *blueprint*, ili uwekezaji uendelee kukua wa ndani na wa nje, *blueprint* bidhaa ya Kitanzania kama isipokuwa na bei ambayo itakuwa ya ushindani ndani na nje, bado bidhaa za nje zitaendelea kutawala ndani ya masoko yetu. Ni vizuri suala hili lisije kidogo kiodgo, lije kwa wakati mmoja ni sawa na mtu ukitaka kupona malaria lazima uchomwe sindano ya Quinine, hivyo hivyo itakuwa na madhara mengi, mapato yanaweza kushuka kwa mwaka mmoja lakini *long run* tutakuwa na mapato mengi zaidi na ajira kwa watu wengi zitaongezeka kwa hiyo jambo hili la *blueprint* ninaomba sana lifanyiwekazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Utawala Bora; nilikuwa naomba nikushauri kwamba Kamati iendelee kusisitiza customer charter iendelee kuhimizwa katika Idara zote, katika Taasisi zote za Serikali ili kila mmoja aweke wazi customer charter yake. Lakini humo humo nilikua naomba sasa tumeingia kwenye mfumo wa kidigitali na kielektroniki, kila mtu anapopeleka barua au nyaraka apewe risiti ya kielektroniki ya ku-acknowledge kwamba barua tumepokea tarehe hii na nyaraka fulani ili haya mambo ya kusumbuana Mwaka mzima hupewi majibu hayatakuwepo, mtu unakuwa na ushahidi kwamba vitu vyangu vimepokelewa na yote haya ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi uwe na ushahidi kwa sababu unaweza kuacha barua baada ya mwaka unaambiwa barua yako haijulikani mahali ilipo zaidi ya wewe kusainiwa kwenye kile kitabu chako ambacho siyo ushahidi wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila Taasisi itoe acknowledgement ya barua au nyaraka ambazo watakuwa wanapokea ili twende na *numbering* na kila *first come, first save* ndiyo iwepo. Hiyo ndiyo italeta Utawala Bora na huduma nydingi zitaendelea kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nishukuru, ninaomba Kamati zote zinafanyakazi zao vizuri lakini haya mambo tukiyasimamia vizuri nina uhakika kwamba katika Utawala Bora lakini pia hii ya TARURA itafanya vizuri lakini kwenye uwekezaji hilo ndiyo eneo pekee na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameunda tena Wizara hii ya Uwekezaji ili kuweza kupata uwekezaji wa ndani na nje na tuweze kupata mafanikio makubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wka kazi kubwa anayofanya lakini ni vizuri semina hizi pia msitutolee sisi Wabunge tu, nendeni mkatoe Wizara ya Fedha kwa sababu changamoto ya Wizara zote ziko Wizara ya fedha. Kwa hiyo, naomba huko Wizara ya fedha mtuite hata sisi tutakuja kutoa hiyo semina tukawasaki changamoto na experience ambazo tunapata kutoka huko kwa raia na kwa Wananchi kwa sababu ndiyo wawakilishi wao, nina uhakika hizi zote tutaweza kuzitatua na tukapata mafanikio na tuisiangalie kupata mapato ya moja kwa moja. Inawezekana usipate *direct tax* lakini *indirectly* ukawa unapata mara 10 ya hiyo na ajira kwa Watanzania ikawa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo ni vizuri tukaangalia hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru wka nafasi uliyonipa, lakini nizipongeze Kamati zote tatu, naunga mkono hoja zote, ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mlowe dakika tano na Mheshimiwa Upendo Peneza dakika dakika tano baadae Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiande.

**MHE. LUCY M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Taarifa za Kamati hizi tatu.

Mhesheshimiwa Mwenyekiti, ni Mjumbe katika Kamati ya Utawala na TAMISEMI, tulijadili mambo mengi sana katika Kamati na hoja nyingi zimewasilishwa na Mwenyekiti wetu wakati anatoa Taarifa, naomba nisisitize mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni miundombinu inayoelekea kwenye Chuo cha Hombolo, barabara ya Ihumwa-Hombolo; hali ya barabara ile ni mbaya sana na ni ya muda mrefu na wakati wataalam wanatengeneza wamekuwa wakitengeneza kwa changarawe. Naiomba Serikali badala ya kutengeneza kwa changarawe basi watengeneza barabara ya lami kusudi isileté tena usumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni uhaba wa Watumishi; karibu sekta zote kuna kilio cha uhaba wa Watumishi. Nikitoa mfano katika hospitali ya Mkoa ya Njombe, watumishi wanaotakiwa ni 320 lakini hadi sasa waliopo ni 149. Kwa kweli inakua ngumu sana katika kutekeleza kazi sawa sawa na kama tunavyojuu kwamba upande wa afya tunahangaika ili kupunguza vifo vya wakinamama lakini tunapokua na Watumishi wachache namna hii itakuwa ni vigumu sana kupunguza vifo vya wakinamama. Niiombe Serikali kwasababu tunaenelekea kwenye kipindi cha Bajeti, basi itengete Bajeti ya kutosha kusudi kuweza kuwaajiri Watumishi wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Watumishi hao hao ni miaka takribani minne sasa na huu ni wa tano hawajaongezewa mishahara yao. Niiombe Serikali iwaongezee kishahara kwa sababu tunaelekea kipindi cha Bajeti sasa basi iwafikirie hao Watumishi kuongezewa mishahara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ni Utawala Bora; Utawala Bora ni pamoja na kuwapa watu au wananchi uhuru wa kutoa mawazo yao. Tumeshuhudia watu wanatoa mawazo yao lakini wanakamatwa. Mfano; kuna Mwanafunzi wiki mbili zilizopita huko UDOM alipiga picha kwenye ndoo za maji kulalamikia tatizo la maji, mwanafunzi yule alikamatwa. Niiombe Serikali itoe uhuru wa wananchi kutoa mawazo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni suala la Utawala Bora; wananchi wana haki ya kuchangua viongozi wanaowataka lakini pia kuchaguliwa. Nimeshuhudia toka kipindi cha chaguzi ndogo za Ubunge na Udiwani na hatimaye Serikali za Mitaa. Wananchi wamelazimika kuwa na viongozi wasiowapenda ndiyo maana hadi sasa hivi ukienda maeneo mbalimbali wananchi wanawagomea wale viongozi waliowekwa, wanasema hawataki kuongozwa na hao wenyevitii. (Makofi/Vigelegelé)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunaabudu na tuna dini zetu. Kila mtu ana imani yake. Tuliapa hapo mbele kwamba tutasema ukweli kwamba yale tutakayoyatekeleza yatakuwa ni kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa nimeshuhudia tunafanya kinyume kabisa. Hata dhamira yangu kama Mkristo, mimi dini yangu ni Mkristo, wakati mwingine najisikia vibaya kwamba sisi Wabunge sio wakweli. Naomba tuishauri Serikali yetu, pale inapokosea tuikosoe ni pamoja na kuisisitizia Serikali kuwa na Utawala Bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, kwa sababu imekuwa haizingatii matakwa ya Katiba, itunge Katiba mpya, pia kuweka Tume huru itakayosaidia kutatua haya mambo ambayo yamejitokeza huko nyuma hasa kipindi hichi cha uchaguzi. Kwa sababu tunaenda kipindi cha Uchaguzi Mkuu, isije ikatokea kama ilivyotokea huko nyuma.

Ninaomba sana, kila mtu atafakari, kama kweli unamwabudu Mungu wako, basi ikuguse hiyo kwamba tunahitaji kuwa na haki, tutende haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi/Vigelegele)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lucia Mlowe. Tunaendelea na Mheshimiwa Upendo Peneza, dakika tano na baadaye Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia. Nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kauli aliyoitoa kwamba uchaguzi mwaka huu utakuwa ni wa huru na haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzungumza hilo, naomba pia nikumbushe kwamba Mheshimiwa Rais huyo aliyetao kauli hiyo ndio Mheshimiwa Rais pia liyesema kwamba atamshangaa Mkurugenzi ambaye amemchagua yeye atakayetangaza mtu wa Upinzani kwamba ameshinda kwenye eneo husika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kauli hizi; hiyo ya kwanza kuhusu Wakurugenzi aliitamka zamani kidogo na hii ametamka siku za hivi karibuni. Nategemea kwamba inawezekana kuna badiliko kidogo Mungu ametusaidia. Kama hivyo ndivyo, basi tunamwomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tufanye mabadiliko kwenye Sheria ya Tume ya Uchaguzi ili kuwaondoa Wakurugenzi hawa ambazo alishawaambia kauli ya kwanza, maana yake itakuwa ni mchanganyiko kidogo. Ulishamwambia mara ya kwana asitangaze, halafu sasa hivi ukimwambia ni huru na haki inaweza isieleweke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tukabadilisha sheria hizi tuweze kuwaondoa na hatimaye tupate wasimamizi wa uchaguzi ambao watu wa Upinzani na wa Chama Tawala watakuwa huru na itaweza kutusaidia kutoka pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pia linawaathiri wananchi, kwa sababu kama Mbunge wa CCM ana uhakika kwamba kwa vyovoyote vile atatangazwa, kuna maana gani hata kurudi kwa wananchi kufanya kazi? Kikubwa zaidi utakuwa unaenda kwenye Chama chako kujitahidi kutengeneza mambo vizuri, basi. Kwamba nikishashinda kwenye kura za maoni, imetosha huku kwingine nitaibiwa halafu mambo yataenda. Hakuna maana kupinga ufisadi kama unahimiza wizi wa kura. Kwa hiyo, ninaomba sana kwamba hilo liweze kuzingatiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala zima la suala la Daftari la Wapiga Kura. Daftari hili limeanza kuandikisha na muda umeenda kidogo. Katika maeneo mengi ambayo uandikishaji umefanyika, imekuwa ni zoezi ambalo siyo rafiki, limekuwa ni zoezi ambalo Serikali haitumii muda kuhimiza wananchi kwenda kujianandikisha na taarifa kutoka kwa wakati. Pia vingine ni kwamba daftari limekuwa likigongana na uandikishaji wakati wa Serikali za Mitaa. Daftari limekuwa likigongana pamoja na uandikishaji wa NIDA. Kwa hiyo, unakuta wananchi wamekuwa wakipata mgongano katika kujianandikisha kwenye daftari hilo la wapiga kura. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji sasa, sheria inasema kwamba uandikishwaji ufanyike mara mbili kabla ya Uchaguzi Mkuu. Hii imefanyika mara moja na leo ni mwezi wa pili sasa. Tunajiangalia: Je, nchi nzima na ukubwa wake tutafanikiwa kuweza kuandikisha kwa ukubwa huo ambao tunahitaji ili kutimiza matakwa ya kisheria ya kuandikisha mara mbili kabla ya kufika kwenye Uchaguzi Mkuu ili wananchi wote wapate fursa ya kuweza kujianandikisha na kuweza kupigia kura viongozi wao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho lazima tuone ni Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni uchaguzi ambaa umefanya dhuluma kubwa sana. Tuna Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ambaa hawahitajiki. Hata hivyo, hili suala limetoa funzo tena kubwa sana. Mkurugenzi anafanya wizi; hapokei fomu za watu, anachafua fomu za Wagombea katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, somo ambalo limepatikana ni kwamba tunapoenda kwenye uchaguzi Mkuu, pamoja na kutafuta hela za kampeni, sasa tunamdhiliti vipi Mkurugenzi? Suala sasa ni kwamba tunamdhiliti vipi Mkurugenzi? Fomu zipokelewe, zibandikwe kama inavyohitajika na uchaguzi uweze kufanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali inavyoenda ni fujo kubwa itakayotokea ndani ya nchi hii, ni mauaji makubwa ambayo yatatokea nchi hii, watu hawatakubali haki yao iendelee kunyang'anywa mwaka hadi mwaka. Kwa sababu hiyo basi, Mheshimiwa Mbowe ametumia busara sana, ni Mwenyekiti wangu wa Chama, namheshimu na pia Mungu amembariki hekima ya ajabu sana. Alipokuwa kwenye Mkutano wa Uhuru Mwanza tarehe 9 Desemba alisema kwamba ifike mahali nchi tufikie maridhiano, tuzungumze, tuondoe changamoto tulizonazo ili kuепusha maafa makubwa ambayo yanaweza kutokea ndani ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana ameweka msisitizo kwamba anamaanisha ombi la maridhiano. Jana ametoa press conference ambayo imeandika barua na vitu gani ambavyo tunahitaji kubadilisha. Sasa mara nyingi katika nchi nyingine maridhiano yanafanyika baada ya watu kuuana, baada ya watu kukatana mapanga ndiyo watu wanakaa kwenye meza kuzungumza kwamba kila mtu ameshaonesha ubabe wake, sasa watu wanazidi kufa, sasa tukae chini tuzungumze mambo yaende. Sasa yeye ametumia busara kwamba tuzungumze kwanza kabla maafa hayajatoka. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa busara hiyo basi, ninaomba Mheshimiwa Rais atumie busara aliyonayo tukae chini tuzungumze, tubadilishe yanayowezekana, twende mbele...

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini kelele wewe!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo malizia.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** ...na tufanye uchaguzi wa haki ili hii amani tunayohitaji ndani ya nchi hii iweze kudumu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitendo cha uzalendo zaidi ya kuitakia nchi yako amani na maridhiano na kuomba maridhiano ni kitendo cha uzalendo mkubwa sana.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo muda wako umeisha.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.  
(Makofi/Vigelegele)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia, baadaye Mheshimiwa Hawa Chakoma na Mheshimiwa Lubeleje wajilanda kwa dakika tano.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika taarifa ambazo zimewasilishwa kuhusu TAMISEMI, Utawala Bora. Nami napenda kujielekeza zaidi kwenye taarifa ya TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa ambao tumeupata katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao haujawahi kutokea. Nina uhakika kabisa kwamba Uchaguzi Mkuu tutashinda kwa asilimia nadhani zile zile au zaidi ya pale. Kinachofanya chama kushinda siyo Tume Huru, ni maandalizi ya Chama na jinsi gani chama kinakubalika ndani ya wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tuliomo humu ndani tumeshinda kupitia Wakurugenzi hao hao ambao leo tunawaona hawafai. Kwa hiyo, mimi naomba tu tuijandae kwa uchaguzi wa mwaka 2020 kwa Tume yetu ile ile ambayo ndiyo imewaingiza humu ndani ya Bunge na nina uhakika wale wenye sifa watashinda na wale wengine ndio hivyo tena. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuipongeza TAMISEMI kwa jinsi ilivyosimamia ujenzi wa Hospitali za Wilaya pamoja na Vituo vya Afya kupitia force account. Gharama ambazo tumezitumia kujenga hospitali moja kwa tulivyozoea nadhani hata robo ya hospitali isingeweza kufikiwa. Naishukuru TAMISEMI kwamba tumepata hospitali ya Wilaya, Vituo vya Afya huko Kilambo, Mahurunga kimekarabatiwa, Mkunwa kinaendelea kujengwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunayo maombi ambayo yako TAMISEMI ya Kituo cha Afya Mango Pachanne na pia kutokea Msimbati, Madimba, Ziwani, Nalingu mpaka Msangamkuu tunahitaji kupata Kituo cha Afya kingine. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuamua kutupatia zaidi ya shilingi bilioni 15 kumalizia Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini. Sikupata nafasi kuchangia Wizara ya Afya, nachukua fursa hii kuishukuru sana Wizara ya Afya kwa jinsi inavyosimamia ujenzi ule kupitia National Housing. Nina imani kabisa baada ya mwaka mmoja Mtwara kwa maana ya Mkoa Kanda ya Kusini, Wilaya zetu zitakuwa zimeboresha kwa kiasi kikubwa huduma za afya. Ndiyo maana nasema sina wasiwasi hata kidogo kwamba tutashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu unaokuja, kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, imetatua kero za wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tena Serikali kwa kutoa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kwa kweli imekuwa ni chachu na imeweza sana kuongezea mitaji wanawake wetu, vijana wetu pamoja na watu wenye ulemavu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutoa mapendeleko kidogo kwa upande wa wenzetu wenye ulemavu hasa maeneo ya vijiji. Tunasema ili wawe na kikundi, wanahitajika wawe angalau 10. Kijiji kingine unakuta labda walemovu wako watatu, wanne kwa hiyo, inakuwa ni ngumu hasa ukizingatia wao ni walemovu. Kwa hiyo, hawesi yeye akasema aungane na mlemovu labda wa Kata nyiningine au wa Tarafa nyiningine na mara nyangi kikundi ni lazima muwe ni watu mnaofahamiana, mnaoleweana. Kwa hiyo, nawaomba wenzetu TAMISEMI waingalie hiyo Kanuni ili waweze kuirekebisha iweze kupunguza idadi ya wanakikundi hasa kwa wenzetu wenye ulemavu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TARURA naiomba Serikali iongeze kiwango ambacho TARURA wanapewa kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Asilimia 30 wanayoipata kwa kweli ukilinganisha na mtandao wa barabara ambao uko katika maeneo yao ni kidogo sana.

Kwa hiyo, tunaomba waongeze kama haiwezekani 50 kwa 50, basi angalau asilimia 40. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninarudia tena kusema tutashinda Chama cha Mapinduzi kwa kishindo kikubwa sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Chakoma dakika tano na Mheshimiwa Lubeleje dakika tano, baadae Mheshimiwa Amina ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia taarifa za Kamati zilizopo mbele yetu. Kwa dakika tano ulizonipatia nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna anavyotekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Pwani ndiyo mfano mzuri sana kwa namna gani Mheshimiwa Rais ameweza kutekeleza llani. Nasema hivyo nikainisha miradi mitano ya kimkakati ama miradi mitano ya Kitaifa yote inaonekana ama inapatikana ndani ya Mkoa wa Pwani. Tuna mradi wa kufua umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere, unapatikana Rufiji Mkoa wa Pwani, tunao mradi wa njia nane ambao unapatikana Kibaha Mkoa wa Pwani, tunao mradi wa ujenzi wa bandari kavu inapatikana Kibaha Mkoa wa Pwani, tuna mradi wa reli iendayo kwa haraka standard gauge ambayo kimsingi pia inapita Mkoa wa Pwani na pia tunao ujenzi wa viwanda unaoendelea takribani kwenye mikoa yote ya Pwani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hili kubwa analolifanya. Sambamba na hilo, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ununuzi wa ndege. Napenda tu kusema kwamba muda siyo mrefu, ndani ya mwaka huu tunatarajia kwenye kupokea ndege nyngine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hapa watu wanashindwa kufungamanisha maisha ya watu pamoja na aspects za uchumi. Wanaposema wananchi hawataki ndege ni kwamba wanashindwa kuainisha ni kwa namna gani ndege zinaweza kuingizia nchi yetu mapato ambayo kimsingi mapato yale yakikusanywa yakiingia kwenye Mfuko Mkuu la Hazina, ndiyo yanaenda kulipa Elimu Bila Malipo, ndiyo yanaenda kwenye miradi ya maji na elimu ya juu. Kwa hiyo, sijajua wenzetu wanafeli wapi? Ila nafikiri wanashindwa kuoinisha hivi vitu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kusema, kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anafanya na hatuna budi kumpongeza na bado nikuchukulia mfano wa Mkoa huo wa Pwani, ametupatia miradi mbalimbali kwenye Wilaya mbalimbali za Mkoa wetu wa Pwani ya ujenzi za Ofisi za Halmashauri. Tuna ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri Kibiti, ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri Kibaha, ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri Mafia na ujenzi wa Ofisi za Halmashauri Kibaha Vijijini. Kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Rais anafanya mambo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ujenzi wa Hospitali za Wilaya, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi 1,500,000,000/= kwa ujenzi wa Hospitali za Wilaya karibia kwenye Wilaya nne za Mkoa wa Pwani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yote na mengine mengi yanayofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli hatuna sababu ya kushindwa ifikapo Oktoba, 2020. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamekuwepo hapa malalamiko juu ya uhamashajji wa daftari la kudumu la wapiga kura, kwamba inasemekana daftari limekuja mwishoni. Daftari

hili lilianza nyuma kidogo, liko linaendelea kutoka Mkoa mmoja kwenda mkoaa mwininge. Mkoani kwetu linatarajia kuingia muda siyo mrefu mnamo tarehe 14 mpaka tarehe 20. Serikali imefanya kazi kubwa ya uhamasishaji, lakini suala la uhamsishaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura lina mahusiano ya karibu na ushikaji wa dola. Kwa maana hiyo, kama unataka Serikali ndiyo ikuhamasishie, hakika itakapifika hapo kesho kutwa tutakapoenda kupata ushindi wa kishindo, bado mtabaki kulalamika na Wakurugenzi, bado mtabaki kulalamika na kuibwa kura, lakini dola inatafutwa, dola inaandaliwa, dola inachakarikiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mziki wa Mheshimiwa Magufuli sioni wa kumuingia mpaka sasa. Kuna mambo makubwa ambayo yamefanywa na Mheshimiwa Rais na pengine wenzetu walikuwa wanadhani pengine Mheshimiwa Rais ana-bip, lakini kwa matokeo ya Serikali za Vijiji na Vitongoji, walipoona mziki umekaa vibaya, ndipo walipoona ngoma ngumu na kuomba maridhiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono taarifa zote tatu. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Chakoma. Mheshimiwa Lubeleje na baadaye tunamalizia na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hizi zote tatu. Nawapongeza Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Kamati zote tatu kwa kazi nzuri wanaliyofanya, kwa sababu wao ndio wanaoichambua bajeti na ndio wanaoikagua hii miradi.

Mimi ni mjambe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na TAMISEMI kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI wamejenga sasahivi vituo vya afya takriban 300, hospitali za wilaya takriban 69. Maeneo hayo wananchi walikuwa wanapata shida sana matibabu, lakini kwa sababu hivi vituo vya afya vimejengwa kwa hiyo huduma za afya zitaboreka. Kwa mfano akina mama wajawazito walikuwa wanapata shida wanafuata matibabu mbali, wataalamu walikuwa wachache, lakini kwa ujenzi wa hivi vituo vya afya mimi nina hakika, kwa sababu katika vituo vya afya hivi madaktari bingwa na manesi watapelekwa, kwahiyo hata operation ndogondogo zitafanyika kule. Kwa hiyo, niipongeze sana TAMISEMI kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la MKURABITA, kwanza nianze TASAF. TASAF imeanza mwaka 2002 au 2003, imefanya kazi nzuri; TASAF awamu ya kwanza na ya pili walikuwa wanajenga shule, barabara, pamoja na zahanati, lakini TASAF awamu ya tatu ni kusaidia kaya masikini. Wale ambaao hawana uwezo kabisa kwa hiyo, ndio wananaufaika na Mfuko huu wa TASAF. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba huu Mfuko wa TASAF unufaishe wananchi ambaao hawana uwezo, wasije wakaorodhesha majina ya watu ambaao wana uwezo, itakuwa si jambo jema sana kwa sababu, lengo la Mfuko huu wa TASAF ni kuboresha au kunufaisha wale watu ambaao wana hali za chini sana. Tumetembelea baadhi ya mikoa na tumewaona watu wamenufaika sana na Mfuko huu wa TASAF. Wamejenga nyumba, wanapeleka watoto shule, wanapeleka watoto kwenye vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA imefanya kazi nzuri sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais hata juzi alikuwa kwangu pale Mpwapwa, tulikwenda Kijiji cha Izomvu na wamepewa Hati Miliki za Kimila. Zamani vyombo vya fedha walikuwa hawazitambui hizi Hati Miliki za Kimila, lakini nashukuru sana na niwapongeze NMB, NBC pamoja na CRDB, wamezitambua Hati Miliki na wanatoa mikopo kwa hawa watu ambaao rasilimali mashamba yamerasimishwa, kwa hiyo, wanapata fedha wanaboresha

maisha yao. Ushauri wangu ni kwamba, wale wananchi ambao wanapata mikopo watumie fedha hizo kwa kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu sheria ndogo. Mimi nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo. Ombi langu ni kwamba, wazishauri au waziagize halmashauri zote kwa sababu, Halmashauri zimeundwa chini ya sheria kwa hiyo, waendeshe vikao kufuatana na utaratibu, sheria na kanuni. Kuna baadhi ya Halmashauri wanaendesha vikao bila kufuata kanuni. Wawe na *Standing Orders* kila Halmashauri itumie *Standing Orders* kuendesha vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nashukuru sana. Na nirudie kumpongeza Waziri wa TAMISEMI kwa kazi nzuri pamoja na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote tatu, asante sana.

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Lubeleje, tunamalizia mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Amina Mollel, badaye tutaenda upande wa Mawaziri.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kusimama hapa mwaka huu wa 2020. Ninapongeza na kuunga mkono kamati zote tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Jambo kubwa ambalo nawapongeza sana kwa jinsi ambavyo wameweza kuizungumzia asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu ambayo ni kazi kubwa pia inafanywa na Serikali yetu. Kipekee kabisa kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Serikali yake kwa jinsi ambavyo leo hii miaka minne tunasimama tukizungumza huku tukijidai kwa yale mambo mazuri aliyofanya katika nchi hii kwa kipindi kifupi, hajawahi kutokea na hii ni historia imeandikwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona matunda mazuri, tumeona ni kwa jinsi gani ambavyo Rais huyu amejitoa kwa Watanzania. Pamoja na lawama zote lakini hata siku moja hajawahi kurudi nyuma amesimama katika kile anachokiamini. Kutokana na mazuri anayoyafanya Mheshimiwa Rais ndio maana hata kelele zinakuwepo nyingi na ukiona kwamba unaporusha jiwe ukasikia kuna kelele ujue kwamba, tayari kuna mtu limempata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Rais wetu tunaona kwamba ni kwa jinsi gani hata hiyo demokrasia ambayo wenzetu wamekuwa wakizungumzia, na kwa miaka zaidi ya miango sasa miwili sijawahi kuona hiyo demokrasia ambayo wao wanaizungumzia kwa upande wa pili, lakini kwao wenywewe utekelezaji umekuwa ni ngumu. Unapozungumzia jambo wanasema kwanza kabla hujanyoosha kidole kwa mwenzako angalia hivyo vidole vingine inarudi wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunasimama hapa tangu miaka hiyo na leo hii tuko katika Bunge, tangu tumeanza kumsikia Mheshimiwa Mboge ni Mwenyekiti na mpaka sasahivi ni Mwenyekiti. Je, hii ni demokrasia gani? Kama si kwamba, ni kuisema upande wa pili wa Chama Cha Mapinduzi ambao ndio wana Serikali? Serikali ambayo inafanya mambo makubwa katika kuwatetea wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakipinga ndege, lakini leo hii wao ndio wa kwanza kupanda hizo ndege, pamoja na kwamba, wanazipinga hizo ndege na wamekuwa wakizikimbia kamera zisiwarekodi kwa ajili ya hizo ndege. Sisi kama Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi tuna kila sababu ya kujivunia kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati ninaomba nimpongeze Waziri wa Mambo ya Nje kwa kazi nzuri aliyoifanya, pamoja na lawama nyingi, lakini umeonesha

kwamba, wewe ni mwamba usiotetereka. Sisi kama Wabunge tuna kila sababu ya kumpongeza na leo hii tunajivunia yale ambayo yalikuwa yanapingwa, leo hii tunayo Twiga ambapo Barrick wamebwaga manyanga na hatimaye kuona ni kwa namna gani washirikiane na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ili Watanzania waweze kufaidika na asilimia 16. Yote hii ni kwa sababu ya Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambaye hababaishwi na hajawahi kuyumba hata siku moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tuna kila sababu ya kujivunia. Walisema kwamba, hapa sisi tungeweza kuwekewa vikwazo kwa kuvunja mikataba, hakuna mikataba iliyovunjwa, sheria zimeletwa hapa na tumezipitia. Mwaka wa nne leo tuna kila sababu huu mwaka wa tano kujivunia yote yaliyofanywa na Serikali ambayo inaongozwa na Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapiga kelele sana, lakini ukweli ni kwamba baadhi yao wamekimbia hata majimbo yao. Sasa unategema nini? Siku zote utavuna ulichopanda, mwaka 2020 tunakwenda kuonesha kwamba Watanzania wanaelewa sasa pumba ni zipi na mchele ni upi. Kwaajili ya kazi nzuri iliyofanywa na Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Wabunge wa CCM wana asilimia kubwa ya kurudi katika Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unajiuiza hivi mtu mzima inakuwaje leo anazungumza anasema tutashiriki kikamilifu kwenye huu uchaguzi, lakini dakika za miso maji ya shingo anasema hatushiriki kwenye uchaguzi? Hebu tunaomba safari hii kama kweli ninyi ni wanasi sasa mahiri msuse uchaguzi wa 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti Kazi kubwa itafanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na wengi wanakwenda kufa kifo cha taratibu. (Makofi/Vigelego)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana. Ninawapongeza sana Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya na wao ndio wanaotufanya tutembee vifua mbele. Vituo vingi vimejengwa, barabara tunaona zimetengenezwa; waulize upande wa pili, hawajui hata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwa kusema kwamba, Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya, iwe wa Viti Maalum, wa Majimbo, tumeshuhudia ni kwa jinsi gani wanajituma. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea sasa upande wa Mawaziri, tutaanza na Mheshimiwa Waitara dakika tano, Mheshimiwa Kandege dakika tano, baadaye atafuatia Mheshimiwa Azzan Zungu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja za kamati zote tatu. Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati zao walitushauri kama Serikali, tumechukua hatua kwa mambo ambayo walielekeza na tunaendelea kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye hoja zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge juu ya elimu, na Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia maboma. Niwaambie tu kwamba, tulitoa fedha hapa shilingi bilioni 29.9 ya kupeleka kwenye maboma mbalimbali yakaleta mabadiliko makubwa, lakini pia hapa tulipo tupo kwenye mkakati wakupeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni 200, ili kuongeza miundombinu ya elimu. Pia tumetenga fedha zaidi ya bilioni 200 kwa ajili ya kwenda kuimarisha elimu ya shule za msingi, na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu watu wakaelewa kwamba kila mtu akisimama anazungumza miundombinu hapa. Juzi tulizungumza mjadala wa fedha hapa tunatarajia

kupata, zingesaidia sana. Tunatafuta vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu yetu. Ufaulu umeongezeka sana. Kwa kauli ya Mheshimiwa Rais na maelekezo yake ni kwamba elimu bure ipatikane kwa watoto wengi wa Tanzania amba walikosa fursa hiyo imesa saidia sana kuwa na watoto wengi shulen; kwahiyio tunahitaji kuboresha huduma hii. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ambzo zinazungumzwsa trilioni 1.5 zingeweza kujenga mabweni zaidi ya 300 Tanzania nzima, madarasa 800 ya sekondari, madarasa 1,200 ya shule za msingi, tungejenga shule 26 mpya za wasichana, tungejenga mabweni maalum mahsus na shule za msingi, ni mambo makubwa sana. Ukitaka kujua hili tafuta taarifa hizi ili tuweze kuzungumza kwa pamoja, kwamba tunapokuwa tunapanga mipango kuboresha elimu yetu tushirikiane kwa pamoja bila kuleta ubaguzi na ubinasi uliopitiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hoja hapa zimezungumzwa; kwa mfano kuna hoja ya Serikali za mitaa. Uchaguzi huu uliashaisha na wenzetu walisusa wenyewe na maelekezo na msimamo wa Serikali ni kwamba uchaguzi umekwisha. Kama kuna mtu anampinga Mwenyekiti wa Mtaa afuate utaratibu, asipofuata mtakuja hapa tena kulialia na kulalamika. Sheria ndogo zipo kwenye vijiji, kamati za ulinzi na usalama zipo pale watafanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na si kweli kwamba ukienda kwenye ngazi za vijiji na vitongoji eti wanachama wa upinzani ni wengi kuliko wa CCM, sijapata kuona hali hiyo. Kwa hiyo, ukitaka kuleta, haiwezekani, wanachama wa Chama Cha Mapinduzi ni wengi kuliko wa upinzani; na ndiyo maana hata huko mtaani wala hakuna kelele. Kwa hiyo kama kuna mtu anahamasisha na kutisha watu Wenye viti waliochaguliwa halali kisheria na kikatiba wafanye kazi zao kama kuna mtu anawabughudhi sheria lazima ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja hapa ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mbunge wa Tanga Mjini. Mheshimiwa Mbaruku amekuja kutoa hoja kwamba kuna Madiwani wamerudi kutoka CUF wameingia CCM na wamehudhuria vikao vya Halmashauri kule. Nimeongea na Mkurugenzi wa Jiji, Mheshimiwa Mbunge amekaa hapa wiki mbili za kamati hakuleta hoja, hakupiga simu, hakuja Wizarani, hajalalamika na hana barua yoyote ile. Hii wiki ya kwanza ya Bunge imeisha. Kwa hiyo natoa hoja ambayo Mkurugenzi wa Halmashauri wa Jiji la Tanga hawezi kufanya kazi mambo ya mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ni kwamba, barua ilipaswa kuandikwa ya kuonesha kama kweli CUF hao madiwani wamehama. Yeye ameona watu wanasesma Katibu Mkuu wa CCM ameenda kwenye mkutano, wamevutiwa na mambo yake mazuri na utekelezaji wa ilani, wakaenda kumsalimia, huenda walikuwa wanaweka booking kwamba, hivi karibuni watarudi CCM. Sasa kama CUF wanasesma madiwani wamehama...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ...wampelekee barua Mkurugenzi ili aweze kuchukua hatua hiyo. Kwa hiyo, utaratibu uliopo kama barua haijaenda wale wataenda kupata stahiki zao na huu ndio utaratibu wa kawaida...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kama kuna mambo yanatolewa ya mlalamiko ndiyo maana tuko hapa kwenye corridor, tunakunywa pale chai canteen tunazungumza tunawasiliana tunapeana taarifa. Ukileta hapa kama taarifa rasmi

tutaku-crush kwa sababu ni taarifa ya uongo; tuwasilisne kama una taarifa za kutosha, barua iandikwe ifanyiwe kazi, haijaandikwa wakurugenzi watafanya kazi na watawatambua hao madiwani wataendelea kuwapa stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, imezungumzwa hapa uchaguzi wa 2020. Niseme tu vizuri bahati nzuri nina uzoefu wa ile kambi na nina uzoefu wa hapa. Waheshimiwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi naomba niwaambie ukweli hawa wanaweweseka hali ni mbaya kwelikweli huko majimboni. Hali ni mbaya kwelikweli! Kwa sababu katika awamu za nchi hii, hii ndio awamu pekee kila Mbunge iwe kisirisiri, iwe chumbani kwake akisimama lazima amtaje Rais John Pombe Magufuli kwa kazi aliyoifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jimbo la uchaguzi halina mkono wa Rais Magufuli. Hakuna mkoa hauna mkono wa Waziri, hakuna maeneo hakuna jiwe ambalo limeacha kuguswa. Kwa mazingira hayo Watanzania hawakutaka upinzani walitaka kazi na ...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ..kiongozi mwenye msimamo, kuondoa rushwa. Upele wa Tanzania umepata mkunaji na 2020 wanatoa zawadi na kura za asante kwa Rais Magufuli ili aweze kusonga mbele na kazi lazima iendelee...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni muhimu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** ...Kwa hiyo, wasiwasi wao ni faida kwetu kamba, mchezo umewashinda kabla ya kuingia uwanjani. Asante.

(Hapa, baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa waitara...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ye ye ndiye anayeweweseka, Mara hatakiwi, Ukonga hatakiwi...

**MWENYEKITI:**...Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Kandege Dakika tano, badae Mheshimiwa Azzan Zungu ajiandae. Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa fursa ili niweze kuchangia machache. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehemaa kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipekee nipongeze taarifa za kamati zote tatu. Kamati zimesheheni weledi wa kutosha na ushauri ambaa sisi tumeupokea kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika taarifa za kamati mbili. Naomba nianze na Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali kipindi hiki tumefaidika sana na ushauri ambaa umekuwa ukitolewa na kamati hii, maana kuna maelekezo, na sisi kama Serikali tumefanya kazi ndio maana zile sheria zote ndogo ambazo zilikuwa zikilalamikiwa hapa zamani sasahivi imebaki ni historia. Naomba niipongeze sana kamati ukianzia na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote kwa ujumla wamekuwa na msaada mkubwa sana kwa Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Kamati ya Utawala na TAMISEMI. Kamati hii imekuwa ya msaada mkuba sana. Hata hivyo naomba nijikite katika suala zima ambalo sisi Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wetu; mwanzo lilivyoanza lilikuwa kama lina ukakasi. Ni suala zima la vitambulisho kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ubunifu ambao Mheshimiwa Rais amefanya ni suala zima la kuwatambua wajasiriamali wadogo na kwamba, kupitia wajasiriamali wadogo tutaweza kuwapata mamilionea wengi wa kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa nikimuwalisha Mheshimiwa Waziri nikaenda Halmashauri ya Kigamboni, kuna wajasiriamali wadogo ambao wamepewa vitambulisho na CRDB kwa kuwatambua imeanza kuwakopesha pasi na riba; hakika pongezi kwa Mheshimiwa Rais ni ubunifu wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaomba nichukue fursa hii kwa Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo tumekuwa tukishauri mambo mazuri basi nitumie fursa hii huko kwetu kwenye majimbo na sisi tuhimize wajasiriamali wadogo waweze kutambuliwa. Na katika fedha ambazo zinapatikana katika hii asilimia 10 ambayo tumekubaliana naomba nipongeze kamati zote ni jithada za kamati ndio zimesababisha asilimia 10 ikatengwa ambayo inakopeshwa bila riba. Sasa ni vizuri tukaanza kuwatambua wajasiriamali hawa wenye vitambulisho ndio wakawa kipaumbele katika kupatiwa mikopo ambayo haina riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja nyingi, katika hoja moja ni pamoja na suala zima la TARURA; tunashukuru kwa pongezi ambazo zimetolewa, lakini imesemwa hoja kwamba, kiasi cha fedha kwa maana ya asilimia 30 haitoshi. Ni kweli inawezekana ikaonekana haitoshi lakini ni vizuri tukakumbushana Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri alivyokuja alitoa ufanuzi kwamba, kuna mapitio ya formular ya namna ya ugawanyaji wa hiyo asilimia 30 kwa 70. Ninaomba niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa pale ambapo utafiti utakuwa umekamilika formular ikaja hakika tunajua kabisa uko uhitaji mkubwa wa kujenga barabara hasa ambazo ziko vijijini. Vilevile lakini tusje tukasahau pale ambapo TANROADS wanajenga ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami pia ni wa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ni kwamba, mapendeleko ya Waheshimiwa Wabunge tunayazingatia na Serikali itafanya kazi ili tuje na formular ambayo itakuwa inazingatia uhalisia na pesa ziweze kwenda kwa mgawanyo uliosahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ongezi ambazo zimetolewa kuhusiana na suala zima la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la Afya Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusiana na Watumishi ambao wanatakiwa waende kwenye Vituo vya Afya na Hospitali zetu ambazo zimejengwa. Naomba tuendelee kuwashakikisha Waheshimiwa Wabunge, Serikali hii ya CCM ambayo sikio lake linasikia kila sauti ambayo inatoka na hivi karibuni ninyi nyote ni mashuhuda kwamba kuna nafasi ambazo zimetangazwa kwa ajili ya ajira ambazo deadline ni tarehe 7 mwezi huu hii yote ni katika kuhakikisha wanaajiriwa Watumishi wa kutosha ili haya majengo ambayo yanajengwa isije ikageuka kuwa white elephant.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la Shirika la Soko Kariakoo kuna michango ambayo imetoka naomba niwashakikishie Waheshimiwa Wabunge na sisi Serikali tumeliona lakini pia kuna maboresho makubwa sana utendaji wa masoko Kariakoo umebadilika na hivi kwa mara ya kwanza wametoa gawio kwa Serikali jumla ya shilingi milioni kumi ni mwanzo mzuri nakushukuru kwa fursa. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Tunaendelea na Mheshimiwa Azzan Zungu baadaye Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mheshimiwa Maige wajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru lakini kuzipongeza Kamati zote tatu kwa kazi nzuri waliyoifanya kuwasilisha hapa Bungeni na naziunga mkono taarifa za Kamati zote tatu kwa namna walivyowasilisha na kufanya kazi na kutoa taarifa ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ni chombo ambacho kinasimamia asilimia kubwa sana utendaji wa Serikali nampongeza sana Mheshimiwa Jafo na Mawaziri hawa Wawili anaofanya kazi nao pamoja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni Wizara ambayo ndiyo ni engine ya Taifa hili, yako masuala ya Elimu, Afya na masuala mengi na hasa mazingira hata sherehe yetu ya mazingira asilimia kubwa ya kazi zetu zinafanya na Watendaji wa halmashauri ambao wako chini ya Mheshimiwa Jafo na Wizara yake ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza sana lakini nichukue nafasi hii vilevile kuunga mkono kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kubuni vitambulisho vya Wajasiriamali sasa hivi suala la Wamachinga, Mama lishe katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa yote Tanzania usumbufu hakuna tena. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati anafunga Kampeni yake pale Dar es Salaam mwaka 2015 alisema atahakikisha anapiga marufuku mgambo na kweli mgambo wote wamepigwa marufuku na hakuna mgambo yoyote anayesumbua wafanyabiashara wadogo wadogo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wadogo wadogo sasa na mitaji midogo waliyokuwa nayo wanahakikisha kuwa mitaji yao iko salama na mali zao haziibiwi wala hawadharumiwi tena. Hii yote ni kutokana na vitambulisho hivi ambavyo Mheshimiwa Rais amewapa vijana wake na wao waone ni sehemu ya Taifa hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza wote waliofaulu katika shule zetu za Sekondari kwa mara ya kwanza katika Mkoa wa Dar es Salaam sasa hivi baada ya kutoka division zero sasa hivi wanafunzi wameanza kupata division one na hakuna division zero. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni jitihada ya Mheshimiwa Rais, Wizara ya Tawala na Serikali za Mitaa kuweka Elimu bure na kuboresha Elimu katika shule zetu. Tumejenga mabweni shule ya Jangwani sababu wanafunzi waweze kusoma na walale kwenye mabweni wasirudi majumbani nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo Wizara hii unaitendea haki wewe na Manaibu Mawaziri wako Wawili baada ya maneno hayo naunga mkono Kamati zote tatu. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Azzan Zungu tunaendelea na Mheshimiwa Angellah Kairuki baadaye Mheshimiwa Maige ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine waliounga mkono hoja hii kipekee nipongeze sana Kamati yetu ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri waliyoifanya lakini kwa taarifa nzuri waliyoiandaa nishukuru kwa namna ambavyo wamekuwa wakishirikiana nasi pamoja na Mheshimiwa Waziri mwenzangu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenyewe Ulemavu Mheshimiwa Jenista kwa kweli wamekuwa wakitupa ushirikiano mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia masuala machache la kwanza kuendelea kuwashakikishia Watanzania kwamba kwa upande wa uhamasishaji na kuvutia mitaji ya uwekezaji tunaendelea kufanya jukumu hilo na wawekezaji wamekuwa wanakuja kwa wingi na kwa mwaka uliopita tumeweza kupata takribani uwekezaji wenye mtaji wa zaidi ya Dola Bilioni 2.8 na tunaendelea kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja nadhani ya Mheshimiwa Jitu ilijitokeza kwamba tuone namna gani tunaendelea kujenga wawekezaji wazawa zaidi jukumu hilo tunaendelea kulifanya na ukiangalia katika Usajili wa Miradi ile ambayo imesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania zaidi ya asilimia 48 ilikuwa ni Miradi ya wazawa na tunaendelea kuhamasisha na tunatoa rai wazawa wengi zaidi ikiwezekana waweze kusajili Miradi yao TIC. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kutokuwa na uratibu au kutokuwa na ushirikiano baina ya Wizara na Taasisi nipende tu kusema kwamba tunaendelea kushirikiana vizuri na tutaendelea kuboresha namna ambavyo tunaendelea kuratibu lakini vilevile kushughulikia masuala mbalimbali ya Uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya ucheleweshwaji wa huduma na Kamati imeweza kutoa ushauri mzuri sana ya kuweza kutumia zaidi huduma za kielektroniki nipende kusema tu kwamba tumeanza na kwa kuanzia kwa sasa walau katika Idara yetu ya kazi wameunganishwa katika Mfumo wetu wa Kituo cha kazi kupitia Mifumo ya Vibali vya Kazi na kwa sasa vingi vinatolewa pia kwa mfumo wa elektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa sasa pia tumeandaa mfumo kwa ajili ya kuweza kutoa mrejesho kutoka kwa wawekezaji na wafanyabiashara lakini vilevile kwa Wafanyabiashara wetu na wawekezaji kuweza kutoa malalamiko yao kupitia mfumo wa kielektroniki na ni jukumu ambalo tunashirikiana Ofisi ya Waziri ya Mkuu, CPSF pamoja na Baraza letu la Biashara la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya suala zima la utelekezaji wa blueprint nipende tu kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ndiyo wamepewa jukumu hili, Wizara ya Viwanda na Biashara tayari wameshaandaa mapendekezo na tunaamini mchakato ndani ya Serikali utakapokamilika basi mapendekezo hayo kwa ajili ya kutunga Sheria ya Uwezeshaji wa Biashara au *business facilitation Act* yatawasilishwa Bungeni mapema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa Sheria yetu ya Uwekezaji ambayo kimsingi tutaupitia upya muundo wa TIC lakini kuangalia masuala mbalimbali ya kitaasisi na namna ambavyo tunashirikiana na Taasisi nyingine.

Vilevile mipaka ya Taasisi moja na Taasisi nyingine katika kuvutia na kuhamasisha uwekezaji na masuala mazima ya uratibu wa Uwekezaji nayo ni masuala ambayo tunakusudia kuyaingiza katika Sheria hiyo ambayo itakuja humu bungeni muda si mrefu na tutaomba ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja pia la ukosefu wa miundombinu wezeshi na ya msingi kwa ajili ya uwekezaji ni jambo ambalo tumeliona na ni kweli na tayari tunashukuru Ofisi ya Waziri ya Mkuu kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumeendelea kuzihamasisha halmasauri zetu kutenga maeneo ambayo yatakuwa na miundombinu ambayo inakidhi lakini vilevile miundombinu ya umeme, maji na Mawasiliano maeneo ambayo yatakuwa yamelipwa fidia hayana mgogoro lakini yaliyopimwa na yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili pia ilijitokeza hoja ya ucheleweshwaji wa suala zima la uhavilishaji kutoka katika ardhi ya Kijiji kwenda katika ardhi ya jumla ni eneo ambalo ni kweli limekuwa ni changamoto wakati mwingine Mwekezaji amekuwa akitumia miaka mitatu mpaka miaka minne kwa sababu ya mlolongo ambao unahitajika katika uhavilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatua ambazo kutokana na mfumo wetu kama Tanzania wa Umliki wa ardhi, ardhi ya Kijiji ukomo wake kuweza kuiuza ni eka hamsini tu. Kwa hiyo, kwenye hili hatuwezi kuliepuka lakini tunashukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeweza kutoa maelekezo kwa halmashauri zote kuweza kuona ni kwa namna gani wataandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili waweze kuainisha maeneo yanayohitajika kwa uwekezaji na tunaamini halmashauri zetu na vijiji zitakapofanya hivyo basi wataweza kupunguza muda wa uhavilishaji lakini vilevile itatuhakikishia kuwa na uhakika wa ardhi ya uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipaye tu kuwatoa hofu Wana Vijiji ukiangalia kwa kila Kijiji kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa takwimu kama nitakuwa sijakosea haizidi kati ya milioni sita mpaka milioni nane. Kwa hiyo, ni muhimu waweze kuona umuhimu wa kutenga fedha kuititia mapato mbalimbali ambayo wanayapata ili kutekeleza jukumu hili ambalo ni la muhimu sana kwa ajili ya kuwa na uhakika wa utatuzi wa Uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa kuna hoja ya mwingiliano wa majukumu ya Kitaasisi kama nilivyoeleza kuititia Sheria ile ya Uwezeshaji wa Biashara au business facilitation tunaamini suala hili pia kwa kiasi kikubwa litawenza kuondoka vilevile kwa sasa Serikali inaendelea kuititia majukumu ya baadhi ya Taasisi ili kuona ni kwa namna gani tutaweza kuondoa mwingiliano katika usimamizi vilevile kuona ni kwa namna gani tutaweza kupunguza muda na gharama kwa ajili ya uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaanza kwa TBS pamoja na TMDA tutaendelea vilevile kufanya kwa Taasisi nyingine za Serikali. Kulikuwa kuna hoja nyingine kuhusiana na kupunguza tozo tayari ndani ya miaka miwili Wizara ya Fedha na Mipango tuliona hapa kuititia Sheria ya Fedha imeleta zaidi ya tozo 163 kwa mwaka 2017/2018 tozo zaidi 109 ziliweza kufutwa lakini kwa 2018/2019 tozo zaidi ya 54 zimeweza kufutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatua nzuri na tunaamini kadri tunavyoendelea na Bajeti ya Serikali basi Wizara ya Fedha na Mipango itakuwa ikiendelea kufanya hatua hiyo muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa kuna hoja ya halmashauri zetu za wilaya pamoja na mikoa kuweza kutumia na kuutekeleza muongozo uliotolewa TNDC katika kufanya majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi tunashukuru bahati nzuri nimefanya Mikutano kwa kushirikiana na Mawaziri wengine wa kisekta zaidi ya Mikoa saba na tumekuwa tukipata ushirikiano mzuri sana kutoka TNDC vilevile kutoka katika mikoa na halmashauri zetu na wamekuwa wakisitisiza kuona ni kwa namna gani wanaweza kutekeleza mwongozo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru lakini niendelee kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kuvutia na kuhamasisha Uwekezaji muhimu tu kwa halmashauri zetu Wabunge na wananchi kwa ujumla waweze kutambua manufaa ya Uwekezaji kwa ajili ya Taifa letu nakushukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Angellah Kairuki tunaendelea na Mheshimiwa Mahiga baadaye Mheshimiwa Mkuchika ajiandae.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoka pongezi kwa Wenyeviti wa Kamati zote tatu ambazo leo zimetoa ripoti zao kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kutoa msisitizo kwa kutoa pongezi na shukrani kwa Kamati ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo ni ya muhimu sana katika utendaji kazi wa Kamati ya Katiba na Sheria kwanza kabisa Mwenyekiti ameonesha werevu na uadili wa hali ya juu kwa sababu yeye mwenyewe ni Mtaalamu wa Sheria lakini pia ameonesha uwezo wa uongozi wa kuwaleta karibu wanachama wake katika mijadala mbalimbali na kutoka Vyama vyote ambavyo ni wanachama wa Kamati hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuona umaja na mshikamano katika mijadala yao kama niliyoshuhudia katika Kamati ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti huyu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshuhudia kwamba wanachama wa Kamati ile wana uelewa wa hali ya juu wa mahitaji ya nchi hii katika kuleta haki katika nchi hii. Haki ni moja ya huduma muhimu katika nchi kama vile tunavyozungumzia Maji, Afya, Elimu haki ni kitu muhimu na Kamati hii imeonesha umuhimu wa kuleta haki kwa watu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati hii imeonesha kwamba ni wasikivu kwa wadau mbalimbali siyo wao tu wanazungumza kama Kamati, siyo wao tu wanazungumza na sisi kama Wizara lakini wanakaribisha wadau mbalimbali kutoka Mashirika mbalimbali na hii inarutubisha demokrasia ambayo tunatakiwa kuwa nayo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria kwa usimamizi wao wa Miradi mbalimbali ambayo Wizara yangu imekuwa ikitekeleza hawazungumzi tu wanakwenda mpaka kuiona mimi nimeshiriki nao tumetembelea Mikoa ya Mbeya, Arusha, Manyara, Kigoma na kule wamehakikisha kwamba wanasimamia Miradi hii inatekelezwa kwa wakati. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wameleta mawazo ambayo teknolojia ya ujenzi ya sasa hivi imeleta mapinduzi makubwa katika ujenzi wa Mahakama zetu huko mikoani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka niwashukuru Mwenyekiti na Kamati kwa jinsi walivyosimamia Bajeti yetu katika Awamu hii ya Tano sijawahi kuona na nikilinganisha na Bajeti nyingine jinsi tulivyopewa pesa na jinsi pesa zilivyopangwa ili tuweze kufikia mwelekeo wa kufikisha haki karibu na wananchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwelekeo huu nina uhakika yale tuliyoyapata katika Awamu hii ya sasa haitachukua zaidi ya miaka mitano kukamilisha yote ambayo malengo Wizara yangu imeweka hasa katika kusogezza haki karibu na wananchi na kuboresha utumishi wa Wizara hii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukrani za pekee na hapa lazima nisisitiza Mheshimiwa Rais ametuteulia Majaji wa Mahakama Kuu na Majaji wa Mahakama ya Rufani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi huu umeleta tofauti kubwa sana katika kusukuma maamuzi ya Mahakama na kuhakikisha kwamba mrundikano wa Mahakama, mrundikano katika Magereza unapungua na kama tutaendelea kupata ushirikiano wa namna hii na hasa katika raslimali watu nina uhakika kwamba malengo yetu yatafikia mahali pazuri na

tutaweza kushona lazima ushone haki na demokrasia na katika mfumo huu tumefika mahali ambapo utawala bora kwa sura ya haki kwa Raia umejidhihirisha kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa shukrani pia kwa kusaidia na kuunga mkono Taasisi zangu hasa *RITA* ambapo tumekwenda na ninyi katika Mkoa wa Iringa kushuhudia uandikishaji na utoaji wa Vyeti vyatoto chini ya miaka mitano na kuendelea kutoa Vyeti katika Mikoa mingine kwa namna ambayo haijawahi kutokea na tunafanya karibu na *NIDA* na katika zoezi hili lililokwisha sasa hivi *RITA* imeshiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Wizara yangu pamoja na Taasisi na zake tutaendelea nimalize kwa kusema ahsanteni sana Wabunge wote kwa mchango wenu leo katika mijadala hii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote mliyoyasema, yote mliyochangia tutayatekeleza nina unga hoja iliyotolewa hapa ahsante sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Augustine Mahiga Waziri wa Katiba na Sheria. Tunaendelea na Mheshimiwa George Mkuchika sasa na baadaye tutamalizia na Mheshimiwa Jenista Mhagama. (Makof)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kushukuru kunipa nafasi kwanza nieleze naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa jinsi wanavyotuongoz vizuri yale mazuri mliyoyaona katika taarifa tumeyatekeleza kutokana na mwongozo na maelekezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekuwa mchache nitagusia mambo matatu manne kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza limezungumzwa humu ndani nadhani katika Kamati zote nyingi suala la uhaba wa Watumishi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Serikali tumejipanga mwaka huu tunaajiri Watumishi 43,000 wa Kada mbalimbali lakini niungane na Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndugu yangu Kandege kuungana naye nami niwahakikishie Watanzania wote ambao wameshiriki kwa mikono yao kujenga Hospitali 67, Vituo vya Afya 350, Zahanati kemkem kwamba hayatakuwa majengo ya maonesho tutaajiri Watumishi na tumeekaa pamoja na Wizara ya Afya tumeekaa na wataalam mbalimbali kuhusu suala la kuagiza vifaa tiba. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishieni kwamba watumishi wataajiriwa na kama mlivysikia wengine wamekwisha anza kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo limezungumzwa humu ndani kwa kirefu ni Mradi wa kunusuru Kaya maskini *TASAF*, *TASAF* tulikuwa tuna tatizo moja kwamba katika Vijiji tulivyokwenda tumefikia asilimia 70 ya walengwa katika vijiji vyote nchini tulifikia vijiji asilimia 70 na shehia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tulikuwa tuna changamoto ya kumaliza walengwa walibaki ambao hatujawafikia, nataka niwaambie Watanzania kwamba Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli imefanya maandalizi tumeepata fedha za kutosha mwisho wa mwezi huu tutafanya maandalizi kabambe ya kuzindua *TASAF* Awamu nyingine

ambayo tutamaliza thelathini wote waliobaki tutafika Vijiji vyote asilimia 100 tutafika walengwa wote asilimia 100 ili kuweza kuwashudumia wale ambao bado hawajafikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Watanzania wenzangu kwamba sisi katika kijiji wasimamizi wa TASAF hatuendi na orodha ya walengwa. Walengwa wanapatikana pale kijijini ninawaomba tu wanakijiji wote tushirikiane katika kuwatambua walengwa wale ambao kwa uhakika tunajua huyu anahitaji msaada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye Kijiji tukaambiwa kuna walengwa ambao hawakustahili kuwemo kwa kweli wa kulaumiwa ni Wanakijiji wenyewe kwa sababu wao ndio wanaoandaa orodha ya walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshauriwa hapa tufanye malipo ki-electronic, tumejaribu kufanya majoribio mahali. Nataka niseme kwamba tutafika mahala tutafanya malipo kwa mtandao, lakini itawezekana tu kwa wale ambao wana simu na wanajua kusoma na kuandika. Kwa wale ambao itashinikana hivyo, sisi tutaendelea kuwafuata na kuwagawia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilozungumzwa hapa ndani ni suala la MKURABITA, naunganana na Kamati. Kamati inasema tuwawezeshe zaidi, sisi tunakubali kwamba tuwawezeshe zaidi. Tukiwawezesha, naamini watafanya kazi nzuri zaidi. Ilitolewa hoja kwa baadhi ya Wabunge kwamba pengine mabenki yanakataa. Juzi kama alivyosema somo yangu Mheshimiwa George pale, nilikuwa Mpwapwa, tumekwenda kugawa vyeti. Bahati nzuri walialikwa mabenki yote pale, yapo manne pale Mpwapwa. Benki zote nne pale Mpwapwa zimetoa mikopo kwa watu waliokuwa wanamiliki hati za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mabenki hayana matatizo. Nataka niseme, mahali popote ambapo mabenki yatawaleta matatizo labda hawawakopeshi kuititia MKURABITA, basi tupate taarifa katika Wizara na sisi tutachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, hapa ndani asubuhi, mchana huu naona kumetulia kidogo, limezungumzwa sana suala la utawala bora. Nitakuwa sifanyi haki kama ni Waziri wa Utawala Bora halafu nisiseme jambo, tena kwa takwimu ili wale waliosema uongo waone haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora katika nchi, maana yake ni watu kuzingatia sheria, taratibu na kanuni ambazo zimepitishwa *democratically*. *Democratically* maana yake sheria imepitishwa na watu walio wengi. Humu ndani hata kama jambo hulitaki, lakini walio wengi wamelipitisha, hiyo ni sheria halali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia nzima kwa watu walioenda shule wanajua kwamba katika demokrasia walio wengi wape, lakini wale wachache uwasikilize. Kusikilizwa mnasikilizwa, si ndio maana mpo humu ndani! Si mpo wachache! (Makofi)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tusioenda shule tunalitambua hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtu mzima, naona aibu kusimama mwongozo, mwongozo! Hivi mtu anachangia, alikuwa anachangia mtu fulani asubuhi, hoja inapigwa pale, wanapiga kelele wee, mtu asisikilizwe. Kupiga kelele humu ndani wakati mwenzio anaongea huo ni ushamba. Huo ni ushamba! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Watanzania wenzangu, nchi hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni na imemweka Waziri maalum wa kusimamia utawala bora.

**MBUNGE FULANI:** Ambaye ni wewe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Ambaye ni mimi. Kumbe unajua eeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niteo mifano hapa. Unajua Baba wa Taifa alipokuwepo aliruhusu column moja katika gazeti la Daily News ilikuwa inasema: "What They Say About Us?" Wanatusemaje walio nje kule? Kwa sababu wengine humu ndani mnapenda sana ku-quote mambo ya nje, sasa nami mzee nataka ku-quote huko huko milikoenda nyie, niwaonyesheni kwamba ninyi hayo mnayoyasema siyo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika kuhitimisha Hoja ya Kamati iliyowekwa Mezani nimeeleza suala utawala bora, nataka nieleze jinsi tulivyo, tunavyopiga hatua katika utawala bora. (Makofi)

(i) Kutokana na takwimu zinazotokana na tafiti, Tanzania imeonekana kuongeza kiwango cha utawala bora na hasa eneo la mapambano dhidi ya rushwa na hasa eneo la kutumia vizuri rasilimali za wananchi, na kodi ya wananchi. Sasa watu wamelipa kodi, hela inatumika vizuri wewe unataka nini zaidi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanya Transparency International; hawa wanazungumza mambo ya uwazi Kimataifa, wanaleshimika Afrika nzima, siyo Tanzania, hapana dunia nzima. Wanasema, 2019 kwa taarifa iliyotolewa na Transparency International, Global Corruption Parameter Africa 2016: "Tanzania imefanya vizuri zaidi kwa kupata alama 37 na kushika nafasi ya 96 katika nchi 180 duniani." Lililopimwa ikiwa ni ongozeko la nafasi 21. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Mheshimiwa Dkt. Magufuli baada ya kuingia madarakani, tunavyofanya vizuri katika utawala bora, Transparency International wamempandisha nafasi 21. Tumsikilize nani, Transparency International au wewe uliyefanya utafiti kwenye kijiji? (Makofi/Kicheko/Vigelele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuendelee. Kwa matokeo ya takwimu za utafiti wa kila mwaka, Tanzania imekuwa inapanda nafasi tangu mwaka 2015 Mheshimiwa Dkt. Magufuli anapoingia madarakani. Mwaka 2018 Tanzania ilipata alama 36 na kushika nafasi ya 99 ikilinganishwa na mwaka 2017 ambapo ilipata alama 36 na kushika nafasi ya 103. Kila mwaka tunapanda, tunapanda, tunapanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Utawala Bora anawaahidi kwamba tunataka siku moja Tanzania tuwe na *digit* moja tu, siyo kumi na ngapi, hapana. Kumi kushuka chini. Hivi mnayoyaona tunayoyafanya, mwendo ni huo wa kufika huko kwenye *digit* moja, hiyo ndiyo Tanzania ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Hiyo ndiyo Tanzania inayopendwa na watu wa nchi wa hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende na matokeo ya kitakwimu hayo hayo na kama mtu anabisha aje nimwoneshe. Katika matokeo, takwimu hizo kwa upande wa Afrika Mashariki, Tanzania ni ya pili kwa Utawala Bora. Tunachuana sisi na Rwanda. Hivyo ndivyo wanavyosema wasomi na watu wenye authority katika mambo haya. Wewe unatuletea figure za ajabu ajabu hapa, ulifanya wapi utafiti? Mao Tse Tung anasema: "no research, no right to speak. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea. Kwa mujibu wa ripoti ya shirkisho Shirika la Mo Ibrahim Award, yule anayetoa zawadi kwa Marais katika masuala ya utawala bora, ambapo hutolewa ripoti yake kuhusu utawala bora kwa nchi za Afrika; mwaka 2018

Tanzania ilipata alama 58.5 kwa 100. Amevuka huyo! Ilikuwa nchi ya 14 katika Bara la Afrika katika suala la utawala bora ambapo ukililinganisha na huko nyuma tulikuwa na alama 57. Hao ndio wasomi, authority katika mambo ya utawala bora, nami wanansomesha wao. Kama mimi wanansomesha wao; je, wewe! (Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende sasa; mimi nitakwenda nje na ndani, lakini nazungumza na watu wenyewe authority tu, wale ambao hawana authority sikuwa-quote hapa. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti mwengine wa taasisi ya ndani ya nchi wanaita Repoa. Mwaka 2017 imeonyesha wananchi saba kati 10 ya waliohojiwa walisema ushiriki wa Serikali katika mapambano dhini ya rushwa ni mzuri sana. Imani hiyo imeongezeka imetoka sasa 37% kwenye matokeo yaliyotolewa ukililinganisha 2018. (Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameulizwa wenyewe nchi yao, mnasemaje kuhusu habari ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Serikali yake na kwa habari ya utawala bora? Wakasema Serikali yake inafanya vizuri sana, sana. Wameulizwa mmoja mmoja; matajiri wameulizwa, masikini wameulizwa, CHADEMA wameulizwa, CUF wameulizwa, sembuse CCM; nao wameulizwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukija hapa, tunapongea watoto wetu wanatusikiliza huko nje; na watoto wa siku hizi shomile, wamesoma, analinganisha alichosoma yeze kwenye kitabu cha watu wenyewe authority anakulinganisa na unayosema wewe. Hivi ukifika nyumbani siyo ajabu akakwambia eeh, baba, mama ulisoma kitabu gani? Kitabu hiki hapa, kisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu kubwa ya mafanikio ya haya ni utashi wa kisia (political will). Ili nchi ipambane na rushwa, lazima kuwe na ipambane na political will. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Magufuli ana political will ya kupambana na ufisadi. Alisema ataanzisha Mahakama ya Mafisadi na ameianzisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimalizie point moja, mbili za mwisho, maana darasa hili huwa linawapotea, hamlipati kila siku. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utashi huo, imani ya wananchi imeongezeka, nidhamu ya watumishi wa Umma ninaowaongoza mimi Serikalini imeongezeka, imeimarika. Matumizi mabovu ya fedha za ndani, ndani ya Serikali yamedhibitiwa. Kwa sababu tunakusanya vizuri mapato, tunadhibiti matumizi mazuri na watalaam wanasema tunazitumia fedha zetu, ndiyo maana tukienda huku ndege huuuuu, mpaka Songea kwa watani zangu amalo ilikuwa ndege hazitui, zinaenda. Mtwara huko sisemi, Mwanza na kwingineko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namsikiliza Rais wangu, amewaulizeni wala hamjamjibu bado. Kwa nini Mheshimiwa Dkt. Magufuli unanunua ndege kwa fedha taslimu? Akawaambieni kama hela ninayo mfukoni kwa nini nikope? Hivi mtu anayekopa si hana kitu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Tusikilizane. Mifumo ya utendaji kazi imeimarishwa ikiwa ni pamoja na kuziimalisha taasisi simamizi ikiwemo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Tulikuwa na Wilaya...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA**

**BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ndivyo walivyo, wala hatuwashangai, ndivyo walivyo. Mimi Waziri nimepewa muda wa kutosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika, naomba umalizie endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA**

**BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hilo neno la mwisho "endelea", ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema hivi, tumepandisha vyombo vya kupambana na rushwa. Tulikuwa na Wilaya 21 hazina ofisi, tumefungua ofisi, tumewapa na magari. Mwaka huu Wilaya zote nchi hii kila Wilaya ina Ofisi ya TAKUKURU. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimewasikiliza sana asubuhi. Vyama vingi tangu vimeanza nchi hii, hoja ni Katiba mpya, Katiba mpya. CCM tukasema haya, tukaja humu ndani kutengeneza Katiba mpya. Tulipopiga kura Serikali tatu au ziwe mbili? Walio wengi wakasema ziwe mbili. Kitu gani kingine? Hawakupata walichotoka. Hivi humu ndani aliyechukua mpira akaweka kwapani tukasababisha Katiba mpya isipatikane, ni CCM au nani? Sasa leo bila aibu mnasimama hapa, tunataka Katiba mpya, Katiba mpya, aliyeimbilia na mpira, mpira ukavunjika alikuwa nani? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naona ndugu zangu wamefurahi, wameelewa. Wale ambaa hawakuelewa, wameelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi/Kicheko/Vigelele)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Mkuchika kwa maelezo ambayo naamini wote wameelewa. Kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Jenista naomba nimpe dakika mbili Mheshimiwa Mahiga ana neno muhimu anata kusema.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeomba dakika moja tu kutenda haki kwa Kamati ya Sheria Ndogo ambayo tunafanya nao kazi kwa karibu sana. Hata mchana huu nimekuwa nafanya nao kazi na kesho tutaendelea, ni watu ambaa wana mawazo chanya. Mwenyekiti wao Mheshimiwa Andrew Chenge ni Mwanasheria aliyebolea na kwa kweli ni mzalendo na mtu mwenye commitment. Hiyo political commitment ya kuhakiksha kwamba utaalam wake wa kisheria unatufikisha mahali pazuri hapa Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani za pekee kwa Kamati hii na kesho tutamalizia kuzungumzia suala letu. Ahsante sana Wana-Kamati wote na tuendelee na mshikamano wetu na mchango wenu ni wa chanya una kile kitu kinaitwa intellectual input. Ahsanteni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri mwenzangu aliyetoa mchango wake sasa hivi. Utawala wa sheria ni pamoja na kuwa na Serikali bora kama alivyosema au utawala bora. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mahiga. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Jenista, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami nianze kwa

kuwapongeza Wenyeviti wote watatu wa Kamati zote tatu kwa ripoti nzuri ambayo ameweka hapa mezani. Pia nawapongeza Wajumbe wa Kamati hizo.

Kamati ya Sheria Ndogo ninawapongeza sana kwani wamekuwa ni msaada mkubwa sana katika maboresha na marekebisho ya makosa ya namna moja ama nyingine ambayo yamekuwa yakijitokeza kwenye sheria ndogo ambazo zimekuwa zikitungwa kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa lakini vilevile kwenye Serikali Kuu, Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mwenyekiti Andrew Chenge kwamba tutaendelea kushauriana na Kamati yake na Wajumbe ili tuweze kuboresha. Kama walivyo sema, kwa kweli tumeanza kwenda vizuri ndani ya Serikali, wametupongeza, tunapokea pungezi hizo tutajitahidi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Kamati ya Tawala za Mikoa, Waheshimiwa Wabunge wamesema mengi, ninawashukuru pia. Kipekee nampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa na Kamati ya Katiba na Sheria. Kamati hiyo nayo imekuwa ni msaada mkubwa sana kwetu kwenye maeneo mbalimbali na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kweli wametusaidia sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisiti kusema, hata wewe uliyekalia kiti kama Makamu Mwenyekiti mmesaidiana sana na Kamati katika kuhakikisha tunafanya kazi zetu vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wajumbe wote ama Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hizi, lakini hasa niungane na wale Wabunge ambao wameanza kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri zinazofanywa na Serikali yetu. Vilevile nami bila kusita, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi anazozifanya. Niwathibitishie tu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, Mheshimiwa Rais wetu amedhamiria kuleta mabadiliko makubwa katika nchi yetu nasi wote tunayashuhudia kwa macho. Tumemshuhudia Mheshimiwa Rais pamoja na utendaji mbalimbali wa kazi ndani ya Serikali na Taasisi amefanya ziara za kikazi katika mikoa yote bila kubagua hata kwenye Majimbo ya Upinzani Mheshimiwa Rais amefika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesikiliza kero za Watanzania, amezitafutia ufumbuzi, amefanya hivyo kwa mapenzi makubwa na dhamira ya dhati kabisa, tuna kila sababu ya kumpongeza na kumshukuru Rais wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Makamu wa Rais na hata Waziri Mkuu mmeona, sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu tunaratibu kazi za Mheshimiwa Waziri Mkuu, mmewona Waziri Mkuu kwa kweli naye amefanya kazi nyingi na kubwa katika mikoa yote na katika nchi nzima ya Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye baadhi ya hoja. Nawashukuru Wajumbe wa Kamati na Taarifa za Kamati nikiacha ile ya Sheria Ndogo nimeshasema, lakini Kamati ya Katiba na Sheria tunawashukuru, mmeendelea kuboresha katika maeneo ya Mfuko wa Vijana; naomba niwahakikishie kwamba mmetupongeza, tunataendelea kuongeza bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua Mfuko wa Vijana sasa hivi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu ubadilishe mwelekeo, kutoka katika kutoa mikoa midogo midogo kwa wajasiriamali wadogo wadogo, ile tutaicha TAMISEMI. Sisi sasa tunataka ku-concentrate na vijana ambao ni graduates, wana certificate, walioanzisha makampuni ili wakopeshwe fedha hizo, wafungue makapuni na miradi mikubwa ambayo itatoa ajira kwa vijana wenzao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumeli-present kwenye Kamati na Kamati mmeshuhudia, tumeshafanya mageuzi makubwa sana kupitia Mfuko wa Vijana;

tunawahakikisha vijana na Waheshimiwa Wabunge, tunataka kuutumia mfuko huu tofauti na 10% ya Halmashauri twende sasa kwenye mitazamo ya ajira ambazo zinahusika na miradi mikubwa itakayofanywa kupitia kwenye mifuko wa vijana. Tutafanya hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tunajitahidi sasa hivi ili kuondoa gap ya ujuzi nchini. Tunazo program na mkakati wa Taifa wa kukuza ujuzi, kuhakikisha kwamba tunaondoa tatizo la ujuzi katika uwekezaji ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, tayari kazi hiyo inafanyika vizuri, Kamati mmeona na mmsema, nasi tutaendelea kufanya hivyo. Ili kutatua tatizo la ajira kwa vijana, tumekuja na program ya *internship* ambayo sasa tunawachukua vijana wetu graduates tunawapeleka kwenye private sector, wanakwenda kufanya mafunzo ya uzoefu na wengi wamekuwa sasa wakiajiriwa huko kwenye private sector. Kwa hiyo, Kamati imetushauri mambo mengi na tunaipongeza tunawashukuru. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa sana pia ndani ya Bunge na hasa Wabunge wa Upinzani kwamba Serikali hii haijali Wizara ya Kilimo na sekta ya kilimo. Naomba tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kwenye utaratibu wa kupitia bajeti; bajeti za Serikali ni bajeti zinazochukua sura ya kisekta. Ukichukua bajeti ya Wizara ya Kilimo utaikuta kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, utaikuta kwenye Wizara Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekuwa budgeted huko na kwenye Wizara nyagine. Hata kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu hata sisi pia tuna bajeti ya kilimo ambayo inaenda kutekeleza miradi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapa mfano, tulikuwa na programu ya MIVARAF ya kuongeza thamani ya mazao na miundombinu ya masoko. Mradi huo peke yake kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwenda kwenye sekta ya kilimo tumetumia bilioni 282.16 na hizo zote zimetoka tena programu hii imewanufaisha Bara na Visiwani pande zote mbili za Muungano. Tumeweza kujenga masoko mapya, masoko mapya peke yake 16 na nyie Wajumbe wa Kamati ni mashahidi, tumekarabati masoko matano, tumejenga maghala mapya 29 katika hiyo programu.

Lakini tumeweza kujenga miundombinu ya barabara na mpaka sasa programu hiyo imeweza kusaidia sana usafirishaji wa mazao kutoka shambani kwa sababu ya kuboresha miundombinu ya barabara kwa sasa tani za usafirishaji wa mazao kwenye programu hii zimetoka tani 230 mpaka 808 kwa sababu ya programu hiyo.

Sasa tunashangaa kama kuna wenzetu wanasimama hapa ndani halafu wanabeza kazi nzuri hii inayofanywa na Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli. Haiwezekani. (Makofii)

Ninaomba tunapokuwa tunachangia humu ndani tupingane kwa facts sasa mtu anaenda anachukua kipande kidogo tu, akichukua hicho kipande kidogo ndiyo anatangaza kama ni jambo zito kweli kweli. Naomba niwaambie Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na mpango wa bajeti za kiwizara tunao mpango na mfumo wa bajeti za kisekta, bajeti ya maafa haiwekwi kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu peke yake, itawekwa miundombinu barabara watawekewa, madarasa wataweka TAMISEMI, wataweka Wizara ya Elimu, vituo vya afya watapeleka Wizara ya Afya huo ndiyo utaratibu tunaenda kileo zaidi na tunawaambia kwamba Serikali hii imejipanga kweli kweli mtatutafuta hamtatupata, lakini sisi tunasonga mbele na vitu vyetu vinaonekana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaendelea programu hii pia imepunguza muda wa kusafirisha mazao. Kusafirisha mazao kabla ya programu hii ni ya kilimo tumebeza sana hapa fedha za kilimo, wakulima walikuwa wanatumia masaa matatu sasa wanatumia chini ya nusu saa moja na nusu kusafirisha mazao yao.

Kwa hiyo naona kwamba tumeboresha sana sana. Lakini naomba nikubaliane na ninyi yako maeneo mengine bado tunatakiwa kuyafanya kazi zaidi, kwa mfano kwenye suala la uwekezaji na biashara tunalo Baraza la Biashara la Taifa wanafanya kazi nzuri lakini

sisi sasa ndani ya Serikali tumeamua kutengeneza mifumo, mfumo wa ki-TEHAMA wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni ili mfumo uwe wazi, usiwe na usumbufu wa kusababisha kero na mlolongo mkubwa kwa wawekezaji wanapotaka kupata vibali vya wageni kama ni TIC ama kwenye sekta nyingine kazi hiyo tunaifanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa masuala ya *local content* na *local content* ipo pia ndani ya ofisi yetu na Baraza la Taifa la Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi, ambalo linasimamia sheria ya mwaka 2004 na sera ya mwaka 2004 imeendelea kufanya kazi zake vizuri. Tulichokifanya Waziri Mkuu amezindua Mkakati wa Taifa wa Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tumezindua muongozo wa uvezeshaji wananchi kiuchumi na baada ya kuyafanya hayo matokeo chanya yamepatikana, kwa mfano wakati wa ujenzi wa Daraja la Mfugale, Daraja la Mfugale lilikuwa linahitaji wafanyakazi 616 lakini wafanyakazi waliofanyakazi katika ujenzi wa daraja la Mfugale, 589 ni Watanzania na 27 ndiyo walikuwa wafanyakazi wa kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi kwenye sekta ya manunuzi tulikuwa tunataka makampuni 15 lakini kwenye manunuzi makampuni 14 yalikuwa ya Kitanzania na kampuni moja tu ndiyo lilikuwa kutoka nje ya nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, miradi hii ya kimkakati inafanyakazi vizuri sana kwenye dhana ya *local content*, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge muendelee kutuunga mkono, tutayasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda kwenye suala la mwisho na lenyewe ni kuhusu uchaguzi sasa hapa naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri. Kwenye suala la uchaguzi tumeshaanza kuboresha daftari la mpiga kura awamu ya kwanza na kwenye kuboresha daftari la mpiga kura awamu ya kwanza, umeshafanya route 13 kati ya route 14 imebakia route moja tu mikoa miwili Pwani na Dar es Salaam, na tukishamaliza route ya 14 tunaanza uboreshaji awamu ya pili kwa mujibu wa sheria, kwa hiyo siyo kweli kwamba eti hatujipanga, tumejipanga vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namuomba tu Halima atulie, ninachotaka kusema tulikadiria kuandikisha, kuboresha daftari kama ni kuandikisha wapiga kura wapya, kama nikubadilisha maeneo ya kupigia kura, kama ni jambo lolote linalohusiana na uboreshaji, tulitarajia uboreshaji huo uwe wa asilimia 17 lakini ajabu wananchi wamejitokeza wengi wamekuja kuboresha, wengi wamekuja kujiandikisha uboreshaji mpaka sasa umefika 29% ya wapiga kura wa mwaka 2015. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba wanaimani na Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli, na wanajiandaa kuhakikisha kwamba wanaingia kwenye uchaguzi. Sasa tunaambiwa kwamba hapa hii tume sijui ya uchaguzi siyo huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-quote tu Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu cha 74 (7) kifungu hicho cha 7 kinasema, kwa madhumuni ...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu jamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima naomba tumwachie amalize

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sasa hizi hoja ni za Wenyeviti sasa huyu hoja siyo yake anajibu kama hoja ya kwake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista naomba umalizie endelea, naomba uendeleee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaanza upya eneo hili. (Makof/Kicheko)

Kwa utaratibu wa shughuli zetu za Bunge...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mtulie amalizie, Mheshimiwa Jenista naomba umalize

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima sana ya kiti chako na ninaomba niendelee kusema, Ibara ya 74(7), (11) na (12) labda nisome ile ya 11 katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri ama maagizo ya mtu yeyote, au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano dhahiri tu na ninaomba Waheshimiwa Wabunge Tume hii imefanya kazi toka ilipoundwa kwa mujibu wa sheria na mfano mzuri mwaka 2010 tulipofanya uchaguzi kwa sababu Tume hii ni huru hata kama kunatoka mashtaka ya matokeo ya uchaguzi, tulijifunza kwa mfano wananchi wa Jimbo la Arusha walikwenda kuinga ushindi wa Godbless Lema mahakamani, lakini Tume ya Uchaguzi kwa sababu ni huru ilisimama na ilimpasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aungane na Tume kumtetea Godbless Lema na akabaki kuwa Mbunge ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwagine mwaka 2015 Mheshimiwa Mbunge Chief Whip Ester Bulaya, Mheshimiwa Wasira alipinga matokeo ya Ester Bulaya, lakini kwa sababu Tume hii ni huru Mwanasheria wa Serikali alisimama na Tume ya Uchaguzi na walimtetea Ester Bulaya na leo ni Mbunge mpaka leo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Ninataka kusema nini, nataka kusema hivi kifungu cha 74(7), (11), (12) kimeeleza kabisa tume yetu ni tume huru labda tu kama tunataka kuibadilisha jina, lakini kwa mujibu wa Katiba tume hii ni huru na inafanyakazi zake kwa uhuru bila kuagizwa na chama chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyio niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuingie kwenye uchaguzi tukapambane kwa hoja chama ambacho kitakuwa na hoja za msingi kitashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, haya sasa tunaendelea na Wenyeviti wa Kamati waje kuhitimisha hoja zao, tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, karibu Mheshimiwa Jasson Rweikiza dakika kumi.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi kuja kuhitimisha hoja yangu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Niwashukuru pia Wabunge wote waliochangia na kutoa mawazo mbalimbali kwenye hoja hii, ambayo yamekuwa ni ya msaada mkubwa lakini pia niwashukuru sana Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao wamejibu nyingi ya hoja hizo na kwahiyio kwenye majumuisho yangu sitagusia yale ambayo wameshajibu Mawaziri nitasema tu yale ambayo nataka kuweka msisitizo kidogo.

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba alisisitiza sana kuhusu suala la TARURA. TARURA inapata pesa kidogo sana 30% ya hela ya road fund. Road Fund ina fedha za kutosha

kujenga barabara za nchi hii lakini hela nyigi inaenda TANROADS, TANROADS barabara nyigi zimekwisha kamiliika zimejengwa kwa lami madaraja yapo TARURA ina barabara nyigi sana za vijiji ambazo ni mpya ambazo zinapeleka pembejeo, zinatoa mazao mashambani huko.

Kwa hiyo kwa kweli nisitisite tu kwamba mchango wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba umekuwa ni wa msaada kuonesha umuhimu wa jinsi ambavyo tumekuwa tukisema mara nyigi kwamba TARURA iongezewe fedha kusudi iweze kumudu majukumu yake, inakwama kwasababu fedha zake ni ndogo sana, lakini pia ameongelea sekta ya afya ambayo Waheshimiwa Mawaziri wamejibu kwa kina na kwa ukamilifu. Kuhusu kuajiri watumishi na mambo mengine.

Mheshimiwa Pauline Gekul naye amezungumza suala la TARURA kupewa 50% amependekeza kwamba ipewe 50% maana yake na TANROADS ipewe 50% ya fedha za road fund hili ni jambo zuri, tunaliunga mkono sisi kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini amesema pia Mheshimiwa Gekul mafunzo kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni jambo zuri sana, wamechaguliwa juzi hapa mwaka jana mwishoni, na kwa kweli hawana ujuzi ule unaotakiwa kumudu majukumu yao, ni vizuri waende kwenye mafunzo niseme tu kwamba mafunzo haya yako tayari, kile Chuo cha Hombolo kina kozi hizo za muda mfupi, za muda wa kati na muda mrefu. Halmashauri zijipange zipeleke hawa wenyeviti na viongozi wengine kwenye mafunzo hayo ili kuweza kupata mafunzo na kumudu shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia wazee iwekwe kwenye mpango wa 10% ni jambo zuri, ni wazo zuri kwa sababu wazee hao kwa kweli wengine hawana uwezo wa kujimudu maisha yao, ni vizuri wakapewa asilimia hizo angalau mbili kwenye hiyo 10 waweze kujisaidia katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi kama kamati tumekuwa wakali sana kwenye halmashauri hizi kwamba wahakikishe wanatenga asilimia 10 na kuzipeleka kwa wanawake na vijana na mwaka 2017 tuliwagomea hata bajeti zao, hatukupitisha bajeti zao kwamba yejote ambaye hakutoa 10% asipewe fedha za bajeti, mwaka uliofufata wakawa wamefanya maboresho makubwa sana na fedha zikawa zimeongezeka. Kwa hiyo nazipongeza Halmashauri hizo ambazo zimeboresha matoleo hayo kwa walemavu, akinamama na vijana. Sasa pendekezo la Mheshimiwa Gekul ni zuri kwamba hata wazee wafikiriwe kuingizwa huko. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Mollel ameongelea mambo kadhaa mambo mengi lakini mojawapo kubwa ni kwamba DART haijahama kutoka pale Jangwani kwenye mafuriko. Ni kweli na sisi tumeshatoa maagizo kwa DART kwamba wahame toka pale Jangwani waende sehemu ambayo ni ya juu haina mafuriko ya mara kwa mara. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Godbless Lema ameongelea mambo mengi pia, moja amesema ushindi ni kwa mtutu badala ya kutumia kura, jambo hili siyo la kweli kwa sababu kama ni kweli hata yeye amegombea na ameshinda, ina maana ameshinda kwa mtutu pia, ameingia humu kwa mtutu ambayo siyo kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vedasto Ngombale amepongeza TASAF, ndugu Mussa Mbarouk amezungumzia mambo mengi amesema uchaguzi haukuwa huru na haki, siyo kweli CCM ilishinda kwa haki kwa kura nyigi, kwa sababu haki ni pamoja na kujitoa, walijitoa walikuwa na haki ya kujitoa, walijitoa wenywewe CCM ikaendelea na uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi amezungumza mambo kadhaa mengi, Mheshimiwa Mwanne Mcemba TARURA, MKURABITA, TAGLA na eGA, Mheshimiwa Joram Hongoli wote wamezungumzia mambo ya TARURA hii inaonesha kwamba TARURA kwa kweli inastahili kuongezewa fedha. Kwa hiyo ni msisitizo mzuri ambao na sisi Kamati tunasisitiza kwamba TARURA iongezewe mgao wa fedha za road fund.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuaajiri walimu Waheshimiwa Mawaziri wamejibu hiyo. Suala la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya kwamba uraia pacha uruhusiwe. Sisi tunaunga mkono kama kamati uraia pacha uruhusiwe kwa sababu hawa wanaokwenda kule nje kwanza hawajaasi uraia wa nchi hii, lakini hawajakimbia nchi pia wameenda kutafuta tu wanatafuta fedha wanarudi wapewe uraia pacha na waweze kuleta fedha Tanzania, tunaunga mkono, TARURA amezungumzia Wizara ya Fedha. (Makofsi)

Mheshimiwa Lucy Mlowe uchaguzi mdogo amesema Wenyeviti hawakubaliki, uchaguzi haukuwa huru na haki, lakini hawakutuambia huo utafiti amefanya kwa njia gani, utafiti wake amefanyaje huo, hakutuambia ametumia mfumo gani wa utafiti, hakutuambia amehoji wananchi wangapi ambao wamesema hawawataki Wenyeviti hao. Kwa hiyo utafiti huo kwa kweli hauna mashiko.

Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia mambo mbalimbali ambayo kama nilivyo sema mengi yamejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri.

Nimalizie kwa kusema kwamba Mheshimiwa Rais Magufuli amefanya mambo mengi sana mazuri, makubwa ya kujenga nchi hii kwa weledi na uadilifu mkubwa sana. Moja ambalo halijasemwa sana ni la kudhibiti ongezeko la maeneo ya utawala, huko nyuma ilikuwa ikikaribia uchaguzi au mdogo au uchaguzi wa mitaa, uchaguzi mkuu inatengwa kata, inatengwa wilaya yanatengwa majimbo, Mikoa, Wilaya sasa hivi hiyo imekoma kupunguza gharama za utawala na hizo fedha zinatumika kujenga hospitali, kujenga barabara, kujenga madarasa na kadhalika.

Kwa hiyo nahitimisha hoja yangu kwa kuwashukuru Wabunge wote waliochangia na nakushukuru mwenyekiti kwa nafasi hii ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofsi)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza na hoja imeungwa mkono sasa nawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaokubaliana na taarifa hii ya mwaka ambayo ina maoni na mapendekezo juu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019 mpaka Januari, 2020  
Ilipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, karibu kuja kuwasilisha au kuhitimisha hoja yako Mheshimiwa Mohamedi Mchengerwa karibu.

**MHE. MOHAMED O. MCCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza

Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia taarifa yetu ya mwaka lakini kipekee kabisa niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri ambao kimsingi wamejibu hoja nyngi ambazo kamati yangu ya katiba na sheria imeziibua. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mzee Mkuchika kwa kutoa darasa zuri kwa Waheshimiwa Wabunge ambalo kwa kweli limeeleweka kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mahiga kwa majibu mazuri Mheshimiwa Kairuki ambaye ametoa ufanuzi mzuri kuhusu suala nzima la uwekezaji lakini pia Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye amefafanua kwa kina kabisa kwa hiyo hoja nyngi ambazo, zimeongeleta na Waheshimiwa tayari zimeshajibiwa na waheshimiwa Mawaziri hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima niseme kwamba tatizo kubwa ambalo nimeligundua kwa baadhi ya waheshimiwa Wabunge si hoja ya kulalamika bali ni hoja ya kutofahamu sheria na taratibu ambazo zinaongoza Taifa letu. Ni kucombe sana wewe kupitia nafasi yako umshauri Mheshimiwa Spika basi pale ambapo Wabunge wapya wanakuja katika Bunge hili kwa kupitia *legislative support programme* awamu ya pili, atumie fursa hiyo kutoa elimu ya ufahamu wa Sheria kwa Wabunge eneo hili iwapo litatimia vizuri hoja nyngi zitakuwa zimejibiwa na hakutakuwa na malalamiko yoyote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nimegundua kwa mfano Mheshimiwa Lema analalamikia malaka ya mkurugenzi ya mashitaka na Waheshimiwa wengine ukiangalia, Bunge hili halina mamlaka kwa Bunge hili kwa taarifa halina mamlaka ya kuoji vipengele vya Katiba Bunge hili halina mamlaka nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tatizo kubwa tulilonalo ambalo nimeligundua ni waheshimiwa Wabunge wengi kutokuwa na ufahamu wa Sheria kutokuwa na *knowledge* ya sheria kwahiyio pengine Mheshimiwa Spika kwa kupitia *legislative support programme* awamu ya pili aweze kutoa elimu ya ufahamu na nina amini iwapo eneo hili likitekelezwa basi maswali kama yale ambayo yalikuwa yanaulizwa ambayo yalikuwa yanaulizwa na Mheshimiwa Lema hayataulizwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na eneo la pili unapo hoji mamlaka ya DPP Mkurugenzi wa Mashitaka maana yake unaoji ibara ya 59 ya katiba zipo taratibu za kuoji katiba, zipo taratibu za kuoji sheria ambazo Bunge hili imezitunga. Kwa hiyo, kwa kutumia utaalamu ule ule ambao Mheshimiwa Spika atatusaidia Waheshimiwa Wabunge itatusaidia san asana kufahamu ni kanuni zipo ambazo kama wabunge tunapaswa kuzitumia pale ambapo tunaona sheria fulani ina mapungufu au kipengele fulani kina itilafu kidogo namna gani Mbunge anapaswa kuja na hoja hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi kama nilivyosema yamejibiwa niendelee kukumbusha tu Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kairuki basi kwa kuwa Serikali hii ni ya Viwanda kama ambavyo imesitizwa sana kwenye Bunge lako hili tukufu tumucombe Mheshimiwa anayetekeleza eneo hili la uwekezaji basi kuharakisha mchakato wa utengenezaji wa mapendekezo ya sheria ya uwekezaji. Sheria ya uharakishwaji ya uvezeshaji ya biashara ili sasa iwe raisi kwa utekelezaji wa yale ambayo malengo ya ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi imekuwa ikiwa meendelea kusitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili Mheshimiwa Jitu Soni ameniandikia akioji kuhusu utekelezaji wa sheria ya *Finance Art*, ya mwaka 2019 ambayo imetoa exemption kwa baaadhi ya utekelezaji wa misamaha ya VAT katika eneo la Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni mucombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha basi eneo hili liweze kushughulikiwa kwa haraka ili kuondoa mapungufu yaliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu vibali vya kazi ambao kimsingi Mheshimiwa Jenistar Waziri wa Nchi ametoa ufanunuzi wa kina kabisa. Lakini Mheshimiwa

Ruth Mollel amesitisiza kwa kina sana kuhusu ucheleweshwaji wa mashauri, nimuombe Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuwa jupo hapa kusitiza mahakimu wetu wote nchini na kutumia kifungu cha 225 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ili kuweza kuharakisha katika mashauri ambayo yanachelewa ili mashauri yale ambayo yamevuka siku 60 basi kuona uwezekano wa mahakimu kuyaondoa mashauri yale ambayo iwapo Serikali basi itaona kwamba iko tayari kuendelea na mashitaka hayo inaweza kuleta kwa kupitia kifungu hicho hicho kifungu kidogo cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo limesitisiza kwa kina ni kuhusu mamlaka ya mkurugenzi wa Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa niwaombe waheshimiwa Wabunge watambue kwamba katiba yetu lakini pia sheria ya kupambana na kuzuia rushwa sura ya 7 sheria hii inatoa ufanuzi kifungu cha 7 kinatoa ufanuzi wa kazi ambazo taasisi hii inafanya kwa kina kabisa sina haya ya kurudia niwaombe Waheshimiwa Wabunge tujielekeze pengine tukisoma sheria hii maswali kama haya ambayo ni mepesi yanaweza yasiilizwe kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo Mheshimiwa Lema alioji ni kuhusu mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashitaka kuliondoa shitaka pale ambapo anapoona ye ye anapendezwa nalo kuliondoa na kulirejesha wakati wowote niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba tukisoma mwenendo wa makosa ya jinai kifungu cha 91 kinampa mamlaka mkurugenzi wa mashitaka na mamlaka yake hayahojiwi sehemu yoyote ukisoma Ibara ya 59 ya katiba mamlaka ya mkurugenzi wa mashitaka haojiwi wakati wowote pale ambapo wataona inafaa anauwezo wa kuliondoa shitaka wakati wowote kabla ya hukumu kutolewa na mahakama. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili jukumu ni la mkurugenzi wa mashitaka na nijukumu la Bunge hili iwapo inaona kwamba kipengele hiki hakifai basi Bunge hili linaweza kujiongeza ili kuona uwezekano wa kurekebisha kifungu hiki. Lakini kwa sasa hatuna mamlaka ya kuhoji mamlaka ya mkurugenzi wa mashitaka ambaye yanapatikana katika ibara ya 59 ya katiba yetu lakini mamlaka ya kufuta shitaka wakati wowote kabla ya hukumu kutolewa yapo kwa mujibu ya kifungu 91 cha sheria hii kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge kujielekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hoja nyingi zimejibiwa na Waheshimiwa Mawaziri na mimi naomba kutoa hoja kwa taarifa yangu kama ambavyo nimesema hapo ahsante.

**MHE. YAHAYA Y. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria hoja imeungwa mkono na sasa niwahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MWENYEKITI:** Wote wamekubali kwa hiyo sasa ni maazimio rasmi ya Bunge. Tunamalizia na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo oje kuhitimisha hoja yake karibu Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria ndogo Mheshimiwa William Ngeleja karibu sana.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019 mpaka Januari, 2020 Ilipitishwa na Bunge)

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNG** **YE SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa niaba ya

mwenyekiti wetu wa Kamati ya Sheria Ndogo Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge ninaomba kuhitimisha hoja yetu iliyowasilishwa asubuhi ya leo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kukushukuru wewe kutuongoza vizuri siku ya leo kama ilivyosiku zote, lakini pili kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hizi taarifa tatu ambazo zimewasilishwa leo kwa upekee nawashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri pamoja na Waziri kwa ujumla wake. Kwa kufafanua hoja ambalimbali ambazo ziliibuliwa na Waheshimiwa wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kamati ya Sheria Ndogo tunaendelea kupokea salamu hizi za upendo salamu za pongezi kwa kadri ambazo zimejitokeza kwenye mjadala huu na tunalihakikisha Bunge lako tukufu kwamba Kamati yetu ya Sheria Ndogo iko tayari itaendelea kuyatenda yaliyomema kwa maslahi ya Taifa letu na tunaendelea kumshukuru sana rafiki yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa coordination nzuri unayoifanya tupo tayari tulishawahili kujadili huko nyuma kwamba kwa kadri ambavyo Serikali na viongozi wetu wa Bunge mtakavyoona inafaa kwa sababu sheria ndogo zimekuwa nyingi leo umesikia habari ya sheria ya mia nane tisini na kitu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposikia kwamba kati ya sheria 897 zilizowasilishwa lakini zinaonekana zinadosari labda ni sheria ya 73 haimaanishi kwamba sheria zingine zote hazikuchambuliwa maana yake kwamba sheria zote kamati imezipitia kwa hiyo, inatumia muda mwingu. Kwa hiyo, tulishawahili kuweka wazo na tunaendelea kushauri kwamba kwa sababu kwamba kwa sababu katika mfumo wetu wa uendeshwaji Bunge kuna baadhi ya Kamati ambazo kwenye mikutano yetu ya kawaida huwa zinatangulia angala wiki moja kabla ili tuondoe tupunguze stress ya muda tunaotumia kuzichambua hizi Sheria Ndogo utawala, mtaangalia kama hilo linawezekana ili Kamati ya Sheria Ndogo pia ipate hiyo fursa hili tufanye kazi kwa utulivu zaidi kuliko tunavyofanya sasa pamoja na kwamba haijaathiri ubora wa kazi tunazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiendelea kuhitimisha hoja yetu kuna mambo matatu tunataka tukumbuswa na ninaikumbusha Serikali kwa sababu wenyewe wamekuwa wakiwasilisha hizi Sheria Ndogo kwetu. La kwanza ni jambo la ujumla kwamba tunauzoefu wa kuona kwamba kwenye taasisi nyingi za Serikali wanasheria hasa wenyewe taaluma ya ususi wa uandishi wa hizi sheria kimsingi kuna uhaba wake na tunahitaji kuongeza ajira katika eneo hili na kuboresha ama kuboresha mafunzo kwa waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunaomba Wizara ya Sheria kwa ujumla wake na hasa kitengo hiki cha Uwandishi wa Sheria *legislative draft file* tunaomba sana kipewe nafasi tupate kuongeza nguvu kazi pale kwa ajili ya kuboresha shughuli za uandishi wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili ambalo tunakumbusha Serikali ni kwamba tumeshuhudia sisi kwenye Kamati zetu katika utendajiwetu wa kazi wa kila siku ziko baadhi ya Sheria Ndogo zinazokuja kwa namna ambavyo zimetungwa ni kama zinapoka mamlaka ya na madaraka ya Sheria ambazo zimeziazisha hizi Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni changamoto inawezekana si rahisi sana kuielewa tulivyozungumza lakini kwenye Kamati tunaweza kuelewa, tuna utungaji wa Sheria Ndogo na misingi yake sasa inapotokea kwamba Sheria Ndogo zile ambazo kimsingi zinatungwa kutokana na Sheria mama zenyewe tena zinakuwa na mamlaka na masharti ya kupoka sheria ya mama ambazo ndiyo kwanzo ndiyo zimetungwa kutokana na hizo Sheria mama tunakuwa na tabu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunaiomba sana Serikali pamoja na vyombo vingine vinavyoshiriki katika utungaji wa sheria ndogo ili kupunguza muda wa kuzipitia hizi

Sheria Ndogo lakini pia usumbufu wa kila wakati kukumbushana ili jambo pia lizingatiwe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho lakini siyo la umuhimu, tunaikumbusha Serikali kwamba katika utungaji wa hizi Sheria Ndogo na hasa tunapoanza kutunga Sheria mama, Sheria yake inamchakato wake kuna Muswada unajadiliwa sasa katika masharti ambayo yamekuwa nyakati nyingine inatokea masharti inayopendekezwa katika Muswada wa Sheria unaokuja kuzaa Sheria ambayo baadaye zinatungwa Sheria Ndogo. Wakati mwingine kunakuwa na baadhi ya masharti ama vifungu vya Sheria hizo mama yanakataliwa kwenye mjadala kama hapa bungeni ama hata upande wa Serikali kutokana na mashauriano ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo masharti hasi ambayo yanakataliwa mara nyingi huwa tunaona yanaibukia tena kwenye Sheria Ndogo sasa hili ni jambo ambalo limekuwa likitukwanza kidogo kama kamati lakini yote kwa yote ndiyo umuhimu wa kuwepo Kamati ya Sheria Ndogo ya Bunge lako Tukufu ndiyo ni sehemu yetu ya kazi yetu tunaamini kabisa kama haya yote yasingekuwepo bali isingekuwa na uhalali wa kuwepo. Lakini jambo jema kukumbusha kwamba kwa yale masharti ambayo yamekuwa yakikataliwa kwenye utungaji wa sheria mama yasije tena kupitia mlango wa nyuma yakaibukia huku kwa sababu huku milango imefungwa, ni jambo la kukumbusha ni jambo jema. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa mara nyingine niwashukuru sana Wabunge wenzangu ahsanteni sana tupo tayari kushirikiana na ninyi na kwahauta hii sasa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo naomba kutoa hoja kwa mara nyingine tena ahsante sana. (Makofii)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti ya Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo hoja yako imeingwa mkono, sasa nawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa wote wamekubaliana na kwamba sasa haya maoni na mapendeleko na taarifa nzima ya Kamati ya mwaka iwe maazimio ya Bunge kwa hiyo natangaza rasmi kwamba taarifa zote tatu ambazo tumeshughulikia kwa siku ya leo zimepokelewa na Bunge hili na zimekuwa sasa ni maazimio ya Bunge.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2019 mpaka Januari, 2020 ilipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, napenda tu nitoe shukrani kwa wote ambao wameshiriki katika kazi hii kamati zote tatu na wenyeviti wao pamoja na wajumbe lakini na Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu yote kwa siku ya leo.

Lakini pia Waheshimiwa Mawaziri kwa ufanuzi ambao mmetoa na niombi kuwajulisha tu Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunasoma taarifa hizi Waheshimiwa Mawaziri nao wanawajibu kama sisi wakuweza kufafanua na kutoa maelezo kuhusiana na zile taarifa sisi kamati tunazileta hata kama ikiwa ngapi lakini wanawajibu wakutoa maelezo kwa hiyo ni wajibu ni haki yao kama ambavyo wana haki na wajibu wa kwenda kutekeleza yale sasa yameshakuwa maazimio ya Bunge. (Makofii)

Lakini hata hivyo pia napokea ombi na ushauri wa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa ambavyo ameniomba nimshauri Mheshimiwa Spika basi pale ambapo kunapopatikana fursa Waheshimiwa Wabunge wapatiwe mafunzo maalum ya kuweza kujua wanawajibika vipi na wakati upi kama ni taarifa za kamati wanachangia nini kama ni bajeti wanafanyaje hii nafikiri itatusaidia kuelewa siyo unatoka nje ya hoja unazungumza kitu ambacho hakipo kabisa kwenye hoja hii itakuwa haitusaidi kujenga Bunge letu wala kuisaidia nchi yetu. (Makofii)

Kwa hiyo, nimekubaliana na Mheshimiwa Mwenyekiti na nitaifikisha kwa Mheshimiwa Spika na ushauri huo utaenda kwa namna inastahiki baada ya kusema hayo nawashukuru nawatakieni jioni njema naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, tarehe tano saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.35 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatano,  
Tarehe 4 Februari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*